RIPOTI YA KAMATI YA KUCHUNGUZA NA KUDHIBITI HESABU ZA SERIKALI NA MASHIRIKA (P.A.C) YA BARAZA LA WAWAKILISHI, ZANZIBAR, 2012/2013.

SEHEMU YA KWANZA:

1.0 UTANGULIZI:

Katika Historia ya Kamati za Baraza la Wawakilishi tokea kuanzishwa kwake mwaka 1980, Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali (P.A.C) imeanza kuwepo tokea mwaka huo (1980), na katika kufanya kazi zake, pamoja na kuwa na majukumu mengi, jukumu maarufu linalotarajiwa kuwanyiwa kazi kila mwaka ni kuchunguza na kutoa ripoti yake juu ya hesabu za mwaka na matumizi ya fedha za Serikali na Mashirika yake na hesabu nyengine zozote zitakazowasilishwa mbele ya Baraza kupitia ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Kwa kawaida, ripoti hiyo ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu huwa ni moja kwa kila mwaka, na imetokezea mwaka 2009/2010, Kamati ilifanyia kazi Ripoti tatu za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa wakati mmoja, lakini mwaka huu, Kamati imefanyia kazi Ripoti tano (Mbili za Ukaguzi wa Hesabu, na 3 za Thamani halisi ya fedha (value for money) kwa pamoja.

Katika kuzifanyia kazi Ripoti hizo, Kamati imegundua namna Wizara na Taasisi mbali mbali za Serikali zinavyotekeleza majukumu yao kwa mnasaba wa hoja mbali mbali zilizoripotiwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu. Aidha, kuna hoja mbali mbali zimepata majibu, na nyingi hazijapata majibu ya kuridhisha. Kibaya zaidi, Kamati imegundua kuwepo kwa ubadhirifu wa fedha za Serikali na ubadhirifu na ufujaji wa mali za Taasisi hizo, huku Sheria ya Fedha na Kanuni zake za mwaka 2005 pamoja na Sheria ya Manunuzi na Ugavi wa Mali za Serikali na Kanuni zake, zinaendelea kuvunjwa. Hali hii inaisikitisha sana Kamati, ambayo kwa muda mrefu sasa inaendelea kusisitiza haja ya kufuatwa kwa Sheria hizo ipasavyo.

1.1 MAJUKUMU YA KAMATI:

Kamati inatekeleza majukumu yake kwa mnasaba wa Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984, Sheria Namba 4 ya mwaka 2007, Sheria Namba 12 na Sheria Namba 9 za mwaka 2005 (pamoja na kanuni zao), na Kanuni za Baraza la Wawakilihi, Zanzibar. Kwa upande wa toleo la mwaka 2012, Kamati inatekeleza majukumu yake zaidi kupitia kanuni ya 118(2) ya Kanuni za Baraza, ambayo hapa chini tunainukuu:

(a) Kuchunguza na kutoa taarifa juu ya hesabu za mwaka za matumizi ya fedha za Serikali na Mashirika yake na hesabu nyengine zozote zitakazowasilishwa mbele ya Baraza kupitia ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

(b) Kuchambua na kutafakari ripoti yeyote ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu pale ambapo Rais aliagiza ukaguzi huo ufanywe.

(c) Kuchunguza kwa njia yeyote inayofaa mambo yote yanayohusu hesabu za Serikali na asasi zake.

(d) Kutoa Ripoti yake baada ya kufanya uchunguzi kuhusiana na matumizi ya ziada ya fedha iliyotolewa kwa mwaka wa fedha unaohusika.

(e) Kufuatilia utekelezaji wa maagizo ya Kamati yaliyotolewa kwenye Ripoti ya Kamati ya mwaka uliotangulia.

(3) Katika kufanya kazi zake Kamati ya PAC itakuwa na wajibu wa kuchunguza kama:

a. Fedha zilizooneshwa katika makadirio ya Matumizi ya Serikali na Mashirika yake zimetumika kama iliyvokubaliwa;
b. Matumizi yalikuwa chini ya mamlaka iliyohusika; na
c. Matumizi yaliyofanywa yalizingatia thamani halisi ya fedha.

1.2 WAJUMBE WA KAMATI:

Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika kwa mwaka 2012/2013, inaundwa na Wajumbe 8 na Makatibu 2. Wajumbe wa Kamati ni hawa wafuatao:

1. Mhe. Omar Ali Shehe — Mwenyekiti
2. Mhe. Fatma Mbarouk Said — Makamo Mwenyekiti
3. Mhe. Abdalla Juma Abdalla — Mjumbe
4. Mhe. Farida Amour Mohammed — Mjumbe
5. Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando) — Mjumbe
6. Mhe. Mohammed Mbwana Hamad — Mjumbe
7. Mhe. Shadya Moh'd Suleiman — Mjumbe
8. Mhe. Shamsi Vuai Nahodha — Mjumbe.

Aidha, kwa upande wa Makatibu (ambao ndio Sekretarieti ya Kamati), kazi zote za uratibu wa Kamati, zimeratibiwa na Watendaji wafuatao:

1. Ndg. Amour Moh'd Amour — Katibu.
2. Ndg. Othman Ali Haji — Katibu

1.3 REJEA ZA KAZI:

Katika kutekeleza jukumu lake lililoainishwa na Kanuni ya 118(2)(a) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi, toleo la 2012, Kamati imefuatilia Ripoti tano za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Ripoti hizo ni hizi zifuatazo:

1) Ripoti ya Ukaguzi Yakinifu wa Miradi ya Maendeleo ya Wananchi na Miradi ya TASAF, kwa mwaka wa fedha 2009/2010.

2) Ripoti ya Ukaguzi Yakinifu wa Udhibiti na Uhifadhi wa Mali za Kudumu za Serikali, kwa mwaka wa fedha 2009/2010.

3) Ripoti ya Ukaguzi wa Hesabu kwa Mawizara, Mashirika na Taasisi za Serikali, kwa mwaka wa fedha 2009/2010.

4) Ripoti ya Ukaguzi wa Hesabu kwa Mawizara, Mashirika na Taasisi za Serikali, kwa mwaka wa fedha 2010/2011.

5) Ripoti ya Ukaguzi Yakinifu kwa Miradi ya Taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kwa mwaka wa fedha 2010/2011.

Mbali na Ufuatiliaji huo wa Ripoti hizo, Kamati kwa kutumia kanuni ya 118(2)(c) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi, Kamati pia ilifuatilia uchambuzi wa Mapato na Matumizi kwa Baadhi ya Taasisi na Mashirika ya Serikali kwa mwaka 2010/2011, ili kuangalia kwa namna gani Taasisi hizo zinakusanya na zinatumia fedha za umma kwa mujibu wa taratibu za Sheria zilizowekwa.

1.4 UHUSIANO ULIOPO BAINA YA KAMATI YA PAC NA AFISI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZANZIBAR.

Kwa kawaida, baada ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, kuwasilisha Ripoti yake ya ukaguzi katika Baraza la Wawakilishi, kazi inayofuata ni Ripoti hiyo kuwasilishwa na kukabidhiwa kwa Kamati ya Kuchunguza Hesabu za Serikali na Mashirika (P.A.C), kwa lengo la kuifanyia kazi, na baada ya kazi hiyo, Kamati nayo hutakiwa kuwasilisha ripoti yake Barazani. Hali hii kwa namna yoyote ile, inazifanya Taasisi hizi mbili kuwa na mashirikiano ya karibu mno kila wakati.

Aidha, Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu inashirikiana na Kamati ya P.A.C katika ufuatiliaji na utekelezaji wa mapendekezo yaliyotolewea na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu katika ripoti yake. Na takriban Afisi ya Mdhibiti na Kamati ya P.A.C zinasimamia kwa pamoja dhana nzima ya matumizi ya fedha za umma kwa mujibu wa Sheria na taratibu zilizowekwa. Kwa namna moja ama nyengine, Afisi hii ya Mdhibiti na Kamati hii ya P.A.C, ni vigumu kuzitenganisha. Katika hali kama hii, ni wazi kwamba, kazi ya kukagua, kuchunguza na kudhibiti fedha za Serikali ni ngumu mno na inahitaji moyo wa kizalendo. Lakini ni muhimu mno kwa Serikali, na Serikali inayojali maslahi na ustawi wa wananchi wake, kama ilivyo kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, hufanya kila njia kuwepesisha utekelezaji wa majukumu ya Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, pamoja na Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali.

Ili kuunganisha ‘spirit’ ya uzalendo na kusimamia ipasavyo majukumu haya mazito, lazima changamoto zinazoikabili Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu, ziondolewe mara moja, ili kuweka wepesi na kujenga ujasiri wa watumishi wa Afisi hii, wa kudhibiti hesabu za Serikali. Hili katika utekelezaji wake, litaanza kwa kupiga kelele juu ya maslahi madogo ya

watendaji wa Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu. Kamati imezoea kulipigia kelele suala hili zaidi ya miaka mitano iliyopita, na itaendelea kufanya hivyo, kwa kuamini kwamba, iwapo tutajenga imani na ukinaifu kwa wakaguzi wa fedha za Umma, tutakuwa tumeshajenga ngome ya kufichuliwa kwa wabadhirifu wa mali za umma.

Aidha, katika kuzipa uwezo Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu pamoja na Kamati ya P.A.C, ni kuzipa wepesi katika kutekeleza Sheria zinazohusiana na utekelezaji mzima wa majukumu yao. Kwa mfano kwa kuwa kuna mapungufu mengi ya kiutendaji katika sheria yake namba 11 ya 2003 ya Uanzishwaji Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu, na kwa kuwa Sheria Namba 12 ya mwaka 2005 na Namba 9 ya mwaka 2005 tayari zinahitaji kurekebishwa kutokana na ama kuwemo kwa baadhi ya vifungu vya sheria hizo vinavyopingana na Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984; ama sheria za kimataifa za ukaguzi au hata kupitwa na wakati, basi ni wazi kwamba, kufanyiwa marekebisho ya haraka kwa Sheria hizo, ni kuzisaidia sana Afisi ya Mdhibiti na Kamati ya P.A.C, kuweza kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi mkubwa.

La mwisho ambalo pia ni muhimu, ni uhusiano wa kitaaluma unaohitajika uwepo baina ya Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu na Kamati ya P.A.C. Hii ina maana, Ripoti yoyote ya ukaguzi inayotelewa na Afisi ya Mdhibiti ni ya kitaalamu. Na kwa bahati njema, Wajumbe wa Kamati sio wote wataalamu wa Ukaguzi, lakini wanalazimika kufanya kazi za ukaguzi (uchunguzi wa fedha na matumizi yake). Katika hali hii, kama Wajumbe hawa wa Kamati, hawasomeshwa vizuri masuala ya fedha na wakayafahamu, kazi tunayowapa ya kudhibiti fedha za Serikali haitafanyika kabisa ama haitatekelezwa kwa ufanisi. Hili linahitaji kwanza kuijengea uwezo wa kifedha na kitaalamu Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu, ili nayo iweze kuiwezesha Kamati ya P.A.C kutekeleza majukumu yake, kitaaluma na kitaalamu.

Hili na lifanyike pia kwa kuongeza utaalamu kwa Sekretarieti ya Kamati, ambayo ndio roho, macho na masikio ya Kamati, lakini pia kwa kuongeza bajeti ya Afisi ya Mdhibiti, ili fursa zaidi za masomo kwa Wajumbe, Sekretarieti ya Kamati pamoja na Watendaji wote wa Afisi ya Mdhibiti ziweze kuongezeka.

1.5 MUUNDO WA RIPOTI:

Kwa mujibu wa kanuni ya 122(5) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi, Ripoti ya Kamati hii imelazimika kugawanywa katika Utangulizi, ambao umejumuisha hadidu rejea na utaratibu uliohusika katika kazi za Kamati; Maudhui yatakayotoa maelezo yote kuhusu mambo yaliyofanyiwa kazi na Kamati na Hitimisho litakalotoa maoni na mapendekezo ya Kamati.

Hata hivyo, kwa kuifanya Ripoti hii isomeke na kufahamika kwa urahisi, Tumeigawa katika Sehemu, ambapo Sehemu ya Kwanza inahusisha Utangulizi; Sehemu ya Pili inahusisha Maudhui, ambapo ndipo tulipotoa Ufafanuzi wa Ripoti zote tano kwa ufafanuzi wa hoja moja baada ya moja na Sehemu ya Tatu inayojumuisha Hitimisho. Aidha, kwa kuwa Kamati ya P.A.C hutakiwa kutoa maoni na mapendekezo katika kila Hoja ya Mdhibiti, basi na ripoti hii imetoa

mapendekezo na maoni ya Kamati juu ya hatua zinazotakiwa kuchukuliwa kwa kila hoja, katika maneno yanayosomeka “Maoni ya Kamati”.

1.6 MAMBO YALIYOBAINIKA KATIKA UFUATILIAJI RIPOTI TANO ZA MDHIBITI NA MKATUZI MKUU WA HESABU:

Ni vigumu kueleza kila jambo lililobainika ambapo hupatikana katika Maudhui ya Ripoti hii, lakini ni vyema tukaainisha baadhi ya mambo hayo kama ifutatavyo:

- Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo haikusimamia ipasavyo fedha za Miradi ya Maendeleo ya Wananchi, na matokeo yake, matumizi ya fedha hizo yameachwa kwa wananchi ambao hawana uelewa wa masuala ya fedha.

- Baadhi ya watendaji wa Kamati za Maendeleo zilizokuwa zinasimamia utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ya Wananchi, hawakuwa waaminifu katika kusimamia fedha za Miradi hiyo, jambo lililopelekea kuwepo kwa migogoro mingi katika Kamati zenyewe, lakini pia Maendeleo yaliyokusudiwa kukosekana.

- Fedha nyingi zimetumika kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo na Miradi ya TASAF, lakini lengo la miradi hiyo halikupatikana.

- Kamati za Maendeleo pamoja na Kamati za Shehia, zinashindwa kutelekeza sheria za fedha ipasavyo, na Wizara zinazohusika zimeshindwa kuwaelimisha wananchi hao. Hali hii imepelekea miradi hiyo kujengwa katika kiwango kilicho chini ya kiwango na baadhi ya miradi kufa kabisa.

- Miradi mingi ya TASAF inayohusiana na Ufugaji, haikuendelea na imekufa kabisa mara tu baada ya Miradi hiyo kukabidhiwa wananchi.

- Taasisi nyingi za Serikali bado zinakabiliwa na tatizo la kutokuwa na Daftari la kuhifadhia mali za kudumu za Taasisi hizo, na baadhi yao ambazo tayari wamekwisha anzisha, Madaftari hayo yana mapungufu kadhaa ikiwa ni pamoja na kukosa taarifa muhimu zinazohitajika.

- Bado Hati miliki imekuwa ni tatizo kwa Taasisi nyingi za Serikali, ambapo tatizo la kukosekana kwa hati miliki kwa mali za Serikali linaendelea. Kinachoishangaza Kamati ni kwamba, maombi ya kupatiwa hati hizo kwa Taasisi za Serikali yanachelewa wakati Taasisi za watu binafsi (sambamba na watu binafsi) zinapata wepesi wa kumiliki hati hizo.

- Kamati imeshuhudia Taasisi nyingi za Serikali, hazijaanzisha Kitengo cha Manunuzi. Tatizo kubwa linalokwamisha hatua hii kufikiwa ni pamoja na kutoajiriwa kwa Maofisa Manunuzi, ambao kwa mujibu wa elimu zao na usimizi wa vitengo hivi, wana mchango mkubwa katika kuanzishwa kwake. Aidha, kwa zile Taasisi ailobahatika kuanzisha Mpango huo, bado zinakabiliwa na tatizo la kutoufuta ipasavyo Mpango huo.

- Bado tatizo la kukosekana kwa vielelezo vya matumizi ya fedha za Serikali linaendeleta. Aidha, kuna baadhi ya Taasisi huisubiri Kamati, ili kuithibitishia vielelezo hivyo ambavyo wakati wa ukaguzi vimekosekana. Hii huleta tafsiri kwamba, Kamati hufanya kazi ithibitishe kuvunjwa kwa Sheria ya Fedha inayoelekeza vielelezo hutakiwa vitapatikane mara tu fedha ya Serikali inapotumika.

- Utekelezaji wa Miradi ya Serikali bado haujazingatiwa kwa upana wake kwa maslahi ya Taifa. Kamati imebaini kwamba, Miradi mingi hutekelezwa bila ya kuzingatia Sheria za fedha, lakini pia hugeuka kuwa ni sehemu ya baadhi ya watengaji kujinuifa kibinafsi.

SEHEMU YA PILI (MAUDHUI YA RIPOTI):

2.0 UFAFANUZI WA HOJA ZA RIPOTI TANO ZA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU KWA MWAKA 2009/2010 NA 2010/2011.

Kama tulivyokwisha eleza katika Muundo wa Ripoti kwamba Sehemu hii inahusiana na Maudhui ya Ripoti. Kwa kuwa Ripoti hii inatoa ufafanuzi wa Ripoti tano za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali; Kamati nayo imezigawa Ripoti hizo na kila moja kutoa ufafanuzi wake. Hata hivyo, tumeziweka zote katika Sehemu hii, ili kutoa maudhui yaliyokusudiwa. Kwa ufupi Ripoti hizo zitafafanuliwa kwa utaratibu ufuatao:

RIPOTI YA KWANZA:

2.1 RIPOTI YA UKAGUZI YAKINIFU WA MIRADI YA MAENDELEO YA WANANCHI NA MIRADI YA TASAF KWA MWAKA WA FEDHA 2009/2010.

Ripoti hii inahusiana na Miradi ya aina mbili; Kwanza ni Miradi ya Maendeleo ya Wananchi ambayo ilikuwa inasimamiwa na Wizara ya Fedha na Uchumi na Aina ya Pili ni Miradu ya TASAF, ambayo ilikuwa inasimamiwa na Afisi ya Waziri Kiongozi (Hivi sasa inasimamiwa na Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais). Chanzo cha Miradi yote miwili ni nguvu za wananchi. Ni wananchi wenyewe huibua miradi hiyo na hatimae huomba fedha ama kutoka Wizara ya Fedha na fedha hizo huwafika moja kwa moja; ama kwa kupitia Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais, ambapo husimamiwa na TASAF.

Katika kuifanyia kazi Miradi hiyo, Kamati iliifuatilia katika ngazi za Mikoa, na hata katika ripoti hii imetambuliwa sana kwa ngazi ya Mikoa, lakini pia Kamati ilikutana na Serikali za Wilaya,Masheha, Kamati za Maendeleo za wananchi zilizosimamia Miradi hiyo, Wizara na Taasisi za Serikali zilizokabidhiwa ama zinazohusika na Miradi hiyo pamoja na Uongozi TASAF na watendaji wa Ofisi ya Rais, Fedha,Uchumi na Mipango ya Maendeleo. Na kwa bahati, katika muda wote wa kazi, Kamati ilikutana na taasisi hizo kwa pamoja.

Ufuatao ni uchambuzi wa Hoja hizo kama zilivyoripotiwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na kufanyiwa uchunguzi na Kamati:

2.1.2. TAARIFA ZA MIRADI; MKOA WA KASKAZINI UNGUJA.

2.2.1 MIRADI YA MAENDELEO YA WANANCHI:

Hoja Namba 3.1.1 Kuhusiana na Mradi wa Uchimbaji wa Kisima, Kigunda.

Mradi huu umeingiziwa Tsh.3,500,000 kwa mwaka 2009/2010 kwa lengo la kuchimba kisima, ili wananchi wa Kigunda waweze kupata maji safi na salama.

Maelezo ya Kamati ya Maendeleo iliyosimamia Mradi:

Tatizo la maji safi na salama kwa Shehia ya Kigunda, lilianza tokea mwaka 2006, na ilipofika 2008, walipata Mfadhili (Meneja wa Nugwi Beach Resort)wa kuwachimbia kisima, lakini sharti lake ni kupewa kibali kinachoruhusu uchimbaji huo, jambo ambalo wananchi hao kwa wakati huo, walishindwa kukipata.

Ilipofika 2009, walipata msaada wa 5,000,000 kutoka kwa 'Action Aids', na hivyo walikwenda Mamlaka ya Maji (ZAWA) kwa ajili ya kuchimbiwa Kisima, lakini kwa bahati mbaya, fedha zilizotakiwa na ZAWA zilikuwa nyingi kinyume na uwezo wa wananchi hao, hata hivyo, baadae walifikia katika Tsh.17,000,000 kama ni gharama za uchimbaji wa kisima hadi kutoa huduma kwa wananchi. Na ndipo wanakijiji hao walivyojitahidi kutafuta wafadhili na hatimae hata Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, ilitoa hizo Tsh.3,500,000 zilizowasaidia kutimiza azma yao hiyo.

Maelezo ya Kamati:

Pamoja na juhudi zilizochukuliwa na wananchi hao, jambo la kusikitisha, bado wananchi hao hawapati huduma ya maji safi na salama kama ilivyokusudiwa. Tatizo kubwa linaloelezwa ni kukosekana kwa 'pump' za maji na mabomba ya kusambazia, hali inayoufanya mradi huu kushindwa kutimia lengo lake lililokusudiwa.

Maoni ya Kamati:

Kamati inaitaka Mamlaka ya Maji, ZAWA kuhakikisha wanawapatia wananchi hawa 'pump' na mabomba yatakayoweza kusambaza maji kama ilivyokusudiwa.

Hoja Namba 3.1.2 Kuhusiana na Mradi wa Ujenzi wa Skuli ya Maandalizi, Pangeni.

Kwa mwaka 2009/2010, Mradi huu uliingiziwa Tsh. 4,000,000 kwa ajili ya Ujenzi wa Skuli ya Pangeni. Kati ya fedha hizo zilizoingizwa kwenye Akaunti ya Kamati ya Maendeleo, ni Tsh.1,000,000 pekee ndizo zilizotumika na Tsh. 3,000,000 zimebaki benki, huku lengo la Mradi huo halikufikiwa, kutokana na kukosekana kwa wataalamu wa ujenzi na mazingira ya mahali ujenzi ulipofanyika.

Maelezo ya Kamati ya Maendeleo iliyohusika na Usimamizi wa Ujenzi:

Kamati hii ina watu 10, huku wakieleza kwamba, fedha hizo, Tsh.4,000,000 zilitumika kwa ujenzi wa tofali, kusajili Jumuiya yao, kuanzisha Katiba ya Jumuiya na mambo mengine. Katibu wa Kamati hii alieleza kwamba, fedha zote Tsh.4,000,000 zimekwishatumika, huku Kamati pekee ndiyo iliyojenga bila ya kupata mashirikiano kutoka kwa wananchi wengine. Hali iliyopelekea gharama za ujenzi kuongezeka.

Maelezo ya Kamati:

Kamati imeshangazwa na Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kutoujua mradi huu na kueleza kwamba hawakuhusika nao, huku Afisa aliyeiwakilisha Ofisi hii, kwa siku hiyo akishindwa kueleza ipasavyo. Aidha, matumizi ya fedha hizo kwa shughuli za Jumuiya, ikiwa ni pamoja na usajili wake, hayaendani na makusudio ya kutolewa fedha hizo.

Kamati ilitaka kupatiwa uchanganuzi wa matumizi ya fedha hizo, na baada ya kuwasilishwa, Kamati ilijiridhisha kwamba fedha zilizoelezwa katika uchanganuzi huo zinahusiana na Ujenzi tu, ikiwa ni pamoja na ununuzi wa matofali, saruji, mchanga, kokoto, mbao, bangili na waya wa kufungia nondo, mafundi, usafiri na ununuzi wa nondo-matumizi yote yakiwa ni Tsh.3740,000/, wakati fedha zote zilitotengwa ni Tsh.4,000,000.

Aidha, kuhusiana na kutokukaa sawa kwa matumizi ya fedha hizo sio jambo geni, kwa sababu hata wanachama wa Jumuiya hii (JUMAFA), wameieleza Kamati kwamba, hata wao hawakupatiwa hata siku moja, ufafanuzi mzuri wa matumizi ya fedha hizo, na hii ni miongoni mwa sababu zilizopelekea Jumuiya hii, kugawanyika.

Maoni ya Kamati:

Lengo la mradi huu halikufikiwa, huku kukiwa na shaka kubwa ya kutotumika vizuri kwa fedha zilizotolewa, na Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo ikishindwa kutoa maelezo ya kina kuhusiana na Mradi huu. Kamati inaitaka Serikali, kuwachukulia hatua za kisheria zinazofaa wale wote waliohusika na matumizi mabaya ya fedha hizo, miongoni mwa viongozi wa Jumuiya ya Maendeleo iliyohusika na usimamizi wa Mradi huu, pamoja na watendaji ambao walikuwa wakisimamia Mradi huu kutoka Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo.

Hoja Nambari 3.1.3 Kuhusu Mradi wa Uchimbaji wa Kisima, Fukuchani:

Mradi huu uliingiziwa Tsh. 4,500,000 kwa lengo la kuchimba kisima ili kiweze kuwahudumia wananchi wa Fukuchani, Kigongoni na Mwanguo kutokana na upungufu mkubwa wanaoupata wa kupata maji safi na salama. Hata hivyo, kutokana na upungufu wa mabomba ya kusambazia maji katika maeneo hayo, Mradi huo haukuweza kufikia lengo.

Maelezo ya Kamati ya Maendeleo iliyohusika na Usimamizi wa Mradi:

Ni kweli waliomba Mradi huo Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo na kuelekezwa zitumike kwa ajili ya kusambazia maji, huku wakifanikiwa kupata ushauri wa kitaalamu na kuekewa Tenki na Mamlaka ya Maji, (ZAWA). Hata hivyo, maji hayo hivi sasa hayatoki hata hapo Fukuchani, kwa sababu mashine ya kisima hicho imeharibika na takriban mwezi sasa (wakati Kamati inafanya ziara), mashine hiyo imeshachukuliwa na ZAWA.

Mashine ya mwanzo ilikuwa inasambaza maji vizuri, ila ilipobadilishwa na kupewa nyengine, ndio haikuweza kutoa huduma hiyo. Mashine hiyo ya mwanzo ilikuwa kubwa yenye uwezo mzuri, ila ZAWA walikuja kuwabadilishia na kuwaekea nyengine, ambayo haiwasadii na wala maji hayapatikani. Vile vile, walifainikiwa kupewa Tsh.370,000/- na kununua mipira na mabomba, lakini hayakutumika na hatimae yamebakia mikononi mwa baadhi ya wananchi, huku lengo la kununuliwa kwake halikufikiwa.

Maelezo ya Kamati:

Kamati imejiridhisha kwamba, fedha za Mradi zimetumika vyema, ingawaje imegundua kwamba, Mamlaka ya Maji, ZAWA, imekuwa mbali kuwasaidia wananchi wa vijiji hivyo.

Maoni ya Kamati:

Mamlaka ya Maji, ichukue hatua za haraka kuirejesha mashine yenye nguvu na itakayoweza kutoa huduma kwa ufanisi. Aidha, ishirikiane na wananchi hawa kwa kumuomba Ndg. Aman Ibrahim Makungu, mwenye kisima karibu na kisima hichi, awaruhusu wananchi hawa wakitumie kisima chake kwani yeye kwa muda mrefu sasa hakitumii kisima hicho.

Kamati pia inaitaka ZAWA kuacha kabisa mtindo wa kubadilisha mashine kubwa kwa kuweka ndogo, kwani huwa wanasababisha usumbufu kwa wananchi kukosa huduma muhimu hii ya maji. Na badala yake, ZAWA wawe na utaratibu wa kwenda kuzikagua mashine hizo kila mara, ili kuepusha uharibifu ambao unaweza kutokea kwani wananchi huwa hawajui vizuri juu ya matumizi haya ya mashine.

Hoja Namba 3.1.4 Kuhusiana na Ujenzi wa Skuli ya Pangatupu.

Mradi huu kwa mwaka 2009/2010, uliingiziwa Tsh. 4,500,000 kwa lengo la kujenga skuli ya msingi ya Pangatupu.

Maelezo ya Kamati ya Maendeleo iliyosimamia Mradi huu:

Mradhi huu ulitarajiwa kumalizika 2011,ingawa mpaka leo bado haujakamilika kutokana na wizi wa vifaa, ushiriki wa wananchi na kukosa fedha za kumalizia ama kuikabidhi skuli hiyo kwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali. Fedha zilizohusika na Mradi huu wamezipokea na kuzitumia kwa kufuata taratibu zilizopo, pamoja na kufanya marejesho ya matumizi hayo. Hatua iliyofikia sasa ni kuezekwa na kumalizia hatua zilizobakia.

Maelezo ya Kamati:

Kamati imejiridhisha kwamba, fedha hizo zimetumika kwa ujenzi wa Skuli ya Pangatupu, huku ikiamini kwamba, ni jukumu la Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, kumalizia hatua iliyobakia, ili lengo lililokusudiwa liweze kutimia. Katika hili, ni vyema Kamati iliyosimamia ujenzi huu, iwaandikie Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, kuwakabidhi jengo kwa hatua zao.

Maoni ya Kamati:

Kamati imeridhika juhudi zilizochukuliwa na Kamati ya Mendeleo, na kuwataka Viongozi wa eneo hilo, kwa kushirikiana na Serikali za Mitaa, kusimamia jengo hilo kwa ulinzi huku Kamati ikiitaka Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, iikamilishe skuli hiyo kwa haraka ili wananchi wa Pangatupu waweze kupata Skuli na kuwaepusha na usumbufu wanaoupata sasa hivi.

2.2.2 MIRADI YA TASAF:

Hoja Namba 10.1.7 Kuhusiana na Mradi wa Ufugaji wa Kuku wa Mayai, Upenja.

Mradi huu uliingiziwa Tsh. 8,300,000 kwa ajili ya kuwawezesha wananchi wenye ulemavu, kufuga kuku wa mayai, ili waweze kujinasua na umasikini.

Maelezo ya Kamati iliyohusika na Usimamizi wa Mradi:

Mradi huu uliweza kufanikiwa vizuri katika awamu ya kwanza, ambapo walijenga mabanda na kufuga bata na kuku, ila awamu ya pili mambo hayakuenda vizuri, kwani kuku hao walipokaribia kutaga, ndipo walipopata matatizo, na hatimae wajumbe wengi walianza kutoka katika Jumuiya kwa kukosa mashirikiano na ustahamilivu.

Kuhusiana na namna Mradi ulivyowanufaisha wananchi hawa, wameeleza kwamba katika kipindi cha kuimarika kwa Mradi, walikuwa wanagawana nguo, fedha katika kila kipindi cha Skukuu na hata Mjumbe yoyote aliyekuwa anapata matatizo ya maradhi, ikiwa ni pamoja kuumwa, alikuwa anasaidiwa dawa.

Aidha, kutokana na kukosa chakula cha kuwalisha kuku hao, kuandamwa kwa maradhi pamoja na kutokea kwa ghafla vifo vya kuku, walishindwa kuendesha mradi huo na hatimae hivi sasa hawana kuku hata mmoja.

Maelezo ya Kamati:

Pamoja na maelezo kwamba, wananchi hawa walikuwa wanagawana faida kwa njia ya fedha, nguo na mengineyo, Kamati imeshindwa kuthibitishiwa hilo. Aidha, Kamati imeelezwa kwamba, hivi sasa fedha zilizobakia katika hesabu ya Kikundi hiki ni Tsh.343,900 huku zikiwa mikononi mwa wazee wa wanachama hao, bila ya kuwekwa benki.

Aidha, kukosekana kwa usimamizi wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, ikiwa ni pamoja na Afisa Mifugo wa Wilaya hii, kutokuwa na uwezo wa kufika eneo hilo mara kwa mara kwa kutoa miongozo bora ya ufugaji, Mradi huu pamoja na kusaidiwa na TASAF, umeshindwa kuleta tija endelevu.

Maoni ya Kamati:

Mradi huu haukuweza kufikia lengo. Kamati imejiridhisha kwamba, Utawala wa eneo hilo, Afisi ya Mkoa, Afisi ya Wilaya na Sheha, hawakuwa wakitoa ushirikiano wa moja kwa moja kwa wananchi hawa, juu ya Mradi waliopatiwa. Na inaitaka Serikali ya Mkoa na Serikali Kuu, kutoa mashirikiano ipasavyo kwa wananchi wanaoamua kujiendeleza ili waweze kuwasaidia.

Vile vile, Maafisa Mifugo ni vyema wakaweka utaratibu wa kupita kwenye miradi hii, ili wananchi hao wakawa wanapata miongozo ya kitaalamu katika ufugaji, kwani imeonekana ni kukosa taaluma ya ufugaji ndiko kunakofanya miradi ya namna hii kufa. Kwa ujumla, Wataalamu wa mifugo, ni jukumu lao kwenda kwa wafugaji na kuwapa taaluma na sio kukaa maofisini tu.

Hoja Namba 1.1.1 Kuhusu Mradi wa Ujenzi wa Skuli ya Sekondari, Potoa.

Kwa ajili ya kujenga Skuli ya Sekondari, Potoa, mnamo mwaka 2009/2010, TASAF walitoa Tsh. 121,638,600 kwa Shehia ya Potoa, Pitanazako na Muwange.

Malezo ya Kamati za Shehia, zilizosimamia Ujenzi wa Mradi huu:

Skuli hiyo imejengwa na Shehia tatu. Shehia ya Potoa ilikabidhiwa na TASAF Tsh. 30,884,599.70; Shehia ya Pitanazako ilikabidhiwa Tsh. 30,094,500.50 na Shehia ya Muwange Tsh. 30,219,800.30 na kuzifanya fedha zote zilizotolewa na TASAF kwa Mradi huu kuwa Tsh. 91,198,900.5, na wananchi nao wamechangia nguvu kazi, huku Uongozi wa TASAF ukitumia 10% (sawa na 30% kwa miradi yote mitatu) ambazo ni kwa ajili ya Usimamizi wa Mradi. Fedha zote hizo zimetumika kwa ujenzi wa Skuli hiyo kama ilivyokusudiwa.

Maelezo ya Kamati:

Kamati imekagua matumizi ya fedha za Mradi na imejiridhisha kwamba, zimetumika, ingawa kuna baadhi ya kasoro za kibinaadamu. Aidha, wakati Kamati inafanya ziara ya jengo husika, imefahamu kwamba, vyoo vya Skuli hiyo havina ‘ceiling’ na kuelezwa kwamba, hali hiyo imetokana na mfumko wa bei. Aidha Chumba cha Mshauri Nasaha hakina viti wala meza.

Maoni ya Kamati:

Kamati inahimiza wasimamizi wa Miradi ya TASAF kuweka bajeti kwa kuzingatia uhalisia wa bidhaa zinazotakiwa kununuliwa kwa ajili ya kukamilisha ujenzi husika. Aidha, imeridhishwa kwa juhudi zilizochukuliwa kujenga Skuli hiyo.

Hoja Namba 10.1.6 Kuhusiana na Mradi wa Kiwanda cha Usagishaji Nafaka, Shehia ya Kibeni:

Mradi huu umeingiziwa Tsh. 20,894,933 kwa mwaka 2009/2010 kwa ajili ya kujenga kiwanda cha usagishaji nafaka, Shehia ya Kibeni.

Maelezo ya Kamati iliyosimamia Ujenzi.

Mradi huo ulihusisha ujenzi wa Kiwanda, na unnunuzi wa mashine 2, moja ya mpunga na nyengine ya kusagishia ngano. Fedha zilitumika kwa ujenzi wa jengo hili pia zimehusisha ujenzi wa Ofisi, Duka na sehemu ya mashine husika za kusagishia. Duka ambalo wakati Kamati inalitembelea lilikuwa linatoa huduma; lilitokana na mtaji wa awali wa Tsh. 1,000,000 kutokana na faida waliyoipata. Aidha, kikundi chao kina wanachama hai 80; wanaume 48 na wanawake 32. Na hivi sasa wana bakaa ya Tsh.2,500,000 ambazo zipo Benki.

Maelezo ya Kamati:

Pamoja na mafanikio ya Kikundi hiki, idadi ya wananchama ni kubwa sana ukilinganisha na ushauri wa Wasimamizi wa Mradi huu, ambapo walitakiwa wasizidi 20. Hata hivyo, Kamati imeridhishwa na hoja ya idadi hiyo iliyokusudia kuwasaidia wananchi wengi, kugawana faida ndogo inayopatikana, kuliko kukosa kabisa.

Maoni ya Kamati:

Kamati imeridhishwa na juhudi zilizochukuliwa na kikundi hicho na kufurahishwa na matumuzi mazuri ya feha za mradi.

Hoja Namba 10.1.2 Kuhusiana na Ujenzi wa Skuli ya Mkwajuni Kibuyuni:

Mradi huu uliingiziwa Tsh. 40,489,066 kwa ajili ya ujenzi wa skuli ya msingi, Mkwajuni Kibuyuni.

Maelezo ya Kamati iliyosimamia Ujenzi wa Skuli hii.

Mradi huu ulihusisha madarasa manne na Ofisi ya Mwalimu Mkuu. Ulitumia Tsh.30,366,800.10 kutoka TASAF na 6,748,777 kutokana na nguvu za wananchi na ukifanya makisio ya 10% ya Uendeshaji wa Mradi husika, ni wazi kwamba, umegharimu Tshu. 40,489,066.

Maelezo ya Kamati:

Kamati imepitia hesabu za Mradi huu na kujiridhisha kwamba zimetumika ipasavyo.

Maoni ya Kamati:

Kamati imeridhika na usimamizi wa mradi huu. Lengo la Mradi huu limefikiwa.

Hoja Namba 10.1.4 Kuhusiana na Mradi wa Usambazaji maji safi na salama, Chaani Kubwa.

Kwa mwaka 2009/2010, Mradi huu uliingiziwa Tsh. 35,181,818 kwa ajili ya kupatikana maji safi na salama kwa wananchi wa Chaani, Kubwa

Maelezo ya Kamati iliyosimamia Mradi :

Fedha waliyopatiwa ilitumika katika ununuzi wa mabomba na viuongo vyake, huku Mamlaka ya Maji (ZAWA) walidhamini na kusimamia uchimbaji wa kisima husika. Hapo mwanzo walichimba kisima cha awali, ila kilifeli kutokana na ushauri wa kitaalamu kutoka ZAWA, na kushauriwa wachimbe chengine. Aidha, kisima hichi cha pili, ilielezwa Kamati kwamba, hakitoi huduma ya maji kwa kukosa mashine. Kisima hicho kilifanya kazi kwa miezi miwili tu, ingawaje maji hayo hayakuwa yakiwafikia wananchi wote wa Chaani Kubwa.

Wao, pamoja na kukosa utaalamu, wanaamini tatizo hilo limesababishwa na udogo wa 'pump' zilizotiwa wakati bomba ni kubwa, ingawaje wataalamu wa ZAWA wanaamini tatizo kubwa lipo katika mashine, na kama ingelipataikana mashine kubwa, maji hayo yatapatikana kama ilivyokusudiwa.

Maelezo ya Kamati :

Hapa kuna tatizo la kitaalamu, ingawaje kwa wananchi, matunda ya kupata maji safi ndio wanachokitaka. Hivyo, ni jukumu la ZAWA kusimamia upatikanaji wa maji hayo. Kamati inafahamu kwamba, ushauri wa kitaalamu unaotolewa na wataalamu wa ZAWA, mara nyingi hautolewi kwa uwazi na kuwafahamisha wananchi kwa lugha rahisi ya upeo wao.

Maoni ya Kamati :

Kamati inaitaka Serikali kwa kushirikiana na Mamlaka ya Maji (ZAWA) kuhakikisha maji safi na salama kwa wananchi wa Chaani Kubwa yanapatikana ndani ya miezi mitatu tokea kuwasilishwa kwa ripoti hii.

Hoja Namba 10.1.5 Kuhusiana na Ukarabati wa nyumba ya Daktari katika Shehia ya Donge Vijibweni.

Kwa mwaka 2009/2010, Mradi huu uliingiziwa Tsh. 23,774,467 kwa ajili ya kukarabati nyumba ya daktari wa hospitali ya Donge Vijibweni. Hali hii itasadia kutoa huduma kwa ufanisi na kwa karibu zaidi kwa wananchi wa eneo hilo.

Maelezo ya Kamati ya Maendeleo iliyosimamia Mradi huo :

Mradi huo ulihusisha ukarabati wa nyumba ya daktari pamoja na hospitali yenyewe. Pamoja na hoja hii kuelekezwa katika suala zima la ukarabati, Kamati ya Maendeleo imeona haja pia ipo kwa kuikarabati hospitali, kufuatia kufikia hatua ya kuridhisha ya kukarabati nyumba hiyo ya daktari. Kamati iliwasilisha namna fedha walivyotumia kwa Kamati ya P.A.C, huku wakisisitiza kwamba matumizi ya fedha hiyo yalikuwa sahihi.

Maelezo ya Kamati:

Kamati imepokea taarifa hiyo, na kuridhika juu ya matumizi yaliyofanywa, ingawa mwanzo ilikuwa na shaka juu ya ukarabati wa hospitali wakati haikuhusika na mradi. Aidha, kwa kuzingatia kwamba, hata ukarabati wa nyumba ya daktrari haukukamilika ipasavyo, suala la

sababu zilizopelekea kukarabatiwa hospitali halikuwa la msingi. Hata hivyo, baada ya kupata ufafanuzi kwamba, ukarabati huo umetokana na kutaka huduma hiyo kwa wananchi iweze kutolewa, hata kwa uwezo mdogo uliopo, Kamati haikuwa na shaka tena.

Maoni ya Kamati :

Kamati imeridhika na hatua zilizochukuliwa na kuridhika matumizi ya fedha yalivyosimamiwa.

Hoja Namba 10.1.3 Kuhusiana na Ujenzi wa Afisi na Madarasa ya Skuli ya msingi, Kinduni :

Kwa mwaka 2009/2010, Mradi huu uliingiziwa Tsh.35,181,818 kwa lengo la ujenzi wa Skuli ya Kinduni.

Maelezo ya Kamati ya Maendeleo iliyosimamia Ujenzi wa Skuli hii :

Mradi huo ulihusisha ujenzi wa madarasa matatu na Afisi ya Walimu, ulimalizika katika muda uliokusudiwa. Aidha, kuhusiana na ujenzi wa vyoo, Kamati hii imesimamia ujenzi wake, ingawa baada ya kuongezeka kwa wanafunzi, vyoo hivyo vimekuwa kidogo. Ilielezwa kwamba, hesabu halisi ya ujenzi huo hapo awali ilikuwa ni mabanda manne ya kusomea, lakini baada ya kufahamu kwamba, hakuna vyoo, ndipo hesabu ya banda moja, likahaulishiwa katika ujenzi wa vyoo.

Maelezo ya Kamati :

Pamoja na ujenzi wa vyoo katika Skuli hiyo, wakati Kamati inafanya ukaguzi imejiridhisha kwamba, vyoo hivyo havina milango, ispokuwa mlango wa kuingilia. Kwa maana, hata wanafunzi wanapoenda haja, ni lazima wataonana, kitu ambacho kiko kinyume na maadili. Hata hivyo, Kamati imeelezwa kwamba, suala hili lilisababishwa na uchache wa fedha kwa mnasaba wa bajeti waliyoiombea, baada ya vifaa kupanda bei wakati wa ujenzi.

Aidha, jambo la kushangaza ni kwamba, wakati Kamati inafanya ukaguzi, ilishuhudia ukarabati wa majengo hayo unaendelea, huku hata miaka miwili haijatimia baada ya kukamilika kwa ujenzi, hali hii inaleta shaka kwamba, ujenzi hapa haukusimamiwa ipasavyo.

Maoni ya Kamati :

Kamati inaitaka Serikali kusimamia ipasavyo miradi ya wananchi, ili lengo lililokusudiwa liweze kutimia.

2.3.0 MKOA WA MJINI MAGHARIBI :

2.3.1 MIRADI YA MAENDELEO YA WANANCHI:

Hoja Namba 4.1.3 Kuhusiana na Ujenzi wa Chumba cha Kompyuta, Skuli ya Bububu.

Kwa mwaka 2009/2010, Mradi huu uliingiziwa Tsh. 4,500,000 kwa ajili ya ujenzi wa chumba cha kompyuta na Afisi ya walimu, katika Skuli ya Bububu.

Maelelezo ya Kamati iliyohusika na Ujenzi:

Ni kweli fedha hizo Tsh. 4,500,000 walipatiwa na Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kwa ajili ya ujenzi na wamezitumia kama ilivyokusudiwa. Hata hivyo, bado hawajakamilisha Ujenzi, kwani bado chumba hicho cha kompyuta hakijaezekwa. Walieleza pia kwamba walifanya juhudi nyingi kukamilisha ujenzi huo ikiwa ni pamoja na kupeleka barua Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, kuomba msaada kwa mashirika mbali mbali ya Kimataifa, lakini bado hawajafanikiwa.

Maelezo ya Kamati:

Katika kuzipitia hesabu za awali, Kamati imegundua kwamba, fedha hizo pia zilitumiwa kwa matumizi mengine yasiyohusika, ikiwa ni pamoja na maunuzi ya chaki na matumizi mengine madogo madogo ya mahitaji ya Skuli. Aidha, suala hili lilielezwa kusababishwa na kutojiandaa kwa Katibu wa Kamati ya Maendeleo. Aidha, Kamati ilipotumia busara ya kumtaka awasilishe hesabu hizo kwa siku ya pili zikiwa ziko sahihi, Katibu huyo aliwasilisha hesabu hizo na Kamati ikagundua kwamba, matumizi yote ni Tsh. 4,586,250, tofauti na fedha ziliozoelezwa kutumika.

Maoni ya Kamati:

Kamati imewataka Makatibu wa Kamati za Maendeleo ambao wakati huo huo ni Walimu Wakuu wa Skuli zinazohusika na Miradi, kuwa makini na matumizi ya fedha za Miradi zinazotolewa na Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo.

Kamati vile vile, inaitaka Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, kuhakikisha wanakamilisha hatua za uwezekaji na hatua za mwisho za ujenzi wa Ofisi hiyo, ili lengo lililokusudiwa liweze kupatikana.

Hoja Namba 4.1.1 Kuhusiana na Ujenzi wa Barabara ya Magomeni.

Mradi huu kwa mwaka 2009/2010 uliingiziwa Tsh. 8,000,000, kwa lengo la ujenzi wa barabara za ndani, kwa hatua ya kuweka kifusi.

Maelezo ya Kamati ya Maendeleo iliyohusika na Usimamizi wa Mradi huu.

Kamati imepokea fedha kupitia Mfuko wa Jimbo kwa hundi ya tarehe 27/5/2010, ambapo baada ya makubaliano ya Wajumbe wa Kamati, waliwalipa TK Builders Engineers Tsh.6,940,000, Kampuni ya Ujenzi iliyokubali kutengeneza Barabara hiyo kwa hatua iliyokusudiwa. Hata hivyo, Mkandarasi huyo hakujenga kama ilivyokusudiwa, kwani ameweka fusi tu bila ya kulitengeneza

kwa kiwango kilichotakiwa na Kamati hii ya Maendeleo walilazimika kufungua kesi Mahakamani, ili kupata haki zao. Fedha zilizobakia, Tsh. 1,060,000 ndizo walizotumia kwa kuwalipa Mawakili na kufuatilia hatua nyengine za kesi hiyo.

Maelezo ya Kamati:

Kamati haikuridhishwa na hatua za Kamati ya Maendeleo, ya Kumtafuta Mkandarasi binafsi, wakati kazi hiyo ingeliweza kufanywa na Idara ya Ujenzi na Utunzaji wa Barabara (UUB). Kamati pia haikuridhishwa na mashikiano yanayotolewa na Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, kwa kutosimamia ipasavyo fedha za miradi hiyo, huku jukumu lote la matumizi likiachwa kwa wananchi ambao hawana uzoefu wala ujuzi wa matumizi ya fedha za Serikali.

Maoni ya Kamati:

Mradi huu haukufikia lengo, na fedha zilizotolewa zimetumika kinyume na malengo yaliyokusudiwa. Kamati inaitaka Serikali kuwa makini na kusimamia ipasavyo fedha zinazotolewa kwa wananchi.

Hoja Namba 4.1.4 Kuhusiana na Ujenzi wa Skuli ya Maandalizi, Welezo:

Mradi huu uliingiziwa Tsh. 4,500,000 kwa lengo la kujenga madarasa matatu ya Skuli ya Maandalizi ya Welezo.

Maelezo ya Kamati iliyohusika na Usimamizi wa Ujenzi:

Ni kweli fedha hizo wameingiziwa na kuzitumia kwa kujenga madarasa hayo, kuanzia hatua ya awali mpaka hatua ya uezekaji iliyomaliziwa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali. Kamati iliwasilisha mbele ya Kamati, matumizi halisi ya fedha hizo kama Kamati ilivyohitaji.

Maelezo ya Kamati:

Kamati imepokea uchanganuzi wa matumizi ya fedha hizo, na kujiridhisha kwamba hatua ya Skuli hii imekamilika na tayari imeanza kutumiwa.

Maoni ya Kamati:

Kamati imeipongeza Kamati ya Maendeleo iliyosimamia Ujenzi huu, tokea kuwa na wazo la ujenzi na kusimamia ipasavyo matumizi ya fedha ilizopewa. Kamati imeridhika na matumizi ya fedha zilizotengwa na imefurahishwa kwa kufikiwa kwa lengo lililokusudiwa.

Hoja Namba 4.1.2 Kuhusiana na Ujenzi wa Vyoo, Skuli ya Magogoni.

Mradi huu wa ujenzi wa vyoo katika Skuli ya Msingi ya Magogoni, umeingiziwa Tsh. 3,000,000 kwa mwaka wa fedha 2009/2010, ili vyoo hivyo viweze kutumiwa na wanafunzi wanaosoma Skulini hapo.

Maelezo ya Kamati ya Maendeleo iliyosimamia Mradi.

Mradi huo umekamilika. Jumla ya fedha zilizotumika ni hizo 3,000,000/- huku Tsh.2,000,000 zikitumika kwa ujenzi wa vyoo na Tsh.1,000,000 zimetumika kwa ujenzi wa banda la Skuli. Ujenzi wa vyoo ndio uliokusudiwa, lakini kutokana na kukamilika kwa kutumia Tsh.2,000,000, Kamati ya Maendeleo ikakubaliana kuziingiza katika ujenzi wa banda la skuli, ili ujenzi wake utakapokamilika, utaweza kuwasaidia wanafunzi wengi waliokuwa wanasoma katika skuli hiyo.

Maelezo ya Kamati :

Pamoja na kwamba Kamati ya Maendeleo ilisema imesimia ujenzi wa vyoo hadi kukamilika, wakati Kamati ilipofanya ziara ilishuhudia kwamba, vyoo hivyo bado havijakamilika. Yaani kuna mlango mmoja tu wa kuingilia katika vyoo vilivyogaiwa sehemu 6, wanaume na wanawake. Kitendo cha vyoo hivyo kutokuwa na milango ya ndani, hakijaifurahisha Kamati, kwa sababu fedha za kutia milango hiyo zilikuwepo.

Aidha, wakati wa ziara, Kamati ilishuhudia Diwani wa Magogoni, akithibitisha kwamba ujenzi huo ameufanya yeye na wala sio wananchi. Fedha za Serikali, Tsh. 2,000,000 zimetumika kwa ujenzi wa matofali hadi kozi ya nne na kuchimba shimo la choo, lakini Diwani huyu ndie aliekamilisha kazi yote hadi vyoo vikawa vinaweza kutoa huduma iliyokusudiwa. Aidha, kitendo cha fedha Tsh.1,000,000 kutumiwa kwa ujenzi wa banda la skuli, kimeshindwa kuthibitishwa kwa sababu jengo hilo lilikuwa limeshaezekwa chini ya msaada wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali. Kwa maana hiyo, Kamati imepata shaka juu ya usahihi wa fedha hizo zilivyotumika.

Maoni ya Kamati :

Kamati inaitaka Serikali kuwachukulia hatua watendaji wote wa Kamati ya Maendeleo iliyohusika na ujenzi huu, kwa kutotekeleza mradi kama ulivyokusudiwa, lakini kuwepo kwa dalili zote za matumizi mabaya ya fedha za Serikali, pamoja na kuchukuliwa kwa hatua hizo kwa Maofisa wa Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, ambao walihusika na usimamizi wa Mradi huu..

2.3.2 MIRADI YA TASAF:

Hoja Namba 8.1.1 Kuhusiana na Ujenzi wa Skuli ya Maandalizi, Mkele:

Mradi huu katika miaka miwili, 2008/2009 na 2009/2010 uliingiziwa Tsh.35,181,818 kwa lengo la kujenga skuli ya maandalizi, Mkele. Mradi huu umeweza kufikia lengo, ingawa kwa upande wa vikalio, lengo halijafikiwa kwa sababu vikalio pekee vilivyopatikana ni 8 badala ya 30.

Maelezo ya Kamati iliyosimamia Ujenzi:

Mradi huo unatokana na ufadhili wa TASAF pamoja na nguvu za wananchi wenyewe. Katika utekelezaji wa mradi huu, kuna mambo yameathiriwa na utaratibu ambao hapo kabla haukutazamiwa. Kwa mfano, katika malipo ya fundi, katika bajeti walipanga kumlipa Tsh. 5000 lakini katika uhalisia walilazimika kumlipa Tsh.10,000. Halikadhalika Msaidizi wake walipanga kumlipa Tsh.2500 lakini walilazimika kumlipa Tsh.5000. Hali hii kwa ujumla wake ndiyo iliyoleta mabadiliko ya bajeti na hatimae kushindwa kununua vikalio katika idadi iliyopangwa.

Maelezo ya Kamati:

Kamati haikuridhishwa na utaratibu uliotumika katika ujenzi wa Skuli kukosa vikalio, pamoja na ukweli kwamba, gharama za ujenzi huo zilipanda kinyume na mipangilio yao kabla. Hata hivyo, Kamati inaliona tatizo hili pia linatokana na Uongozi wa TASAF katika kusimamia miradi hii tokea uandaaji wa bajeti za miradi husika hadi wakati wa kutekelezwa.

Aidha, Kamati imefahamishwa kwamba, pamoja na kwamba skuli hii imeshakamilika, lakini bado haijakabidhiwa kwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, tofauti na Miradi mingi ya aina hii.

Maoni ya Kamati:

Kamati inaitaka Serikali kuisimamia ipasavyo miradi ya wananchi ili malengo yaliyokusudiwa yaweze kupatikana.

Hoja Namba 8.1.4 Kuhusiana na Ukarabati wa Skuli ya Sekondari ya Bububu.

Mradi huu umeingiziwa Tsh. 37,372,805/ kwa lengo la ujenzi wa Madarasa matatu ya Skuli ya Bububu Sekondari.

Maelezo ya Kamati ya Maendeleo, iliyohusika na Ujenzi wa Skuli hii:

Mradi huo ni wa ujenzi wa madarasa matatu, ulikusudiwa kuongeza wingi wa madarasa ya Skuli ya Sekondari ya Bububu, kwa lengo la kupunguza uchache wa madarasa unaotokana na kuongezeka kwa wanafunzi. Ujenzi ulihusisha fedha hizo Tsh. 37,372,805; kwa kuzingatia fedha zilizotoka TASAF Tsh. 27,231,386.36; Mchango wa Wanachi Tsh. 7,145,696.14 na 10% ya Uongozi wa TASAF uliohusika na usimamizi wa Mradi huu. Kwa lengo la kufahamika kwa ufasaha matumizi ya fedha hizo, Kamati hii iliwasilisha taarifa yake, mbele ya Kamati ya P.A.C.

Maelezo ya Kamati:

Pamoja na kuwasilishiwa kwa taarifa hiyo, Kamati imeikataa taarifa iliyowailisilishwa na Kamati ya Maendeleo ya Ujenzi, kwa kutozingatia ama kutowiyana na uhalisia. kwa Mfano, ilielezwa katika taarifa ya Kamati, kwamba, fedha za Ujenzi wa Ubao (mbao tatu za saruji za ukutani, kwa kila darasa) ziligharimu Tsh 1,199,400, Usafishaji wa kiwanja kwa ajili ya ujenzi, iligharimu Tsh. 1,407,500 na matumizi mengineyo, ambapo kwa ujumla hazingii akilini.

Maoni ya Kamati:

Kamati haikufurahishwa na mtumizi ya fedha kwa Mradi huu, na kwa kutumia kifungu cha 52(5)(b) cha Kanuni za Fedha za mwaka 2005, suala hili linahitaji uchanganuzi zaidi, ili kufikia maamuzi yanayofaa.

Hoja Namba 8.1.2 Kuhusiana na Ujenzi wa Skuli ya Sekondari ya Jang'ombe.

Kwa Mwaka 2009/2010, Mradi huu uliingiziwa Tsh. 35,1818,818 kwa lengo la ukarabati wa Skuli ya Jang'ombe.

Maelezo ya Kamati ya Maendeleo iliyosimamia Ujenzi husika:

Mradi huu umehusika na Jengo la Mitihani katika Skuli ya Kidongo Chekundu, tofauti na ilivyoripotiwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu, Zanzibar. Kamati yao iliyopo Shehia ya Jang'ombe, ndio iliyosimamia ujenzi huo kwa kupewa Tsh. 27,272,727.27 na TASAF, nao wananchi wakachangia nguvu kazi kwa thamani ya Tsh. 5,181,818 huku 10% ikitumiwa na Uongozi wa TASAF uliohusika na usimamizi wa Mradi huo.

Maelezo ya Kamati:

Pamoja na juhudi zilizochukuliwa na Kamati ya Maendeleo, Kamati ya P.A.C, haikuridhishwa na matumizi ya fedha kinyume na uzito wa kazi iliyofanywa. Kwa mfano, wakati Kamati inafanya ukaguzi wa matumizi ya fedha, imegundua kwamba, takriban fedha zote zimetumiwa kwa kununulia vifaa vya ujenzi kutoka kwa Mfanyabiashara mmoja. Aidha, matumizi ya fedha kwa mfano ujenzi wa msingi, ujenzi wa jengo lenyewe, utiaji dari (ceiling) na matumizi mengineyo, hayana uhalisia na fedha zilizotumika.

Maoni ya Kamati:

Kamati inautaka Uongozi wa TASAF kusimamia ipasavyo matumizi ya fedha wanazozitoa, ili ziwe halisi na ujenzi unaofanywa. Aidha, kwa kuwa Uongozi wa TASAF ndio wasimamizi wakuu wa Miradi hii, ni lazima wahakikishe wanasimamia ipasavyo matumizi ya fedha za Serikali, na isiwe wanalichukulia kwa wepesi suala hili. Hivyo basi, pamoja na ujenzi kufanyika, Kamati imejiridhisha kwamba, fedha za Serikali hazikutumiwa ipasavyo. Na Kamati inaitaka Serikali kuwachukulia hatua za kisheria Wajumbe wote wa Kamati ya Maendeleo ya Shehia, iliyohusika na usimamizi wa ujenzi huo.

Hoja Namba 8.1.3 Kuhusiana na Ujenzi wa Chumba cha Kompyuta na Ukarabati wa Skuli ya Sekondari ya Kidongo Chekundu.

Miradi hii miwili imeingiziwa Tsh. 70,363,636 kwa mwaka wa 2009/2010 ili lengo la kuikarabati Skuli ya Sekondari ya Kidongo Chekundu na kujenga chumba cha kompyuta kwa matumizi ya Skuli hiyo, liweze kufikiwa.

Maelezo ya Kamati zilizosimamia Ujenzi huo:

Kwa upande wa Shehia ya Kidongo Chekundu, iliingiziwa Tsh. 27,272,727.27 kutoka TASAF, huku na wananchi wakichangia Tsh.2,812,636 na 10% zikiwa ni gharama za usimamizi wa Mradi kwa upande wa TASAF. Fedha hizo zimetumika kwa kukarabati vyoo, kutia madirisha, kupiga plasta, kununua samani na kukarabati paa na shughuli nyengine zilizohusika.

Aidha, ujenzi wa chumba cha kompyuta ulisimamiwa kwa kununua kompyuta 5,kutia umeme, kujenga dari, sakafu, kupiga plasta na shughuli nyengine zilizohusika, zilizopelekea kutumika kwa Tsh.37,551,000 zikiwa ni pamoja na fedha za TASAF Tsh.27,772,727.27; Tsh.7,551,000 mchango wa wananchi na 10% ya usimamizi wa Mradi.

Maelezo ya Kamati:

Kamati imepokea taarifa ya matumizi ya fedha zote hizo na kuridhishwa na uhalisia. Hata hivyo, haikufurahishwa na hali ya vyoo ambavyo kwa upande wa wanaume tayari milango yote takriban imeshaibiwa, huku bado vyoo vikibakia katika hali ya uchafu.

Maoni ya Kamati:

Kamati imewashauri Sheha wa Shehia ya Kidongo Chekundu pamoja na Shehia ya Jang'ombe, washirikiane na Mwalimu Mkuu wa Skuli hiyo kwa ajili ya kusimamia ulinzi wa mali za Skuli. Aidha, Kamati inapongeza hatua ya ujenzi ilivyofikiwa.

Hoja Namba 8.1.5 Kuhusiana na Ujenzi wa Skuli ya Msingi, Mtoni Kidatu.

Mradi huu umeingiziwa Tsh. 35,181,818 kwa ajili ya kujenga madarasa manne na Ofisi katika Skuli ya Msingi, Mtoni Kidatu. Fedha hizo zimeingizwa kwa mwaka 2009/2010.

Maelezo ya Kamati iliyohusika na Usimamizi wa Mradi huu:

Ni kweli waliingiziwa fedha na TASAF pamoja na wao kutumia nguvu zao na hatimae waliweza kujenga tokea hatua ya awali hadi ya kuezekwa. Walitafuta mafundi watatu ambapo kila mmoja anatoka katika zoni zilizochini ya Shehia yao, na kuufanya ujenzi huo kupata mashirikiano mazuri.

Maelezo ya Kamati:

Kamati imepokea taarifa ya matumizi ya fedha zilizohusika na taarifa ya Kamati ya Maendeleo kuhusiana na ujenzi huu. Hata hivyo, imegundua kwamba, baadhi ya risiti zilizotumika hazina Namba ya Usajili wa ZRB, huku ununuzi wa vifaa ukifanywa kwa wafanyabiashara hao hao. Jambo ambalo huwa linatia shaka. Hivyo, ni vyema kukawa na utaratibu mzuri wa kutafuta wauzaji mbali mbali, ili kuweza kupata ushindani.

Maoni ya Kamati:

Kamati imeridhishwa na juhudi zilizochukuliwa na kuutaka Uongozi wa TASAF wahakikishe kwamba wanawasimamia wananchi ipasavyo, ili matumizi ya fedha yaendane na sheria zilizowekwa.

2.4.0 MKOA WA KUSINI UNGUJA:

2.4.1 MIRADI YA MAENDELEO YA WANANCHI:

Hoja Namba 2.1.1 Kuhusiana na Ukarabati wa Kituo cha Afya, Unguja Ukuu.

Mradi huu kwa mwaka 2009/2010 uliingiziwa Tsh.4,500,000 kwa ajili ya kufanyiwa ukarabati Kituo cha Afya, Unguja Ukuu, ili wananchi wa kijiji hicho waweze kupata huduma hiyo kwa ufanisi zaidi. Mbali na hilo, tatizo kubwa linalowakabili wananchi hao, ni kukosekana kwa nyumba ya daktari na hivyo, utoaji wa huduma kwa kijiji hicho kukwazwa na tatizo hilo.

Maelezo ya Kamati ya Maendeleo iliyosimamia Mradi huu.

Jumla ya Tsh. 4,800,000 zilitumika kwa kufanya ukarabati wa kituo cha Afya, ambazo zilitolewa na Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, ukarabati uliohusisha utiaji rangi, utiaji wa ceiling na matengenezo mengine.

Kuhusiana na vyoo, Kamati haikuweza kuvishughulikia kutokana na kutokuwa na fedha na hivyo, vimebaki katika hali mbaya kama ilivyo awali.

Maelezo ya Kamati:

Pamoja na kufanyiwa ukarabati, Kituo hicho kina matatizo kadhaa, ikiwa ni pamoja na dari (ceiling) yake katika chumba cha mama wajawazito tayari imeshaanza kuporomoka, hili limeelezwa kusababishwa na mtikisiko wa mabomu unaofanyika katika maeneo hayo, unaosababishwa na mazoezi ya Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ). Katika hili, Kamati imefahamu kwamba, hiyo sio hoja ya msingi, kwani hata ceiling yenyewe inaonekana haipo katika hali ya uimara. Aidha, kama ndio sababu, kwa nini Wahusika wasitoe ripoti wa Uongozi wa jeshi, ili kuangalia utaratibu wa kulipwa fidia.

Aidha, Kamati inaupongeza Uongozi wa Wilaya ya Kati, kwa uwajibikaji wao wa haraka, kwani mara tu Kamati ilipoona ipo haja ya taarifa za Kituo hicho kuwafikia walalamikiwa (JWTZ), Afisi ya Wilaya iliwarifu wahusika nao kufanya utafiti na ndipo Mkuu wa Wilaya ya Kati alipoijibu Kamati kwa barua ya tarehe 11/10/2012, yenye kumbu kumbu namba WKT/U/A.10/1/198 VOL.VIII kwamba hakuna ukweli wa madai ya athari za mazoezi ya ambomu kwa Kituo hicho na kilichogundulikana ni sehemu kubwa ya dari ya kituo hicho imeathiriwa na wadudu waharibifu (Mchwa) na kuta za jengo la kituo hicho hazina nyufa wala mipasuko itokanayo na athari za ulipuaji wa mabomu.

Maoni ya Kamati:

Wizara ya Afya ichukue hatua za haraka kuvitengeneza vyoo vilivyo katika eneo la Kituo cha Afya cha Unguja Ukuu, ili kiweze kuwasaidia wananchi na madaktari wanaotoa huduma katika kituo hicho, lakini kutofanya hivyo sio tu kurudisha nyuma hatua za usafi, lakini kinaweza kuwa sababu ya kusambaa kwa maradhi ya mripuko.

Hoja Namba 2.1.3 Kuhusiana na Ujenzi wa Barabara na Soko, Makunduchi.

Mradi huu wa kujenga soko katika eneo la Koba na Tangini Makunduchi pamoja na Ujenzi wa barabara za ndani, uligharimu Tsh.8,000,000, huku kila mradi ukiingiziwa Tsh.4,000,000.

Maelezo ya Kamati iliyosimamia Ujenzi huo:

Ujenzi wa Soko pamoja na barabara ulisimamiwa na Kamati ya Maendeleo ya Jimbo, Makundichi. Miradi yote hiyo ilipata misaada kutoka kwa wahisani mbali mbali, ikiwa ni pamoja na Viongozi wa Jimbo. Aidha, matumizi ya Soko wakati Kamati inafanya ukaguzi, yamefikia Tsh.20,197,375, huku Kamati hiyo bila ya kujali fedha hizo zimetoka katika chanzo kipi, huzitumia fedha hizo baada ya kuzipokea kupitia Akaunti yao.

Kuhusiana na elimu yoyote ya fedha juu ya matumizi ya miradi hiyo, wameeleza kwamba, wanakamati hawa hawakupata mafunzo kutoka popote pale, ila hutumia ujuzi wao wa kuendesha shughuli za matumizi ya fedha husika.

Kwa upande wa Ujenzi wa barabara, gharama zote zinakisiwa Tsh.71,380,000, huku Kamati ikihoji Tsh.4,000,000 kutoka Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo.

Maelezo ya Kamati:

Pamoja na matumizi yafikiayo Tsh.20,197,375 ya ujenzi wa soko, bado ujenzi haujakamilika na ni sawa na kusema kwamba, lengo lililokusudiwa bado halijafikiwa. Wakati Kamati ilipohitaji mapitio ya fedha za matumizi, ilijiridhisha kwamba, kuna shaka kubwa juu ya usahihi wa matumizi yake.

Kwa upande wa Ujenzi wa barabara, Kamati imeshindwa kupata vielelezo vilivyohusika ikiwa ni pamoja na kuelezwa kwamba, Kamati hii ya Maendeleo haikupatiwa vielelezo hivyo kutoka Idara ya Ujenzi na Utunzaji wa Barabara (UUB) haikutoa vielelezo vilivyotakiwa. Kwa mfano, Kamati imepata maelezo ya Tsh.2,870,000 zilizotumika kwa mafuta na chakula, zikiambatana na vielelezo ambavyo Kamati imejiridhisha kwamba vina kasoro kadhaa ikiwa ni pamoja na kuwa ni vya udanganyifu.

Aidha, matumizi ya Tsh.1,130,000 yameshindwa kuthibitishwa mbele ya Kamati. Vile vile katika mambo ya kuonesha kasoro ya Kamati ya Maendeleo, mahudhurio yao ni dhaifu sana mbele ya Kamati, hali inayoonesha kukosa mashirikiano na umoja baina yao. Kwa mfano, kati ya wanachama 20 wa Kamati hiyo, ni watu watatu pekee ndio waliohudhuria huku wakiitwa

mara kadhaa na Afisa Tawala bila ya kujali.

Maoni ya Kamati:

Kamati haikuridhishwa na matumizi ya fedha za maendeleo ya wananchi kwa miradi yote miwili na kuitaka Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kuwa makini na usimamizi wa fedha za wananchi. Kamati pia inautaka Uongozi wa UUB, kuwa waadilifu katika kutoa risiti na marejesho ya huduma wanayoitoa kwa wananchi. Kwa ujumla, Kamati inaiagiza Serikali kuwachukulia hatua za kinidhamu watendaji wa UUB waliohusika na kutoa huduma ya kifusi, Makunduchi kupitia Mradi huu, huku wasitekeleze majukumu yao ipasavyo, lakini pia kushidwa kutoa risiti halali, ambapo kutofanya hivyo, maana yake fedha hizo zimeibwa.

Hoja Namba 2.1.2 Kuhusiana na Uchimbaji wa Kisima, Ndijani (Cheju).

Kwa mwaka 2009/2010, Mradi huu ulioingiziwa Tsh. 4,500,000 kwa lengo la kusaidia kilimo cha umwagiliaji maji katika bonde la mpunga, huko Cheju.

Maelezo ya Kamati ya Maendeleo iliyosimamia Mradi:

Tokea wachimbe kisima hicho, hawajapata matatizo yoyote ispokuwa tatizo liliopo ni udogo wa pump, kiasi ya kushindwa kusukuma maji kwa ufanisi. Aidha, baada ya kufungiwa mita ya TUKUZA, sasa wanalazimika kutumia maji kwa zamu miongoni mwa wakulima, wakati kabla ya kufungwa kwa mita hii, walikuwa wanasaidiwa na Serikali kulipia maji huku wakulima hao wakilipia takriban 4,000 kwa kila mwisho wa mavuno.

Maelezo ya Kamati:

Pamoja na kuelezwa kwamba mradi huu unatokana na fedha za Maendeleo, Kamati imeelezwa kwamba, mradi huu ni wa PADEP na wala hauhusiani moja kwa moja na Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo.

Maoni ya Kamati:

Kamati imekubali kwamba, mradi huu unahusiana na PADEP kwa barua ya tarehe 17/12/2012. Hivyo, mradi huu sio wa Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo.

2.4.2 MIRADI YA TASAF:

Hoja Namba 9.1.2 Kuhusiana na Ujenzi wa Nyumba ya Mwalimu,Kitogani:

Mradi huu umeingiziwa Tsh. 35,181,818 kwa ajili ya kujenga nyumba ya walimu Kitogani, walimu hao waweze kuwa karibu na wanafunzi na kuwasaidia wakati wowote.

Maelezo ya Kamati ya Maendeleo iliyohusika na Ujenzi huo:

Nyumba hiyo imejengwa kwa ajili ya kupunguza usumbufu waliokuwa wanaupata walimu wa

sayansi wa Skuli ya Kitogani, waliokuwa wanatoka masafa marefu. Hata hivyo, haja yao ni kupata nyumba mbili za kukaa walimu wanne wa sayansi, na ni sawa na kusema kwamba nyumba hii moja yenye sehemu mbili, inasaidia kupunguza tu tatizo liliopo.

Nyumba hiyo inakaliwa na walimu wawili, mmoja wa primary na mwengine wa sekondari, jambo lililotokana na makubaliano ya wananchi wa eneo hilo, ingawaje kabla ya kugaiwa sehemu mbili, ujenzi wa skuli hiyo ulikusudiwa kwa Skuli ya Kitogani pekee. Sababu iliyoelezwa ni kutokana na nyumba aliyokuwa anakaa mwalimu huo wa primary kuwa mbovu na hivyo imelazimika ahamie katika nyumba hiyo mpya inayohusika na hoja hii.

Maelezo ya Kamati:

Wakati Kamati inafanya ukaguzi katika nyumba hiyo, tayari ilikuwa imeshahamiwa na hivyo, ile hoja kwamba nyumba hiyo haijahamiwa, haipo tena. Kamati haikufurahishwa na kuachwa kwa nyumba ya Wizara chihi ya Skuli ya Kitogani Msingi katika hali ya uchakavu unaopelekea kuanguka kwa nyumba hiyo. Aidha, wakati Kamati inafanya ukaguzi wa matumizi ya fedha zilizohusika na ujenzi huo, tayari fedha hizo zilikuwa zimeshakaguliwa na vielelezo vinaonesha usahihi wa matumizi yake.

Maoni ya Kamati:

Kamati imeridhishwa na hatua ya kuhamiwa kwa nyumba hiyo, huku ikiitaka Wizara ya Elimu na Mfunzo ya Amali kuifanyia matengenezo ya haraka nyumba mbovu iliyokuwa kabla inatumiwa na Mwalimu wa Skuli ya Kitogani Msingi. Ili iweze kusaidia kutoa huduma kwa walimu wa Kitogani, kwani hadi hivi sasa bado tatizo la makazi kwa walimu hawa ni tatizo.

Hoja Namba 9.1.3 Kuhusiana na Ujenzi wa Tangi la Maji, Kizimkazi:

Kwa mwaka 2009/2010, Mradi huu uliingiziwa Tsh. 84,343,296 kwa kujenga Tangi la Maji, ili wananchi wa maeneo ya karibu katika Kijiji cha Kizimkazi, waweze kupata huduma ya maji safi na salama.

Maelezo ya Kamati zilizohusika na Ujenzi huu:

Mradi huu ulisimamiwa na Shehia mbili kwa lengo la kununua matangi kutokana na fedha walizozipata TASAF huku sehemu iliyobakia ilisaidiwa na Mradi wa Mamlaka ya Maji, ZAWA kwa kutoa zaidi ya Tsh.350 milioni, na fedha zilizobakia zikachangiwa na Serikali. Mradi huo uliofunguliwa mwaka 2011, ulilengwa zaidi kutoa huduma ya maji kwa vijiji vya Kizimkazi, ingawaje Shehia ya Kizimkazi Mkunguni bado huduma hiyo haijawafika ipasavyo, kutokana na udogo wa mabomba ya kusambazia maji, kuzimwa kwa umeme, kukosekana kwa pump kubwa ya maji na sababu nyengine zinazohusiana.

Maelezo ya Kamati:

pamoja na kuelezwa kwamba kila Shehia iliingiziwa Tsh.30,000,000, mbali na mchango wa

wananchi, ununuzi wa tangi la maji kama ilivyokusudiwa kwa mradi huu, haukufuata taratibu za manunuzi. Ununuzi wa tangi hilo lenye thamani takriban Tsh. 64,000,000, haukupaswa kufanywa kwa 'three qoutation' zilizoshindwa kuthibitishwa usahihi wake mbele ya Kamati.

Kamati imeshuhudia msutano wa wazi baina ya wananchi wa Kizimkazi Mkunguni na Kizimkazi Dimbani na iwapo ZAWA pamoja na Viongozi wa TASAF wangeliwaelimisha ipasavyo wananchi wa Shehia hizo, mgogoro wowote usingelitokea.

Maoni ya Kamati:

Kamati inaitaka Serikali kwa kushirikiana na Mamlaka ya Maji ZAWA kulipatia ufumbuzi tatizo la maji linalowakabili wananchi wa Kizimkazi Mkunguni, pamoja na kuwa waadilifu katika kutoa huduma ya maji kwa wananchi wote, bila ya ubaguzi.

Aidha, katika unuzi wa tangi, Kamati haikuridhika na maelezo yaliyotolewa na inaamini taratibu za manunuzi zimekiukwa. Hivyo, inaiagiza Serikali kuwachukulia hatua za kinidhamu watendaji wakuu wa TASAF, waliosimamia Mradi huo.

Hoja Namba 9.1.4 Kuhusiana na Ufugaji wa Ng'ombe wa Maziwa, Binguni.

Mradi wa ufugaji wa ngo'mbe wa maziwa Binguni, uliingiziwa Tsh.7,622,300 kwa mwaka 2009/2010 ili uweze kuwasaidia wananchi wa eneo hilo. Hata hivyo, kutokana na utendaji usioridhisha wa Kamati ya Maendeleo, mradi huu haukuweza kufikia lengo.

Maelezo ya Kamati ya Maendeleo iliyosimamia Mradi huu.

Mradi huu ulihusika na ujenzi wa banda; utolewaji wa mafunzo ya ufugaji kwa wanachama wa Kamati husika, ununuaji wa ng'ombe na ufugaji wa ngo'mbe wenyewe. Idadi ya Ng'ombe waliohusika na mradi ni watatu, ingawa ufugaji wenyewe haukwenda vizuri kinyume na matarajio ya Kamati.

Katika hatua za ufugaji wa ng'ombe hao, walifikia hatua ya kuzaa lakini baadhi ya ng'ombe hao walikufa na wanawe na baadhi waliwahi kuwachinja hali iliyopelekea kushindwa kuwahudumia ng'ombe wa maziwa kwa kutumia hakiba iliyobakia, waliamua kununua ng'ombe wa kienyeji kwa azma ya kuendelea mfugo. Pamoja na hayo, bado walikabiliwa na tatizo kuwahudumia ambapo walianza kuchangishana angalau kila mtu Tsh.500 lakini baadae walishindwa, na matokeo yake baadhi ya wanakikundi wakaanza kukimbia.

Maelezo ya Viongozi wa Mradi mbele ya Mkuu wa Wilaya ya Kati:

Baada ya Kamati kushindwa kupata maelezo ya kina kuhusiana na mradi huu kwa sababu Katibu wa Kikundi ambae ndie aliekuwa na taarifa za kina, kushindwa kuhudhuria mbele ya Kamati, Kamati iliutaka Uongozi wa Wilaya pamoja na Mkoa kulifuatilia suala hili, ili ukweli wake uweze kufahamika. Kwa hali hiyo, Mnamo tarehe 05/10/2012, Mkuu wa Wilaya alikaa pamoja na Uongozi wa Kikundi hicho na kuweza kutoa maelezo juu ya masuala ambayo yalishindwa

kuwekwa wazi wakati wa ziara ya Kamati: Mradi huo ulikuwa unaongozwa na hawa wafuatao:

- Ndg. Bakari Khamis Ali, ambae ni Mwenyekiti;
- Ndg. Mussa Kombo Mrisho - Katibu,
- Ndg. Othman Mussa Makungu - Sheha; na
- Ndg. Fatma Khamis Rufai - Mshika Fedha.

Wakati Katibu wa Kikundi hicho, Ndg. Mussa Kombo Mrisho alipokuwa akitoa ufafanuzi wake, alieleza kwa Mkuu wa Wilaya ya Kati kwamba, Mradi huo ni wa watoto yatima, ila ulikuwa unasimamiwa na wazee wao. Kuhusiana na Ng'ombe, Ndg. Mussa alieleza kwamba, baada ya kukabidhiwa Ng'ombe watatu na TASAF, ng'ombe hao hawakudumu kutokana na sababu zifuatazo:

- Ng'ombe mmoja alifariki kwa bahati mbaya.
- Ng'ombe mmoja aliuzwa kwa mchinja ng'ombe, Bw. Hamid Yakub, Mkaazi wa Ndijani Mseweni.
- Ng'ombe wa tatu wamembadilisha kwa kutoa dume na kupewa Mke, na Mchinja Ng'ombe, Ndg. Hamid Yakub, lakini mpaka muda huo, ng'ombe aliebadilishwa hajuulikani alipo (Inasemekana kwamba anauzwa).

Maelezo ya Kamati:

Miongoni mwa Miradi iliyoishangaza Kamati ni pamoja na mradi huu, ambapo wakati Kamati ikielezwa kwamba wananchi wa Binguni wameweza kujinasua kwa kufuga ng'ombe wa maziwa, wakati Kamati inatembelea eneo la tukio, ilishuhudia zizi tupu halina hata ng'ombe mmoja. Jambo la kushangaza, baada ya kugundua kuwa zizi lipo tupu, Kamati ilielezwa kwamba, ng'ombe hao wamefariki, lakini baada ya mahojiano ya kina, Kamati ikagundua kwamba ng'ombe hao hawapo tena na mradi huu umekufa kabisa.

Tatizo jengine ni kwamba Afisi ya Wilaya haikuwa na taarifa za mradi huo na namna ulivyotekelezwa, na uelewa wao ni baada ya ziara ya Kamati. Aidha, Sheha wa Shehia hiyo ambae ni mlezi wa mradi huo, hakuhusishwa ipasavyo katika maendeleo ya mradi, na ni sawa na kusema kwamba, mradi huu na namna ulivyokuwa unaendelea, ulifahamika na Katibu wa Kikundi na kidogo Mwenyekiti wake.

Maoni ya Kamati :

Kamati inaagiza kuchukuliwa kwa hatua za kisheria, Katibu wa Kikundi hiki Ndg. Mussa Kombo Mrisho, kwa kujbinafsisha zaidi ng'ombe wa mradi na kuhusika kwake katika kufa kwa mradi huu.

Hoja Namba 9.1.7 Kuhusiana na Ufugaji wa Kuku wa Mayai, Muyuni C.

Mradi huu umeingiziwa Tsh. 8,106,252 kwa mwaka 2009/2010, lengo ni kuwasaidia wananchi

wa Muyuni C kujikwamua na umasikini kupitia ufugaji wa kuku wa mayai.

Maelezo ya Kamati ya Maendeleo iliyohusika na Usimamizi wa Mradi.

Mradi wao ulianza vizuri kwa awamu ya kwanza baada ya kuingiza kuku 200 na kufanikiwa kupata faida. Hata hivyo, katika awamu ya pili, walipoingiza kuku wafikao 200 hawakufanikiwa kutokana na vifo vilivyosababishwa na kukosa chanjo. Aidha, waliingiza kuku 150 kwa awamu ya tatu, lakini walipofikia hatua ya kukaribia kutaga, walishindwa kuwaendesha kwa kukosa fedha za chakula, hali iliyosababishwa na kukosa msaada wa Viongozi wao wa Jimbo, pamoja na kupanda kwa gharama za chakula, na kukosa chanjo bora katika kipindi cha mwishoni mwa 2009/2010 wakati Zanzibar ilipokosa umeme kwa takriban miezi mitatu.

Maelezo ya Kamati:

Kamati imepokea taarifa ya Kamati ya Maendeleo kuhusiana na Mradi huu na kufahamu kwamba, kufa kwa mradi huu pia kumesababishwa na utaratibu wa Miradi ya TASAF ya kutowasimamia tena wananchi baada ya kukamilika kwa mradi. Aidha, Wizara inayohusika na Mifugo nayo ilipaswa kumuwezesha Afisa Mifugo kuwa karibu na wananchi na kuweza kuwasaidia.

Maoni ya Kamati:

Kamati inaitaka Serikali kuangalia tena utaratibu wa Miradi ya TASAF, iweze kuwa endelevu kwa kuwasimamia wananchi kwa miradi yao hata baada ya kumalizika kwa awamu ya mradi iliyokusudiwa. Kamati haikufurahishwa kwa Mradi huu kutofikia lengo lake lililokusudiwa.

Hoja Namba 9.1.1 Kuhusiana na Ujenzi wa Skuli ya Sekondari, Muyuni.

Kwa mwaka 2009/2010, Mradi huu ulikusudiwa kujenga skuli ya Sekondari ya Muyuni, ili wananchi wa Muyuni waweze kupata huduma hiyo na isiwe wanaendelea kutegemea skuli zilizo katika vijiji vya mbali. Hivyo, Mradi huo uligharimu Tsh.125,831,904.

Maelezo ya Kamati za Maendeleo zilizosimamia Mradi:

Mradi huu ulisimamiwa na Shehia tatu, Muyuni A; Muyuni B na Muyuni C, chini ya msaada wa Mchoro na utaalamu kutoka Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali. Hapo awali, kila Shehia ilikuwa inakusudia kuwa na mradi wake, lakini baada ya kukaa pamoja walikubaliana kujenga Skuli hii.

Aidha, matumizi ya fedha zote pia yanahusisha na samani zilizo katika skuli hiyo.

Maelezo ya Kamati:

Kamati imepokea taarifa ya Shehia zote na kupitia matumizi yaliyohusika na kugundua kwamba, fedha zimetumiwa ipasavyo ingawa kuna baadhi ya makosa ya kibinaadamu.

Maoni ya Kamati:

Kuna haja ya kuendelezwa kwa Skuli hiyo jukumu ambalo kwa sasa lipo kwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali. Hivyo, Kamati inaitaka Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, kufanya jitihada ya kuiendeleza skuli hiyo, ili wananchi waweze kufaidi matunda ya Mapinduzi.

Hoja Namba 9.1.6 Kuhusiana na Upandaji Miche, Ndijani Muembepunda.

Kwa mwaka 2009/2010, Mradi huu ulikwishaingiziwa Tsh. 8,990,950 kwa ajili ya Upandishaji miche, ujenzi wa kisima na ujenzi wa jengo kwa matumizi ya Ofisi.

Maelezo ya Kamati ya Maendeleo iliyosimamia Ujenzi.

Kamati yao yenye watu 10, wote ni walemavu imepokea fedha hizo na kuzitumia kwa kuchimba kisima, kujenga jengo na kuweka Nursery ya miche mbali mbali, Ununuzi wa Matenki ya maji na mota pamoja na matumizi mengine yaliyohusika. Pamoja na kuanza vizuri kwa mradi huu, baadae ulisita kwa kukosekana maji katika kipindi cha kuzimwa umeme kwa muda wa miezi mitatu, Unguja.

Maelezo ya Kamati:

Kamati imepongeza juhudi zilizochukuliwa na Kikundi hicho, huku ikisikitishwa kutoendelea kwa mradi huo ambao hapo awali ulianza vizuri. Tatizo kubwa la mradi huu kusita, ni pamoja na kukosa uendelevu wake kutoka TASAF, huku miradi ya aina hii ikikwama kwa kukosekana msaada kutoka Serikalini, mara tu inapokamilika katika hatua ya awali.

Maoni ya Kamati:

Kamati inaitaka Serikali kuhakikisha kwamba, Miradi ya wananchi inakua endelevu, na isiwe kama mzigo wanaoachiwa wananchi kuitekeleza huku wakikosa msaada kutoka Serikalini.

Hoja Namba 9.1.5 Kuhusiana na Ufugaji wa Ng'ombe wa Maziwa, Mchangani:

Mradi wa Ufugaji wa Ng'ombe wa Maziwa Mchangani, umeingiziwa Tsh.7,633,300 kwa lengo la kuwasaidia wananchi kujinasua na umasikini.

Maelezo ya Kamati ya Maendeleo iliyosimamia Mradi:

Kikundi cha wananchi hawa kiitwacho Mstahamilivu chenye wanachama 20 bado hakijasajiliwa, huku mradi waliousimamia uliingiziwa Tsh. 6,936,050 na mchango wao wa nguvu kazi ni wa Tsh.585,000. Mradi wao ulianza vizuri, ila baadae kutokana na uchache wa fedha, walishindwa kuusimamia na kutokana na ugomvi uliopo miongoni mwao, walilazimika kugawana ng'ombe hao kinyume na makusudio ya mradi.

Maelezo ya Kamati:

Kitendo cha kugawana ng'ombe na fedha kwa wanakikundi hiki hakikionesha uungwana kwa sababu kinatofautiana na malengo ya mradi uliokusudiwa. Wakati Kamati inalifanyia kazi suala hili, ni kikundi kimoja tu ndicho kulichokuwepo kikiwasilisha hali halisi ya mradi, wakati kikundi chengine kilichoundwa baada ya mgogoro, kimeshindwa kuhudhuria. Bado wananchama wa vikundi vyote wanakabiliwa na utendaji usioridhisha na kukabiliwa na hali ngumu ya kuwaendesha ng'ombe hao. Lishe duni, ukosefu wa huduma bora kwa mfugo huu, ni miongoni mwa changamoto zinazowakabili wananchi hao.

Maoni ya Kamati:

Pamoja na kwamba, baadhi ya ng'ombe wapo hai na wanaendelea kufugwa, bado lengo la mradi huu halikuweza kufikiwa kama ilivyokusudiwa. Kamati inaishauri Serikali kutoa mashirikiano ya karibu baada ya kumalizika kwa miradi hii, ili wananchi waweze kuisimamia kwa maslahi ya maisha yao.

2.5.0 MIRADI YA WANANCHI (PEMBA):

2.5.1 TAARIFA ZA MIRADI; MKOA WA KUSINI PEMBA.

Hoja Namba 6.1.2 Kuhusiana na Mradi wa Maendeleo wa Skuli ya Msingi, Ng'ombeni 'A'

Mradi huu uliingiziwa Tsh. 3,000,000 kwa mwaka 2009/2010, kwa lengo la kumaliza ujenzi wa mabanda ya Skuli.

Maelezo ya Kamati ya Maendeleo iliyohusika na Usimamizi wa Ujenzi:

Waliingiziwa Tsh.5,000,000 kutoka Wizara ya Fedha na Uchumi, (Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo) kwa awamu mbili tofauti. Awamu ya kwanza walipewa Tsh. 2,000,000 na awamu ya pili Tsh. 3,000,000. Fedha za awamu ya kwanza walizitumia kwa ujenzi wa mabanda hayo ya Skuli kutoka kozi ya nne (kwa tofali) hadi kozi ya kutia linta; kutia linta na nguzo, na Tsh.3,000,000 za awamu ya pili zilitumika kwa kuinua wa tofali katika hatua za gebo, hadi kufikia hatua ya kulikabidhi jengo hilo kwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa hatua za kumalizwa.

Maelezo ya Kamati:

Kamati imepitia na kujiridhisha matumizi yaliyofanyika, ingawaje kumekuwa na kasoro ndogo ndogo za kibinaadamu ikiwa ni pamoja na kukosekana kwa baadhi ya saini za hati za malipo na muhuri wa skuli, kasoro hazioneshi kutumika vibaya kwa fedha hizo, bali kunatokana na ufahamu mdogo wa Kamati hizi katika kusimamia fedha za Serikali, lakini pia kunatokana na ugumu wa kupata risiti kutoka kwa wauzaji wa vifaa vya ujenzi kwa mnasaba wa matumizi husika.

Maoni ya Kamati:

Lengo la Mradi huu limefikiwa na Kamati imepongeza utendaji wa Kamati ya Maendeleo kwa kusimamia vizuri matumizi ya fedha hizi. Kamati inashauri Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, kuhakikisha skuli hii inajengewa uzio, ili kuepusha kuvamiwa kwa eneo lao.

Hoja Namba 6.1.1 Kuhusu Mradi wa Ujenzi wa Skuli ya Msingi, Jambangome.

Kwa mwaka 2009/2010, Mradi huu uliingiziwa Tsh. 3,500,000 kwa ajili ujenzi wa Skuli ya Msingi ya Jambangome.

Maelezo ya Kamati ya Maendeleo iliyohusika na Usimamizi wa Mradi huu.

Fedha hizo zilihusika na ujenzi wa madarasa manne, Ofisi ya Mwalimu Mkuu na ujenzi wa Ghala. Mradi ulianza mwaka 2007 na ulikwenda hatua kwa hatua, hadi kuezekwa mwaka 2010. Hata hivyo, Kamati ilitumia takriban 9,000,000 kabla ya kuikadhi Skuli hii kwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa hatua za kuezeka, kutia rangi, samani na mambo mengine.

Melezo ya Kamati:

Kamati imejiridhisha namna Mradi huu ulivyoanzishwa pamoja na kuipongeza Kamati iliyosimamia kuanzia hatua ilizochukua kupatikana kwa fedha hadi kuzitumia kwake.

Maoni ya Kamati

Kamati imeridhika na matumizi ya fedha zilizohusika na kuipongeza Kamati ya Maendeleo iliyohusika. Hata hivyo, inaishauri Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kuitafutia hati miliki Skuli hii na eneo lote lililoizunguka; kutia madirisha ya chuma ili kuepusha uharibifu na hujuma za wizi; kutatua tatizo la upungufu wa walimu wa Skuli hii huku ikiutaka Uongozi wa Skuli hii kuitunza Skuli kwa maslahi ya vizazi vijavyo.

Hoja Namba 6.1.3 Kuhusiana na Mradi wa Ujenzi wa Soko, Tundauwa:

Ofisi ya Rais, Fedha Uchumi na Maendeleo iliingiza jumla ya Tsh. 4,500,000 kwa mwaka wa fedha 2009/2010 kwa Kamati ya Maendeleo ya Tundauwa, kwa lengo la kukamilisha Ujenzi wa Soko. Aidha, Mradi huu hapo awali uliingiziwa Tsh. 21,809,018 kutoka TASAF kwa lengo hilo hilo.

Maelezo ya Kamati ya Maendeleo iliyohusika na Usimamizi wa Mradi:

Ni kweli hapo kabla walipata fedha kutoka TASAF na baada ya kumaliza fedha hizo, huku lengo lao likiwa halijafikiwa, ndipo walipoamua kuomba fedha Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo na kufanikiwa kuingiziwa Tsh. 4,500,000/- zilizotumika kwa ununuzi wa mbao, vifaa vya ujenzi, vifaa vya umeme na malipo ya fundi.

Maelezo ya Kamati:

Pamoja na kukamilika kwa jengo hili tokea mwaka 2010, hadi Kamati inalitembelea tarehe 01/03/2013 bado halijaanza kutumika. Aidha, wakati Kamati inapitia vielelezo kadhaa vya malipo ya fedha zilizotumika (Tsh. 4,500,000), ilijiridhisha kwamba, fedha hazikutumika ipasavyo, ikiwa ni pamoja na Hati ya Malipo ya Tsh. 2,500,000/-, fedha zilizonunuliwa saruji pekee, huku saruji hiyo hiyo ikinunuliwa kwa hati za malipo tofauti, wakati ujenzi halisi haukuthibitika kutumika kwa saruji yote hiyo.

Maoni ya Kamati:

Mradi huu haukuweza kufikiwa lengo kutokana na kutotumika kwa Soko hilo, huku kukiwa na migogoro na migawanyiko kadhaa kwa wananchi wa Tundauwa. Kamati imeushauri Uongozi wa Shehia ya Tundauwa, Uongozi wa Mkoa, Wilaya kwa pamoja na Mwakilishi na Mbunge, kukaa pamoja na wananchi ili kuondosha kasoro zilizopo na hatimae, jengo hili liweze kutumika kikamilifu.

2.5.2 MKOA WA KASKAZINI, PEMBA:

Hoja Namba 5.1.4 Kuhusu Mradi wa Ujenzi wa Skuli ya Msingi, Kiuyu Kipangani:

Kwa mwaka 2009/2010, Kamati ya Maendeleo ya Wananchi wa Kiuyu Kipangani, iliingiziwa Tsh.3,300,000 kutoka Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kwa ajili ya ujenzi wa madarasa.

Maeleo ya Kamati ya Maendeleo iliyohusika na Usimamizi wa Mradi huu:

Baada ya usumbufu wa muda mrefu wa wananchi wa Kiuyu Kipangani kufuata skuli takriban kilomita 7, waliamua kujenga Skuli na kufanikiwa kupata wafadhili mbali mbali, ikiwa ni pamoja na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Jumla ya fedha Tsh.3,300,000 zilitumika kwa ujenzi wa tofali baada ya msingi, hadi ufungaji wa linta. Matumizi ya fedha hizo zilihusika na ununuzi wa matofali; kokoto; saruji; nondo; uchukuzi wa saruji na matumizi mengineyo.

Maelezo ya Kamati:

Kamati imeshuhudia ujenzi huo na kujiridhisha kwamba, fedha zilizotolewa zilitumika ipasavyo.

Maoni ya Kamati:

Kamati inaishauri Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, kukamilisha utiaji wa samani, baada ya kuipongeza kwa kukamilisha hatua ya uezekaji na utiaji rangi, huku ikisisitiza kupatikana kwa hati miliki na ujenzi wa uzio, bila ya kusahau kutafuta uwezekano wa kutia madirisha ya nondo, ili kuepusha uharibifu na hujuma za wizi.

Hoja Namba 5.1.3 Kuhusiana na Mradi wa Ujenzi wa Kituo cha Afya, Kifundi.

Mradi huu uliingiziwa Tsh. 4,000,000 kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa kituo cha Afya, Kifundi kwa mwaka 2009/2010.

Maeleo ya Kamati ya Maendeleo iliyohusika na Usimamizi wa Mradi huu:

Pamoja na Mradi huu kupata fedha kutoka vyanzo tofauti, matumizi ya Tsh. 4,000,000 yalihusu uezekaji, ujenzi wa tofali kwa hatua za uezekaji na matumizi mengine yaliyohusika.

Maelezo ya Kamati:

Kamati imethibitisha matumizi ya fedha hizo na kuridhika kwamba zimetumiwa ipasavyo.

Maoni ya Kamati:

Kamati imepongeza juhudi zilizochukuliwa na Kamati ya Maendeleo huku ikiishauri Wizara ya Afya kuhakikisha inajipanga na kukipatia vifaa vya kutosha kituo hichi, ili kiweze kuwasaidia wananchi. Aidha, Wizara ya Afya iandae utaratibu wa kuwasomesha vijana wenye sifa na ikiwezekana kuwasaidia wale wenye mwelekeo wa kuwa na sifa zilizohitajika, wa eneo hili ama vijiji vilivyo jirani, kwa lengo la kuwa Madaktari, Wauguzi na wataalamu wengine wa Afya, ili Kituo hichi kiweze kujitosheleza kihuduma.

Hoja Namba 5.1.2 Kuhusiana na Mradi wa Ujenzi wa Barabara ya Maziwani/Shengejuu.

Mradi huu ulihusika na Tsh. 4,500,000 zilizotolewa na Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kwa ajili ya utengenezaji wa barabara ndogo ndogo za ndani kwa hatua ya kuweka kifusi.

Maeleo ya Kamati ya Maendeleo iliyohusika na Usimamizi wa Mradi huu:

Kamati iliyohusika na Mradi huu, ya Maendeleo ya Shehia ya Shengejuu haikuweza kufika mbele ya Kamati ya P.A.C, na badala yake ni Kamati ya Maziwani pekee ndiyo iliyofika na kutoa ufafanuzi. Fedha hizo Tsh.4,500,000 alikabidhiwa Ndg. Dadi Hamad Dadi, mkaazi wa Maziwani, kwa kujiundia Kamati hewa ya Shengejuu huku fedha hizo akizitumia kinyume na makusudio yaliyowekwa.

Ndg. Dadi alipeleka Greda katika bara bara husika, ila hakufanya vizuri na badala yake Kamati ya Maendeleo ya Maziwani ilitumia Tsh. 4,700,000 kwa kutia greda, kuweka sawa zaidi sehemu zilizokuwa na mashimo na hatimae Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano walimaliza kazi husika kwa hatua ya kifusi, baada ya awali nao kutumia greda.

Maelezo ya Kamati:

Ndugu Dadi alipewa Tsh.4,500,000 kama Katibu Kamati ya Maendeleo ya Shengejuu na kujaza Mkataba na kupewa fedha, huku baada ya Wizara ya Fedha kumtaka arejeshe risiti na hati nyengine za matumizi, alifanya hivyo, pamoja na ukweli kwamba, hakuna ujenzi wowote unaothibitisha kutumika kwa fedha hizo, wala Kamati ya Maendeleo ya Shengejuu iliyomtambua Ndg. Dadi. Kwa ujumla fedha hizo zimetumika kinyume na taratibu.

Maoni ya Kamati:

Kamati inaiagiza Serikali kumchukulia hatua za Kisheria Ndg. Dadi Hamadi Dadi huku ikiitaka Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kuwa makini na kufanya uhakiki ipasavyo katika Miradi inayohusisha wananchi. Kamati pia inaishauri Serikali kukaa pamoja na Mwekezaji wa Kampuni ya Mipira iliyopo katika eneo hili la Maziwani, ili aweze kuwasaidia wananchi waliomzunguka.

Hoja Namba 5.1.1 Kuhusiana na Mradi wa Ujenzi wa Kituo cha Afya, Bwagamoyo-Mtambwe.

Kwa mwaka 2009/2010, Kamati ya Maendeleo ya Shehia ya Bwagamoyo Mtambe, iliingiziwa Tsh. 4,000,000 kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha Afya cha Kijiji hicho.

Maeleo ya Kamati ya Maendeleo iliyohusika na Usimamizi wa Mradi huu:

Mradi huu ulianza kwa njia ya ujenzi wa Taifa, kutokana na kukosa huduma ya Kituo cha Afya katika eneo la karibu. Hali hii iliwapelekea kuomba fedha katika vyanzo tofauti na kwa upande wa matumizi ya Tsh. 4,000,000 zilizotolewa na Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, uezekaji wa kituo hicho uliwezekana. Fedha hizo zilitumika kwa kununulia misumari, mbao, bati, mafundi, usafirishaji, huku zikitumika Tsh. 40,000 tu kwa ufuatiliaji wa kazi hiyo.

Maelezo ya Kamati:

Matumizi ya fedha hizo yameiridhisha Kamati.

Maoni ya Kamati:

Kamati imeipongeza Kamati ya Maendeleo ya Shehia, na kuwataka kufanya juhudi za mwisho ili kituo kiweze kumalizika na kuanza kazi. Aidha, Kamati inaitaka Wizara ya Afya kuangalia uwezekano wa kukimaliza Kituo hicho na kujiandaa kwa vifaa na huduma zilizobakia, mara tu kitakapomalizika. Wizara ya Afya, pia itoe msaada maalum wa kuwasomesha vijana waliopasi angalau 'Biology' kwa kiwango cha 'D' wa Shehia eneo hili pamoja na Shehia za karibu, ili waweze kutoa huduma iliyokusudiwa.

(RIPOTI YA PILI)

3.0 RIPOTI YA UKAGUZI YAKINIFU WA UDHIBITI NA UHIFADHI WA MALI ZA KUDUMU ZA SERIKALI KWA MWAKA WA FEDHA 2009/2010.

Ripoti hii inahusiana na Ukaguzi Yakinifu (Value for Money), kwa Mali za Kudumu za Serikali, katika kuangalia namna gani mali hizo zinahifadhiwa na kutunzwa, ili ziweze kudumu kwa muda mrefu na kutumika kama ilivyokusudiwa. Kwa mujibu wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, alikusudia kwa kufanya ukaguzi huu, kutoa picha halisi ya namna ya mali za Serikali zinavyohifadhiwa na kudhibitiwa ili kuhakikisha kwamba, taratibu na sheria kuhusu usimamizi wa mali za Serikali zinafuatwa ipasavyo. Mali zilizokaguliwa na Mdhibiti na kufuatiliwa na Kamati ya P.A.C ni zile zinazohamishika na zisizohamishika ambazo zinamilikiwa na kusimamiwa na Taasisi mbali mbali za Serikali ya Mainduzi ya Zanzibar.

Kamati ilipokuwa inafanya uchunguzi wake, ililazimika kukagua mahesabu ya Serikali kwa kuzingatia misingi ya uchumi, ufanisi na malengo yaliyokusudiwa katika matumizi yaliyofanyika. Katika uchunguzi huo wa Kamati, mbali na kukagua mahesabu kwa kuzingatia kama sheria, taratibu na miongozo mbali mbali ya fedha kama zimefuatwa, pia ililazimika kuangalia hali ya uchumi, kupatikana kwa ufanisi katika utekelezaji na hatimae kuona kwamba, malengo yaliyokusudiwa, yamefikiwa.

Katika kupata ufafanuzi wa majibu ya Hoja mbali mbali za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu, Kamati imefuatilia ripoti hii na ni busara tukapata ufafanuzi ufuatao:

3.1 WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, UTALII NA MICHEZO :

Hoja Namba 1.1 Kuhusu Kukosekana kwa Mpango wa Manunuzi :

Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo haikuwa na Mpango wa Manunuzi kwa mwaka wa 2009/2010 na hivyo matumizi ya fedha zake hayakufuata mpango huo, bila ya kujali maelekezo ya kifungu cha 19 cha Sheria Namba 9 ya mwaka 2005.

Maelezo ya Wizara

Wizara ilikiri juu ya kutokuwepo kwa mpango huo kwa wakati huo (mwaka 2009/2010), lakini kwa hivi sasa tayari Mpango huo umeshaanzishwa.

Maelezo ya Kamati :

Pamoja na kwamba mwanzo mpango huo haukuwepo lakini hatua ya sasa imeiridhisha Kamati kwani ilipata kuukaguwa Mpango wa Matumizi kwa mwaka 2011/2012 pamoja na mchanganuo wa manunuzi wa mwaka 2012/2013.

Maoni ya Kamati:

Kamati inaitaka Wizara kuhakikisha manunuzi yote ya Wizara, yanafuata ipasavyo mpango wa manunuzi, ili kuleta ufanisi katika manunuzi ya vifaa na mali mbali mbali za Wizara.

Hoja Namba 1.2 Kukosekana kwa Daftari la kuhifadhia Mali za Kudumu.

Ukaguzi umebaini kwamba, Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo haiweki Daftari la kuhifadhia mali za kudumu (fixed Asset Register), kitendo kinachokwenda kinyume na maelekezo ya kifungu cha 264 cha kanuni za fedha za mwaka 2005. Aidha, hali hii huweza kusababisha upotevu wa mali hizo.

Maelezo ya Wizara:

Ni kweli hapo awali Daftari hilo halikuwepo lakini kwa sasa tayari lipo ambalo ni la mwaka 2011/2012 na mwaka 2010/2011 ambalo linakidhi haja na matakwa ya Sheria.

Maelezo ya Kamati.

Pamoja na kuwepo kwa daftari hilo lakini lina mapungufu katika ujazaji wake. Kwa mfano maelezo ya chombo huwa hayakamiliki hakuna chasis wala engine number. Aidha vifaa vyengine kama vile viti na meza havikuwekea alama, nayo huwa ni kasoro katika kuviainisha kwenye daftari.

Maoni ya Kamati:

Kamati inaitaka Wizara kukamilisha taarifa zote muhimu katika daftari hilo.

Hoja Namba 1.3 Kuhusu Udhibiti wa Utunzaji wa Mali za Wizara

Ukaguzi umebaini kwamba, udhibiti na utunzaji wa baadhi ya mali za Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo hauridhishi. Hali hii imetokana na kutokuwepo kwa utunzaji mzuri, kutofanyiwa matengenezo kwa muda husika na kuwepo kwa usimamizi usioridhisha. Hali hii imepekea Wizara kuingia katika gharama kubwa ya utunzaji na utengenezaji wa mali hizo na hatimae kushindwa kutoa huduma husika.

Maelezo ya Wizara.

Wizara imekiri kuwepo kwa hali hiyo. Hata hivyo magari yasiyotengenezeka au yaliyoharibika siku nyingi yameuzwa. Mitambo inayaribiwa nayo wameifanyia matengenezo na wamefanikiwa kuifufuwa.

Maelezo ya Kamati

Kwa nini Wizara ikubali kuyauza magari tu na kuviacha vifaa vyengine ambavyo havitumiki. Aidha kwanini Wizara ing'ang'anie kufufua mitambo ambayo hata vipuri vyake ni adimu duniani kwani sasa viwanda vya dunia vimeshabadili uzalishaji wa mitambo hiyo.

Maoni ya Kamati:

Suala zima la uuzaji wa mali za Serikali, linahitaji kuangaliwa upya. Kwa upande wa Kamati, inasisitizwa kufuatwa ipasavyo kwa sheria ya Mannunuzi na kanuni zake, lakini pale Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo inapopelekewa maombi ya kuuzwa kwa vifaa hivyo, ni lazima waangalie haja na uhalisia wa kuuzwa kwake.

Aidha, Mitambo ya kizamani ambayo bado ipo na matumizi yake ni ya hasara kwa Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo ambayo yanahitaji matengenezo ya mara kwa mara. Ni busara iuzwe au kwa utaratibu mwengine unaofaa, na inunuliwe mitambo ya kileo ambayo vipuri vyake vinapatikana.

Hoja Namba 1.4 Kuhusu Kukosekana kwa Hatimiliki ya mali za Wizara.

Ukaguzi umebaini kwamba, Wizara inamiliki majengo mbali mbali, lakini hati miliki za majengo hayo hazikupatikana kwa ukaguzi. Suala ambalo linashindwa kuthibitisha uhalali wa umiliki huo.

Maelezo ya Wizara

Wizara tayari imeshawasiliana na Wizara ya Majenzi, Makaazi, Ardhi na Nishati katika kufanikisha suala hili kwenye maeneo yote ambayo haina hatimiliki.

Maelezo ya Kamati

Kwa vile maeneo ya Taasisi nyingi za Serikali hazina hatimiliki, ni dhahir kwamba Wizara inayohusika na utoaji hatimiliki itakuwa na maombi mengi. Hilo Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo ilijue na isibweteke tu. Iwe inafatilia kwa karibu.

Maoni ya Kamati

Kamati inaitaka Wizara ihakikishe kwamba majengo yote yana hatimiliki.

3.1.1 HOTELI YA BWAWANI :

Hoja Namba 2.1 Kukosekana kwa daftari la kuhifadhia mali za kudumu.

Ukaguzi umebaini kwamba, Hoteli ya Bwawani haiweki daftari la kuhifadhia mali za kudumu, kinyume na maelekezo ya kifungu cha 264 cha Kanuni za Fedha za mwaka 2005, pia hali hii huweza kusababisha upotevu wa mali hizo.

Maelezo ya Hoteli :

Ni kweli kwa kipindi cha miaka ya nyuma Hoteli y Bwawani haikuwa na daftari la kuhifadhia mali zake za kudumu, ingawa Uongozi wa Hoteli ya Bwawani kwa kupitia Kitengo cha Uhasibu hapa hotelini, tayari kimeshakamilisha kitabu hicho cha kumbu kumbu cha thamani za Hoteli

pamoja na kuingizwa taarifa zake muhimu kwa wakati husika, ili Hoteli kuweza kujizuia na kuzidhibiti thamani zilizopo hapa Hotelini.

Maelezo ya Kamati :

Pamoja na maelezo ya Uongozi wa Hoteli, daftari lililowasilishwa kwa Kamati bado halijafuata muongozo uliotolewa na Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, kwa ujumla Kamati imeridhika kwamba Hoteli bado haina Daftari la kuhifadhia mali za kudumu. Kamati imeendelea kusimamia hoja yake, kwa kuzingati pia kwamba Mhasibu huyu wa Hoteli ya Bwawani hajapata mafunzo ya kuweka daftari hilo kama inavyotakiwa, hata alipokuwa Wizara ya Katiba na Sheria.

Maoni ya Kamati :

Kwanza Kamati inautaka Uongozi wa Hoteli ya Bwawani kufahamu kwamba, wamevunja Sheria kwa kukiuka maelekezo ya kifungu cha 264 cha Kanuni za Fedha za mwaka 2005. Kamati inauagiza Uongozi wa Hoteli ya Bwawani, kuandaa mara moja daftari la kuhifadhia mali za kudumu, huku likiwa na taarifa zote zinazotakiwa. Aidha, kushindwa kufanya hivyo ndani ya miezi mitatu tokea kuwasilishwa kwa ripoti hii, Kamati inaiagiza Serikali kumuwajibisha kinidhamu, Afisa Mhasibu wa Hoteli ya Bwawani.

Hoja Namba 2.2 Kukosekana kwa Hati Miliki ya Hoteli ya Bwawani.

Ukaguzi umebaini kwamba, Hoteli ya Bwawani inamiliki jengo, lakini hati miliki ya jengo hilo haikupatikana kwa ukaguzi, suala ambalo linashindwa kuthibitisha uhalali wa umiliki huo.

Maelezo ya Hoteli:

Ni kweli kwamba Hoteli ya Bwawani haina hati miliki, Uongozi wa Hoteli uliwasiliana na mamlaka husika kutaka kuja kupima maeneo ya Hoteli ili kupatiwa hati miliki ya maeneo hayo. Hatua hii imeshachukuliwa kwa kuja kuwapimia eneo la hoteli ya Bwawani na hatua zinaendelea za kupatiwa hiyo hati miliki.

Maelezo ya Kamati:

Kamati imewasilishiwa ramani inayoonesha upimaji wa maeneo ya Hoteli. Hata hivyo, Kamati imeikataa ramani hiyo na inaamini imetolewa pasi na kuzingatia eneo halisi la hoteli. Katika majibizano na Uongozi wa Hoteli, iliafikiwa kwamba, Uongozi huu ufike mbele ya Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati katika kikao cha Kamati na hatimae waithibitishe ramani hiyo.

Jambo la kushangaza wakati wa kikao hicho, Uongozi wa Hoteli ulikiri kwamba, ni wao waliokosea kwa kulazimisha kwamba ramani hiyo imetolewa na Wizara hii, na kukubali kwamba imetolewa na Kampuni binafsi waliyoikodi wao.

Kwa ujumla walilipa Tsh.6,000,000 kwa kupimiwa ramani, fedha ambazo zimeshindwa kuthibitishwa kupokelewa kwake, na hata ramani yenyewe ni feki. Kwa maana haijazingatia eneo halisi na sahihi la Hoteli, hamna beacons zoinazoonekana na kwa ujumla kama suala hili litaachwa liende hivi hivi, eneo kubwa la Hoteli hiyo litanyang'anywa na kuporwa, na hatimae wajanja wachache watajinufaisha eneo halali la Hoteli.

Maoni ya Kamati:

Kamati inawaonya Watendaji wa Hoteli ya Bwawani kujaribu kudanganya Kamati na kuwataka mara moja wawasiliane na Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati, kwa ajili ya kupimiwa eneo lao halali. Na Kamati inatoa angalizo kwa Wizara hii, kuhakikisha eneo halisi la Hoteli linapimwa na kupatiwa hati miliki.

Kamati inaitaka Serikali kuwachukulia hatua za kinidhamu Viongozi wa Hoteli, ikiwa ni pamoja na Mkurugenzi, Mhasibu na wote waliohusika na upimaji wa eneo la Bwawani kinyume na utaratibu.

Hoja Namba 2.2 Kuhusu Mapungufu katika ukusanyaji wa mapato sehemu ya New Pemba Bar.

Imebainika kwamba, Hoteli ya Bwawani imefunga mkataba na African Trust Co. Ltd ya ukodishwaji wa sehemu ya uuzaji wa vileo (Bar) kwa Tsh. 13,000,000. Aidha, ukaguzi umebaini kwamba sehemu hiyo haitumiki ipasavyo tokea Februari 2009 na kupelekea Hoteli ya Bwawani kushindwa kukusanya mapato hayo. Hali hii imepelekea Hoteli kufungua kesi Mahakama Kuu Zanzibar.

Maelezo ya Hoteli:

Ni kweli 'New Pemba Bar' ilifungwa tokea 2009 kutokana na mkodishwaji kushindwa kulipa kodi anayodaiwa na hivyo kufungua kesi Mahakamani. Kesi hiyo inaendelea , kwa ushauri wa Mwanasheria Mkuu aliwashauri ni vyema shauri hili walimalize nje ya Mahakama kwa hivyo wamo kwenye jitihada za kulimaliza kama walivyoshauriwa na Mwanasheria Mkuu.

Maelezo ya Kamati:

Kamati imeshtuka kuelezwa kwamba, Mwanasheria anaesimamia kesi hii yupo katika Kamati ya Marekebisho ya Katiba na hivyo kesi hiyo inaendelea kutajwa.

Maoni ya Kamati:

Kamati inaitaka Hoteli kuhakikisha wanarejea tena kwa Mwanasheria Mkuu na kupata ushauri zaidi, na hoja kwamba kesi hiyo inakwama kwa sababu mwanasheria anaesimamia (Ndg. Ali Ali Hassan) aliyepo katika Kamati ya Mabadiliko ya Katiba, haina mashiko. Hata hivyo, ushauri wa Mwanasheria Mkuu wa kumalizwa kesi hiyo nje ya Mahakama, hauna tatizo kwa Kamati, iwapo tu maslahi ya Hoteli yatazingatiwa na kupatikana.

Hoja Namba 2.4 Kuhusu Udhibiti na Utunzaji wa Mali za Hoteli:

Ukaguzi umebaini kwamba, udhibiti na utunzaji wa baadhi ya mali za kudumu za Hoteli ya Bwawani hauridhishi. Hali hii imetokana na kutokuwepo kwa utunzaji mzuri, kutofanyiwa matengenezo kwa muda husika na kuwepo kwa usimamizi usioridhisha. Hali hii imepekea Hoteli kuingia katika gharama kubwa ya utunzaji na utengenezaji wa mali hizo na hatimae kushindwa kutoa huduma husika.

Maelezo ya Hoteli:

Ni kweli kwamba Hoteli ilikuwa na uangalizi mdogo wa mali zake ila kwa sasa uongozi wa hoteli umeshagawa majukumu ya usimamizi wa mali hizo kwa kila Mkuu wa Idara wa Hoteli ya Bwawani na hivyo Hoteli inaendelea kuzifanyia matengenezo mali zote za Hoteli kama vyumba vya kulala wageni, kumbi za mikutano pamoja na mashine za kufulia, kadri hali itaporuhusu.

Maelezo ya Kamati:

Kamati imepokea taarifa hiyo ya Hoteli na kuhoji iwapo Mikataba inayoingiwa na Hoteli na watu ama Taasisi mbali mbali inapata idhini na kupitiwa na Mwanasheria Mkuu.

Maoni ya Kamati:

Kamati inautaka Uongozi wa Hoteli kumshauri ipasavyo Mwanasheria Mkuu katika kuingia Mikataba mbali mbali. Aidha, imeitaka Hoteli kuhakikisha inatunza ipasavyo mali zake.

3.1.2 SHIRIKA LA MAGAZETI YA SERIKALI :

Hoja Namba 3.1 Kuhusu kukosekana kwa daftari la kuhifadhia mali za kudumu.

Ukaguzi umebaini kwamba, Shirika la Magazeti la Taifa haliweki daftari la kuhifadhia mali za kudumu, kinyume na maelekezo ya kifungu cha 264 cha Kanuni za Fedha za mwaka 2005, pia hali hii huweza kusababisha upotevu wa mali hizo.

Maelezo ya Shirika.

Ni kweli hali hiyo imejitokeza wakati huo kutokana na upya wa Shirika, ambalo limeanzishwa rasmi tarehe 1 Januari 2009 baada ya Sheria inayoanzisha kutiwa saini na Mhe. Rais, tarehe 31 Disemba 2008. Kwa sasa daftari hilo pamoja na madaftari mengine yanayohusiana na fedha na masuala mengine kisheria yameshatayarishwa na yanafanya kazi.

Maelezo ya Kamati:

Pamoja na taarifa hiyo ya kujitetea, Kamati imehitaji kupatiwa daftari hilo ili kujiridhisha kama kweli limeanzishwa ipasavyo. Na Kamati imegundua kwamba, daftari hilo lina kasoro kadhaa ikiwa ni pamoja na kutotiwa nambari za utambulisho (identification codes) kwa fanicha na vifaa mbali mbali vya Shirika. Yaani kumbu kumbu hizo hazionekani katika daftari wakati katika vifaa vyenyewe vinaonekana tayari vimeshatiwa namba hizo za utambulisho.

Maoni ya Kamati:

Kamati imelitasha Shirika hilo kukamilisha taarifa zote zinazohitajika katika daftari la kuhifadhia mali za kudumu za Shirika. Kwa kuwa kutofanya hivyo ni kosa kwa mujibu wa kifungu cha 264 cha Kanuni za Fedha za mwaka 2005, na kuwa tatizo hili ni la muda mrefu. Kamati inaiagiza Serikali kumchukulia hatua za kinidhamu, Afisa Mhasibu huyu iwapo atashindwa kuweka daftari la kuhifadhia mali za kudumu za Shirika hili la Magazeti.

Hoja Namba 3.2 Kuhusiana na Udhibiti na Utunzaji wa Mali za Shirika:

Ukaguzi umebaini kwamba, udhibiti na utunzaji wa baadhi ya mali za Shirika hauridhishi. Hali hii imetokana na kutokuwepo kwa utunzaji mzuri, kutofanyiwa matengenezo kwa muda husika na kuwepo kwa usimamizi usioridhisha. Hali hii imepekea Shirika kuingia katika gharama kubwa ya utunzaji na utengenezaji wa mali hizo na hatimae kushindwa kutoa huduma husika.

Maelezo ya Shirika:

Ni kweli hoja ya Mdhibiti ilithibiti wakati huo. Hata hivyo, suala hilo sasa limerekebiswa na suala la utunzaji wa mali za Shirika umeweka vyema kwa kuwepo kwa madaftari husika wa kazi hizo. Kuhusiana na vifaa vinavyoharibika, kulitokana na uhaba wa fedha ambapo kunapopatikana fedha kidogo, kipaumbele huwa ni matumizi ya kazi za msingi ya Shirika, ambayo ni uchapishaji wa magazeti pamoja na usambazaji wake. Aidha, suala hili pia linahusika na kufanyiwa matengenezo vifaa vinavyhitajika kwa matumizi ya haraka.

Kuhusu vifaa vibovu na chakavu kwa wakati huo havikuweza kuuzwa au kuondolewa kutokana na agizo la Serikali Kuu kuzuia kuuzwa au kuharibiwa vifaa chakavi hadi utakapomalizika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2010 kwa kuhofia watu kujiuzia mali za Serikali kwa kutumia mwanya wa mabadiliko ya Serikali. Aidha, baada yua kuondolewa marufuku hiyo, tayari kwa kupitia Idara ya Uhakiki Mali ya Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, vifaa hivyo vimeondolewa kwa kupigwa mnada wa wazi ha hivi sasa havipo tena.

Maelezo ya Kamati:

Kamati imepokea taarifa ya Shirika na imeridhika kuelezwa kwamba wamekiri makosa waliyoafanya na kwa sasa wameanza kuchukua hatua za kurekebisha.

Maoni ya Kamati:

Kamati inalitaka Shirika kuwa makini katika kutunza na kuhifadhi mali zake.

Mambo mbali mbali yaliyoibuka na kujadiliwa wakati wa Uchunguzi wa Kamati:

Kuhusu mapato, Shirika la Magazeti ya Serikali lilikisiwa kukusanya Tsh. 250,000,000 kwa mwaka 2010/2011, na kufanikiwa kukusanya Tsh. 315,669,194, sawa na 126.677% ya makisio. Aidha, Shirika limeidhinishiwa kutumia Tsh. 246,000,000, na fedha zilizopatikana ni Tsh. 226,017,248 ingawaje walihitaji kupatiwa bilioni 1.5.

Kamati imegundua kwamba, Shirika la Magazeti ya Serikali haina Afisi yake. Sehemu waliyopo sasa sio yao, ni mali ya Shirika la Utangaji za Zanzibar na wametakiwa kuhama si zaidi ya tarehe 30/09/2012, bila ya kupewa eneo maalum ilililoandaliwa kwa ajili ya matumizi ya shughuli zao. Hali inayowapa usumbufu mkubwa wa utekelezaji wa majukumu yao.

Kamati haikuridhishwa zaidi kwa kuelezwa kwamba, hapo awali Shirika hili lilipatiwa Ofisi ya ZBC Redio kunako jengo kongwe liliopo hapo hapo Rahaleo, ila baadae walihamishwa na jengo hilo kufanyiwa ukarabati na kuwa Kituo cha Muziki na Sanaa, huku tayari na Shirika hili la Magazeti ya Serikali lilikuwa tayari limeshatumia fedha kwa kufanya ukarabati ili jengo hilo waweze kulitumia kwa kazi zao. Aidha, suala hili lilipoulizwa kwa Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo aliyehudhuria kikao cha Kamati, alijibu kwamba, fedha zilizotengwa kwa ukarabati wa Studio hiyo hazikuwahi kutumika kwa vile muda wake wa kutumika ulimalizika na kulazimika kurejeshwa Serikalini, na hivyo wao kama Wizara waliharakisha ukarabati wa jengo hilo kwa ajili ya Kituo cha Muziki na Sanaa.

Hata hivyo, Kamati haikuridhishwa na majibu hayo, kwa sababu inachofahamu Wizara iliomba kujenga Kituo cha Muziki na Sanaa katika eneo la Chumbuni na sio kukarabati jengo ambalo tayari lilikuwa linatumiwa na Shirika la Serikali.

Maoni ya Kamati:

Kamati inaitaka Wizara ya Habari Utamaduni, Utalii na Michezo kutoa maelezo ya kina juu ya matumizi ya fedha za Ujenzi wa Kituo cha Muziki na Sanaa, sambamba na matumizi halisi ya fedha zilizotumika kufanyia ukarabati wa kituo hicho cha Redio kilichopo Rahaleo, kuwa Jengo la Kituo cha Muziki na Sanaa.

Mbali nahayo, Kamati inasikitishwa sana mpaka leo gazeti la Zanzibar Leo kuchapishwa Tanzania bara. Imelitaka Shirika liharakishe uwezekano wa gazeti hilo kuchapishwa hapa hapa Zanzibar.

3.1.3 KAMISHENI YA UTALII:

Hoja Namba 4.1 Kuhusiana na Kukosekana kwa Kitengo cha Manunuzi:

Ukaguzi wa Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu umebini kwamba, Kamisheni ya Utalii haikuunda Kitengo cha Manunuzi. Hali hii inapingana na sheria Namba 9 ya mwaka 2005, kifungu cha 14. Huku hali hiyo hupelekea kutokuwepo kwa mpango madhubuti wa manunuzi na hatimae kununuliwa kwa bidhaa zisizohitajika na katika wakati usiostahiki.

Maelezo ya Kamisheni:

Ni kweli kuhusiana na hoja ya Mdhibiti na Mkauguzi Mkuu wa Hesabu, ingawaje baada ya hoja hiyo, Kamisheni ilichukua juhudi za kuwasiliana na Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, tarehe 18/10/2011 yenye kumbu kumbu namba K/UT/1/1/VOL IV kwa kupatiwa Afisa Manunuzi. Hata hivyo, kutokana na kuchelewa kuletwa kwa Afis huyo, Kamisheni ya Utalii iliamua kumteua Ndg. Khamis Abubakar Khamis ambae elimu yake ni Uchumi kwenye Uhasibu (Econimist in Accoounting Analysis ana Auditing), kushika dhamana za manunuzi mpaka Kamisheni watakapompata mtaalamu husika kutoka Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo.

Maelezo ya Kamati:

Kamati haikuridhishwa na kitendo cha Kamisherni ya Utalii kusubiri Afisa Manunuzi kutoka Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, ukizingatia kwamba, suala hilo lipo katika mamlaka ya Kamisheni kufanya Uajiri. Pamoja na hoja hiyo, hoja ya Mdhibiti ni kuanzishwa kwa Kitengo cha Manunuzi, ambapo pamoja na ukweli kwamba Afisa Manunuzi ni muhimu sana katika uanzishwaji wa Kitengo, hoja ya Kamisheni ya kutoanzisha Kitengo hicho hadi watakapompata Afisa Manunuzi kutoka Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, hakikubaliki.

Maoni ya Kamati:

Kamati imeitaka Kamisheni ya Utalii ifanye uajiri wa Afisa Manunuzi ili aweze kuisaidia katika utekelezaji wa majukumu ya Kamisheni. Aidha, Kamati inaitaka Kamisheni kuanzisha mara moja Kitengo cha Manunuzi, ili manunuzi na ugavi wa Kamisheni uweze kufanywa kwa mujibu wa Sheria.

Kamati inasisitiza kwamba, kitendo cha kutounda Kitengo cha Manunuzi ni kosa kwa mujibu wa Sheria Namba 9 ya mwaka 2005, kifungu cha 14. Na iwapo baada ya miezi sita tokea kuwasilishwa kwa ripoti hii, Afisa Mhasibu wa Kamisheni ya Utalii ameshindwa kuunda Kitengo cha Manunuzi, Kamati inaiagiza Serikali kumchukulia hatua za kinidhamu Afisa huyo Mhasibu kwa kukiuka Sheria.

Hoja Namba 4.2 Kuhusu Kukosekana kwa daftari la kuhifadhia mali za Kudumu.

Ukaguzi umebaini kwamba, Kamisheni ya Utalii haiweki daftari la kuhifadhia mali za kudumu. Hali hiyo inapingana na kifungu cha 264 cha Kanuni za Fedha, 2005, na hali hii inaweza kusababisha upotevu wa mali hizo

Maelezo ya Kamisheni ya Utalii:

Ni kweli wakati wa ukaguzi hakukuwa na daftari hilo na badala yake Kamisheni ya Utalii ilirikodi taarifa za mali zake za kudumu katika Madaftari ya Ghalani (Store Ledgers). Hata hivyo, hivi sasa tayari Kamisheni wameshaanzisha daftari hilo.

Maelezo ya Kamati:

Pamoja na majibu ya Kamisheni, Kamati haioni daftari hilo kuwa limeandaliwa ipasavyo. Kwanza halijafuata taratibu na muongozo wa Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, na hivyo, Kamati haikufurahishwa na hatua hiyo.

Maoni ya Kamati:

Kamati inawaagiza Kamisheni ya Utalii kuhakikisha daftari hilo linaanzishwa mara moja ili kukidhi haja na matakwa ya Sheria.

Hoja Namba 4.3 Kuhusu Udhibiti na utunzaji wa mali za Kamisheni ya Utalii.

Kaisheni ya Utalii pamoja na kumiliki mali nyingi, haina udhibiti mzuri wa mali zake, ikiwa ni pamoja na kukosa matengenezo kwa muda husika. Hali ambayo pia inapelekea Kamisheni kuingia katika hasara kubwa ya matengenezo ya mali zake na hatimae hushindwa kutoa huduma husika.

Maelezo ya Kamisheni:

Kwa kuwa Mdhibiti kaainisha kwa picha magari yaliyochakaa, ni vyema wakaeleza kwamba magari hayo tayari yameshachukuliwa ikiwa ni pamoja nagari namba SMZ 5066 imelazimika kuuzwa kwa idhini ya Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kupitia Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo kwa barua ya tarehe 17/10/2012 yenye kumbu kumbu namba WHUUM/F.10/1/VOL.IV/143, kwa Ndg. Maulid Fadhil Haji kwa thamani ya Tsh.700,000/. Malipo ya ununuzi wa gari hiyo yamefanyika kwa awamu mbili; awamu ya kwanza zililipwa Tsh.500,000 na awamu ya pili Tsh. 200,000.

Maelezo ya Kamati:

Kamati inafahamu kwamba, taratibu za uuzaji wa mali za Serikali hufanywa zaidi kimazoea, kuliko kisheria ambapo kwa mujibu wa Kanuni za Sheria Namba 9 ya mwaka 2005, lazima Bodi

ya Zabuni baada ya kupokea vifaa vinavyotakiwa kuuzwa kutoka kwa Kitengo cha Manunuzi, ni hatua muhimu ambayo mara chache hufuatwa na Taasisi za Serikali.

Maoni ya Kamati:

Kamati inaitaka Serikali kuachana na uuzaji huu wa kimazoea, na badala yake sheria ifuatwe. Aidha, Kamati inaitaka Serikali kuhakikisha inawapatia gari Kamisheni ya Utalii kwa ajili ya shughuli zao za doria na Kiutawala.

3.1.4 SHIRIKA LA UTALII:

Hoja Namba 5.1 Kuhusiana na Kukosekana kwa Mpango wa Manunuzi

Ukaguzi umebaini kwamba, Shirika la Utalii haliandai Mpango wa Manunuzi, kitendo kinachokiuka kifungu cha 19 cha Sheria namba 9 ya mwaka 2005.

Maelezo ya Shirika.

Shirika limekiri kwamba mpango huo haupo kwani kwa sasa shughuli za manunuzi na hesabu zote zinafanywa chini ya usimamizi wa Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo hivyo wao ni watumiaji tu ila anaepanga na kununua ni Ofisa kutoka Wizara.

Maelezo ya Kamati:

Kitendo cha Wizara kuisimamia Shirika, kama vile ilivyokuwa kwa Wizara ya Biashara, Viwanda na Msoko, kabla Shirika hili kuhamishiwa kwa Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo kinachukuliwa kwa hadhari kubwa na Kamati hii, ikizingatiwa kwamba, tayari imeshaeleza sana miaka ya nyuma, namna Shirika hili lilivyochukuliwa mali zake kwa mgongo wa Viongozi wa Wizara hiyo.

Inapokuwa mpaka leo, khatma ya Shirika hili haijajuulikana, Kamati inaendelea kuona kwamba jambo hilo linaweza tena kusababisha matumizi mabaya ya fedha na Mali za Shirika, basi kama Shirika halina uwezo wa kujisimamia wenyewe basi hakuna sababu ya uwepo wake.

Maoni ya Kamati:

Serikali iharakishe mabadiliko inayoyafanya kwa Shirika hili. Kitendo cha kuwepo kwake lakini shughuli zote zinasimamiwa na Wizara, hakikubaliki na huenda kikapelekea madhara mengi ikiwa ni pamoja na utumiaji mbaya wa jina la Shirika na mali zake kwa manufaa ya wachache.

Vile vile Shirika kutokuwa na Bodi ya Wakurugenzi kwa muda mrefu, sio tu kunaidhoofisha Shirika, lakini pia madhumuni ya kuanzishwa kwake. Kwa hivyo, Kamati inaitaka Serikali, ifanye haraka kuunda Bodi mpya ya Shirika hili.

Hoja Namba 5.2 Kuhusu Kukosekana kwa daftari la kuhifadhia Mali za Kudumu.

Ukaguzi umebaini kwamba, Shirika la Utalii haliweki daftari la kuhifadhia mali zake za kudumu, kinyume na matakwa ya kifungu cha 264 cha Kanuni za Fedha za mwaka 2005.

Maelezo ya Shirika.

Shirika limekiri kwamba daftari hilo halipo na hivi sasa ndio Shirika kwa kushirikiana na Wizara linaandaa huo utaratibu wa kuwepo kwa daftari hilo.

Maelezo ya Kamati :

Kwa ujumla, Kamati imeshazoea kupokea majibu hayo hayo tokea mika ya nyuma. Kitendo cha Shirika la Utalii kuwa chini ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo,imekuwa kama kisingizio cha kila majukumu yake kusimamiwa na Wizara, wakati hili ni Shirika linalojitegemea.

Maoni ya Kamati

Kamati haikuridhishwa na majibu ya hoja hiyo, na itabaki hadi hapo Mdhibiti na Mkaguzi atakapothibitisha kuwepo kwa daftari hilo. Huku ikiliagiza Shirika kuharakisha daftari hilo.

Hoja Namba 5.3 Kuhusiana na Udhibiti na Utunzaji wa Mali za Shirika:

Ukaguzi umebaini kwamba, Shirika la Utalii limekosa udhibiti wa mali zake pamoja na kumiliki mali nyingi. Hsli hii pia inajumuisha kwa Shirika kutokuwa na utanzaji mzuri, kutofanya matengenezo kwa mali hizo ndani ya muda husika na takriban kutokuwepo kwa usimamizi unaoridhisha. Hali ambayo pia inapelekea Shirika kuingia katika hasara kubwa ya matengenezo ya mali zake na hatimae hushindwa kutoa huduma husika.

Maelezo ya Shirika.

Shirika limekiri juu ya kuwepo kwa magari ambayo hayakuwa katika hali nzuri kutokana na uchakavu wake na kutofanyiwa matengnezo ya kila baada ya muda mfupi. Hata hivyo magari hayo yameshauzwa kwa mujibu wa Sheria

Maoni ya Kamati.

Ili Shirika liweze kwenda vyema kibiashara basi ni vyema kutunza nyenzo zake ambapo magari ndio nyenzo kuu. Zilizo mbovu zote ziuzwe na zitafutwe nyengine mpya.

Hoja Namba 5.4 Kuhusiana na Kukosekana kwa Hatimiliki za Majengo ya Shirika.

Ukaguzi umebaini kwamba, Shirika linamiliki majengo mbali mbali, lakini hati miliki za majengo hayo hazikupatikana kwa ukaguzi, hali inayoshindwa kuthibitisha uhalali wa umiliki huo.

Maelezo ya Shirika.

Shirika linazo hatimiliki za Majengo yake na ziliwasilishwa mbele ya Kamati.

Maelezo ya Kamati.

Kamati imekabidhiwa hati hizo na kuzipitia..

Maoni ya Kamati.

Ni vyema watendaji washirikiane vyema na Mkaguzi kwani hakuna sababu kwanini Mkaguzi katika ukaguzi asipewe hatimiliki na zisionekane hadi inapotembelea Kamati Mkaguzi awe anapewa taarifa zote anazozihitaji zinazohusiana na mapato na matumizi ili aweze kujiridhisha na uhalali wa matumizi na mapato ya Serikali. Hivyo basi, Kamati inapendekeza hoja hii ifutwe.

Hoja Namba 5.5 Kuhusu Mapungufu katika Mikataba ya Ukodishwaji wa Majengo ya Shirika.

Ukaguzi umebaini kwamba, Shirika la Utalii limefunga mikataba na baadhi ya wawekezaji kwa kutoa huduma za Hoteli na Utalii. Katika mwaka 2009/2010, Shirika lilitegemea kukusanya jumla ya Tsh. 9,360,000 na USD 2400 kutoka kwa wawekezaji wa nyumba za Shirika ziliopo Bwejuu, Makunduchi juu na Makunduchi chini. Tatizo ni mapato halisi yaliyokusanywa ni Tsh. 2,340,000 tu. Hali hii inatokana na usimamizi mbaya wa ukusanyaji wa mapato

Maelezo ya Shirika.

Shirika limekiri kwamba kulikuwa na matatizo kidogo katika ukodishwaji wa baadhi ya majengo, hata hivyo kwa sasa limeanza mpango/utaratibu wa kuhakikisha kwamba wale wote waliokodishwa basi mikataba iwe inafanyiwa marejeo na wawe wanalipa kwa wakati.

Aidha nyumba za Jambiani na Makunduchi hazijakodishwa na kwa upande wa Hoteli ya Wete, na Mkoani nazo baada ya marejeo ya mkataba kwa sasa hazijakodishwa kwa mtu yoyote.

Maoni ya Kamati

Shirika kubaki na majengo ambayo haliyafanyii kazi ni hasara. Hivyo nyumba ambazo hazina mpangaji au mtu aliyekodi, zifanyiwe maarifa ya kutafuta mtu atakaekodi au Shirika lenyewe lizifanyie biashara.

3.1.5 CHUO CHA MAENDELEO YA UTALII:

Hoja Namba 6.1 Kuhusiana na Kukosekana kwa Kitengo cha Manunuzi.

Ukaguzi umebaini kwamba, Chuo cha Maendeleo ya Utalii hakikuunda Kitengo cha Manunuzi, kinyume na kifungu cha 14 cha Sheria namba 9 ya mwaka 2005. Aidha, hali hiyo hupelekea kutokuwepo kwa mpango madhubuti wa manunuzi na hatimae kununuliwa bidhaa zisizohitajika na katika wakati usiostahiki.

Maelezo ya Chuo.

Chuo kimekiri kuwa hakikuwa na Kitengo cha manunuzi kwa wakati huo kwani hakukuwa na mfanyakazi mwenye sifa na tayari kimetuma maombi ya kumpata mfanyakazi mwenye sifa.

Maelezo ya Kamati

Pamoja na kwamba Kamati imeonyeshwa barua yenye kumbukumbu Nam. AB.80/234/01/62 ya Tarehe 31/10/2012 inayohusu suala la hatua ya uajiri na mfanyakazi wa kuanzisha Kitengo hicho cha Manunuzi, lakini ilitaka kujua ni kwanini muda wote huo ununuzi unafanyika wakati Hoja ya Mdhibiti ni ya mwaka 2009/2010 na hata Kamati ilipotembelea tarehe 15/11/2012, Bado Chuo cha Utalii hakijaandaa Kitengo hicho.

Maoni ya Kamati:

Kamati inakiagiza Chuo cha Maendeleo ya Utalii kiache mara moja kufanya manunuzi kinyume na sheria, na badala yake kianzishe Kitengo cha Manunuzi haraka sana. Aidha, Kamati inaukumbusha Uongozi wa Chuo cha Maendeleo ya Utalii kwamba, kitendo wanachokifanya sasa ni kukiuka Sheria ya Manunuzi na Ugavi wa Mali za Seriakali (Namba 9 ya mwaka 2005), kifungu cha 14. Na Kamati inatoa miezi sita (6) tokea kuwasilishwa kwa ripoti hii, kuchukuliwa hatua za kinidhamu kwa Afisa Mhasibu wa Chuo cha Maendeleo ya Utalii, iwapo atashindwa kuanzisha Kitengo cha Manunuzi baada ya kumalizika muda huo (miezi 6).

Hoja Nam. 6.2 Kukosekana kwa Daftari la Kuhifadhia Mali za Kudumu.

Ukaguzi umebaini kwamba Chuo cha Maendeleo ya Utalii hakina daftari la kuhifadhia mali za kudumu, hii ni kwenda kinyume na kifungu cha 264 cha Kanuni za fedha za mwaka 2005. Pia hali hii husababisha upotevu wa mali hizo.

Maelezo ya Chuo

Chuo kimekiri kutokuwepo kwa Daftari hilo wakati Mkaguzi anakagua mahesabu, lakini kwa sasa daftari hili tayari limeshaandaliwa na limeanza kutumika mwezi Januari, 2011.

Maelezo ya Kamati

Pamoja na kwamba kwa sasa Daftari la kuhifadhia mali za kudumu lipo lakini mfumo/muundo wake unatofautiana na ule ulioelekezwa na Serikali kupitia Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, ingawaje taarifa zipo na zinaeleweka.

Maoni ya Kamati:

Kamati inakiagiza Chuo kuhakikisha taarifa hizo zinawekwa na kuhifadhiwa kwa mujibu wa muongozo uliotolewa na Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo.

Hoja Namba. 6.3 Kuhusu Udhibiti na Utunzaji wa Mali za Chuo cha Maendeleo ya Utalii.

Ukaguzi umebaini kwamba, Chuo cha Maendeleo ya Utalii kimekosa udhibiti wa mali zake pamoja na kumiliki mali nyingi. Hali hii pia inajumuisha kwa Chuo hiki kutokuwa na utanzaji mzuri, kutofanya matengenezo kwa mali hizo ndani ya muda husika na takriban kutokuwepo kwa usimamizi unaoridhisha. Hali ambayo pia inapelekea Chuo kuingia katika hasara kubwa ya matengenezo ya mali zake na hatimae hushindwa kutoa huduma husika.

Maelezo ya Chuo

Chuo kimekiri kwamba ni kweli wakati Mkaguzi hakikuwa na udhibiti mzuri wa mali zake. Ukaguzi ulipobaini kwamba kompyuta 7 zimeharibika ni sahihi na hali hii inatokana na ukweli kwamba kompyuta hizo ni kwa ajili ya kufundishia na wanafunzi huzitumia kwa mafunzo yao ya vitendo huku zikiwa rahisi kupoteza umadhubuti wake kwa haraka.

Maelezo ya Kamati:

Kamati hairidhishwi na sababu iliyotolewa kwamba ndio ikifanye Chuo kijibweteke kwa kisingizio tu kwamba, wanafunzi ndio wanaotumia kompyuta hizo. Aidha, suala la utunzaji wa mali za Chuo ni jukumu la Chuo chenyewe.

Maoni ya Kamati :

Kamati inakitaka Chuo cha Maendeleo ya Utalii kuhakikisha kwamba inafanya matunzo na uhifadhi mkubwa wa mali zake.

Hoja Namba 6.4 Kukosekana kwa Hati Miliki za Chuo cha Maendeleo ya Utalii.

Ukaguzi umebaini kwamba, Chuo cha Maendeleo ya Utalii kinamiliki jengo na kiwanja, lakini hati miliki wa mali hizo hazikupatikana kwa ukaguzi. Sala hili linashindwa kuthibitisha uhalali wa umiliki huo.

Maelezo ya Chuo :

Hadi sasa Chuo kinamiliki hati inayoitwa ‘Right of Occupancy’ ambayo inafafanua uhalali wa umiliki wa maeneo ya Chuo. Hata hivyo, Chuo cha Maendeleo ya Utalii kimefanya mawasiliano na Idara husika kwa kupata hati miliki ya majengo.

Maelezo ya Kamati :

Pamoja na watu wengi na Taasisi nyingi za Serikali kufahamu kwamba, ‘Right of Occupancy’ ndio hati miliki husika, ufahamu huo sio sahihi mpaka Taasisi hiyo itakapopata hati miliki husika.

Maoni ya Kamati :

Kamati imekitaka Chuo kiharakishe upatikanaji wa hati miliki ya majengo na kiwanja chake haraka iwezekanavyo.

3.2 WIZARA YA BIASHARA, VIWANDA NA MASOKO.

Hoja Namba 7.1 Kuhusu Kukosekana kwa Mpango wa Manunuzi:

Wizara haikuwa na Mpango wa Manunuzi kwa mwaka wa 2009/2010, na hivyo matumizi ya fedha zake hayakufuata mpango huo, bila ya kujali maelekezo ya kifungu cha 19 cha Sheria Namba 9 ya mwaka 2005,

Hoja Namba 7.2 Kuhusu Kukosekana kwa thamani za mali za Kudumu.

Ukaguzi umebaini kwamba baadhi ya mali za kudumu za Wizara hazikuwekewa thamani, hali iliyozuia kupatikana kwa sura halisi ya hesabu hizo na ni kukiuka matakwa ya Sheria ya Fedha ya mwaka 2005, kifungu cha 24(2(e).

Hoja Namba 7.3 Kuhusu Mali za Kudumu ambazo hazikuingizwa katika daftari la kuhifadhia mali.

Ukaguzi umebaini kwamba baadhi ya mali za kudumu za Wizara hazikuingizwa katika daftari la kuhifadhia mali. Hali hii ni kwenda kinyume na kanuni za Sheria ya fedha ya mwaka 2005, kifungu cha 264.

Hoja Namba 7.4 Kuhusu kukosekana kwa Hati miliki za mali za Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko.

Ukaguzi umebaini kwamba, Wizara inamiliki majengo, mashamba na vyombo vya moto lakini haina hati za umiliki wa mali hizo, suala ambalo linashindwa kuthibitisha uhalali wa umiliki huo.

Hoja Namba 7.5 Kuhusu Kukosekana kwa Kitengo cha Manunuzi.

Ukaguzi wa Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu umebini kwamba, Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko haikuunda Kitengo cha Manunuzi. Hali hii inapingana na sheria Namba 9 ya mwaka 2005, kifungu cha 14. Huku hali hiyo hupelekea kutokuwepo kwa mpango madhubuti wa manunuzi na hatimae kununuliwa kwa bidhaa zisizohitajika na katika wakati usiostahiki.

Hoja Namba 7.6 Kuhusu Udhibiti na Utunzaji wa mali za Wizara.

Ukaguzi umebaini kwamba, udhibiti na utunzaji wa baadhi ya mali za Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko hauridhishi. Hali hii imetokana na kutokuwepo kwa utunzaji mzuri, kutofanyiwa matengenezo kwa muda husika na kuwepo kwa usimamizi usioridhisha. Hali hii imepekea Wizara kuingia katika gharama kubwa ya utunzaji na utengenezaji wa mali hizo na hatimae kushindwa kutoa huduma husika.

Maelezo ya Kamati:

Katibu Mkuu wa Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko (Ndg Julian B. Rafaeli), hakuwa tayari kutoa mashirikiano na kukubali Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali kufanya kazi katika Wizara yake. Hali hii imejitokeza baada ya Kamati kuandaa ratiba ya kazi na kuwapelekea Wizarani pamoja na Taasisi nyengine, na siku ya kuthbitisha ratiba, Katibu Mkuu alihuduhuria mbele ya Kamati na kukubali Kamati ifanye kazi katika Wizara yake, tarehe 20/9/2012.

Hata hivyo, Katibu Mkuu hakuweza kutoa mashirikiano kwa Kamati siku ya kazi ilipowadia, kwa hoja ya kwamba Wizara yake inafanya kazi na Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo kwa siku hiyo, huku ikizingatiwa kwamba, ratiba ya pamoja na Taasisi zote za Serikali zilizohusika na kazi ya Kamati ya P.A.C ilithibitishwa saa 5 Asubuhi, na Katibu Mkuu pamoja na watendaji wake walihudhuria katika kikao hicho, huku ratiba ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo ilithibitisha ratiba yake saa 3:00 Asubuhi. Kwa maana hii hakuwa na sababu ya kuzikutanisha Kamati mbili za Baraza wakati mmoja, wakati haiwezekani kwa Kamati mbili kufanya kazi kwa Taasisi moja, wakati watendaji muhimu ni hao hao (hawataweza kujigawa).

Maoni ya Kamati:

Kamati haikuridhishwa na kitendo alichokifanya Katibu Mkuu wa Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko na kinaonesha dharau ya hali ya juu kwa Kamati za Baraza la Wawakilishi inayofanywa na Watendaji wa Serikali. Kamati inaitaka Mamlaka husika, kumchukulia hatua za kinidhamu Mtendaji huyu kwa kuidharau Kamati, ambacho ni sawa na kulidharau Baraza la Wawakilishi.

3.2.1 WIZARA YA BIASHARA, VIWANDA NA MASOKO, PEMBA:

Pamoja na kukataa kwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Biashara, Viwanda na Msoko, (Unguja) kufanya kazi na Kamati kama tulivyoeleza hapo juu, kwa Upande wa Wizara hii, Pemba Kamati imepata mashirikiano ipasavyo na kuweza kufanya kazi. Kwa ujumla Kamati imefanya uchunguzi wa Hoja hizo hizo ambazo pia zinatakiwa zihojiwe Unguja, na ufafanuzi wa hoja hizo ni kama ifuatavyo:

Hoja Namba 7.1 Kuhusu Kukosekana kwa mpango wa manunuzi (Pemba).

Wizara haikuwa na Mpango wa Manunuzi kwa mwaka wa 2009/2010, na hivyo matumizi ya fedha zake hayakufuata mpango huo, bila ya kujali maelekezo ya kifungu cha 19 cha Sheria Namba 9 ya mwaka 2005.

Maelezo ya Wizara (Pemba):

Ni kweli wakati wa ukaguzi, Wizara haikuwa na Mapango wa Manunuzi, kwa sababu hapo awali ulikuewpo kwa Wizara nzima ingawaje baada ya kukaa na Afisi ya Mdhibiti na kupata maelekezo, ndipo Wizara hii kwa upande wa Pemba chini ya Afisa Mdhamini, walifanya marekebisho kwa kuanzisha mpango wa Manunuzi kama wanavyotakiwa na Sheria.

Maelezo ya Kamati:

Pamoja na juhudi zao za kuanzisha mpango huo wa manunuzi, Kamati imepata wasi wasi wa utekelezaji wa majukumu ya Kitengo cha Manunuzi ambacho bado hakina mtaalamu wa fani hiyo, yaani, Afisa Manunuzi. Ilielezwa kwamba, Wizara ina tatizo la ajira kwa ujumla na walipoomba hatimae waliruhusiwa kuajiri wafanyakazi watatu pekee, lakini kati ya hao hamna Afisa Manunuzi.

Kamati ilihitaji kujiridhisha kwa kupewa barua inayothibitisha kwamba, Wizara hii iliomba nafasi za ajira ikiwa ni pamoja na Afisa Manunuzi, lakini linaloipa wasi wasi zaidi ni uwezekano wa kuwa na Mpango wa Manunuzi wakati mwenye ujuzi huo hajaajiriwa na Wizara.

Maoni ya Kamati:

Kwa ujumla Kamati pamoja na kuelezwa kuanzishwa kwa Mpango wa Manunuzi, Kamati haijaridhika na mpango huo na inaelekeza haja ya kuajiriwa kwa Afisa Manunuzi, ili aweze kuwasaidia namna gani ya utayarishaji bora wa mpango huo, hii isifahamike kwamba, Wizara haina jukumu hilo hadi hapo atakapoajiriwa Mhusika, lakini Kamati inaona vyema huyo aliyepo akapewa mafunzo haya na hatua nyengine zichukuliwe, ilimradi tu Mpango wa Manunuzi uliokamilika, uweze kuandaliwa.

Hoja Namba 7.2 Kuhusu Kukosekana kwa thamani za mali za Kudumu (Pemba).

Ukaguzi umebaini kwamba baadhi ya mali za kudumu za Wizara hazikuwekewa thamani, hali iliyozuia kupatikana kwa sura halisi ya hesabu hizo na ni kukiuka matakwa ya Sheria ya Fedha ya mwaka 2005, kifungu cha 24(2(e).

Maelezo ya Wizara:

Ni kweli wakati ukaguzi unafanyika, thamani halisi za mali za kudumu hazikuwekwa katika mali hizo, lakini Wizara iliwasiliana na Wizara ya Ardhi kwa ajili ya kufanyiwa tathmini na hatimae maombi hayo wameshayakabidhi kwa Katibu Mkuu wa Wizara hii ya Ardhi.

Maelezo ya Kamati:

Kamati haina pingamizi ya kufanya mawasiliano na Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati kwa jili ya kutiliwa thamani ya mali husika, ingawa ina wasi wasi mkubwa wa kuwezekana kwa jambo hili kwa ufanisi na haraka. Hii haimaanishi kwamba Wizara haina uwezo, isipokuwa urasimu uliokuwepo Wizarani hapo ikitiliwa mfano hata kwa hati miliki zinavuyokosekana kwa Taasisi za Serikali. Aidha, Wizara yenyewe pia ina tatizo hilo hilo la thamani halisi ya mali zake.

Maoni ya Kamati:

Kamati inaitaka Wizara kutoendelea kusubiri kutiliwa thamani hiyo kutoka Wizara ya Ardhi, Makaazi,Maji na Nishati, lakini inapaswa kuwa karibu na Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kwa kutarajiwa katika Wizara zitakazofanyiwa tathmini na Mshauri Mwelekezi aliyeajiriwa wa kazi hiyo.

Hoja Namba 7.3 Kuhusu Mali za Kudumu ambazo hazikuingizwa katika daftari la kuhifadhia mali (Pemba).

Ukaguzi umebaini kwamba baadhi ya mali za kudumu za Wizara hazikuingizwa katika daftari la kuhifadhia mali. Hali hii ni kwenda kinyume na kanuni za Sheria ya fedha ya mwaka 2005, kifungu cha 264.

Maelezo ya Wizara:

Kuhusiana na gari ya SMZ 6321 (T.L) tayari imeshauzwa isipokuwa kwa upande wa Vespa zenye SMZ 5889 na SMZ 5888, tayari taarifa zake zimeshaingizwa katika daftari la kuhifadhia mali.

Maelezo ya Kamati:

Kamati imelipita daftari hilo kwa ajili ya kujiridhisha namna uingizaji huo ulivyofanyika. Kuhusiana na gari iliyouzwa, Kamati inaendelea haja ya kufuatwa ipasavyo taratibu za uuzaji kama zilivyo katiak kifngu cha 175 cha Kanuni za Sheria ya Manunuzi, na isiwe kama hali ilivyo hivi sasa kwamba, ridhaa moja kwa moja inatafutwa kwa Ofisi ya Rais, Fedha,Uchumi na

Mipango ya Maendeleo, huku Bodi ya Zabuni, Kitengo cha Manunuzi na Kitengo cha Watumiaji wakawa hawana taarifa zozote.

Maoni ya Kamati:

Kamati inaitaka Wizara kuhakikisha suala la kuingiza taarifa za mali za kudumu katika daftari la kuhifadhia mali linafanyika, mara tu zinaponunuliwa mali hizo.

Hoja Namba 7.4 Kuhusu kukosekana kwa Hati miliki za mali za Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko (Pemba).

Ukaguzi umebaini kwamba, Wizara inamiliki majengo, mashamba na vyombo vya moto lakini haina hati za umiliki wa mali hizo, suala ambalo linashindwa kuthibitisha uhalali wa umiliki huo.

Maelezo ya Wizara.

Ni kweli hati miliki zimekosakana wakati wa ukaguzi, na pia hata wakati wa Kazi za Kamati zimeshindwa kupatikana. Kwa ujumla Wizara imewasiliana na Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati, ingawaje bado hawajafanikiwa na matokeo yake wanaiomba Kamati iwasaidie kupatikana kwa hati miliki hizo.

Maelezo ya Kamati:

Kamati inaendelea kushangazwa na urasimu wa kupatikana kwa hati miliki kwa Taasisi za Serikali, huku watu binafsi na wafanya biashara hupatiwa hati hizo mara moja. Kamati inaamini suala hili linahitaji msukumo wa ziada mbali na huu unaofanyika kila siku.

Maoni ya Kamati:

Kamati inaitaka Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati kuacha urasimu na inatakiwa izipe kipaumbele Taasisi za Serikali kwa kuwapatia hati miliki, kwani hujitahidi sana kufuata taratibu zilizowekwa.

Hoja Namba 7.5 Kuhusu Kukosekana kwa Kitengo cha Manunuzi (Pemba).

Ukaguzi wa Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu umebini kwamba, Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko haikuunda Kitengo cha Manunuzi. Hali hii inapingana na sheria Namba 9 ya mwaka 2005, kifungu cha 14. Huku hali hiyo hupelekea kutokuwepo kwa mpango madhubuti wa manunuzi na hatimae kununuliwa kwa bidhaa zisizohitajika na katika wakati usiostahiki.

Maelezo ya Wizara:

Kitengo cha Manunuzi kwa mujibu wa Sheria huundwa na Mkuu wa Kitengo hicho ambae mwenye sifa za fani ya Ununuzi na Ugavi. Kwa kuwa Wizara haina Afisa huyo, bado haijaweza kuwa na Kitengo cha Manunuzi.

Maelezo ya Kamati:

Kamati inaendelea kusisitiza haja ya kuwepo kwa Afisa Manunuzi, ambae atasaidia sana kuanzishwa na kufanya kazi kwa Kitengo cha Manunuzi. Suala hili liposhindikana kwa njia ya Uajiri, ni vyema Wizara ikafikiria haja ya kuwasomesha Maofisa wake, ili waweze kuwa na sifa zinazohitajika.

Maoni ya Kamati:

Kamati inaitaka Wizara kuanzisha mara moja Kitengo cha Manunuzi.

Hoja Namba 7.6 Kuhusu Udhibiti na Utunzaji wa mali za Wizara (Pemba).

Ukaguzi umebaini kwamba, udhibiti na utunzaji wa baadhi ya mali za Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko hauridhishi. Hali hii imetokana na kutokuwepo kwa utunzaji mzuri, kutofanyiwa matengenezo kwa muda husika na kuwepo kwa usimamizi usioridhisha. Hali hii imepekea Wizara kuingia katika gharama kubwa ya utunzaji na utengenezaji wa mali hizo na hatimae kushindwa kutoa huduma husika.

Maelezo ya Wizara:

Wizara inaendelea kuzifanyia ukarabati mali zake, ikiwa ni pamoja na maghala inayoyamiliki. Changamoto kubwa inayoikabili Wizara ni ukubwa wa gharama za matengenezo hayo. Kwa mfano kama utaangalia ghara za ghala la Kilimandege, linahitaji Tsh.100,788,000 wakati kodi yenyewe ni Tsh.25,000 kwa mwezi, tena kodi yenyewe ni ya miaka 10. Ghala la Kizimbani nalo linahitaji Tsh.93,620,000 kwa matengenezo.

Maelezo ya Kamati:

Kamati inahitaji sana kupatiwa ripoti kamili ya maghala ya Wizara hii. Hii itasaidia kuipa uwezo mpana wa kuyafanyia kazi katika siku zijazo.

Maoni ya Kamati:

Wizara iendelee kutunza mali zake ikiwa ni pamoja na kuzifanyia matengenezo makubwa zile zote zilizoharibika. Aidha, Kamati bado inahitaji muda wa ziada kufuatilia suala la maghala ya Wizara.

3.4 WIZARA YA USTAWI WA JAMII, MAENDELEO YA VIJANA, WANAWAKE NA WATOTO:

Hoja. Nam. 8.1 inahusu Kukosekana kwa Mpango wa Manunuzi:

Bila ya kujali maelekezo ya kifungu cha 19 cha Sheria Namba 9 ya mwaka 2005, Wizara haikuwa na Mpango wa Manunuzi kwa mwaka wa 2009/2010, na hivyo matumizi ya fedha zake hayakufuata mpango huo.

Maelezo ya Wizara kuhusiana na Hoja:

Ni kweli kwa mwaka 2009/2010 Wizara hakuwa na Mpango huo wa Manunuzi, nah ii ilitokana na kutokuwepo utaratibu wa kufuatwa na zaidi baada ya Wizara hii kugawanywa; masuala ya Manunuzi kwa mujibu wa Sheria Namba 9 ya mwaka 2005 na Kanuni zake, ni mapya na ufahamikaji wake unachukua muda; aidha, hawakuwa na Ofisa wa Manunuzi aliesomea masuala hayo. Hata hivyo, kwa mwaka 2011/2012, Wizara ilikwishaandaa Mpango wa Manunuzi kama ilivyotakiwa.

Maelezo ya Kamati:

Kamati haijakubaliana na usahihi wa Mpango wa Manunuzi uliowasilishwa kwa kukosa ufafanuzi wa matumizi; manunuzi wala uhaulishaji, huku vifungu vya matumizi ya fedha zilizoainishwa havijafafanuliwa. Kamati pia haijakubaliana na hoja za Wizara kwamba, masuala ya Manunuzi ni mapya na hoja nyengine zinazowiyana, kwa kuzingatia kwamba, Sheria inayohusika imetungwa tokea 2005, na kabla yake pia kulikuwa na Sheria iliyohusika ya mwaka 2002. Aidha, Wizara hii bado mpaka leo haina Kitengo cha Manunuzi, na wana Afisa mmoja tu wa Manunuzi.

Maoni ya Kamati:

Kamati imeitaka Wizara kuanzisha Kitengo cha Manunuzi bila ya kusahamu Mpango wa Manunuzi kama Sheria ya Manunuzi ya mwaka 2005, inavyoelekeza. Ifahamike tu kwamba, kitendo cha kutokuwa na Mpango wa Manunuzi ni kuvunja Sheria, kwa kukiuka masharti ya kifungu cha 19 cha Sheria Namba 9 ya mwaka 2005, na hivyo, Kamati inampa Afisa Mhasibu wa Wizara hii, miezi mitatu tu tokea kuwasilishwa kwa ripoti hii, awe ameshaandaa Mpango huo. Vyenginevyo, Serikali imchukulie hatua za kinidhamu kwa kukiuka sheria.

Hoja Nam. 8.2 inayohusu kukosekana kwa thamani za mali za kudumu:

Wizara haikuwa na Mpango wowote wa kutia thamani kwa baadhi ya mali zake, hali iliyozuia kupatikana kwa sura halisi ya mali za Wizara pia kukiuka matakwa ya Sheria ya Fedha ya mwaka 2005.

Maelezo ya Wizara kuhusiana na Hoja:

Wizara imekiri hali hiyo huku ikieleza kwamba, hivi sasa kuna Wizara 5 zipo katika ‘pilot’ ya kufanyiwa kazi hii ya tathmini ya mali zake na ikimaliza awamu hiyo, awamu itakayofuatia, pia itaihusisha Wizara hii.

Maelezo ya Kamati:

Maelezo hayo hayawezi kutegemewa kuwa ni hoja moja kwa moja, kwa kuzingatia ukweli kwamba, suala la kuzitambua mali husika, kuzitia thamani zile zinazofahamika thamani yake ni kazi ya Wizara. Aidha, Kamati pia ilipolikagua daftari linalohusika, imejiridhisha kwamba, halina taarifa kamili za mali za Wizara.

Maoni ya Kamati:

Kamati inaitaka Wizara kuharakisha zoezi hili la kutia thamani mali zake ikiwa ni pamoja na kujaza taarifa kamili za mali hizo katika Daftari la Mali za Wizara, huku Wataalamu wakiwa na kazi ya kuzitia thamani mali za Wizara ambazo tayari Wizara imeshazitambua.

Hoja Nam. 8.3 Kuhusiana na Udhibiti na Utunzaji wa Nyumba za Wazee, Sebleni.

Ukaguzi uliofanyika umebaini kwamba, udhibiti na utunzaji wa nyumba za wazee Sebleni hauridhishi. Hali hii imetokana na kutokuwepo wka utunzaji mzuri, kutofanyiwa matengenezo kwa muda husika na kuwepo kwa usimamizi usioridhisha.

Hali hii inapelekea Wizara kuingia katika gharama kubwa za utunzaji na utengenezaji wa mali hizo na hatimae kushindwa kutoa huduma husika.

Malezo ya Wizara:

Wizara imo katika jitihada za kuwaenzi wazee hao kwa kuweza kuimarisha maeneo yao ya makaazi. Wizara tayari imeshakarabati nyumba moja, ukumbi mkubwa, kujenga ukuta wa kuzunguukia eneo lote la nyumba za wazee (fance), vyoo kufanyiwa ukarabati, kujenga msikiti na kurekebisha mtandao wa maji kwa kuchimba kisima kipya na kujenga mnara wa kuwekewa matangi ya maji. Wizara itaendelea kuzifanyia matengenezo nyumba hizo kadiri ya upatikanaji wa fedha utakavyoruhusu.

Maelezo ya Kamati:

Kamati imepokea taarifa ya Wizara na haikutosheka isipokuwa kufanya ziara ya sehemu zilipo nyumba hizo za Wazee. Kamati imeshuhudia maelezo ya Wizara na kuridhishwa na utekelezaji wa hatua iliyofikia, ingawa bado kuna safari ndefu ya kuimarishwa kwa makaazi hayo.

Maoni ya Kamati:

Kamati inaipongeza Wizara kwa kufanya marekebisho ya nyumba za wazee na kuitaka Serikali kushirikiana na Wizara katika kuzitunza zaidi nyumba hizo pamoja na kuwapatia huduma kamili, wazee wanaoishi hapo.

Aidha, Kamati inapendekeza kwamba, sehemu ya holi liliopo katika nyumba hiyo iliyofanyiwa ukarabati, kuangaliwe uwezekano wa kukodishwa kwa shughuli za harusi na mikutano mbali mbali, ili fedha zitakazopatikana, moja kwa moja zirudi kuwanufaisha wazee hao.

Hoja Namba 8.4 Kuhusu Umiliki wa kiwanja katika kijiji cha Muungoni, Wilaya ya Kusini Unguja.

Ukaguzi umebaini kwamba, Wizara inamiliki kiwanja katika kijiji cha Muungoni, Wilaya ya Kusini Unguja kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha Vijana. Hadi ukaguzi unakamilika, kiwanja hicho bado hakijatumika kama ilivyokusudiwa. Aidha, ukaguzi umebaini kuna baadhi ya wananchi hawajalipwa malipo yao ya fidia kwa kuchukuliwa maeneo yao.

Maelezo ya Wizara:

Ujenzi wa awali ulikuwa ufadhiliwe na ILO, hata hivyo ILO walibadili muelekeo wa ujenzi wa vituo hivyo. Kwa upande wa Serikali ilielekeza kwamba, suala la ujenzi na umiliki wa vituo vya ujasiriamali vibakie chini ya udhibiti na usimamizi wa Wizara ya Elimu na Mfunzo ya Amali.

Kuhusu malipo ya fidia, kwa mujibu wa makubaliano na Uongozi wa Wilaya, wanaopaswa kulipwa fidia ni wale wenye vipando vya kudumu sio vipando vya muda, hivyo walilipwa kabla ya ujenzi.

Maelezo ya Kamati:

Pamoja na maelezo hayo, Kamati imeona jambo la msingi pia ni kupata hati miliki ya kiwanja hicho, ili ijiridhishe juu ya usahihi wa umiliki wake. Kwa bahati njema, Kamati ilipatiwa hati hizo na kujiridhisha. Kuhusiana na suala la kiwanja hicho sasa kisimamiwe na Wizara ya Elimu, Kamati haina tatizo nalo ilimradi tu lengo lililokusudiwa litekelezwe kwa haraka mno.

Maoni ya Kamati:

Kamati inaitaka Serikali kuharakisha Ujenzi wa Kituo cha Vijana, na suala hili sio lazima lisubiri wafadhili. Ni vyema tukatafuta fedha, kupita vyanzo vyetu vya ndani.

3.5 WIZARA YA ARDHI, MAKAAJI, MAJI NA NISHATI:

Hoja Namba 9.1 Kuhusu Kukosekana kwa Mpango wa Manunuzi:

Wizara haikuwa na Mpango wa Manunuzi kwa mwaka wa 2009/2010, na hivyo matumizi ya fedha zake hayakufuata mpango huo, bila ya kujali maelekezo ya kifungu cha 19 cha Sheria Namba 9 ya mwaka 2005.

Maelezo ya Wizara:

Mpango wa Manunuzi ulikuwepo tokea wakati wa Ukaguzi, ingawaje kutokana mazingira yaliyokuwepo, Mkaguri huyo hakuuona Mpango huo. Aidha, Wizara pia ilifanya mawasiliano na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu, kueleza kwamba, Wizara inao mpango huo na hoja hiyo ni vyema ikaondolewa katika kumbu kumbu zao.

Maelezo ya Kamati:

Kamati inahoji kwa nini wakati wa Mdhibiti Mpango huo usionekane wakati katika taratibu zake za ukaguzi, hufanya mikutano ya kuingia (Entry Meeting) kwa kuwajuulisha wahusika na mkutano wa kutoka (Exit Meeting). Hata hivyo, Kamai ilitaka ipatiwe ushahidi wa mpango huo pamoja na mawasiliano yaliyofanyika kwa Mdhibiti baada ya Wizara kujua kwamba, hoja hii ilikuwemo katiak ripoti zake. Kwa bahati njema ushahidi huo umeweza kupatikana.

Maoni ya Kamati:

Kamati inakiri kuewpo kwa mpango wa manunuzi, na inaitaka Wizara itekezele manunuzi yake kwa mujibu wa mpango huo. Aidha, Kamati inaitaka Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo. Kuandaa mfumo mmoja wa namna ya mpango wa manunuzi unavyotakiwa uandaliwe kwa kila Taasisi ya Serikali.

Hoja Namba 9.2 Kukosekana kwa Daftrati la kuhifadhia mali za kudumu.

Ukaguzi umebaini kwamba, Wizara haina daftari la kuhifadhia mali za kudumu. Huku ni kwenda kinyume na kifungu cha 264 cha kanuni za Fedha za mwaka 2005 na huweza kusababisha upotevu wa mali hizo.

Maelezo ya Wizara:

Daftari hilo la kuhifadhia mali za kudumu za Wizara lipo, ingawaje kwa muda lilichukuliwa na Idara ya Uhakiki Mali. Hata hivyo, Wizara inakabiliwa na tatizo la kutia thamani kwa mali zake za kudumu, suala ambalo inaamini Serikali imeanza kulitafutia ufumbuzi kwa kuteuliwa Mshauri Mwelekezi aliyeanza kuifanya kazi hiyo.

Maelezo ya Kamati:

Kamati imewasilishiwa baadhi ya sehemu ya daftari hilo na kushuhudia mapungufu mengi yaliyokuwemo. Yaani taarifa kamili za mali hizo hazijawekwa ipasvyo. Kwa mfano, baadhi ya gari hazina chasesi namba, suala ambalo halihitaji utaalamu mkubwa. Kwa ujumla daftari hilo sio kamili.

Maoni ya Kamati:

Kamati inaitaka Wizara kuliwasilisha daftari hilo kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, ili aweze kulipita na kuridhika nalo. Na kuitaka Wizara kuharakisha kutia kila taarifa inayotakiwa.

Hoja Namba 9.3 Kuhusu Uuzwaji wa Vyombo vya Moto kwa watumishi wa Idara ya Majenzi.

Ukaguzi umebaini kwamba, Idara imefanya mauzo ya baadhi ya vyombo vya moto kwa watumishi wake. Aidha, hadi unafanyika ukaguzi huo, vyombo vya moto hivyo havijabadilishwa namba za usajili kama taratibu zinavyoelekeza. Huku ikifahamika kwamba, kutosajili vyombo vya moto kunaikosesha Serikali mapato.

Maelezo ya Wizara:

Ni kweli wakati wa ukaguzi hali ilikuwa hivyo, igawaje sasa tayari Wizara imeshafanya marekebisho na tayari vyomvo hivyo vyote vimeshabadilishwa magamba ama namba za usajili kama utaratibu unavyotaka.

Maelezo ya Kamati:

Kamati pamoja na kupokea majibu hayo ilitaka ushahidi wa kupewa magamba ama namba hizo za usajili, aidha Kamati imetaka pia ipatiwe ushahidi wa barua ama mawasiliano ya hoja hii yalivyofanywa kwa hatua za marekebisho. Hata hivyo, ushahidi huo haukupatikana na Kamati inashindwa kuthibitisha maelezo hayo kuwa ni sahihi.

Maoni ya Kamati:

Kamati imetaka Wizara kuhakikisha ushahidi huo unawasilishwa kwa Kamati katika kazi zijazo. Aidha, kabla ya siku hiyo ya Kazi, Wizara iiandikie Afsi ya Mdhibiti kuhusu suala hili na Kamati ipatiwe nakla ya barua hizo.

Hoja Namba 9.4 Kuhusu Udhibiti na Utunzaji wa Mali za Wizara.

Ukaguzi umebaini kwamba, udhibiti na utunzaji wa baadhi ya mali za Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko hauridhishi. Hali hii imetokana na kutokuwepo kwa utunzaji mzuri, kutofanyiwa matengenezo kwa muda husika na kuwepo kwa usimamizi usioridhisha. Hali hii imepekea Wizara kuingia katika gharama kubwa ya utunzaji na utengenezaji wa mali hizo na hatimae kushindwa kutoa huduma husika.

Maelezo ya Wizara:

Kuhusu eneo la Maruhubi ambalo limeainishwa katika ripoti, ni kweli limevamiwa na wavuvi huku wavuvi hao wakisema kwamba hawataondoka. Aidha, pia kuna mgonano wa maslahi katika eneo hilo baina ya Wizara hii na Idara ya Nyaraka na Mambo ya Kale ambayo inasema eneo hilo lipo chini ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali. Aidha, Shirika la Bandari nalo lina minara yake na hata mpango wa ujenzi wa gati ya Mpiga Duri huenda ukaathiri eneo hilo.

Kuhusiana na kiwanda cha matofali kilichopo katika eneo hilo, kwanza ieleweke kwamba kiwanda hicho ni cha Wizara na tayari wameshakifanyia marengenezo ikiwa ni pamoja na kutoa paa. Hapo awali, kiwanda hicho kilikuwa hakifanyi kazi ingawaje sasa tayari

kimeshatengenezwa na kikawa kinafanya kazi kama kawaida, igawa sasa kwa bahati mbaya mashine pia imeharibika na kimerejea tena kutofanya kazi.

Kuhusiana na gari ya SMZ ilikuwa imechakaa wakati wa ukaguzi wa Mdhibiti na Mkaugiz Mkuu wa Hesabu, tayari imeshauzwa na Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, nao Wizara waliletewa barua tu kwamba ni taarifa ya kuuzwa kwake. Hata hivyo, alieuziwa ni mfanyakazi wa Idara ya Majenzi.

Katika suala zima la uchakavu wa Kiwanda cha upasuaji mbao kinachomilikiwa na Wizara kilichopo Jadida, kimekusudiwa kufanyiwa ukarabati mkubwa ambapo katika hatua ya mwanzo makisio yalikuwa ni Tshs. 200,000,000 kwa ujumla wake hata hivyo katika kuanza ukarabati huo kwa mwaka wa fedha wa 2011/2012 fedha iliyokubaliwa ni Tshs. 10 milioni hata hivyo fedha iliyopatikana ni Tshs. 4,000,000/-.Ambapo ziliwezesha kufanyia ukarabati mdogo tu.

Maelezo ya Kamati:

Kamati imetaka Wizara zaidi ijikite katika kutoa ufafanuzi wa mpango wao wa kulitunza eneo hilo na kuelezwa kwamba, wao wamejitahidi kuzitambua mali zilizopo katika vipindi vya muda mfupi, muda wa kati na muda mrefu. Hali hii inaonekana ni ya mabadiliko kutokana na hapo awali Wizara ilikuwa haizitambui mali zake.

Kuhusiana na kiwanda cha Matofali, Kamati imesikitishwa na taarifa kwamba, kiwanda hicho kimeharibika tena. Kwa hoja kama hii, suala zima la utunzaji na udhibiti wa mali za Wizara, linakuwa gumu kulithibitisha kwa Wizara hii kwamba, limechukuliwa hatua zipasazo.

Kamati inashangazwa na taarifa kwamba, Wizara ambayo inamiliki gari, iuzwe gari hiyo bila ya taarifa yao. Wakati taratibu za uuzaji lazima zianze kwa Wizara ama Taasisi husika, kupita vyombo vya Bodi ya Zabuni, Kitengo cha Manunuzi, Kitengo cha Watumiaji taratibu nyengine.

Kuhusu Kiwanda cha Upasuaji Mbao cha Jadida, Kamati ilielezwa kwamba kwa sasa kiwanda hicho kinaingiza kati Tshs. 70,000 na Tshs. 80,000 kwa mwezi. Hali hii iliipa wasiwasi mkubwa juu ya upoteaji wa rasilimali zilizopo pale. Hata hivyo Kamati imegundua kwamba utaratibu wao wa malipo kwa ajili ya huduma kiwandani hapo, siyo mzuri kwani malipo hufanyika Afisini mbali na huduma inatolewa kiwandani, katikati hapa panatokea tatizo ambalo husababisha pato liwe dogo kiasi hicho. Pamoja na kwamba madhumuni makubwa ya kuwepo kwa kiwanda hicho ni kuhudumia shughuli za Wizara katika kutoa huduma kwa vifaaa vya ujenzi lakini kitakapokuwa na huduma za kuendelea kutakiwa ni chanzo cha mapato ya Wizara.

Maoni ya Kamati:

Pamoja na maelezo ya Wizara, Kamati haikuridhishwa moja kwa moja na hatua zinazochukuliwa katika kutunza mali za Wizara. Aidha, pamoja na kuonekana kwa kiwanda cha matofali kilichopo hapo Maruhubi kuonekana kina faida kwa Wizara, Kamati itaitaka Wizara

kuangalia faida inayopatikana kama inainufaisha Wizara, kuliko hasara inayoingia kwa kukiendesha kiwanda hicho.

Kamati imesikitishwa kwa kukiukwa kwa taratibu za manunuzi na uuzaji wa mali za Serikali, na Kuitaka Serikali kuwa tayari kuisimamia sheria hiyo kwa maslahi ya wananchi wake.

Aidha, kuhusiana na kiwanda cha Jadida, Kamati inaitaka Wizara ifanye juhudi za makusudi za kukifufua kiwanda hicho ili kiweze kufanya kazi zake kwa ufanisi kwa kuweka mashine za kileo. Huku Karani wa hesabu kwa ajili ya malipo ya huduma zinazotolewa kiwandani hapo awepo hapo hapo kiwandani (Eneo la kazi) na Wizara pia ipate nafasi ya kuona kwamba kwa mujibu wa gharama za kuwa na kiwanda hapo basi lipi ni bora, kuendelea au kuachana nacho.

Hoja Namba 9.5 Kuhusu Mikataba ya Ukodishaji wa Nyumba za Idara ya Nyumba na Makaazi:

Ukaguzi umebaini kwamba, Idara ya Nyumba na Makaazi imefunga mikataba ya ukodishwaji wa nyumba za kuishi wananchi mbali mbali. Ukaguzi umebaini kwamba wengi wa wakodishwaji hao hawalipi kodi ipasavyo na baadhi yao wamekodisha kwa watu wengine kwa bei ya juu zaidi. Hali hii hupelekea kukosekana kwa mapato kwa Idara husika na Serikali kwa ujumla kutokana na usimamizi mbaya wa ukusanyaji wa mapato hayo.

Maelezo ya Idara na Wizara:

Ni kweli kuna changamoto kubwa ya ulipaji wa madeni ya nyumba kutoka kwa wakodishwaji. Na miongoni mwa changamoto zake ni baadhi ya wakodishwaji hao wameona hawastahiki kulipa kutoka na kupewa nyumba hizo na Mzee Karume, wengine wamewakodisha wapangaji wengine, huku Wizara na Idara inayohusika na usimamizi wa Nyumba hazina taarifa.

Maelezo ya Kamati:

Kamati haifahamu maelezo ya kila siku kwamba, eti Wizara inaendelea kusubiri ripoti ya kufuatilia nyumba hizo ambayo mpaka leo haijawasilishwa kwa Kamati, pamoja na kuelezwa kwamba imeshamalizika. Aidha, Kamati inasikitishwa na taarifa ya nyumba 2 zilizoko Mahakamani huku ukifikia mwaka wa 2, kesi haijaisha. Aidha, inaamini kwamba, Mkurugenzi wa Nyumba hafanyi ukaguzi yakinifu wa kuzikagua nyumba hizo na kufahamu ni ngapi zimekodishwa kwa watu wengine ama kuuzwa kabisa.

Maoni ya Kamati:

Hoja hii haipati majibu sahihi mpaka ripoti ilioyohusiana na uhakiki wa nyumba hizo itakapokabidhiwa kwa Kamati. Kamati kwa kutumia kifnugu cha 52(5)(b) cha Kanuni za Fedha, inapendekeza kufuatiliwa zaidi baada ya kupatikana ripoti hiyo (ya Kamati ya Mhe. Abdalla Mwinyi).

3.6 WIZARA YA KILIMO NA MALIASILI:

Hoja Namba 10.1. Kukosekana Kitengo cha Manunuzi:

Ukaguzi wa Afisi yaMdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu umebini kwamba, Wizara haina Kitengo cha Manunuzi. Hali hii inapingana na sheria Namba 9 ya mwaka 2005, kifungu cha 14.

Maelezo ya Wizara:

Ni kweli wakati wa ukaguzi hawakuwa na kitengo hicho, ingawaje sasa tayari wameshakiunda na kinafanya kazi. Kitengo hicho kina wajumbe 6 wakiongoziwa na Afis Manunuzi na wajubme watano wafuatao:

1. Ndg. Makame Mbarak Abdulrahman.
2. Ndg. Zubeda Malik Hassan
3. Ndg. Kaukab Ali Hassan.
4. Ndg. Moh'd Makame Kombo na
5. Ndg. Mwenezi O. Said.

Aidha, kwa upande wa Pemba, nako tayari Kitengo kimeshaanzishwa kikiwa na wajumbe watano, wakiongozwa na Afisa Manunuzi.

Maelezo ya Kamati:

Kamati imepokea taarifa ya kuundwa Kitengo cha Manunuzi na Wizara, na imejiridhisha kwa kwa kupata ushahidi wa uteuzi wa wajumbe hao.

Maoni ya Kamati:

Kamati imepongeza kuundwa Kitengo cha Manunuzi, na inaamini sasa majukumu yote yanayohusiana na kazi zao, yatatekelezwa ipasavyo, kinyume na ilivyokuwa awali.

Hoja Namba 10.2 Kuhusu Kukosekana kwa mpango wa manunuzi:

Ukaguzi wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu, umebaini kwamba, Wizara haifanyi mpango wa manunuzi na kufanya hivyo kunakiuka maelezo ya kifungu cha 19 cha Sheria ya Manunuzi ya mwaka 2005.

Maelezo ya Wizara:

Ni kweli mpango maalum wa manunuzi ulikuwa haupo katika Wizara na walichokifanya kwa mwaka 2012/2013 ni kuwataka kila Mkuu wa Idara kutayarisha mpango wake wa manunuzi (Annual Work Plan) na kuuwasilisha kwa Katibu, ili baadae Kitengo cha Manunuzi kikae na kuandaaa mpango mmoja wa Wizara nzima.

Aidha, kwa upande wa Pemba nako tayari nako mpango wa manunuzi hhuo umeshatayarishwa. Ingawaje mapango huo unakabiliwa na changamoto ya kutopatikana kwa fedha kwa mujibu wa 'cash flow'

Maelezo ya Kamati:

Kamati haikutarajia kupata maelezo ya Wizara yasionesha namna gani wameandaa mpango wa manunuzi. Pamoja na ukweli kwamba, wamechelewa kutokana na kuchelewa kuundwa kwa Kitengo cha Manunuzi, suala hili lilitarajiwa kutekelezwa mara moja na isiwe linaisubiri Kamati.

Maoni ya Kamati:

Kamati inawataka Wizara waharakishe kuandaa Mpango wa Manunuzi, ili waweze kuutekeleza kwa maslahi ya Wizara. Kukosekana Mpango wa Manunuzi ni kuvunja Sheria Namba 9 ya mwaka 2005, kifungu cha 19. Hivyo, Afisa Mhasibu wa Wizara hii ndani ya miezi mitatu tokea kuwasilishwa kwa Ripoti hii, awe ameanzisha Mpango wa Manunuzi, na kutokufanya hivyo, Kamati inaitaka Serikali kumuwajibisha kinidhamu, Afisa Mhasibu wa Wizara hii.

Hoja Namba 10.3 Kuhusiana na Mapungufu katika Daftrati la kuhifadhia mali za kudumu:

Ukaguzi umebaini kwamba, daftari la kuhifadhia mali za Wizara lina mapungufu kwa kukosekana thamani halisi ya mali hizo, eneo la mali zilipo, alama za utambulisho pamoja na kiwango cha uchakavu, huku baadhi ya mali hizo hazikuingizwa kabisa katika daftari hilo.

Maelezo ya Wizara:

Wizara inaendelea kulitekeleza suala hili kama ilivyoshauriwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu huku ikiandaa mpango wa kuwasomesha maofisa wake waweze kufahamu namna ya kufanya thamani na utunzaji wa mali za Wizara na uwekaji mzuri wa daftari la kuhifadhia mali za Wizara.

Maelezo ya Kamati:

Kamati haioni hoja ya Wizara kuwa ni ya busara ukizingatia kwamba, ni muda mrefu sasa Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo imekwishakutoa mafunzo ya uwekaji bora wa daftari hilo, huku suala pekee lililobakia katika utekelezaji wake ni uwekaji wa thamani halisi ya mali za Taasisi husika.

Maoni ya Kamati:

Kamati inaitaka Serikali kutoa onyo kwa Afisa Manunuzi wa Wizara, pamoja na Katibu Mkuu wa Wizara hii, kwa kufanya uzembe wa kuandaa daftari la mali za kudumu lililokamilika, ukizingatia kwamba, mafunzo ya uwekaji wa daftari hilo yalikwishatolewa awali na Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo.

Hoja Namba 10.4 Kuhusu Kukosekana kwa Hati za Umiliki za Wizara:

Ukaguzi umebaini kwamba, Wizara inamiliki majengo, mashamba na vyombo vya moto lakini haina hati za umiliki wa mali hizo, suala ambalo linashindwa kuthibitisha uhalali wa umiliki huo.

Maelezo ya Wizara:

Ni kweli wakati wa ukaguzi mali hizo zilishindwa kuthibitishwa hati zake za umiliki, ingawa Wizara imefanya juhudi kadhaa katika kuondosha kasoro zilizopo. Kwa upande wa Mashamba na majengo, tayari Wizara inaendelea kutekeleza kwa vitendo mazingatio ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu, huku ikiendelea na hatua za kutafuta hati hizo, na kwa kuanzia tayari wameshaanza kupima na kuchora mashamba na majengo husika. Aidha, wameshawasiliana na Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati kwa ajili ya hatua za kupatiwa hati miliki. Changamoto kubwa inayowakabili ni upungufu wa fedha.

Kwa upande wa Nyumba, Wizara baada ya kugawanywa na Wizara ya Mifugo na Uvuvi, baadhi ya nyumba hizo tayari zimeshahamishiwa katika Wizara hii mpya. Nyumba zinazoendelea kutunzwa na kumilikiwa na Wizara hii sasa ni tano tu, ambazo zipo Mbweni na Mazizini.

Kwa upande wa vyombo vya moto, Wizara inakubali kwamba baadhi ya mali hizo sasa zimeshakuwa kongwe na chakavu na baadhi ya mali hizo zinahitajai matengenezo makubwa sana na vyengine vimebaki kuwa ni sehemu ya kutoa vipuri na kusaidia vyombo vyengine, kiasi ambacho haziwezi kutengenea tena. Aidha, kwa upande wa Pemba tayari hati miliki ya vyombo vya moto zipo.

Maelezo ya Kamati :

Kamati imesikitishwa kuelezwa kwamba, nyumba za Pemba zote hazina hati miliki, ingawa juhudi bado zinaendelea za kuzitafutia huku ramani ya nyumba hizo pamoja na mashamba zipo chini ya Wizara. Aidha, vyombo vya moto navyo baadhi yao vina magamba ya umiliki na vyengine havina.

Maoni ya Kamati:

Kamati inaitaka Wizara kuhakikisha inapata hati miliki za mali zake haraka iwezekanavyo. Aidha, Kamati inasikitishwa na uchelewaji wa kutolewa kwa hati miliki chini ya Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati zaidi kwa taasisi za Serikali, wakati watu binafsi wanapatiwa hati hizo ndani ya muda mdogo tena bila ya usumbufu mkubwa.

Hoja Namba 10.5 Kuhusu Udhibiti na Utunzaji wa Mali za Wizara:

Wizara pamoja na kumiliki mali nyingi, haina udhibiti mzuri wa mali zake, ikiwa ni pamoja na kukosa matengenezo kwa muda husika. Hali ambayo pia inapelekea Wizara kuingia katika hasara kubwa ya matengenezo ya nyumba hizo kwa wakati unaofaa.

Maelezo ya Wizara:

Wizara inakiri kwamba, nyumba tano zilizo chini ya Wizara hii, mbali na zile ambazo tayari zimeshahamishiwa kwa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, nyumba hizo zipo katika hali nzuri na Wizara inaendelea kuzitunza. Pamoja na hayo, inakiri kwamba, baadhi ya nyumab hizo tano zinatumiwa kinyuma na makusudio, ingawa ni Wizara imeshachukua hatua kadhaa lakini bado hali haijawa ya kuridhisha. Kwam Mfano, Nyumba namba 3 iliyopo Mbweni, inakaliwa na Ndg. Fuad Rashid Omar, Mfanyakazi wa Baraza la Wawakilishi, ambae hapo awali alikuwa Mfanyakazi wa Wizara hii, ingawa sasa hahusiki tena na Wizara hii. Kwa Upande wa Pemba, Wizara inaendela kuziffanyia matengenezo nyumba zake kwa kadiri hali inavyoruhusu.

Maelezo ya Kamati:

Kamati imesikitishwa na kitendo cha Wizara kutochukua hatua muafaka kwa wakaazi wasiohusika na nyumba hizo, kwani hatua tu ya kuwaandikia barua, haitoshi, na Wizara ingelipaswa kuchukua hatua nyengine madhubuti, ili nyumba hizo zitumike kama ilivyokusudiwa.

Kwa mfano, Nyumba ya Wizara iliyopo Mazizini anayokaa Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini, ingelipaswa irejeshwe Wizarani ili iweze kutumiwa kwa maslahi ya Wizara, kinyume na hali ilivyo hivi sasa.

Maoni ya Kamati:

Kamati inaagiza nyumba zote mbili, inayokaliwa na Ndg. Fuad Rashid Omar, Mfanyakazi wa Baraza la Wawakilishi, pamoja na inayokaliwa na Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini zirudishwe kwa Wizara ya Kilimo na Maliasili, ili ziweze kutumiwa kwa maslahi ya Wizara.

3.6.1 IDARA YA KILIMO:

Hoja Namba 11.1 Kukosekana kwa kadi za Usajili kwa Magari ya Idara.

Ukaguzi umebaini kwamba, Idara inamiliki vyombo vya moto mbali mbali lakini kadi za usajili wake hazikupatikana kwa ukaguzi na hivyo uhalali wa umiliki wake umeshindwa kuthibitika.

Maelezo ya Idara:

Ni kweli wakati wa ukaguzi mali hizo hazikuwepo, ingawa sasa tayari zipo na zipo tayari kwa kukaguliwa.

Maelezo ya Kamati:

Kamati imezipitia kadi hizo na kujiridhisha kwamba ziko sahihi.

Maoni ya Kamati:

Kamati inapendekeza hoja hii ifutwe.

Hoja Namba 11.2 Kuhusiana na Udhibiti na utunzaji wa mali za Idara:

Ukaguzi umebaini kwamba, udhibiti na utunzaji wa baadhi ya mali za Idara ya Kilimo, hauridhishi. Hali hii imetokana na kutokuwepo kwa utunzaji mzuri wa mali hizo, kutofanyiwa matengenezo kwa muda husika na kuwepo kwa usimamizi usioridhisha.

Maelezo ya Idara ya Kilimo:

Ni kweli juu ya hoja hiyo, ingawaje kwa muda huu, kuna baadhi ya mali hizo tayari zimeshaharibika kabisa, huku Idawa ikisubiri muongozo wa Wizara pamoja na Serikali kwa ujumla ili waweze kuziuza mali hizo. Vyombo hivyo takriban vimechakaa kwa miaka 10 sasa ama zaidi, huku Idara ikikosa uwezo wa kuvihudumia ipasavyo.

Utaratibu wa utunzaji wa mali hizo hufanywa na Idara yenyewe kupitia bajeti yake, ingawaje tatizo liliopo ni upatikanaji wa fedha hizo. Aidha, kutokana na kukosa fedha za kununulia ‘spare’ wanafika wakati, wanachukua ‘spare’ kutoka ‘tractor’ moja kwenda jengine, ili angalau japo moja ama machache, yaweze kufanya kazi.

Kwa upande wa ‘Double Cabin’ SMZ 4825, ipo katika hali mbaya sana, tena ipo ‘garage’ pamoja na Tractor SMZ 4675 imelala kabisa kutokana na kukosa ‘spares’

Maelezo ya Kamati:

Ka ujumla Kamati imeshangazwa na uchakavu wa mali hizo za Wizara, na kufahamu kwamba, kwa kiasi kikubwa upatikanaji wa fedha unapelekea kuchakaa kwa haraka kwa mali za Wizara.

Maoni ya Kamati :

Kamati inamuagiza Katibu Mkuu wa Wizara ya kilimo na Mliasili kuziuza mali zote zilizochakaa ambazo haziwezi tena kutengenea ili kuepusha hasara ya kubakia na mali kachara. Aidha, uuzwaji huo lazima uzingatie taratibu za Sheria. Vile vile, Kamati hairidhishwi na utunzaji wa mali za Wizara na inaiagiza Serikali kuwa makini katika kuipa fedha Wizara, ili iweze kusimamia uimara wa mali zake.

3.6.2 IDARA YA MISITU:

Hoja Namba 12.1 Kuhusu Kukosekana kwa kadi za Usajili kwa Magari ya Idara.

Ukaguzi umebaini kwamba, Idara inamiliki vyombo vya moto mbali mbali lakini kadi za usajili wake hazikupatikana kwa ukaguzi na hivyo uhalali wa umiliki wake umeshindwa kuthibitika.

Maelezo ya Idara:

Ni kweli kwamba, kadi hizo zimekosekana wakati wa ukaguzi na hili limesababishwa na uchakavu mkuwa wa muda mrefu wa vyombo hivyo na vingi vyao vimelala kabisa. Aidha, hali hii inatokana pia na vyombo hivyo kupewa na wafadhili ambao walifadhili vyombo hivyo bila ya kubadili usajili. Aidha, baadhi yao vimepata angalau kopi ya magamba hayo.

Maelezo ya Kamati:

Kamati hairidhishwi na hali hii.

Maoni ya Kamati:

Kamati inaitaka Serikali kuandaa utaratibu mzuri wa ubadilishaji wa kadi za usajili kwa vyombo vyote vinavyotolewa kutoka kwa wafadhili.

Hoja Namba 12.2 Kuhusiana na Udhibiti na utunzaji wa mali za Idara:

Ukaguzi umebaini kwamba, udhibiti na utunzaji wa baadhi ya mali za Idara ya Misitu, hauridhishi. Hali hii imetokana na kutokuwepo kwa utunzaji mzuri wa mali hizo, kutofanyiwa matengenezo kwa muda husika na kuwepo kwa usimamizi usioridhisha.

Maelezo ya Idara.

Ni kweli kuhusiana na udhibiti na utunzaji huo, hali inayosababishwa zaidi na uhaba wa fedha na vyombo hivyo tayari vimeshakaa muda mrefu na vingi vimeshachakaa kabisa.

Maelezo ya Kamati :

Suala la udhibiti na utunzaji wa mali za Idara, takriban ni tatizo la Wizara hii nzima.

Maoni ya Kamati :

Kamati inaitaka Serikali kutoa onyo kwa Katibu Mkuu wa Wizara hii kwa kutokuwa makini juu ya usimamizi wa mali za Serikali, kwani yeye ndie msimamizi wa mali hizo kwa niaba ya Serikali. Aidha, Kamati inaitaka Serikali kusimamia ipasavyo utunzaji mzima wa mali za Wizara na Idara kwa ujumla. Suala hili lisiachiwe kwa Idara pekee ambayo haina uwezo wa kifedha katika kusimamia hilo.

3.6.3 IDARA YA UMWAGILIAJI :

Hoja Namba 13.1 Kukosekana kwa kadi za Usajili kwa Magari ya Idara ya Uwagiliajimaji.

Idara inamiliki vyombo vya moto mbali mbali lakini kadi za usajili kwa vyombo vya moto hivyo hazikupatikana kwa ukaguzi. Uhalali wa umiliki huo kwa hivyo, umeshindwa kuthibitika.

Maelezo ya Wizara:

Kuhusu Gari ya Toyota Hice yenye namba ya usajili SMZ 5599 na Motor Bike SMZ 5556 zipo na Motor Grader SMZ 3194 Idara wanafuatilia kuombea magamba yake kwa kumuandikia Mkurugenzi wa Manispaa kwa lengo la kupatiwa magamba hayo. Hata hivyo, gari hizo ni chakavu na hazifanyi kazi.

Maelezo ya Kamati :

Pamoja na kwamba gari hizo ni chakavu, Suala la umiliki wa vyombo hivyo ni muhimu wakati wowote.

Maoni ya Kamati:

Kamati inaitaka Idara kufuatilia umiliki wa vyombo hivyo hata kama ni chakavu.

Hoja Namba 13.2 Kuhusu Udhibiti na Utunzaji wa mali za Idara ya Umwagiliaji Maji.

Ukaguzi umebaini kwamba, udhibiti na utunzaji wa baadhi ya mali za Idara ya Umwagiliaji Maji, hauridhishi. Hali hii imetokana na kutokuwepo kwa utunzaji mzuri wa mali hizo, kutofanyiwa matengenezo kwa muda husika na kuwepo kwa usimamizi usioridhisha.

Maelezo ya Idara:

Ni kweli kasoro hiyo, lakini hili husababishwa na na uchakavu wa mali hizo, kiasi ambacho takriban hazitengenezeki.

Maelezo ya Kamati:

Kamati inaendelea kusikitishwa na Taasisi za Serikali kuziacha mali zake hadi kufikia kuchakaa bila ya uwezekano wa kutengenezeka.

Maoni ya Kamati:

Kamati inamuagiza Katibu Mkuu wa Wizara hii kuhakikisha kwamba, Mali za Taasisi zake zinafanyiwa marekebisho na matunzo yanayofaa. Kwani kuziacha bila ya kuzifanyia matengenezo ni kuiongezea hasara Serikali. Hali hii huipelekea Serikali kununua vyombo vyengine hata kama vyombo vya mwanzo vingelitengea kwa kufanyiwa matengenezo na kutunzwa vizuri.

3.7 WIZARA YA KATIBA NA SHERIA:

3.7.1 MAHAKAMA:

Hoja Namba 14.1.1 Kuhusu Kukosekana kwa Mpango wa Manunuzi:

Mahakama imebainika kwamba haiandai Mpango wa Manunuzi na hivyo kwa mwaka wa 2009/2010, imefanya manunuzi bila ya kuwa na Mpango wa Manunuzi, ingawaje inafahamu kwamba kufanya hivyo kunakiuka masharti ya kifungu cha 19 cha Sheria Namba 9 ya mwaka 2005.

Maelezo ya Mahakama:

Kwa mwaka wa fedha 2009/2010, Mpango wa Manunuzi wa Mahakama ulikuwa haujaandaliwa, na hii ilitokana na sababu kwamba, Mahakama Kuu haikuwa na Afisa Manunuzi. Mahakama ilichukua hatua ya kuomba Afisa huyo kutoka Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, ambae atakuwa na jukumu la kuandaa Mpango wa Manunuzi wa Mahakama.

Maelezo ya Kamati:

Kitendo cha kusubiri kuletewa Afisa Manunuzi kutoka Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, bila ya kuzingatia kwamba, Afisa huyo anatakiwa kuajiriwa na Mahakama, hakikubaliki kwa Kamati. Halikadhalika, Kamati intahadharisha kwamba, hoja ya Mdhibiti ni kuanzishwa kwa Kitengo cha Manunuzi, ambapo pamoja na ukweli kwamba Afisa Manunuzi ni muhimu sana katika uanzishwaji wa Kitengo, Mahakama kwa utaratibu wowote unaofaa, lazima wasisubiri mpaka waletewe Afisa Manunuzi kutoka Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo bali kitengo lazima kiandaliwe.

Maoni ya Kamati:

Kamati imeitaka Mahakama kuajiri Afisa Manunuzi ili aweze kuisaidia katika utekelezaji wa majukumu yake. Aidha, Kamati inaitaka Mahakama kuanzisha mara moja Kitengo cha Manunuzi, ili manunuzi na ugavi wa Kamisheni uweze kufanywa kwa mujibu wa Sheria. Katika kulitilia nguvu jambo hili, Kamati inamtaka Afisa Mhasibu wa Mahakama, ndani ya miezi sita tokea kuwasilishwa kwa ripoti hii, awe ameshaanzisha Kitengo cha Manunuzi, na kufanya vyenginevyo sio tu kuendelea kuvunja Sheria ya Manunuzi na Ugavi wa Mali za Serikali (Namba 9 ya mwaka 2005), kifungu cha 19, lakini Kamati inaitaka Serikali kumchukulia hatua za kinidhamu kwa kukiuka maelekezo ya Sheria.

Hoja Namba 14.1.2 Kuhusu Mapungufu katika Daftari la Kuhifadhia Mali za Kudumu.

Ukaguzi umebaini kwamba, daftari la kuhifadhia mali za kudumu za Mahakama, lina mapungufu kwa kukosekana kwa taarifa muhimu kama vile thamani halisi za mali hizo, eneo la mali zilipo,

alama za utambulisho pamoja na kiwango cha uchakavu. Aidha, baadhi ya mali hizo ambazo hazikuingizwa kabisa katika daftari hilo. Hii ni kwenda kinyume na kifungu cha 264 cha Kanuni za Fedha za mwaka 2005, na pia hali hii huweza kusababisha upotevu wa mali hizo.

Maelezo ya Mahakama:

Kazi ya utiaji thamani wa Mali na kukokotoa kiwango cha uchakavu wa mali ni kazi inayohitaji utaalamu wa hali ya juu, ili kuepuka kuzidisha au kupunguza thamani ya mali. Mahakama haina Mtaalamu wa kutatua tatizo hilo, ila imewasiliana na Afisi ya Mhakikimali za Serikali, ili kupata Mtaalamu na muongozo wa namna ya kutia thamani mali za Mahakama.

Maelezo ya Kamati:

Suala la Daftari la kuhifadhia mali za kudumu za Mahakama, tayari muongozo wake umeshatolewa na Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, na walioshiriki katika mafunzo hayo ni watendaji wa Fedha wa kila Taasisi. Leo kamati kuambiwa kwamba, Mahakama haiwezi kuandaa daftari hilo mpaka impate Mtaalamu kutoka Uhakikimali, hakukubaliki.

Hii ni sambamba na ujazaji wa taarifa zote zinazohitajika, ispokuwa Kamati itaridhika inapoambiwa kwamba, suala la thamani bado linahitaji muongozo maalum lakini taarifa zote zilizobakia lazima zijazwe na zionekane katika daftari.

Maoni ya Kamati:

Kamati inaitaka Mahakama kuhakikisha inaweka taarifa zote zinazohitajika katika daftari la kuhifadhia mali zake za kudumu, ili kukidhi matakwa ya Sheria.

Hoja Namba 14.1.3 Udhibiti na Utunzaji wa Mali za Mahakama:

Ukaguzi umebaini kwamba, hali ya udhibiti na utunzaji wa baadhi ya mali za Mahakama hauridhishi. Hii imetokana na kutokuwepo kwa utunzaji mzuri, kutofanyiwa matengenezo kwa muda husika na kuwepo kwa usimamizi usioridhisha. Hali hii imepekea Mahakama kuingia katika gharama kubwa ya utunzaji na utengenezaji wa mali hizo na hatimae kushindwa kutoa huduma husika.

Maelezo ya Mahakama:

Mahakama imechukua hatua ya kuingiza kwenye mpango wa Bajeti, Majengo yote machakavu. Hata hivyo, upatikanaji wa fedha na ufinyu wa bajeti wanayoitegemea, inakwamisha ukarabati kw wakati kwa kuzingatia kuwa majengo ya Mahakama yanauchakavu mkubwa. Mahakama inawaomba Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, wasaidie ili Mahakama ipate bajeti inayoweza kujenga upya na kufanya ukarabati majengo ya Mahakama zote.

Kuhusu vyombo vya moto, Mahakama imechukua hatua za kuwaita wahakiki mali za Serikali na uhakiki ulifanyika na kuonesha vyombo vimechakaa sana kama Mkaguzi alivyoonesha kwenye ripoti. Hivyo basi, vyombo hivyo vimeondoshwa kwenye daftari la Mahakama ili kupunguza gharama kubwa ya matengenezo. Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo imeviuza vyombo hivyo kwa kufuata utaratibu, kupitia Afisi ya Mhakiki Mali.

Kuhusiana na viwanja vya Mahakama, kiwanja kilichopo Mwanakwerekwe kwa ajili ya ujenzi wa Mahakama ya Kadhi, bado kinamilikiwa na Mahakama na tayari kimeshazunguushiwa uzio ili kukitunza na hati miliki ya kiwanja ipo pia.

Kiwanja kwa ajili ya ujenzi wa Mahakama ya Mkoa Tunguu, bado ni miliki ya Mahakama nacho pia kimezunguushiwa uzio na kina hati miliki. Aidha, kiwanja kwa ajili ya Ujenzi wa Mahakama Makunduchi, bado nacho ni milki ya Mahakama na wanayo hati miliki.

Maelezo ya Kamati:

Suala la kuhifadhiwa mali za Mahakama kwa kuziwekea utaratibu mzuri wa kuzitunza, utasaidia sana kupunguza gharama za matengenezo yake, iwapo juhudi na hatua hizo zitafanywa kwa wakati. Kamati imepokea taarifa ya Mahakama na juhudi zake inazochukua katika kutunza majengo yake, ingawa inajulikana kwamba, suala hilo bado halijafika kwa Mahakama za Wilaya.

Maoni ya Kamati :

Kamati inaitaka Mahakama kuendelea na juhudi zake za kuyafanyia ukarabati majengo yake, huku vyombo vya moto navyo vifanyiwe utaratibu wa kuuzwa kama haiwezi tena kutumika kwa matumizi ya Ofisi.

3.7.2 MWANASHERIA MKUU :

Hoja Namba 14.2 Kuhusu Ukosekana kwa Mpango wa Manunuzi.

Ukaguzi umebaini kwamba, Afisi ya Mwanasheria Mkuu haiandai Mpango wa Manunuzi na hivyo kwa mwaka wa 2009/2010, imefanya manunuzi bila ya kuwa na Mpango wa Manunuzi, ingawaje inafahamu kwamba kufanya hivyo kunakiuka masharti ya kifungu cha 19 cha Sheria Namba 9 ya mwaka 2005.

Maelezo ya Afisi ya Mwanasheria Mkuu:

Katika kutayarisha bajeti ya kila mwaka, Afisi huwa inatayarisha mpango wa kazi kwa mwaka mzima. Miongoni mwa mipango hiyo ni mpango wa manunuzi. Hata hivyo, kwa mwaka 2009/2010 Afisi haikuwa na Mpango huo ingawaje mara tu baada ya kushauriwa na Wakaguzi, Afisi ilianza kuufanyia kazi. Kwa mwaka 2010/2011, Afisi ilianza kutayarisha Mpango wa

Manunuzi kwa manunuzi yaliyofadhiliwa na Mradi wa BEST na mwaka 2011/2012 na 2012/2013, ilitayarisha mpango wa manunuzi kwa bajeti yake ya Serikali.

Maelezo ya Kamati :

Kamati imehoji iwapo Afisi imeajiri Mtaalamu wa Manunuzi na kuelezwa kwamba, Afisi bado haijaajiri Afisa huyo ila wameshapeleka maombi ya kupatiwa Afisa Manunuzi Tume ya Utumishi Serikalini, ingawa bado hawajafanikiwa kupatiwa. Hivyo, katika kukidhi hali ilivyo, Afisa wao mwenye elimu ya Diploma ya Rasilimali watu (Human Reseorce), ndie wanaemuanduaa aweze kutekeleza majukumu yake.

Maoni ya Kamati.

Kamati imeishauri Afisi ya Mwanasheria Mkuu kumsomesha ngazi ya Diploma ama Degree ya fani ya Manunuzi, Afisa wanaemtumia kwa kazi za manunuzi ili aweze kuwasaidia. Hata hivyo, ushauri wa kuajiri Afisa Manunuzi aliyesomea na mwenye uzoefu ni bora zaidi.

Pamoja na kasoro zilizopo, Kamati inamtaka Afisa Mhasibu wa Afisi ya Mwanasheria Mkuu, kutayarisha Mpango wa Manunuzi, ndai ya miezi mitatu tokea kuwasilishwa kwa ripoti hii. Vyenginevyo, Kamati inaiagiza Serikali kumchukulia hatua za kinidhamu Afisa huyu Mhasibu iwapo atashindwa kutekeleza masharti ya Sheria.

Hoja Namba 14.2.2 Kuhusu Kukosekana kwa Hati Miliki pamoja na Kadi za Usajili.

Ukaguzi umebaini kwamba, Afisi ya Mwanasheria Mkuu inamiliki jengo na vyombo vya moto mbali mbali lakini haina hati za umiliki ambazo pia hazikupatikana kwa ukaguzi.

Maelezo ya Afisi ya Mwanasheria Mkuu.

Ni kweli Afisi inamiliki majengo, viwnja na vyombo vya moto. Kwa upande wa viwanja vinavyomiolikiwa na Afisi, ambavyo ni Kiwanja cha Mazizini Unguja na Mguye Tibirinzi Pemba ambapo Afisi pia ina hati miliki ya viwanja hivyo. Kwa upande wa vyombo vya moto ambazo ni gari mbili na vespa tano, Afis pia ina kadi zao za usajili.

Maelezo ya Kamati :

Kamati imehitaji kupatiwa uthibitisho wa hati miliki pamoja na kadi za usajili, ambapo vyote vimepatikana kwa uchunguzi.

Maoni ya Kamati :

Kamati imeridhika na hoja hii ilivyojibiwa na inapendekeza kwamba, hoja hii ifutwe.

Hoja Namba 14.2.3 Kuhusu mapungufu katika daftari la kuhifadhia mali za kudumu.

Ukaguzi umebaini kwamba, daftari la kuhifadhia mali za kudumu za Afisi ya Mwanasheria Mkuu, lina mapungufu kwa kukosekana kwa taarifa muhimu kama vile thamani halisi za mali hizo, eneo la mali zilipo, alama za utambulisho pamoja na kiwango cha uchakavu. Aidha, baadhi ya mali hizo ambazo hazikuingizwa kabisa katika daftari hilo. Hii ni kwenda kinyume na kifungu cha 264 cha Kanuni za Fedha za mwaka 2005, na pia hali hii huweza kusababisha upotevu wa mali hizo.

Maelezo ya Afisi ya Mwanasheria Mkuu :

Katika kuhakikisha mali za Afisi ya Mwanasheria Mkuu zinatambuliwa, Afisi imekuwa ikijitahidi kuahkikisha inaziwekea alama za utambulisho (identification code) mali zote. Kwa zile chache ambazo hazikuwa na alama za utambulisho wakati wa ukaguzi, tayari zimeshatiwa alama hizo kwa mujibu wa taratibu zilivyo. Kuhusu baadhi ya mapungufu yaliyojitokeza katika daftari la mali za Seriakli (Asset Register) ikiwemo kiwango cha uchakavu (depraciation rate). Suala hili ni la Serikali nzima na linashughulikiwa na Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo.

Maelezo ya Kamati :

Pamoja na maelezo ya Afisi, katika hatua ya awali Kamati haikuridhika na maendeleo ya daftari hilo hali iliyopelekea kutowa wiki mbili kwa Afisi ya Mwanasheria Mkuu, ili akamilishe na kuikabidhi kwa Kamati.

Maoni ya Kamati.

Kamati imeridhishwa kwamba, taarifa nyingi muhimu zimeweza kuingizwa katika daftari hilo na inasisitiza kwamba, daftari hilo lizindi kuendelezwa kwa kutiwa taarifa zote muhimu kama ilivyoelekezwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu.

3.7.3 AFISI YA MKURUGENZI WA MASHTAKA:

Hoja Namba 14.3.1 Kuhusu kutofuatwa kwa mpango wa manunuzi.

Ukaguzi umebaini kwamba, Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka imeandaa mpango wa manunuzi lakini mpango huo haufuatwi kulingana na taratibu zilizopo. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu cha 19 cha Sheria Namba 9 ya mwaka 2005.

Maelezo ya Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka:

Nia ya Afisi kuona kwamba inatekeleza majukumu yake kwa mujibu wa mpango ilojipangia. Afisi imekuwa ikipata fedha pungufu kulinganisha na mipango iliyojipangia ikiwa ni pamoja na mpango wa manunuzi. Kutokana na hali hiyo, Afisi inalazimika kununua kwa mujibu wa

maingizo madogo madogo ya fedha inayopata. Kwa mfano Afisi inatarajia kuingiziwa Tsh. 40,000,000 kwa mwezi lakini zinaingiwa Tsh.9,000,000 pekee.

Jambo hili hulifanya Afisi kununua vitu visivyokidhi mahitajio ya wakati husika kama yalivyoainishwa kwenye mpango wa manunuzi. Hivyo inapelekea ugumu wa kuufuata kikamilifu mpango huo. Hata hivyo, Afisi itachukua juhudi za makusudi kuona kwamba, mpangpo wa manunuzi unafuatwa.

Maelezo ya Kamati:

Kamati imepokea maelezo ya Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka na kukubali kwamba, tatizo la Serikali ni kutiziwezesha Taasisi zake kufuata ipasavyo Sheria za manunuzi kwa kuzitaka zitumie kwa mujibu wa mpango wa manunuzi, wakati fedha inazowapatia ni kidogo wala hazikidhi kutumika kama zinavyojipangia.

Maoni ya Kamati:

Kamati inaitaka Serikali kuwa tayari kuzipatia fedha taasisi zake kwa wakati na kwa kadiri mahitaji yao yalivyo, ili ziweze kununua kwa mnasaba wa mahitaji yao.

Hoja Namba 14.3.2 Kuhusu kukosekana kwa kadi za usajili.

Uakguzi umebaini kwamba, Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka inamiliki vyombo vya moto mbali mbali lakini hati za umiliki wa mali hizo hazikupatikana kwa ukaguzi, hali hii inashindwa kutihbitika uhalali wa umiliki wa vyombo hivyo. Vyombo vyenyewe ni Land Rover, SMZ 5995; Suzuki Grand Vitara SMZ 6247; Toyota Land Cruiser DFP 2369; Suzuki DFP 2415; Vespa SMZ 6549 na Vespa SMZ 7066.

Maelezo ya Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka:

Ni kweli wakati wa ukaguzi hati hizo za umiliki hazikuwepo. Ingawaje Afisi imechukua juhudi na kufanikiwa kupata hati zote za usajili kama zilivyotakiwa kupitia ripoti ya Mdhibiti.

Maelezo ya Kamati:

Kamati imejiridhisha kuwepo kwa hati za umiliki kwa Land Rover na Suzuki zote za SMZ. Kuhusiana na Toyota Land Cruiser na Suzuki zote za DFP, Kamati imeelezwa kwamba, Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka wamepewa gari hizo na UNDP watumie tu, lakini kadi za umiliki zimebaki mikononi mwa UNDP wenyewe. Aidha, Vespa kadi za umiliki zimearifiwa kuwepo Pemba, na Kamati imethibitishiwa kwa njia ya fax.

Maoni ya Kamati:

Kamati imejiridhisha kwamba, hoja hii imepata majibu muafaka. Aidha, inaishauri Serikali kuzungumza vizuri na Wahisani kwamba, wakabidhi hati za umiliki wa gari wanazozisaidia Taaisis za Serikali, ili kuondosha tatizo la kutokuwa na hati hizo.

Hoja Namba 14.3.3 Kuhusu Mapungufu katika daftari la kuhifadhia mali za kudumu:

Ukaguzi umebaini kwamba, daftari la kuhifadhia mali za kudumu za Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka, lina mapungufu kwa kukosekana kwa taarifa muhimu kama vile thamani halisi za mali hizo, eneo la mali zilipo, alama za utambulisho pamoja na kiwango cha uchakavu. Aidha, baadhi ya mali hizo ambazo hazikuingizwa kabisa katika daftari hilo. Hii ni kwenda kinyume na kifungu cha 264 cha Kanuni za Fedha za mwaka 2005, na pia hali hii huweza kusababisha upotevu wa mali hizo.

Maelezo ya Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka:

Ni kweli wakati wa ukaguzi hali ilikuwa hivyo, ingawaje Afisi imechukua juhudi na kufanikiwa kuingiza mali zote inazozimiliki katika daftari la kuhifadhia mali za kudumu. Kuhusiana na suala la uwekaji wa thamani, Afisi inakiri kukabiliwa na changamoto hiyo kwa kukosa mtaalamu wa kufanya tathmini. Hata hivyo, Afisi inaendelea na hatua ya kuziomba taasisi husika ziwasaidie kufanya tathmini hiyo.

Maelezo ya Kamati:

Kamati imepitia madaftari hayo, kwa mfano daftari linalohusiana na majengo bado halijawekwa taarifa zote muhimu ikiwa ni pamoja na 'Title Deed' Bei ya ujenzi, tarehe ya ujenzi, jina la mjenzi, bado taarifa zake hazijaingizwa, wakati ni vitu ambavyo havihitaji mtaalamu. Aidha, kuhusiana na daftari la khifadhia vyombo vya moto, pia kasoro ndogo ndogo zimejitokeza, ikiwa ni pamoja na gari Land Rover SMZ 198A taarifa za Engine namba na Chasis namba, weight, capacity na taarifa nyengine bado hazijajazwa.

Maoni ya Kamati:

Pamoja na Kamati kutowa wiki mbili kwa Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka na wao kulikabidhi daftari hilo kwa Kamati, bado taarifa muhimu hazijakamilika kujazwa. Kamati inawataka Afisi hii ikamilishe kazi hiyo.

Hoja Namba 14.3.4 Kuhusu Udhibiti na Utunzaji wa mali za Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka:

Ukaguzi umebaini kwamba, udhibiti na utunzaji wa baadhi ya mali za Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka hauridhishi. Hii imetokana na kutokuwepo kwa utunzaji mzuri, kutofanyiwa matengenezo kwa muda husika na kuwepo kwa usimamizi usioridhisha. Pia hali hii imepekea Afisi hii kuingia katika gharama kubwa ya utunzaji na utengenezaji wa mali hizo na hatimae kushindwa kutoa huduma husika.

Maelezo ya Afisi ya mkurugenzi wa Mashtaka:

Afisi imejitahidi kufanya matangenezo kwa mali mbali mbali zinazomilikiwa na Afisi. Kwa mfano Gari ya Suzuki Grand Vitara, iliyosita kufanya kazi zaidi ya miaka 2 nyuma, tayari imeshafanyiwa matengenezo makubwa na sasa inafanya kazi kama kawaida. Fotokopi mashine iliyosita miaka miwili nyuma, Afisi imeona kutokana na uchakavu wake na kutumika muda mrefu, Afisi imetafuta fotokopi nyengine na hii wanashauri iuzwe.

Maelezo ya Kamati:

Kamati imeridhishwa na juhudi zilizochukuliwa na Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka katika kufufua gari iliyogoma kufanya kazi kwa takriban miaka miwili nyuma. Juhudi hizo hazitakiwi kukomea hapo, ni lazima pia vyombo vyengine vilivyoorodheshwa na Mdhibiti na ambavyo sasa vishakuwa katika hali mbaya, lazima vifanyiwe utaratibu wa matengenezo makubwa ili viweze kutumika.

Maoni ya Kamati.

Ni kweli Kamati inaungana na ushauri wa Afisi hii kwamba fotokopi iliyogoma kufanya kazi kwa muda mrefu na kuchaa, inastahiki iuzwe, kwa sharti tu, Sheria ya Uuzaji na Ugavi wa Mali za Serikali, Namba 9 ya mwaka 2005 lazima ifuatwe ipasavyo katika kuuzwa huko.

3.8 WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA AMALI:

Hoja Namba 15.1 Kukosekana kwa Daftari la kuhifadhia mali za kudumu:

Ukaguzi umebaini kwamba, Wizara haina daftari la kuhifadhia mali za kudumu. Huku ni kwenda kinyume na kifungu cha 264 cha kanuni za Fedha za mwaka 2005 na huweza kusababisha upotevu wa mali hizo.

Maelezo ya Wizara:

Kwa mwaka wa fedha 2009/2010, Wizara ilikuwa na madaftari mawili, la kuwekea vifaa vya Ofisini na vifaa vya Maskuli. Hali hii inakubalika kwamba, kwa mwaka huo hawakuwa na madaftari ya kutosha nay a utaratibu kama uliopendekezwa na Mdhibiti. Hata hivo, kunzia mwaka 2010/2011, Wizara imejitahidi kuweka daftari hilo katika utaratibu unaotakiwa.

Maelezo ya Kamati:

Kwa ujumla daftari ambalo liliwasilishwa kwa Kamati, halioneshi sura halisi ya daftari linalokubalika. Na ni sawa na kusema kwamba, daftari halipo ingawaje walichofanya Wizara ni kuzitambua mali zao. Aidha, taarifa hizo hazipo katika muongozo wa Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo.

Maoni ya Kamati:

Kamati inaitaka Wizara kuchukua hatua za mara moja kuanzisha daftari la mali za kudumu kwa utaratibu na muongozo uliotolewa na Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo na taarifa zote muhimu lazima zionekane katika daftari hilo.

Hoja Namba 15.2 Kuhusu Udhibiti na Utunzaji wa Mali za Wizara:

Ukaguzi umebaini kwamba, udhibiti na utunzaji wa baadhi ya mali za Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko hauridhishi. Hali hii imetokana na kutokuwepo kwa utunzaji mzuri, kutofanyiwa matengenezo kwa muda husika na kuwepo kwa usimamizi usioridhisha. Hali hii imepekea Wizara kuingia katika gharama kubwa ya utunzaji na utengenezaji wa mali hizo na hatimae kushindwa kutoa huduma husika. mali husika ni gari Joe Fang Truck SMZ 6019; Faw SMZ 4616; Tata SMZ 4630; Asia Bus SMZ 3610; na Bus SMZ 5667. Kwa upande wa Pemba, ni Skuli ya Muwambe Shamiani; Ng'ambwa; Chanjamjawiri; Micheweni; Kiuyu Micheweni; Kengeja Secondary; Tumbe na Konde Msingi.

Maelezo ya Wizara:

Wizara inakiri kumiliki gari zilizoainishwa. Aidha, Joe Fang Truck linaandaliwa kuuzwa baada ya kufuatwa kwa taratibu husika. Gari aina ya Faw limeshauzwa kwa Ndg. Rahma Mussa Said; Tata limekabidhiwa kwa Chuo cha Taifa cha Zanzibar (SUZA); Asia Bus na Bus wanangojea vifaa kutoka kwa Al Yousef au ikishindakana wanataraji kuuzwa.

Kwa upande wa Pemba, nako baadhi ya Skuli ambazo tokea mwanzo zilikuwa katika hali nzuri kidogo, wamejitahidi kuzifanyia matengenezo ikiwa ni pamoja na Skuli ya Konde Msingi, Tumbe na Chanjamjawiri. Aidha, Skuli ya Micheweni wameiezua kwa ajili ya matengenezo kutokana na kuwa katika hali mbaya, ila wamekwama njia kwa kukosa fedha.

Maelezo ya Kamati:

Kamati imehitaji kuelezwa zaidi juu ya taratibu zilizochukuliwa katika kuuzwa kwa baadhi ya magari, na kuelezwa kwamba waliwasiliana na Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, jambo ambalo lilithibitishwa. Aidha, kuhusiana na utaratibu mzima wa kuzifanyia matunzo, suala hili linahitaji kutiliwa makazo wa makusudi, ili gari hizo ziweze kudumu.

Kuhusiana na skuli za Pemba, Kamati imeridhishwa na maelezo ingawaje inasikitika kutokana na uchache wa muda, haijabahatika kutembelea na kujionea namna gani skuliz hizo zimefanyiwa matengenezo.

Maoni ya Kamati:

Kamati inaitaka Wizara kuchukua juhudi za makusudi katika kutunza mali zake. Suala la kuuzwa kwa gari halina pingamizi, isipokuwa Kamati inaendelea kusisitiza haja ya kufuatwa ipasavyo, Sheria zinazohusika.

3.9 WIZARA YA AFYA

Hoja Namba 16.1 Kuhusu Kukosekana kwa Daftari la kuhifadhia Mali za Kudumu:

Ukaguzi umebaini kwamba, Wizara haina daftari la kuhifadia mali za kudumu. Hali hii inapingana na masharti ya kifungu cha 264 cha Kanuni za Fedha za mwaka 2005. Aidha, huweza kusababisha upotevu wa mali hizo.

Maelezo ya Wizara:

Ni kweli wakati wa ukaguzi hali ilikuwa hivyo. Hata hivyo, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo tayari wameshafungua daftari hilo nakazi ya kuhakiki mali hizo kwa ajili ya kutiwa thamani, bado inaendelea.

Maelezo ya Kamati :

Kamti imejiridhisha kwa upande wa Wizara ya Afya Unguja kwamba, hakuna daftari hilo, kawni walichonacho ni kumbukumbu ya mali zao ambapo bado hazijawekwa katika utaratibu uliokubalika na Ofisi ya Rais, Fedha Uchumi na Mipango ya Maendeleo. Kamati katika hili haiwezi kuvumilia ukizingatia kwamba tayari mafunzo yameshatolewa zamani.

Aidha, kwa upande wa Pemba, Daftari hilo tayari limeshawekwa ijapokuwa bado lina kasoro ndogo ndogo. Kama vile kutokuwekwa thamani ya baadhi ya vifaa hata vile vyenye thamani inayoeleweka. Mfano viti na meza.

MAONI YA KAMATI

Kamati inaitaka Wizara ya Afya Unguja kuandaa haraka Dfatrai la kuhifadhia mali za kudumu. Sambamba na hilo, taarifa zote zinazotakiwa katika daftari hilo ziwe zimeshakamilika na kwa upande wa Pemba, Kamati inawataka wasisubiri mpango wa Serikali wa kufanya tathmini mali zake, ni vyema kwa vile vifaa ambavyo bei zake zinajulikana zikaingizwa kwenye daftari hilo pamoja na kuziwekea alama (Code) mali zote zitakazoonekana kwenye pia kwenye daftari.

Hoja Namba 16.2 Kuhusu Kukosekana kwa Mpango wa Manunuzi

Wizara haikuwa na Mpango wa Manunuzi kwa mwaka wa 2009/2010, na hivyo matumizi ya fedha zake hayakufuata mpango huo, bila ya kujali maelekezo ya kifungu cha 19 cha Sheria Namba 9 ya mwaka 2005,

Maelezo ya Wizara.

Ni kweli wakati wa ukaguzi Wizara haikuwa na mpango wa manunuzi. Na hili limesababishwa na kutokuwepo kwa bajeti ya kuandaa mpango huo. Aidha, Wizara hata hivyo imefanya juhudi kubwa ya kuuandaa. kwa upande wa Pemba, tayari wameshaandaa mpango huo.

Maelezo ya Kamati:

Mpango wa manunuzi uliowasilishwa kwa Kamati kwa upande wa Wizara, Unguja hauwezi kukubalika kwa sababu haujazingatia uhalisia. Baadhi ya mambo yamepangwa kutumika hadi mwaka ujao, wakati mpango huu unatakiwa uwe wa mwaka mzima. Aidha, Kamati haijaukubali. Kwa upande wa Wizara ya Afya, Pemba hadi kufikia mwaka wa fedha wa 2011/2012 haikuwa na Mpango wa Manunuzi wa mwaka wa fedha wa 2012/2013. Hata hivyo Mpango huo ulikuwa na kasoro kwani haukuanisha muda wa utekelezaji kwa mwaka huo husika. Kama vile kuonesha manunuzi kwa robo mwaka (Quarterly)

Maoni ya Kamati:

Mpango wa Manunuzi wa Wizara urekebishwe na uendane na mahitaji yote yanayotakiwa pia uwe na uhalisia ambao kweli utaweza kutekelezeka.

Hoja Namba 16.3 Kuhusu Kukosekana kwa Kadi ya Usajili wa Baadhi Vyombo vya Moto.

Ukaguzi umebaini kwamba, Wizara inamiliki vyombo mbali mbali vya moto, lakini hati za umiliki wake hazikupatikana kwa ukaguzi. Na hivyo, uhalali wa mali hizo hauwezi kuthibitika.

Maelezo ya Wizara:

Ni kweli wakati wa ukaguzi umiliki wa vyombo hivyo haukuweza kuthibitika, jambo ambalo lilikuwa tofauti baadae kwa kufuatilia na kupata uthibitisho wa umiliki wake.

Maelezo ya Kamati:

Kamati imeelezwa kwamba, magamba ya umiliki kwa baadhi ya vyombo vinavyohusiana na mradi, yaaani zenye usajili wa DFP, umiliki wake hubakia kwa wafadhili wa mradi ambapo Wizara kwa kawaida, hupokea vyombo hivyo bila ya kukabidhiwa kwa kadi za usajili. Kwa ujumla, hoja hii ilijikita katika vyombo vifuatavyo:

1) DFP 301 (Ilipata ajali Februari, 2011 na ripoti ya ajali hiyo kutoka Polisi iliwasilishwa baadae kwa Kamati)
2) DFP 2404
3) DFP 2579
4) DFP 7463

5) DFP 4389

6) DFP 4346

7) Honda (Trail) SMZ 5713

8) HONDA (Trail) SMZ 5731

9) HONDA (Trail) SMZ 6250

10) HONDA (Trail) SMZ 6248

11) HONDA (Trail) SMZ 6249.

12) HONDA (Trail) SMZ 5926

Kamati iliarifiwa kwamba Honda (Trail) yenye nam. SMZ 6181 nayo haina kadi ya usajili lakini pia haimo kweenye orodha ya vipando vya Wizara na hivyo haikuonekana wakati wa ukaguzi.

Aidha Kamati ilibaini kwamba hakuna utaratibu mzuri wa kiutawala katika suala zima la utunzaji na udhibiti wa mali za Serikali hasa hivyo vyombo vya moto kiasi cha kwamba Wakuu wa Vitengo vilivyo chini ya Wizara ya Afya, Pemba hawamuarifu Afsa Mdhamini wanapopata vipando hivyo kutoka Makao Makuu ya Vitengo vyao Unguja.

Pamoja na kukosekana kwa kadi za usajili wa baadhi ya magari, lakini Kamati imebaini matumizi mabaya ya magari hayo na mengine ni makongwe kiasi cha kwamba matengenzo yake yanaongeza matumizi yasiyo ya lazima na kuitia hasara Serikali. Vile vile Kamati ilitaka kupata taarifa ya ajali ya gari yenye nam. DFP 301 iliyotokea Februari, 2011 na ripoti yake kuwasilishwa baadae ingawa Kamati kutokana na uchache wa muda, haikupata muda wa kuifuatilia ripoti hiyo kutoka Polisi na kufanya uchunguzi unaofaa. Ila imearifiwa kwamba gari hiyo kwa sasa haitengenezeki tena na haijafanyiwa utaratibu wowote wa kuondolewa.

Maoni ya Kamati:

Kamati haikuridhika hata kidogo kutokana na Wizara kutokuweka kadi za usajili wa magari na vyombo vyengine. Hoja hii kwa ufupi haikujibika. Kamati inaagiza kwamba Magari yaliyokuwa mabovu yafanyiwe utaratibu wa kisheria ili yaweze kuondolewa kwenye umiliki wa Serikali.

Aidha, kuwe na usimamizi madhubuti wa utunzaji wa mali za Serikali, wakuu wa Idara wanahusika moja kwa moja katika hili huku Kamati ikisisitiza kwamba, Afsa Mdhamini wa Wizara awe anajua kila kitu kilchopo chini ya Wizara yake. Kwa maana hiyo kuwe na utratibu mzuri wa kupashana habari.

Hoja Namba 16.4 Kuhusu Kutokutumika kwa mtambo wa X- Ray.

Ukaguzi umebaini kwamba, Wizara ya Afya Pemba, imepokea mitambo miwili ya X-Ray kutoka Makao Makuu tangu mwaka 2008/2009 kwa ajili ya utoaji wa huduma za afya katika hospitali za Pemba. Aidha, jhadi ukazugi unakamilika, Mitambo hiyo bado haijaanza kutumika na kutotumika kwa mitambo hiyo kunaathiri hali ya utendaji wa Wizara ya Afya kwa kutofikiwa kwa malengo yaliyokusudiwa, pia kuna uwezekano mkubwa wa kuharibika mitambo hiyo.

Maelezo ya Wizara :

Ni kweli wakati wa ukaguzi Mitambo hiyo ilikuwa haifanyi kazi, ingawaje imeshashughulikiwa na hivi sasa inafanya kazi kama kawaida.

Maelezo ya Kamati

Kamati iliarifiwa juu ya utendaji wa mtambo huo wa X-Ray kwamba kwa sasa unafanya kazi kama kawaida tatizo lake ni uwezo wake. Kwa sasa una uwezo wa kumfanyia mtu mwenye *range* ya kuanzia 100 hadi 300 zaidi ya hapo mtambo huo hauna uwezo.kwa bahati asilimia kubwa ya wagonjwa maumbile yao yanaendana na uwezo wa mtambo.

Aidha, Kamati iliarifiwa kuwa tatizo kubwa liliopo katika Kitengo hicho ni sehemu ya utoaji wa filamu baada ya mgonjwa kupigwa X-Ray. Mfumo wa kazi hiyo ni wa kizamani sana wa kutumia mikono zaidi kuliko mashine *(Manual)*. Jambo ambalo sio tu halilileti ubora wa picha zinazo safishwa bali pia mfumo huo unahatarisha mno afya za wafanyakazi wa sehemu hiyo.

Pamoja na mazingira ya kazi yaliyopo lakini pia idadi ya wafanyakazi hao ni kidogo . kwa sasa ni wafanyakazi wawili tu wanaofanya kazi hiyo.

Halikadhalika Wizara haina mafundi wa kuzifanyia marekebisho mashine hizo na hivyo kwa maharibiko madogo tu inabidi zitumike fedha nyingi katika kuzifanyia matengenezo.

Maoni ya Kamati:

Serikali iondokane kabisa na mfumo wa usafishaji filamu uliyopo na badala kuwe na mtambo utakao rahisisha kazi na ulio salama kwa afya za wafanyakazi

Wizara itayarishe kwa makusudi kuwasomesha wafanyakazi wake ili waweze kumudu kufanya kazi za matengenezo kwa mitambo yetu badala ya kutegemea mafundi kutoka nje ya Wizara hata kwa matatizo madogo.

Suala la uajiri liendane na mahitaji halisi. Kwa maana hiyo Kitengo cha X-Ray kinahitaji wafanyakazi kwani waliyopo ni wachache mno.

Hoja Namba 16.5 Kuhusu Udhibiti na Utunzaji wa Mali za Wizara:

Ukaguzi umebaini kwamba, udhibiti na utunzaji wa baadhi ya mali za Wizara ya Afya hauridhishi. Hali hii imetokana na kutokuwepo kwa utunzaji mzuri, kutofanyiwa matengenezo

kwa muda husika na kuwepo kwa usimamizi usioridhisha. Hali hii imepekea Wizara kuingia katika gharama kubwa ya utunzaji na utengenezaji wa mali hizo na hatimae kushindwa kutoa huduma husika.

Maelezo ya Kamati:

Kamati iliyaona baadhi ya magari ambayo yako katika hali mbaya na hayawezi kufanya kazi tena tangu miaka ya thamanini sasa limechakaa mno, bodi yake limeanza kuoza. Aidha gari yenye Nam. SMZ 5719 CANTER ambayo ililala wakati Kamati inapita kwenye Wizara hiyo, gari hiyo ilikuwa inafanyakazi na gari yenye nam.SMZ 5657 tayari imeshauzwa.

Maoni ya Kamati:

Madereva ni lazima wasimamiwe kikamilifu katika suala zima la utunzaji wa vyombo wanavyovitumia.

Gari lenye Nam. ya usajili SMZ 3501 ambayo kwa sasa imeshaoza kabisa na gharama za matengenezo ni kubwa sana hivyo ifanyiwe utaratibu wa kuiondoa kisheria.

(RIPOTI YA TATU)

4.0 RIPOTI YA UKAGUZI WA HESABU KWA MAWIZARA, MASHIRIKA NA TAASISI ZA SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR KWA MWAKA WA FEDHA 2009/2010.

Ripoti hii inahusiana na ukaguzi wa mahesabu ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar pamoja na Taasisi zake mbali mbali na Mashirika. Katika kukagua hesabu za Serikali na Taasisi zake kwa ujumla, Ukaguzi uliofanyika umehusisha taarifa za mapato na matumizi ya fedha kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuzingatia Sheria ya Fedha na Kanuni zake za mwaka 2005, Sheria ya Manunuzi na Ugavi wa Mali za Serikali na Kanuni zake na Sheria zote zinazotungwa na Baraza la Wawakilishi, zinazohusiana na masuahala haya. Aidha, ripoti hii sambamba na uchunguzi uliofanywa na Kamati, imehusisha pia taarifa ya

matumizi ya kawaida kwa mnasaba wa majukumu na uwezo wa Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na matumizi ya kazi za Maendeleo. Na kwa upande wa mapato, Kamati ilifanya ukaguzi wa vyanzo mbali mbali vya ukusanyaji wake, na katika ripoti hii pia imehusisha taarifa za mapato hayo kwa kipindi cha mwaka 2009/2010. Ripoti hii imefafanuliwa kama ifuatavyo.

4.1 OFISI YA RAIS, FEDHA, UCHUMI NA MIPANGO YA MAENDELEO:

Hoja. Nam. 42.0, Kuhusiana na Mradi wa Huduma za Jamii (Zanzibar Urban Services Projects (ZUSP)):

Kwa mwaka 2009/2010 Mradi ulikusudiwa kutumia USD 1,228,474.99 ikiwa ni Mkopo kutoka Benki ya Dunia, na kwa mwaka huo wa 2009/2010, Mradi ulipokea USD 532,366.71 kwa ajili ya kuendeleza shughuli za kuimarisha mazingira na huduma za kijamii katika maeneo ya Mjini Unguja na Pemba. Mradi umepokea USD 35,332.03 ikiwa ni mchango wa Serikali ambapo kwa mujibu wa bajeti, ulipangwa kutumia USD 107,692.85.

Maelezo ya Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kuhusiana na Mradi:

Mradi huu haukuanzia 2008 hadi 2013 kama ilivyoelezwa na Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu, na badala yake umeanzia Juni 2011 hadi Juni 2016. Hadi kufikia Oktoba, 2012, Mradi huu umeshatumia USD 4,449,146.26, ambazo ni sawa na 11.71%, ingawaje fedha zenye thamani ya USD 1,478,349.88 ambazo zilitumika wakati wa marayarisho ya Mradi, hazihusiki katika idadi ya fedha zilizokwisha ingizwa. Fedha zilizotolewa na Benki ya Dunia ni 100%, ingawaje Serikali imeamua kuchangia katika maeneo ambayo Benki ya Dunia haiyagharamii kwa mujibu wa taratibu zake, kama vile Ujenzi wa Ofisi, Mishahara, Maposho pamoja na fidia kwa watakaoathirika katika utekelezaji wa Mradi. Aidha, hadi Oktoba 2012, USD 200.674 zimeshatumika kama mchango wa Serikali.

Maelezo ya Kamati:

Pamoja na maelezo ya hapo juu, Kamati ilipokuwa inafanya kazi katika Baraza la Mji wa Chake Chake, pamoja na Baraza la Mji, Wete, imepokea malalamiko mengi kuhusiana na utekelezaji wa Mradi huu, ikiwa ni pamoja na eneo la manunuzi ya magari ya kuzolea taka. Aidha katika Baraza la Manispaa Zanzibar, Kamati ilipokea malalamiko ya Uongozi wa Baraza hilo kutokuhusishwa katika utekelezaji wa Mradi, huku Uongozi huo ukiamini kwamba, ni wao waliohusika katika utayarishaji wake.

Maoni ya Kamati:

Kwa kuwa Mradi huu umeanza kutelezwa mwaka 2011, ambapo Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu bado hajatoa ripoti yake, Kamati inashauri kufanyiwa uchunguzi wa kina, ili hatimae

taarifa zake ziweze kufanyiwa kazi na Kamati. Aidha, kwa kutumia kanuni ya 52(5)(b) ya Kanuni ya Fedha ya mwaka 2005, Kamati inahitaji kupokea taarifa ya kina kutoka kwa wasimamizi wa Mradi, ili iweze kuuchunguza ipasavyo.

4.2 OFISI YA RAIS NA MWENYEKITI WA BARAZA LA MAPINDUZI :

4.2.1 BARAZA LA MANISPAA :

Hoja Namba 13.8 Kuhusu Ufungaji wa Hesabu za Mwisho wa Mwaka :

Kwa mujibu wa sheria ya fedha ya mwaka 2005, kifungu cha 24(2), ni wajibu wa kila Taasisi ya Serikali kufunga na kuwasilisha hesabu zake za mwisho wa mwaka katika Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali katika kipindi cha miezi mitatu baada ya kukamilika kwa mwaka wa fedha.

Baraza la Manispaa limeshindwa kufunga na kuziwasilisha hesabu za mwisho wa mwaka katika Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu, hali hii ni kwenda kinyume na sheria ya fedha Namba 12 ya mwaka 2005, kifungu cha 24(2). Aidha, Afisi ya Mdhibiti na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu, imeshindwa kutoa maoni juu ya hesabu za Baraza la Manispaa kutokana na kushindwa kuwasilishiwa hesabu hizo.

Maelezo ya Baraza :

Ni kweli walikuwa na tatizo hilo, ingawaje baada ya kupata muongozo wa Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu, wamerekebisha kasoro zao. Na katika kufanya hivyo, huwa wanapeleka mapato na matumizi yao ya kila mwaka kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu, ingawaje huwa hawapeleki ‘Fixed Asset Register’, kwani bado hawana utaalamu wa kuliandaa linavyotakiwa. Hata hivyo, wamo katika hatua za kuwasiliana na Chuo cha Uongozi wa Fedha, Chwaka, ili kuona namna gani watapata msaada huo.

Maelezo ya Kamati :

Pamoja na maelezo yote hayo, Kamati inasimamia hoja ya Mdhibiti kwamba Afisi ya Baraza la Manispaa haliwasilishi hesabu zake kwa Mdhibiti, na kufanya hivyo ni kukiuka sheria.

Maoni ya Kamati :

Kamati imeutaka Uongozi wa Baraza la Manispaa kuhakikisha kasoro hii haitajitokeza tena kuanzia mwaka 2013/2014. Aidha, kwa kitendo cha uzembe na kukiukwa sheria, kama ilivyofanyika awali, Kamati inaitaka Serikali kutoa onyo kwa Uongozi wa Baraza la manispaa na kutaka hili lisirejewe tena.

4.3 WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA AMALI:

Hoja Namba 41.1 Kuhusu Utekelezaji wa Mradi wa Elimu ya Lazima (Zanzibar Basic Education Improvement Project).

Mradi huu unaoshughulikia huduma za elimu kwa ajili ya maendeleo ya elimu Zanzibar, umehusika na ujenzi wa Maskuli, kutoa huduma za maabara, huduma za maktaba na huduma nyenginezo. Mradi ulipata fedha kutoka Serikalini na Benki ya Dunia kwa miaka mitano kuanzia 2008 jhadi 2013. Thamani ya Mradi wote ni USD 48,000,000 sawa na 72,000,000,000, huku 63,000,000,000 zikitolewa kuwa ni mkopo kutoka Benki ya Dunia na Tsh.6,000,000,000 kutoka Serikalini.

Lengo la Mradi ni kuongeza idadi ya wanafunzi wanaoingia skuli za sekondari na kuimarisha miundombinu na ubora wa skuli za sekondari; pamoja na kuimarisha ubora wa elimu kwa kuwapatia mafunzo walimu na kufanya mapitio ya mitaala na upatikanaji wa vifaa vyua kufundishia. Skuli zilizohusika na mradi huu ni hizi zifuatazo:

i. Skuli ya Matemwe; iliyopo Mkoa wa Kaskazini Unguja, ilikitengewa Tsh. 1,475,761,520 na ipo katika hatua za mwisho za ujenzi.

ii. Skuli ya Muwanda iliyopo Kaskazini Unguja, imetengewa Tsh.1,534,986,827, ipo katika hatua za mwisho za ujenzi.

iii. Skuli ya Chaani, iliyopo katika hatua ya mwisho ya ujenzi, imetengewa Tsh.1,297,683,591.

iv. Skuli ya Uzini, iliyopo Mkoa wa Kusini Unguja, ipo katika hatua za mwisho na imeingiziwa Tsh. 1,287,099,957, ipo katika hatua za mwisho za ujenzi.

v. Skuli ya Dole iliyopo Mkoa wa Mjini Magharibi, imeingiziwa Tsh.1,025,727,359 na ipo katika hatua za mwisho za ujenzi.

vi. Skuli ya Paje Mtule, iliyopo Mkoa wa Kusini Unguja, ipo katika hatua za mwisho za ujenzi na ilitengewa Tsh.1,329,956,779.

vii. Skuli ya Tunguu iliyopo Mkoa wa Kusini Unguja, ipo katika hatua za mwisho za ujenzi na ilitengewa Tsh.1,069,713,280.

viii. Skuli ya Dimani iliyopo Mjini Magharibi imetengewa Tsh.1,178,194,424, na ipo katika hatua za mwisho za ujenzi.

ix. Skuli ya Pandani iliyopo Kaskazini Pemba imetengewa Tsh.1,444,057,290 na ipo katika hatua za mwisho za ujenzi.

x. Skuli ya Chwaka/Tumbe iliyopo Kaskazini Pemba ipo katika hatua za mwisho za ujenzi na imetengewa Tsh.1,512,898,346.

xi. Skuli ya Konde iliyopo Kaskazini Pemba imetengewa Tsh.1,179,616,867 na ipo katika hatua za mwisho za ujenzi.

xii. Skuli ya Wawi iliyopo Kusini Pemba ipo katika hatua za mwisho za Ujenzi na imetengewa Tsh. 1,489,460,402.

xiii. Skuli ya Kiwani Mauwani, ipo Kusini Pemba na imetengewa Tsh.1,489,723,627 na ipo katika hatua za mwisho za ujenzi.

xiv. Skuli ya Ngwachani iliyopo Kusini Pemba imetengewa Tsh.1,044,394,909 na ipo katika hatua za mwisho za ujenzi.

xv. Skuli ya Utaani iliyopo katika hatua za mwisho za ujenzi, ipo Mkoa wa Kaskazini Pemba na imetengewa Tsh.1,232,866,581.

xvi. Skuli ya Mchanga Mdogo iliyopo Kaskazini Pemba, ipo katika hatua za mwisho za ujenzi na imetengewa Tsh. 1,947,433,900.

xvii. Skuli ya Shamiani ipo Mkoa wa Kusini Pemba imetengewa Tsh.1,663,434,950 na ipo katika hatua za mwisho za ujenzi.

xviii. Skuli ya Fidel Castro iliyopo Mkoa wa Kusini Pemba, inaendelea na ujenzi na imetengewa Tsh 1,822,811,000.

Aidha, kwa upande wa Huduma za Ushauri (Consultancy Services); Mradi huu pia umelenga kufanya mambo yafuatayo:

- Kitengo cha CS/12, kazi ya Kuimarisha walimu wa skuli za msingi kwa sayansi na hisabati, tarehe iliyopangwa kukamilika ni 22/07/2009, fedha zilizotengwa ni USD 4,000 wakati hatua ya utekelezaji inaeleza kwamba ripoti ya mwanzo imeshatayarishwa.
- Kitengo cha CS/29, kwa ajili ya mapitio ya mitaala kwa elimu ya Diploma ya msingi, ilitarajiwa kukamilika tarehe 20/12/2010, huku fedha zilizotengewa ni USD 45,000 na hatua ya utekelezaji inaonesha kwamba, ripoti ya mwanzo imetayarishwa.
- Kitengo cha CS/31 kwa ajili ya kufanya tathmini ya ushiriki wa wanafunzi wa kike katika masomo ya sayansi, ilitarajiwa kukamilika tarehe 6/6/2011, kwa thamani ya USD 20,000 na hatua iliyofikia ni kuendelea kwa tathmini.

Kuhusiana na kazi za Ujenzi, Mradi umegawiwa kwa vitengo kadhaa kama ifuatavyo:

- Kitengo cha CW/4 kazi zilizopangwa zinahusiana na Ujenzi wa Skuli ya Kwamtipura Unguja; Skuli ya Kiembesamaki, Unguja na Skuli ya Mpendae, Unguja. Skuli zote hizo

zilitajariwa kukamilika 22/02/2011, huku zikitengewa USD 2,350,524, ingawaje hadi wakati wa ukaguzi, skuli hizo zilikuwa zinasubiri ruhusa kutoka Benki ya Dunia.

- Kitengo cha CW/8 kilihusika na Ukarabati wa Skuli ya Forodhani, Unguja; Ukarabati wa Skuli ya Tumekuja, Unguja na Ukarabati wa Skuli ya Hamamni, Unguja. Kazi zote zilitarajiwa kukamilika tarehe 2/12/2010, huku zikitengewa USD 964,775, na ujenzi wa Skuli ya Forodhani na Tumekuja umechelewa kuanza ingawaje baadae kazi za ujenzi zilikuwa zinaendelea, huku Skuli ya Hamamni haijaanza kabisa shughuli za ujenzi.
- Kwa Kitengo cha CW/9 kazi iliyopangwa ni Ukarabati wa Skuli ya Fidel Castro, Pemba; Ukarabati wa Skuli ya Uweleni, Pemba na Ukarabati wa Skuli ya Utaani, Pemba. Kazi ilitarajiwa kukamilika tarehe 2/12/2010, na fedha zilizotengwa ni USD 3,124,021 wakati Ukarabati wa Skuli ya Fidel Castros na Skuli ya Utaani ulichelewa kuanza, huku Skuli ya Uweleni wakati wa ukaguzi ilikuwa bado haijaanza kukarabatiwa.

Maelezo ya Kamati:

Hoja hii imejadiliwa kwa kina katika Ripoti ya Ukaguzi Yakinifu kwa Miradi ya Taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kwa mwaka 2010/2011.

4.4 MASHIRIKA NA TAASISI ZINAZOJITEGEMEA:

4.4.1 SHIRIKA LA BIASHARA LA MAGARI :

Hoja Namba 30.1.2 Kuhusu Matokeo baada ya kufunga hesabu.

Shirika la Biashara la Magari, kwa mwaka 2009/2010, lilikuwa na mali za Mpito Tsh. 540,544,361.45 ambazo ni kidogo kuliko mwaka 2008/2009 ambapo ilikuwa ni Tsh. 621,428,122.26. Na kwa upande wa dhima za Mpito zilikuwa ni Tsh. 32,545,060 kwa mwaka 2009/2010, wakati mwaka 2008/2009 dhima hizo za mpito zilikuwa ni Tsh. 156,437,000. Hivyo, mali halisi za mpito kwa mwaka 2009/2010 ilikuwa ni Tsh. 507,999,301.45 wakati mwaka wa 2008/2009 ilikuwa ni Tsh.464,991,122.26.

Kuhusu uwezo wa kujiendesha kwa faida, Shirika limepata faida ya Tsh.73,019,914.90 kwa mwaka 2009/2010, faida ambayo imezidi mwaka 2008/2009 kwani ilikuwa ni Tsh. 63,722,386.09. hii inaonesha kwamba, faida ya Shirika imepanda kwa 14.58%. Kwa hivyo, Shirika linatakiwa kuchukua juhudi za makusudi za kuongeza mapato yake na kupunguza gharama za uendeshaji.

Maelezo ya Shirika:

Shirika limeupokea ushauri wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu na wanaendelea kuchukua juhudi mbali mbali za kuimarisha mapato ya Shirika. Aidha, katika juhudi walizozichukuwa pia ni pamoja na kupunguza madeni mbali mbali yanayoikabili, ingawaje

juhudi zao mara nyingi zinakabiliwa na utata wa hali halisi ya Shirika Serikalini. Hii inahusiana na mtazamo wa kuvunjwa kwa Shirika hili na Serikali kwa kuonekana halina faida.

Maelezo ya Kamati:

Kamati imepokea taarifa hiyo na imefahamishwa kwamba, Shirika pia linalipia kodi Serikalini ingawaje halipati ruzuku yoyote kutoka Serikalini. Hali ya wafanyakazi waliopo sasa ni 34 na wanataka kuajiri wafanyakazi wengine, ingawaje hawawezi kutokana na dhana ya kufungwa kwa Shirika hilo. Kwa mfano, Kamati iliarifiwa kwamba, mwaka huu wa fedha 2012/2013, Shirika halikuweza kufunga hesabu zake, kwa sababu hakuna Mhasibu.

Maoni ya Kamati:

Kamati inaitaka Serikali kutolivunja Shirika hili, kwa sababu kazi inayolifanya ni muhimu na itasaidia sana kukuza maendeleo ya Taifa. Aidha, Kamati inalitaka Shirika kuongeza juhudi za kuimarisha maendeleo yake.

4.4.2 SHIRIKA LA BIASHARA LA TAIFA (UNGUJA) :

Hoja Namba 32.1.1 Kuhusu Matokeo baada ya kufunga Hesabu :

Kwa mwaka 2009/2010, mali za Mpito za Shirika zilikuwa kidogo ukilinganisha na dhima za mpito za mwaka 2008/2009, ambazo zilikuwa ni Tsh. 4,989,749.111.80. Na kwa mwaka 2009/2010, Dima za Mpito zilikuwa ndogo kulinganisha na mwaka 2008/2009, huku hali halisi ya mali za Mpito kwa mwaka 2009/2010 ilikuwa ni Tsh. 1,871,015,750.36 wakati kwa mwaka 2008/2009 ilikuwa ni Tsh. 1,507,601,162.87. hali hii inaonesha Shirika lina uwezo wa kulipa dhima zake za mpito kwani uwiyano wa mali za mpito unaonesha ni 3:1 katika kipindi cha mwaka 2009/2010 ukilinganisha na mwaka 2008/2009 ambapo uwiyano wa mali za mpito na dhima za mpito zilikuwa ni 1.4:1.

Kuhusu uwezo wa kujiendesha kwa faida, Shirika lilipata mapato ya Tsh. 4,524,255,308.57 na kutumia Tsh. 7,579,246,950 ni sawa na hasara ya Tsh. 3,054,991,641.64 kwa mwaka 2009/2010. Kwa hivyo, Shirika linaonekana limepata hasara kubwa kwa mwaka 2009/2010 ukilinganisha na hasara iliyopata mwaka 2008/2009, ambayo ilikuwa ni Tsh. 272,484,828.11. Sababu kubwa ya hasara hiyo ni kuongezeka kwa gharama za kuendeshea kazi na gharama nyenginezo.

Maelezo ya Shirika:

Hasara iliyoelezwa hapo juu inatokana na Shirika kufuta deni lake lililokuwa linadai Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kwa mujibu wa makubaliano yaliyofikiwa. Hata hivyo, kutokana na ushauri waliopewa na Mshauri Mwelekezi wa Kimahesabu, deni lilipaswa lionekane kuwa ni mgawanyo wa mchango (Dividend) wa Shirika kwa mmiliki (shareholder) ambae ni Serikali.

Maelezo ya Kamati:

Kamati inalifahamu deni hilo na imekuwa ikilieleza tokea miaka iliyopita. Hata hivyo, Shirika linawajibika kutafuta njia mbali mbali za kuongeza mapato, huku matumizi ya Shirika, yanapaswa yazingatie uwezo halisi wa kifedha wa Shirika.

Maoni ya Kamati:

Kamati inalitaka Shirika kuongeza umakini katika suala zima la karafuu ili kuongeza mapato na kuondokana na kutumia fedha nyingi zaidi kuliko makusanyo yake.

Malipo ya Mkataba wa Ukodishwaji wa Ghala:

Shirika la Biashara, limeingia mkataba na Vitotoz Hatcheries & Poultry Co. kwa ajili ya ukodishaji wa ghala mnamo mwezi wa Agosti 2008, kwa mujibu wa makubaliano hayo, Mkodishwaji alitakiwa kuilipa Shirika la ZSTC jumla ya Tsh. 400,000 kwa mwezi kuanzia Januari 2009, lakini hadi ukaguzi unakamilika, mkodishwaji huyo bado hajalipa kodi hiyo.

Malipo yaliyotakiwa kulipwa na Mkodishwaji kuanzia Januari 2009 hadi Juni 2010, ambayo ni jumla ya miezi thalathini ni Tsh. 12,000,000.

Maelezo ya Shirika:

Ni kweli Shirika liliingia katika Mkataba huo na kustahili kulipwa Tsh. 400,000 kwa mwezi kuanzia mwezi wa Januari 2009, ni kweli malipo hayo hayakulipwa. Baada ya Shirika kutolipwa fedha zake na mteja huyo, lilichukua hatua mbali mbali za kumkumbushia kulipwa fedha zake, na mkodishaji hakuonesha dalili zozote za kutaka kulilipa deni hilo.

Hivyo, Shirika liliamua kufungua kesi ya Madai Mahakamani, hukumu ya kesi hiyo imeshatolewa na Mdaiwa alitakiwa kuhama, kulipia deni lake lote na gharama zote za kuendesha kesi hiyo.

Hata hivyo, bado Mdaiwa hajahama wala kulipa chochote, jambo ambalo liliifanya Shirika kurudi tena Mahakamani. Hivyo, hadi sasa bado wanaendelea kufanya mawasiliano na Mahakama kuhusiana na suala hili.

Maelezo ya Kamati:

Kamati imepokea kwa masikitiko taarifa hiyo, kwamba kesi tayari ilikwishamaliza na Shirika limeshinda, lakini utekelezaji wake bado mpaka leo unasuasua. Kamati haikuridhishwa na hatua zilizochukuliwa na Shirika, baada ya kupitia barua ya tarehe 21/03/2011 inayotoka Mahakamani yenye kumbu kumbu namba LD350 VOL:II/61, ilijiridhisha kwamba, Tayari Mahakama imeshamaliza kesi hiyo sasa ni upande wa Shirika kuitilia nguvu hukumu hiyo kwa ajili ya kupata haki zao. Kinachoonekana kwa Shirika ni kuridhika kuona wanadhulumiwa huku wakikunja mikono kwa kisingizio cha Mahakama bado haijawatendea haki.

Maoni ya Kamati:

Kamati inawaagiza Shirika la ZSTC, kutilia nguvu hukumu hiyo, ili waweze kupata haki.

4.4.3 SHIRIKA LA BIASHARA LA TAIFA (ZSTC-DAR ES SALAAM) :

Hoja Namba 33.1.1 Kuhusiana na Matokeo ya Hesabu za Mwaka, 2009/2010.

Kwa mwaka 2009/2010, mali za Mpito za Shirika zilikuwa kubwa ukilinganisha na dhima za mpito. Mali hizo zenye thamani ya Tsh. 191,808,935.60/- na dhima za Mpito Tsh.2,140,450/- zinafanya mali halisi ya mali za Mpito kuwa Tsh.189,668,485.60/-, hali iliyosababishwa zaidi na kuwepo kwa kiasi kikubwa cha mali ghafi za Shirika kwani mali ghafi hizo zimefikia wastani wa 76.43% ya mali zote za mpito, na kuufanya mzunguko wa biashara (Stock turnover) ni wa kuridhisha sana.

Kuhusu uwezo wa kujiendesha kwa faida, Shirika limepata faida ya Tsh.12,269,693.44 kwa mwaka 2009/2010, faida ambayo imepungua ukilinganisha na mwaka 2008/2009, iliyokuwa Tsh. 12,893,343.36. na hivyo, hakuna muwiyano mzuri wa mapato na matumizi.

Maelezo ya Shirika kuhusiana na Hoja hii:

Hali na Mali halisi za Mpito imechangiwa na hali halisi ya kibiashara kwamba, fedha ama mali zinazopatikana huzunguushwa tena katika mzunguko wa biashara. Aidha, uwezo wa Shirika umepungua kutokana na Bodi ya Shirika kuamua kufuata Tsh.13,736,660.10 ya deni lililokuwa inalidai kwa Taasisi mbali mbali za Serikali, kutokana na deni hilo kuwa la muda mrefu, bila ya mafanikio ya kulipwa.

Aidha, wakati huo, Tawi lilikuwa kama wakala wa Taasisi za Serikali, kulitumia na kupata huduma ya kununuliwa bidhaa na mahitaji mbali mbali Tanzania bara (Dar es Salaam), lakini kutokana na taasisi hizo kuamua kufuata bidhaa hizo wenyewe, Tawi limepoteza soko na kusababisha kuona hakuna haja tena ya kufanya biashara hiyo kwa Taasisi hizo.

Aidha, mapato ya kodi ya Nyumba yamepungua kwa sababu, tayari Shirika limejizuia kuendelea kukodisha sehemu ya Afisi yake, kwa sababu nao wamekodi kutoka Shirika la Nyumba la Taifa la NHC, aidha, kodi pekee wanayoitegemea ni ya Nyumba yao ya Sinza.

Maelezo ya Kamati:

Kuhusiana na Shirika kuwa wakala wa Taasisi za Serikali zilizopo Zanzibar, Kamati inaona ni jambo linalostahiki kuendelezwa na ni wajibu wa Serikali kulipa nguvu na kuweka utaratibu mmoja utakaosaidia na kuzifanya Taasisi hizo kulitumia Shirika ipasavyo.

Kamati imehoji uwezo wa Bodi ya Shirika, kuamua kufuta madeni ya Shirika, huku Baraza la Wawakilishi lililopewa dhamana hiyo kwa mujibu wa Sheria ya Fedha, kutokuwa na habari yoyote juu ya madeni hayo.

Maoni ya Kamati:

Kamati inaishauri Serikali kuweka utaratibu mmoja unaoeleweka kwa Taasisi zake kuangiza bidhaa Dar es Salaam, kwa kulitumia Shirika la Biashara la Taifa. Kufanya hivi kutasaidia ufanisi na matumizi mazuri ya fedha za Serikali.

Serikali iweke utaratibu mzuri wa kuwasilisha madeni ya Taasisi zake katika Baraza la Wawakilishi, ili yafahamike na yaweze kufuatwa kwa mujibu wa maelekezo ya Sheria.

Kuhusiana na kodi ya Nyumba ya Shirika, iliyopo Sinza, Kamati imelitaka Shirika kuandaa taarifa yake kwa kina, ikiwa ni pamoja na kuonesha gharama za kodi kwa kwa mujibu wa Mkataba, Taarifa za wapangaji na hata Mkataba wa ukodishwaji, ili suala hili liweze kufahamika kwa uwazi.

4.4.4 SHIRIKA LA BANDARI:

Hoja Namba 34.1.1 Kuhusu Matokeo baada ya Kufunga Hesabu.

Kwa ujumla Shirika linafunga mahesabu yake kwa wakati na matokeo ya hesabu yanonesha kwamba Shirika lina uwezo mkubwa wa kujiendesha, kwani katika mwaka wa 2009 mapato yalikuwa ni Tshs. 7.230 bil. Wakati ongezeko la mabadiliko ya thamani ya Dola ni Tshs. 0.642 bil. Na matumizi ni Tshs. 7.526 bil. Na kwa maana hiyo faida ni Tshs. 0.346 bil.

Kwa hivyo, takwimu za hesabu hiyo zinaonesha kwamba Shirika limeendelea kupata faida, ijapokuwa faida hiyo imechangiwa mno na ongezeko la mabadiliko ya thamani ya Dola pamoja na madeni ambayo uwezekano wa kulipwa kwake ni mdogo.

Maelezo ya Shirika

Wadaiwa wa Shirika

Shirika limekiri kuwa na wadaiwa wengi ambapo thamani ya deni hilo inafikia Tshs. 3.222 bil. Kiwango ambacho ni kikubwa mno na kinaathiri sura halisi ya mali za mapato za Shirika. Hasa kwa vile deni hilo ni la muda mrefu na uwezekano wa kulipwa ni mdogo.

Hii imesababishwa na utaratibu unaotumiwa kwamba Shirika hutoa huduma mwanzo na baadae na ndio Taasisi inayopewa huduma hiyo ndio hufanya malipo baada ya kutumiwa nyaraka zinazohusika.

Pamoja na madeni hayo yanayotokana na huduma aidha kuna madeni yaliyotokana na mikopo ya fedha taslim ambayo Shirika imeitoa. Lakini jambo jengine ni kwa zile Taasisi ambazo hupokea

huduma hizo na malipo yakawa kwa fedha za Kigeni kwa mfano Shirika la Meli kwa ajili ya huduma za mali za nje. Ambao deni lao lilifikia USD 1,861,029.05 kwa pamoja na fedha za ndani (Tshs. 66,917,169.48) ambapo mahesabu hayo yanaonesha kwamba Taasisi hiyo pekee deni lake ni asilimia 68.64 ya wadaiwa wote anaofata ni Wizara ya Fedha yenyewe deni lake linafikia asilimia 22.56.

Shirika limechukua jitihada za kutosha kufuatilia madeni hayo Serikalini na hatimae jitihada hizo zimepelekea kuundwa kwa Tume maalum ya kuangalia mwenendo wa mzima wa Shirika na wakati huohuo Tume hiyo kuunda Kamati Maalum ya Wataalamu ili kuweza kulipatia suala hili ufumbuzi wa haraka.

Maoni ya Kamati.

Shirika la Meli na Shirika la Bandari pamoja na Serikali kupitia Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleoili kumaliza suala la madeni yaliyopo.

4.4.5 SHIRIKA LA MELI NA UWAKALA :

Hoja Namba 35.1 Kuhusu Ufungaji wa Hesabu za Mwisho wa Mwaka 2009/2010.

Shirika la Meli na Uwakala, halikuwasilisha hesabu za mwisho wa mwaka kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa ajili ya kifanyiwa ukaguzi. Kwa vile ukaguzi wa mahesabu hayo haukufanyika, itakuwa vigumu kuweza kupata tathmini kuhusu hesabu hizo pamoja na hali ya kifedha ya Shirika.

Maelezo ya Shirika:

Pamoja na maelezo ya Mdhibiti, Shirika liliwasilisha hesabu hizo kinyume na maelezo ya Mdhibiti, na kama halikuwasilisha hesabu hizo, hata hizi hoja zilizowasilishwa kuhusiana na uwezo wa Shirika, zisingeliweza kuonekana katika ripoti hiyo. Aidha, hoja hii tayari Shirika lilifanya mawasiliano mapema kwa Mdhibiti nae alikubali kuiondoa katika ripoti, ingawaje wanashangaa bado kuona hoja hiyo hiyo imejitokeza tena.

Maelezo ya Kamati:

Pamoja na majibu hayo, Kamati inaamini kwamba Shirika halikuwasilisha hesabu hizo. Hii ina maana, kama hesabu hizo zingeliwasilishwa mapema ipasavyo, ni wazi kwamba hata katika ripoti hii lisingeliweza kuonekana. Hata hivyo, Shirika baadae limekiri kwamba ni kweli halikuweza kufunga zao za mwaka kwa wakati matokeo yake ziliwasilishwa kwa Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu zikiwa zimechelewa. Hata hivyo Shirika liliahidi mbele ya Kamati kwamba kwa sasa limejipanga na halitachelewesha tena kufunga na kuwasilisha mahesabu Afisi ya Mdhibiti.

Maoni ya Kamati:

Kamati inalitaka Shirika kuwasilisha hesabu zake za mwisho wa mwaka mapema kwa Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu.

4.4.6 BODI YA MAPATO:

Hoja Namba 38.0 Kuhusu Kutokuwasilisha Hesabu za Mwaka 2009/2010.

Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRB) haikuwasilisha hesabu zake za mwisho wa mwaka kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu kwa ajili ya kufanyiwa ukaguzi.

Maelezo ya Bodi

Bodi ya Mapato wamekiri juu ya jambo hilo na sababu kubwa ilikuwa ni kutokuwa na wafanyakazi mahiri na wenye uwezo huo katika sehemu ya Hesabu (Idara ya Uhasibu). Hivyo ilikuwa ni kasoro na sasa tayari wamekiimarisha kitengo hicho.

Maelezo ya Kamati

Kamati isingependa hata kidogo kuona chombo kama hicho kikubwa kinashindwa kuwa na watendaji wenye uwezo hasa katika kada ya Uhasibu ikizingatiwa kwamba wao ndio wakusanyaji kodi.

Maoni ya Kamati:

Kamati inaitaka Bodi ya Mapato kuwasilisha hesabu zake kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

(RIPOTI YA NNE)

5.0 RIPOTI YA UKAGUZI YA UKAGUZI WA HESABU KWA MAWIZARA, MASHIRIKA NA TAASISI ZA SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR, KWA MWAKA 2010/2011.

Ripoti hii inahusiana na ukaguzi wa mahesabu ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar pamoja na Taasisi zake mbali mbali na Mashirika. Katika kukagua hesabu za Serikali na Taasisi zake kwa ujumla, Ukaguzi uliofanyika umehusisha taarifa za mapato na matumizi ya fedha kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuzingatia Sheria ya Fedha na Kanuni zake za mwaka 2005, Sheria ya Manunuzi na Ugavi wa Mali za Serikali na Kanuni zake na Sheria zote zinazotungwa na Baraza la Wawakilishi, zinazohusiana na masuahala haya. Aidha, ripoti hii sambamba na uchunguzi uliofanywa na Kamati, imehusisha pia taarifa ya matumizi ya kawaida kwa mnasaba wa majukumu na uwezo wa Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na matumizi ya kazi za Maendeleo. Na kwa upande wa mapato, Kamati ilifanya ukaguzi wa vyanzo mbali mbali vya ukusanyaji wake, na katika ripoti hii pia imehusisha taarifa za mapato hayo kwa kipindi cha mwaka 2010/2011. Ripoti hii imefafanuliwa kama ifuatavyo.

5.1 OFISI YA RAIS, FEDHA, UCHUMI NA MIPANGO YA MAENDELEO:

Hoja Namba 9, kuhusiana na Ukaguzi wa Mafao ya Wastaafu:

Katika ukaguzi uliofanywa kuhusiana na viinua mgongo pamoja na fidia yanayolipwa na Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, pamoja na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (ZSSF), kumebainika kuwepo kwa udanganyifu unaofanywa na baadhi ya watendaji wanaotayarisha mafao ya wastaaafu kwa kuongeza kiwango cha mshahara kwa baadhi ya wafanyakazi wanaostaafu ili kuongeza kima cha mafao ya kiinua mgongo na pencheni. Hali hii imejitokeza kwa Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano, kama vile ilivyojitokeza kwa Kikosi cha Kuzuia Magendo (KMKM), kwa baadhi ya wafanyakazi ambao wameshastaafu na kutayarishiwa mafao yao ya kiinua mgongo na pencheni, bado mishahara yao inaendelea kupelekwa na kupokelewa kwenye Kikosi hicho, bila ya kufanya marekebisho ya kuwafuta au kurejesha fedha zilizopelekwa katika Kikosi hicho. Hivyo, kiasi ya Tsh.18,624,155 kwa kila mwezi zilikuwa zinapelekwa Kikosini kwa ajili ya mishahara na maposho na hivyo, hadi kufikia Marchi 2012, jumla ya Tsh.55,872,465 zimekwishapelekwa.

Maelezo kutoka kwa Ofisi ya Rais, Fedha Uchumi na Mipango ya Mendeleo; Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano pamoja na Kikosi cha KMKM kuhusiana na Hoja hii:

Hoja hii, ni kubwa na inahusisha mambo mengi, ni vyema kwa Kamati kuanza kuifuatilia kwa kukutana na Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano pamoja na Kikosi cha KMKM, Afisi ya

Mdhibiti na baadae Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo au kwa utaratibu itakaojipangia. Aidha, kuna Tume imeundwa na Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu, kuhusiana na suala hili, na kwa utaratibu, taarifa ya Tume hiyo itaipa nafasi na wepesi kwa Kamati kuifuatilia hoja hii kwa undani.

Maelezo ya Kamati:

Hoja hii inahitaji kufanyiwa kazi kwa muda mrefu na kwa kina, na kwa kuwa tayari kuna Tume imeundwa, Kamati haina pingamizi kuisubiria itoe taarifa yake, ili Kamati nayo ipate muelekeo mzuri wa kuifuatilia hoja hii.

Maoni ya Kamati:

Kwa kuzingatia kanuni ya 52(5)(b) ya Kanuni ya Fedha ya mwaka 2005, Kamati inahitaji taarifa za ziada juu ya hoja hii, na itaifanyia kazi siku zijazo.

Hoja Namba 1.1, Kuhusu Malipo ya Malimbikizo ya deni la Umeme kwa Taasisi za Serikali.

Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo imefanya malipo kwa ajili ya malimbikizo ya madeni yanayohusiana na matumizi ya umeme kwa Taasisi mbali mbali za Serikali, huku chanzo cha deni hilo hakitambulikani, aidha vielelezo vya mchanganuo na uthibitisho wa malipo hayo havikupatikana kwa Ukaguzi.

Maelezo ya Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kuhusiana na Hoja:

Chanzo cha madeni hayo inatokana na huduma ya umeme iliyotolewa katika vituo vya Afya vilivyopo chini ya usimamizi wa Wizara ya Afya na vituo vya maji vilivopo chini ya Mamlaka ya Maji (ZAWA) kwa upande wa Unguja na Pemba. Hali hii ilitokana na Taasisi hizo kushindwa kulipa deni hilo kwa wakati na hatimae kusababisha malimbikizo ya madeni hayo, huku mwanzo utaratibu uliokuwepo ni kwamba, madeni yote ya umeme yalikuwa yanalipwa na Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, kabla ya kuwa na utaratibu wa madeni hayo kulipwa na Taasisi iliyohusika. Aidha, kwa madeni hayo, na kutokana na upungufu wa fedha kwa taasisi hizo, iliamuliwa madeni hayo kuhamishiwa Mfuko Mkuu wa Serikali. Aidha, vielelezo vilivyohusika na ulipaji wa Tsh.250,000,000/- kati ya bakaa la Tsh.1,317,770,425 vipo.

Maelezo ya Kamati.

Kamati imeridhika na maelezo yanayoonesha chanzo cha deni, huku pia ikipokea vielelezo vya Tsh.250,000,000/- zilizolipwa kupitia Hati ya Malipo ya tarehe 17/09/2010, na kuambatanishwa na risiti ya malipo yenye namba 15258 ya tarehe 27/09/2010.

Maoni ya Kamati.

Kamati inasisitiza deni lililobakia la Tsh.1,317,770,425/ lilipwe kwa Shirika la Umeme, ili Shirika liweze kupata fedha za kujiendesha na kusimamia vyema majukumu yake.

Hoja Namba 1.2 kuhusiana na Jenereta lililonunuliwa kwa Tsh.302,351,400/-

Jumla ya Tsh.302,351,400 zimenunuliwa jenereta set 725 KVA, kutoka kwa Kampuni ya Mantrac Tanzania Limited, kwa kutumia njia ya T.T ya Public Debt ya tarehe 3/6/2011,ununuzi ambao haukufuata taratibu za Sheria ya Manunuzi, kinyume na Sheria Namba 9 ya mwaka 2005.

Maelezo ya Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kuhusiana na Hoja.

Utaratibu wa sheria umefuatwa katika ununuzi wa jenereta hilo. Ofisi imetumia njia ya 'Emergence Procurement', kwa mnasaba wa Kanuni ya 27(1) ya Kanuni ya Manunuzi ya mwaka 2005. Aidha, utaratibu wa Afis Mhasibu (Accounting Officer) kuweza kutoa taarifa kwa Katibu Mkuu wa OFisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo pamoja na kueleza sababu za kutumia njia hii, na nakla yake ikapelekwa kwa Bodi ya Zabuni ya Ofisi hii na nakla nyengine kwa Idara ya Uhakiki Mali, imefuatwa ipasavyo, kwa mnasaba wa tafsiri waliyoitumia wao.

Hali ya kutumia njia hii, imetokana na umuhimu wa kupatikana kwa jenereta hilo kwa Afisi ya Baraza la Wawakilishi, ili liweze kutekeleza majukumu yake ikiwa ni pamoja na kuendeshwa kwa vikao vya Baraza.

Maelezo ya Kamati:

Kamati imeshidhwa kuthibitishiwa uandishi wa barua kwa Naibu Katibu Mkuu wa Ofisi hii ambae ndie Afisa Mhasibu, kwenda kwa Katibu Mkuu wake, huku nakla zikawa zimepelekwa kwa Bodi ya Zabuni na Idara ya Ukahiki Mali. Kitendo cha kushindwa kuithbitishia Kamati kwamba, Bodi ya Zabuni haikukaa kama Bodi na kuridhia kutumika kwa njia hii, kinyume na maelekezo ya kifungu cha 32(2) cha Sheria Namba 9 ya mwaka 2005, na badala yake kutafsiriwa kumpa Kopi Afisa Manunuzi, kwa sababu yeye ndie pia Katibu wa Bodi ya Zabuni kwa niaba ya Bodi, kinahitaji zaidi kuthibitishwa kisheria.

Maoni ya Kamati:

Kamati haikuwa na uelewa mpana wa ufafanuzi uliotolewa na Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, kuhusiana na tafsiri na njia zilizotumiwa na Ofisi hii, na hivyo, haiwezi kuthibitisha kwamba Jenereta hilo limenunuliwa kwa kufuata ipasavyo taratibu za Manunuzi. Kamati inahitaji muda zaidi ili kulifuatilia kulifuatilia suala hili.

Hoja Namba 1.3 Kuhusiana na Hesabu za Mwisho wa Mwaka, 2010/2011.

Inahusiana na taarifa za Mapato ya Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, Matumizi yake ya kazi za Kawaida na Kazi za Maendeleo kwa mwaka huo. Kwa mwaka 2010/2011, Ofisi ilikadiriwa kukusanya Tsh.2,763 bilioni na kufanikiwa kukusanya Tsh.6.159 bilioni, sawa na 223% ya makadirio.

Kwa upande wa matumizi ya kazi za kawaida, iliidhinishwa kutumia Tsh.24.945 bilioni na kufanikiwa kukusanya 23.799 bilioni sawa na 95.41%, huku kazi za maendeleo ziliidhinishiwa Tsh.10.447 bilioni na kufanikiwa kuingiziwa Tsh.4.89 bilioni, sawa na 46.81%.

Maelezo ya Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, kuhusiana na Hoja.

Maelezo yaliyoelezwa na Mdhibiti kuhusiana na Hesabu zao ni sahihi.

Maelezo ya Kamati:

Ofisi inaweza kuongeza kukusanya mapato ya Serikali kwa kuwa makini zaidi na kuongeza wigo wa makusanyo. Kuna haja pia ya Ofisi hii kuangalia namna ya Serikali itakavyoweza kukusanya mapato kupitia mikataba inayofungwa na watu binafsi kwa kukodisha nyumba zao ama majengo yao, kwa Taasisi za Serikali ama watu wengine.

Maoni ya Kamati:

Kamati imeridhishwa na Ofisi kwa kwa kuongeza idadi ya makusanyo, huku ikishauriwa kuzidisha umakini wa makusanyo hayo.

Hoja Namba 1.4, Kuhusiana na Ufungaji wa Hesabu kwa Afisi ya Mtakwimu Mkuu pamoja na Mamlaka ya Ukuzaji Vitega Uchumi, Zanzibar (ZIPA):

Afisi ya Mtakwimu Mkuu pamoja na Mamlaka ya Ukuzaji Vitega Uchumi, Zanzibar (ZIPA), haziwasilishi hesabu zao kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu, pamoja na ukweli kwamba, ni Taasisi zinazojitegemea kiutawala na kiutendaji, na badala yake huunganisha taarifa hizo katika hesabu ya Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo. Hali hii, inapelekea Taasisi hizi kukosa uwezo wa kujipima kiufanisi katika mapato na matumizi.

Afisi ya Mdhibiti imezishauri Taasisi hizo kutayarisha hesabu zao moja kwa moja kwa Mdhibiti, ili ziweze kukaguliwa na kupima ufanisi katika mapato yao na matumizi, na utendaji kwa ujumla.

Maelezo ya Taasisi hizo kuhusiana na Hoja hii:

Ni kweli hapo awali hawakuwa wakiwasilisha hesabu zao moja kwa moja kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu, ingawa baada ya ushauri huo, wameshaaza kuwasilisha hesabu zao tofauti na hesabu za Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, kama walivyoshauriwa.

Maelezo ya Kamati:

Kamati imepokea taarifa hizo za mabadiliko yaliyotakiwa na kujiridhisha kwamba, hivi sasa Taasisi hizo zinawasilisha hesabu zao moja kwa moja kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu.

Maoni ya Kamati:

Kamati imeridhishiwa kwa kutekelezwa kwa maoni ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu, kwa lengo la kuleta ufanisi wa kifedha na kiutendaji kwa Taasisi hizo.

5.1.1 IDARA YA MHASIBU MKUU WA SERIKALI:

Kwa miaka yote hiyo ambayo Kamati ilikuwa inafuatilia Ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Idara ya Mhasibu Mkuu haikuwa na hoja kwani hakuna ukaguzi uliofanyika kama Idara, na badala yake imehusika na Wizara (Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo) moja kwa moja.

Hata hivyo, kwa mamlaka ya Kamati kama yanavyoelezwa katika kanuni ya 118(2)(c), ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi, Toleo la 2012, Kamati imefika katika Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali kwa lengo la kupata Ufafanuzi wa kazi zao na hesabu za matumizi yao kwa kazi za kawaida na kazi za maendeleo kwa mwaka 2010/2011.

Maelezo ya Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali:

Pamoja na Kamati kupatiwa maelezo ya matumizi ya Idara kama ilivyoomba, ilielezwa Muundo wa Idara na kazi zake. Na katika suala linalohusiana na Wakaguzi wa Ndani kwa Taasisi za Serikali, kama lilivyohojiwa na Kamati, ilielezwa kwamba, kuna ukosefu wa Wakaguzi hao, hali inayopelekea kukosekana kwa kila Taasisi ama Idara ya Serikali. Tatizo hili linachangiwa zaidi na kukosekana ruhusa ya Uajiri wao, huku Serikali ikikabiliwa na uhaba wa fedha.

Kamati pia ilihitaji kufahamu hatua gani zinazochukuliwa na Idara hii kwa Wahasibu wanaokiuka maadili ya kazi zao, na kuelezwa kwamba, ni suala linalohitaji zaidi mtazamo wa sheria zinazohusika.

Maelezo ya Kamati:

Kwa upade wa Wakaguzi wa Ndani, Kamati bado inaendelea kusisitiza haja ya kuajiriwa, ili kila Wizara, Idara ama Taasisi ya Serikali, iwe na Wakaguzi wa Ndani wa kutosha. Kuhusiana na suala la hatua zinazotakiwa kuchukuliwa kwa Wahasibu wanaokiuka maadili yao ya kazi, Kamati ina azma ya kukaa pamoja na wadau wote wanaohusika na Sheria na majukumu ya Kamati, kwa lengo la kueka mkakati wa pamoja juu ya njia zinazofaa kuchukuliwa.

Aidha, kwa upande wa matumizi ya Idara, baada ya kuwasilishwa kwake, Kamati imehitaji ufafanuzi wa Tsh.65,920,000/- zilizotumika kwa matumizi ya ‘Domestic’; Tsh.5,138,000/- zilizotumika kwa matumizi ya ‘Foreign’ na Tsh. 75,000,000/- zilizotumika kwa ‘Tuition Fee’, kwa mwaka 2010/2011. Ufafanuzi huo uambatane na vielelezo vilivyohusika. Vilelelezo hivyo kwa bahati mbaya havijawasilishwa kwa Kamati.

Maoni ya Kamati:

Kuna haja kubwa kwa Kamati kupatiwa mafunzo ya fedha, na kufahamu kwa karibu mfumo wa fedha za Serikali kupitia Idara hii. Kuhusiana na hesabu za Idara kama zilivyoelezwa hapo juu, Kamati haikupata muda wa kuzichunguza hesabu hizo na hivyo basi inahitaji kupata muda wa ziada kwa lengo la kufuatilia kwa kina, namna fedha hizo zilivyotumika.

Aidha, kuhusiana na ukaguzi wa hesabu mbali mbali zilitakiwa na Kamati, Kamati inahitaji muda wa ziada kuwasilishiwa taarifa zake na kuzikagua ipasavyo.

5.2 OFISI YA MAKAMO WA PILI WA RAIS:

5.2.1 TUME YA UCHAGUZI:

Hoja Namba 21.1 Kuhusiana na Manunuzi yenye thamani ya Tsh. 577,286,400/- ambayo hayakufuata Sheria za Manunuzi.

Afisi ya Tume ya Uchaguzi imefanya manunuzi ya vifaa mbali mbali, yaliyozidi kiwango kinachostahiki kuitishwa utaratibu wa zabuni, lakini manunuzi hayo hayakufuata sheria na kanuzi zinazohusika na manunuzi.

Maelezo ya Tume ya Uchaguzi:

Ni kweli kuna manunuzi yamefanyika, lakini wanaeleza kwamba wametumia kifungu cha 27(1) kinachoelekeza kufanyika kwa manunuzi kwa njia ya Haraka 'Emergency Procurement". Wamefanya hivi kwa sababu muda waliopata fedha ulikuwa hautoshi kutumia taratibu zilizobakia za Kuitisha Zabuni. Aidha, suala la ununuzi wa vifaa vya Uchaguzi lina mgongano wa kimaslahi, kwani hata Bodi ya Tume inataka manunuzi yote ya vifaa vya uchaguzi yafanywe chini ya usimamizi wake, huku Sheria ya Manunuzi nayo inaelekeza vyenginevyo.

Aidha, kwa kutumia njia ya 'Emergency Proccurement' Afisi ya Tume iliomba ruhusa ama kutoa taarifa kwa Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kama inavyoelekezwa na Sheria, lakini haikuweza kutoa nakla za barua hiyo kwa Bodi ya Zabuni wala Idara ya Mhakiki Mali, kama ambavyo Sheria hiyo hiyo inavyoelekeza.

Yote haya yamaesababishwa na kuwa na kazi mbili wakati mmoja, kusimamia kura ya Maoni ya July 2010, na Uchguzi Mkuu wa Oktoba, 2010.

Maelezo ya Kamati:

Kwanza manunuzi hayo yamefanyika baina ya mwezi wa August, wakati Uchaguzi Mkuu ulikuwa Oktoba, kuna kipindi cha kutosha cha kuifanya Afisi ya Tume angalau kutumia njia ya 'Qoutation and Proposal' kama ilivyoelezwa na kifungu cha 37 cha Sheria Namba 9 ya mwaka 2005, na sio kutumia 'Emergency'. Vile vile, manunuzi hayo hayahusishi Uchaguzi wa Kura ya

Maoni, na badala yake, yanahusiana na Uchaguzi Mkuu, hivyo, hoja za Afisi haziwezi kutegemewa.

Suala la Mgongano wa Kimaslahi halina mashiko, kwa sababu Bodi ya Tume haihusiki na masuala ya manunuzi. Aidha, Tume ilitakiwa kuwa na Mpango wa Manunuzi, ili kujipanga na kujua tokea mapema mahitaji iliyonayo.

Vile vile, wakati Kamati inapitia vielelezo vilivyohusika na malipo, imejiridhisha kwamba, manunuzi yote haya yamefanywa na Afisa Uagizaji, na wala sio Kitengo cha Manunuzi, kama inavyoelekezwa na Sheria. Sambamba na hilo, Kamati katika Hati za Malipo zilizohusika, hakukuwa na barua yoyote ya maombi ya mahitaji ya vifaa, na badala yake, ni Mikataba tu pamoja na Invoice ama Risiti ndizo zilizohusika. Ni sawa na kusema kwamba, Hati hizi za Malipo, zimekosa vielelezo vyote vilivyohitajika na Sheria.

Vile vile kuna baadhi ya Hati hizo zimekosa hata risiti za kupokelewa fedha, ili kujiridhisha kwamba, malipo yamefanyika. Kwa mfano Hati ya tarehe 27/10/2010 ya Tsh. 56,000,000/- haina maombi wala risiti. Ni hivyo hivyo kwa Hati Namba 0165 ya tarehe 22/10/2010 yenye thamani ya Tsh.68,000,000/- imekosa risiti kama vile ilivyokosa barua ya maombi. Jambo la kusikitisha ni kwamba, Mikataba ya hati hizo imesainiwa na Afisa Uagizaji, badala ya kusainiwa na Mkuregenzi wa Afisi ya Tume, ambae ndio Afisa Mhasibu wa Taasisi hii. Pamoja na kasoro zote hizo, Mkurugenzi wa Tume, ameomba radhi udhaifu uliojitokeza, huku akiiahidi Kamati kutorejea tena kwa kasoro hizo.

Maoni ya Kamati.

Kamati haikuridhika na inapendekeza hatua zaidi zichukuliwe ikiwa ni pamoja na kupewa onyo kwa Watendaji waliohusika na kasoro hizo, huku ikiitaka Afisi hii ichukue hatua za haraka kurekebisha kasoro na hatimae zisiweze kujitokeza tena.

5.2.2 IDARA YA UPIGAJI CHAPA:

Hoja Namba 20.1 Kuhusu Madeni ya Idara ya Upigaji Chapa, Tsh. 15,889,530/-.

Idara ya Upigaji Chapa inadaiwa na wafanyabiashara mbali mbali kwa huduma zilizotolewa katika taasisi hizo. Wadeni hao ni Abrahman Ismail Vuai; Habari Maelezo; Almafazy Computer Services; Visiwani General Suplier ; Government Print, Dar es Salaam; One to One Ltd; Zanzibar University; Siti Mohammed Mussa na Nopal Engeneering.

Maelezo ya Idara ya Upigaji Chapa kuhusiana na Hoja hii.

Deni la Abrahman Ismail Vuai, la Tsh. 219,100/- tayari limeshalipwa. Deni la Habari Maelezo la Tsh. 110,000/- tayari limeshalipwa. Deni la Almafazy Computer Services, tayari limeshalipwa. Deni la Visiwani General Suppliers la Tsh. 718,030/- tayari limeshalipwa. Deni la Government Print, bado halijalipwa. Deni la One to One Ltd, tayari limeshalipwa. Deni la Zanzibar

University lilitokana na mfanyakazi wao aliesoma na kubahatika baadae kupata mkopo, tayari anakatwa mshahara wake na Bodi ya Mkopo wa Elimu ya Juu. Deni la Siti Mohammed Mussa, tayari limeshalipwa na deni la Napol Engineering limeshalipwa. Kwa ujumla Idara sasa inadaiwa Tsh. 11,250,000/- kutoka Government Print, Dar es Salaam.

Maelezo ya Kamati:

Pamoja na malipo hayo kufanyika, fedha zilizotumika zimehaulishwa kutoka kifungu cha 'Printing Materials', huku Kamati ikielezwa kwamba, Idara haihusiki na taratibu za Uhaulishaji ambazo zinafuatwa Wizarani. Aidha, madeni hayo yanatokana na uhaba wa fedha kwa Idara hii, huku wakilazimika kwenda kwa Mfanyabiashara huyo huyo, kinyume na taratibu za manunuzi, kwa lengo la kukopa na baadae kurejesha. Baadhi ya Hati za malipo zilizohusika, zimekosa barua ya maombi kutoka kwa Kitengo cha Mtumiaji, ili kuona uhalali na haja ya matumizi yaliyofanyika.

Deni lililobakia la Government Print, Dar es Salaam, la Tsh.11,250,000/- limeelezwa kusababishwa na haja ya kupring kopi 5000 za Katiba ya Zanzibar, huku kila kopi iligharimu Tsh.2500/-. Iwapo kazi hiyo ingelifanyika katika mashine za Idara hii, Zanzibar, kusingekuwa na haja ya kuwepo kwa deni hilo.

Maoni ya Kamati :

Kamati imeridhishwa na juhudi za Idara za kulipa madeni. Aidha, Kamati inaishauri Serikali, kuiendeleza Idara hii ikiwa ni pamoja na kuingizia fedha za kutosha, ili isitokezee haja ya kazi za Uchapishaji wa taarifa za Serikali, kuchapiswa Tanzania bara ama nje ya nchi.

5.3 OFISI YA MAKAMO WA KWANZA WA RAIS:

Hoja Namba 23.1 Kuhusiana na Hesabu za Mwisho wa Mwaka, 2010/2011:

Afisi imefanikiwa kukusanya 1,890,000/- pekee kati ya makadirio ya Tsh. 6,000,000/-, huku ikiingiziwa Tsh. 624,914,000/- kwa matumizi ya kawaida mbali na makadirio ya Tsh. 686,736,000/-. Aidha kwa kazi za Maendeleo, Ofisi iliingiziwa Tsh. 180,000,000/-.

Maelezo ya Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais, kuhusiana na Hoja hii:

Makadirio ya 6,000,000/- yanajumuisha ukusanyaji wa vyeti vya mazingira na vibali vya misitu. Kwa kuwa vibali vya misitu sasa vimehamishiwa katika Idara ya Misitu, chini ya Wizara ya Kilimo na Maliasili, uwezekano wa kufikia kima kilichowekwa kwa mujibu wa makisio ni mdogo. Aidha, kuhusu matumizi ya fedha kwa kazi za kawaida na Maendeleo, Uongozi wa Wizara umesema kwamba, fedha zilizoingizwa na kutumika, hazikuwa zile zilizokadiriwa kutokana na upya wa Wizara hii.

Maelezo ya Kamati:

Pamoja na makusanyo ya Wizara kuathiriwa na muundo wa Wizara hii, kuna haja ya kufanya mapitio ya Sheria inayohusiana na Mazingira, ili kuona namna itakavyoweza kudhibiti utunzaji wa mazingira lakini pia kuongeza kima cha mapato husika.

Maoni ya Kamati:

Kamati haikuridhika na hali halisi ilivyo, na hivyo inapendekeza Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais, ichukue juhudi za kuongeza mapato yake.

Mradi wa Mitaro ya Maji ya Mvua na Machafu, Shehia ya Msingini na Kichungwani, Chake Chake, Pemba.

Mradi huu haukuhusika na hoja yoyote ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu, ingawaje, Kamati imetembelea eneo liliopo Mradi huu, na kuona ipo haja ya kupata ufafanuzi zaidi.

Maelezo ya Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais:

Baada ya kuonekana uchafuzi mkubwa wa kimazingira, ndipo ilioonekana haja ya kuwepo kwa Mradi huo ulianza mwaka 2009 na kugharimu Tsh. 589,883,490/- hadi kumalikia kwake, hata hivyo, bado haujakabidhiwa kwa Mamlaka husika, ingawa unaaminika umeshakamilika kwa asilimia kubwa. Mradi huu pia ulihusisha Mchango wa TASAF kwa Shehia Mbili, ya Msingini na Kichungwani.

Mradi ulihusisha Ujenzi wa Mtaro wa maji ya mvua; ulazaji wa mambomba ya kupitishia maji machafu; ujenzi wa mabwawa mawili ya kuhifadhia maji machafu na kusafishia maji machafu; Uunganishaji wa mabomba ya maji machafu kutoka majumbani na ujenzi wa chemba za ukaguzi, pia ulihusisha pia mafunzo mbali mbali kwa wahusika.

Maelezo ya Kamati:

Kamati imepatiwa maelezo ya fedha zilivyotumika, bila ya kukabidhiwa kwa vielelezo vinavyohusika na matumizi ya fedha hizo. Ili kujiridhisha kwa njia ya mfano halisi (sampling), Kamati imehitaji kupata ufafanuzi wa Posho la Meneja wa Mradi, Tsh.6,420,000/-; Gharama za safari kwa Mshauri Mwelekezi Tsh. 2,365,000/-; na safari za kimafunzo kwa Wasimamizi, Wahandisi na Wapimaji katika Manispaa ya Moshi, Tsh.1,750,000/-. Vielelezo hivyo viliwashilishwa kwa Kamati, lakini kutokana na uchache wa muda, Kamati imeshidwa kuvikagua.

Maoni ya Kamati:

Kamati haikuridhika na utekelezaji wa Mradi huu, hasa kwa kwa kiwango duni cha utaalamu ulivyotumika. Hivyo, kuna haja kubwa ya kushirikishwa ipasavyo kwa wananchi wanaozunguka eneo la Mradi, ili uelewa wao ukasaidia katika utekelezaji wa mradi.

Kwa kuzingatia taarifa ilizoarifu kupatiwa, na kwa kutokana na uchache wa muda, Kamati bado inahitaji kupata taarifa hizo na muda wa ziada, ili kuchambua matumizi ya fedha husika.

5.4 OFISI YA RAIS NA MWENYEKITI WA BARAZA LA MAPINDUZI :

5.4.1 KIKOSI CHA KUZUIA MAGENDO (KMKM) :

Hoja Namba 5.1 Kuhusu Matumizi yaliyofanyika kinyume na vifungu, Tsh.23,752,820

Ukaguzi umebaini kwamba, kuna baadhi ya malipo yamefanyika kinyume na vifungu vilivyoidhinishwa na Baraza la Wawakilishi. Aidha, ukaguzi umebaini taratibu za uhaulishaji hazikufuatwa.

Maelezo ya Uongozi wa Kikosi, kuhusiana na hoja hii :

Kikosi cha KMKM kimekiri kwamba kimefanya matumizi hayo kinyume na vifungu vilivyopangiwa, hii imetokana na sababu zifuatazo:-

a) Uharaka wa matumizi husika

b) Vifungu kuishiwa na fedha

c) Utaratibu wa uhaulishaji kuwa na urasimu mkubwa.

Hata hivyo kuna baadhi ya vifungu vimeainishwa na Mkaguzi kimakosa kwamba matumizi yake yalikuwa sahihi na yaliyofata utaratibu, kinyume na Mdhibiti alivyonukuu. Kwa mfano Hati Nam. 3/6 vocha Nam. 3737308 yenye thamani ya malipo ya Tss. 2,034,000 ambapo jina la kifungu ni matengenezo ya majengo na matumizi yake yalikuwa sahihi kwani yalihusu Ujenzi.

Maelezo ya Kamati:

Pamoja na utetezi uliowasilishwa mbele ya Kamati, Kamati imejiridhisha kwamba, kwa ujumla taratibu za uhaulishaji hazikufuatwa, na hoja kwamba Sheria imeweka urasimu juu ya utekelezaji wake, haina mashiko wala haiwezi kukubalika.

Maoni ya Kamati.

Pamoja na ukweli kwamba mazingira ya aina hiyo yanaweze kutokea lakini bado taratibu za uhaulishaji wa vifungu na nyengine kwa mujibu wa taratibu za matumizi ya fedha zitumike. Kamati imejiridhisha kwamba, taratibu za kisheria hazikufuatwa na hivyo, inaitaka Serikali kutoa onyo kwa Afisa Mhasibu wa KMKM.

Hoja Nam. 5.2 Kuhusiana na Malimbikizo ya Madeni Tshs. 201,620,000.

Ukaguzi umebaini kwamba, kikosi cha KMKM kinadaiwa na wafanyabiashara pamoja na Taasisi mbali mbali kwa ajili ya utowaji wa huduma tofauti kwa kikosi hicho. Ukaguzi umeshindwa kuthibitisha uhalali wa madeni hayo kutokana na kukosekana kwa vielelezo vilivyosababisha deni hilo.

Maelezo ya Kikosi

Kikosi kimekiri kuwa na deni hilo ijapokuwa kiwango hicho cha Tshs. 201,620,000 sio deni la sasa kwani hesabu hiyo ni ya deni la nyuma sana ambalo tayari limeshaanza kupunguzwa. Hadi Kamati inatembelea deni lililobakia ni Tshs. 131,320,000/-

Hata hivyo kikosi kinaendelea na uchanganuzi wa uhalali wa madeni hayo na kila deni litakalobainika kwamba ni halali litalipwa. Hii yote imetokana na utata ambao umesababishwa na kwamba hapo awali Kikosi hakikuwa kikitangaza Tenda katika manunuzi yake, hakukuwa na mpango wa manunuzi (***Procurement Plan)*** halkadhalika maombi ya kazi na kupatiwa huduma yalikosa utaratibu.

Maelezo ya Kamati:

Kwa kuwa Sheria inayozungumzia utaratibu wa manunuzi na ugavi wa mali za Serikali imeanza tokea mwaka 2005, na hapo kabla pia kulikuwa na Sheria inayohusiana, Kamati haioni busara kwa Uongozi wa Kikosi, kuridhika kwamba hapo awali hawakuwa wakifuata taratibu zinazostahiki, kwa hoja tu kwamba, sasa wameshajipanga kutekeleza majukumu yao ipasavyo. Hata hivyo, Kamati imefurahishwa na ukweli unaoelezwa na Kikosi kuhusiana na hali halisi ilivyo, jambo ambalo litaisaidia Serikali kurekebisha kasoro hizo kwa vikosi vyengine vilivyosalia.

Maoni ya Kamati.

Kwa vile sasa kuna utaratibu mzuri wa matumizi ya fedha katika kununua na kupata huduma nyenginezo, Kamati inasisitiza haja ya kuendelezwa huku mchakato wa kuyachanganua madeni ya nyuma ukiendelea ili hatimae wale wote wanaostahiki kulipwa walipwe. Kwa ufupi, Kamati inaagiza madeni hayo yalipwe.

Hoja Nam. 5.3 Kuhusiana na Mapato ya Kikosi Tshs. 610,507,490.

Ukaguzi umebaini kwamba, Kikosi cha KMKM katika mwaka 2010/2011 kimelipwa kiasi kikubwa cha fedha kutoka Taasisi mbali mbali za Serikali, kutokana na na utowaji wa huduma ya ujenzi. Hata hivyo, mapato hayo yameshindwa kukaguliwa kutokana na kukosekana kwa taarifa na madaftari yanayohusiana na makusanyo hayo. Aidha, makusanyo hayo hayakuingizwa katika hesabu za mwisho wa mwaka za Kikosi.

Maelezo ya Kikosi

Kikosi kimekiri kwamba kimekuwa kikipata mapato ambayo yalikuwa yakitumika katika kupunguza nakisi ya Bajeti wanayopewa na Serikali. Katika kufanya hivyo utaratibu wa malipo yao hupitia Nambari ya Akaunti yao ya Canteen na kutolewa kwake kunategemea kazi iliyotolewa. Hesabu zake za mapato na matumizi huwasilishwa mwishoni mwa kila mwaka mbele ya Mkutano mkuu wa Kikosi.

Aidha hakukuwa na utaratibu wa kuyaingiza mapato hayo kama ni sehemu ya mapato ya Serikali jambo ambalo utaratibu wake haukumuwezesha Mdhibiti kuweza kuzikagua hesabu zake.

Hata hivyo baada ya maelekezo hesabu hizo zimeahidiwa kwamba sasa zitafata utaratibu wa kukaguliwa kama zilivyo hesabu nyengine.

Maelezo ya Kamati.

Kwa kawaida mapato na matumizi mara nyingi hutia shaka yasipokuwa na usimamizi lakini pia ukaguzi wake. Hivyo, bado taratibu zinahitajika ili kuondoa shaka hiyo na kuleta ufanisi ulio wazi kwa kile kilichokusudiwa.

Maoni ya Kamati.

Kamati inakiagiza Kikosi kuyawasilisha mapato hayo katika hesabu zao za mwisho wa mwaka ili ziweze kukaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Aidha, mapato ya Miradi na kazi za Kikosi yaainishwe kwa kufata utaratibu na Kikosi kiwe na Mkaguzi wa Ndani wa Hesabu atakaeweza kushauri matumizi mazuri ya rasilimali kwa majibu wa taratibu za Sheria ya fedha.

Aidha, kutowasilisha hesabu hizi za Canteen katika hesabu ya mwisho wa mwaka, ni kukiuka kifungu cha 24(2) cha Sheria Namba 12 ya mwaka 2005, na kwa kuwa Afisa Mhasibu wa Kikosi cha KMKM amekiuka maelekezo hayo ya Sheria, Kamati inaitaka Serikali kutoa onyo na kumtaka yeye na Mhasibu wake, kuhakikisha hesabu hizo zinawasilishwa na kukaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu.

5.4.2 KIKOSI CHA VALANTIA:

Hoja Namba 6.1 Kuhusu Matumizi yaliyofanywa kinyume na vifungu, Tsh. 21,529,660:

Imebainika kwamba,kuna baadhi ya malipo yamefanyika kinyume na vifungu vya matumizi, kama vilivyoidhinishwa na Baraza la Wawakilishi, huku taratibu za uhaulishaji nazo hazikufuatwa.

Maelezo ya Kikosi

Kikosi kimekiri kwamba ni kweli baadhi ya vifungu matumizi yake hayakuendana na vifungu halisi vilivyopangiwa matumizi hayo na hii inatokana na mambo yaliyojitokeza wakati kwenye Kasma za matumizi mkiwa hamna fedha, ama hazijaingizwa au zimemalizika lakini haja ya

matumizi ikiwa bado ipo. Walitoa mfano wa uchakavu mkubwa wa magari na mahitaji makubwa ya mafuta.

Kwa ujumla matumizi yote yalikuwa yanahusu malipo ya vipuri na ununuzi wa diseli na hayo ndio yaliyoonekana kwenye matumizi ya vifungu vingine.

Maelezo ya Kamati:

Pamoja na udhuru uliotolewa na Kikosi, Kamati haikubaliani na hoja zilizowasilishwa, kwa sababu sheria inatoa muongozo mzuri juu ya hatua zinazofaa kuchukuliwa kwa lengo la kukabiliana na hali hii.

Maoni ya Kamati.

Kamati imekitaka Kikosi kiendelee kufata sheria za fedha katika matumizi ili kuweza kujenga muamala mzuri wa bajeti ***(Budget discipline)***.

Aidha, kuwa na mipango mizuri ya bajeti kuhakikisha kwamba linalopangwa basi liendane na matumizi halisi na kama dharura ikitokea basi isiwe kwenye kiwango kikubwa kama hicho cha Tshs. 21,529,660/-.

Vile vile, Kamati inawafahamishwa watendaji wa Kikosi cha Valantia kwamba, kutumia fedha kinyume na kufuata taratibu za uhaulishaji ni kukiuka masharti ya kifungu cha 51 cha Kanuni za fedha za mwaka 2005, na kwa kuwa Afisa Mhasibu wa Kikosi hiki, Mhasibu Mkuu wa Kikosi pamoja na watendaji wengine wa fedha waliohusika, wamekengeuka masharti ya kifungu hicho, Kamati inaitaka Serikali kutoa onyo kwa Uongozi wa Kikosi pamoja na watendaji wa fedha waliohusika.

Hoja Nam. 6. 2 Kuhusiana na Malimbikizo ya deni Tshs. 246,474,000.

Kikosi kinadaiwa na Taasisi zinazotoa huduma za upatikanaji wa sare kwa ajili ya matumizi ya Vikosi. Malimbikizo hayo ni ya muda mrefu na hakuna dalili za kulipwa kwa madeni husika.

Maelezo ya Kikosi

Kikosi kimekiri kuwepo kwa deni hilo na kuhusiana na deni la Regalia Tanzania Ltd, wameshauriwa na mkaguzi wa nje kutolilipa kwani hawana fedha maalum za kulipia deni hilo, kwa mwaka huu wa fedha. Kuhusiana na deni la Zanzibar Tailoring Ltd, wamejitahidi kulipunguza na sasa linafikia Tsh.3,840,000.

Maelezo ya Kamati:

Pamoja na maelezo hayo, suala la malipo ya deni ni lazima lifanywe na hivyo, ni wajibu wa Kikosi na Serikali kwa ujumla kuhakikisha kwamba madeni hayo yanalipwa.

Maoni ya Kamati

Kamati imeridhishwa na juhudi zilizochukuliwa za kulipa madeni kwa Zanzibar Tailoring Ltd, na kukitaka Kikosi kihakikishe deni hilo linamaliza kulipwa. Aidha, kwa Regalia, Kikosi kihakikishe deni linalipwa haraka iwezekanavyo, ili kuepusha kuwa na mzigo mkubwa wa madeni kwa Kikosi.

5.4.3 JESHI LA KUJENGA UCHUMI:

Hoja Namba 7.1 Kuhusiana na Matumizi yaliyofanyika kinyume na Vifungu, Tsh.66,603,060.

Ukaguzi umebaini kwamba, kuna baadhi ya malipo yamefanyika kinyume na vifungu vilivyoidhinishwa na Baraza la Wawakilishi, pia utaratibu wa uhaulishaji haukufuatwa.

Maelezo ya Uongozi wa J.K.U kuhusiana na hoja hii:

Pamoja na maelezo ya Mdhibiti kuhusu idadi kamili ya fedha hizo kuwa ni Tsh.66,603,060, lakini usahihi wa fedha hizo ni Tsh.61,453,060, ambapo Tsh. 21,013,800 zilizotumika kununulia mafuta zilizotoka katika mafungu mawili tofauti. Hii inatokana na fungu halisi la mafuta hadi kufikia Disemba 2010 lilikuwa limebakisha kiasi ya Tsh.3,000,000 tu ambazo zisingelikidhi kwa matumizi yaliyokusudiwa. Kwa kuwa suala la ulipaji wa mafuta lilikuaw ni la haraka sana, ndipo JKU wakalazimika kutumia mafungu mengine ambayo matumizi yake waliyaakhirisha kwa kipindi.

Tsh.1,500,000 ambazo zilianishwa kwamba, zimetumika kwa safari, usahihi wake ni kutumika kwa kulipia umeme. Na Tsh.9,000,000 kutoka fungu la mafunzo ya ndani, zimetumika kulipia sehemu ya deni la gari kutokana na kujitokeza haja ya kuwa na gari na wakati huo fungu la gari halikuwa na fedha. Aidha, fungu la safari nalo hadi kufikia April 2011 lilikuwa limekwisha na ndipo walilazimika kutumia mafungu mengine ambayo yalikuwa na fedha ili kuweza kusaidia gharama mbali mbali zikiwemo za safari. Na ndipo Tsh.7,500,000 zimetumika kuwasafirishia Wajumbe wa Kamati ya Mashirikiano ya JKU na JKT pamoja na kufanya kikao cha pamoja na kikao cha Kamati hiyo.

Vile vile JKU walikuwa wanapata wastani wa Tsh.1,720,000 kwa kila mwezi kama ni kasma ya chakula ambayo walikuwa wanaiongezea katika fedha wanazokatwa askari ili kuboresha huduma ya chakula chao, na ilipofika April/May 2012, kasma hii ilikuwa imebakia Tsh.620,000 pekee na hivyo ililazimika kutoa fedha kutoka katika fungu hili la Hoteli, Tsh. 1,100,000 ili kukidhi matumizi hayo.

Kwa ujumla hali ya kufanya matumizi kinyume na vifungu vilivyoidhinishwa na Baraza la Wawakilishi, inatokana na ukosefu wa fedha kwa Jeshi la Kujenga Uchumi (JKU).

Maelezo ya Kamati:

Kamati haikuridhsishwa na maelezo ya Kikosi kuwa tayari kuvunja sheria za fedha kwa hoja tu ya uchache wa fedha. Kamati inaamini iwapo JKU wangelikuwa makini wakati wa utayarishaji wa bajeti yao, matatizo haya yasingelitokezea.

Maoni ya Kamati:

Kamati inawafahamisha Afisa Mhasibu, Mhasibu Mkuu wa Kikosi na watendaji wote wa fedha waliohusika na matumizi haya kinyume na taratibu zilizoelezwa na kifungu cha 51 cha Kanuni za Fedha za mwaka 2005. Kwa hivyo, Kamati imetoa onyo kwa Afisa Mhasibu wa Kikosi cha JKU pamoja na Mhasibu na watendaji wengine wa fedha kuwa kutofuata taratibu za fedha.

Hoja Namba 7.2 Kuhusiana na Malimbikizo ya Madeni Tsh.297,748,444.

Kikosi cha JKU kinadaiwa na Taasisi zinazotoa huduma za upatikanaji wa sare pamoja na huduma mbali mbali kwa ajili ya matumizi ya Vikosi. Malimbikizo hayo ni ya muda mrefu na haioneshi kwamba kama kuna juhudi zinazochukuliwa ili kusawazisha madeni hayo.

Maelezo ya Kikosi cha JKU.

Ni kweli JKU wanakabiliwa na changamoto kubwa ya madeni katika bajeti yake, ambayo kwa kiasi kikubwa yanaathiri utekelezaji wa malengo na kazi za kila siku za JKU. Hata hivyo, pamoja na hali hiyo, JKU wanaendelea kuchukua hatua za namna yoyote kupunguza madeni inayodaiwa, huku ikielekeza kwamba, madeni hayo zaidi yalisababishwa na matumizi makubwa ya uniform zilizonunuliwa kwa ajili ya sherehe za Mapinduzi.

Juhudi zilizochukuliwa na hatua iliyofikia ni kama ifuatavyo :

- Mdai Regalia aliekuwa anadai Tsh. 125,200,000, JKU wanaendelea kulipa kidogo kidogo huku Serikali pia imetaka kulikabidhi kwake kwa hatua zaidi.
- Mdai Sabah Store, aliyekuwa anadai Tsh. 66,000,000 wameshamaliza kumlipa deni lake.
- Mdai Moh'd Zahor aliekuwa anadai Tsh. 22,955,200, tayari JKU wameshamlipa fedha zote na limebaki deni la Tsh.5,000,000 pekee.
- Mdai Ali Mussa Makame, aliekuwa anadai Tsh.2,800,000, tayari wameshamaliza deni lote.
- Mdai Shirika la Umeme, aliekuwa anadai Tsh.76,828,244 bado hawajalipa deni hilo, ingawa kuna mazungumzo juu ya deni hilo yanaendelea na kwa kuanzia wamefungiwa mita za luku ambapo kila wakinunua umeme, huwa wanalipa deni lao la awali.
- Mdai Zanzibar Quality Tailoring Ltd, aliekuwa anadai Tsh. 1,605,000, tayari wameshamaliza deni lote
- Mdai Mamlaka ya Maji, Pemba, aliekuwa anadai Tsh.5,360,000, JKU wanaendelea na hatua za malipo.

Maelezo ya Kamati:

Pamoja na maelezo ya JKU kuhusiana na deni hilo, Kamati kwanza imehitaji kupatiwa uthibitisho wa deni hilo, ambapo baada ya kujiridhisha ndipo ilipopokea taarifa ya JKU kuhusiana na juhudi zao za kupunguza madeni hayo. Hata hivyo, Kamati pia imefahamishwa kwamba, mbali na madeni mengine, bado wanakabiliwa na tatizo la uniforms na zaidi inapokaribia kipindi cha Sherehe za Mapinduzi, kiasi ambacho pamoja na juhudi zao, bado wataendelea kukabiliwa na deni hilo.

Maoni ya Kamati.

Kamati inawataka JKU kulipa madeni hayo, na huku inaendelea kuitaka Serikali kuangalia utaratibu wa kuwasaidia katika malipo ama manunuzi ya sare za askari, ili deni hilo liweze kuondoka kabisa.

Hoja Namba 7.3 Kuhusiana na Hesabu za Mwisho wa Mwaka:

Kwa mwaka wa fedha 2010/2011, JKU waliidhinishiwa kutumia Tsh.4,570,000,000 kwa kazi za kawaida na hadi kufikia Juni 2011,fedha zote hizo ziliingizwa na kutumiwa kwa kazi za kawaida, sawa na 100% ya makadirio. Aidha, kwa upande wa kazi za Maendeleo, JKU waliidhinishiwa kutumia Tsh.500,000,000 na hadi kufikia Juni 2011, waliingiziwa fedha zote hizo sawa na 100%.

Kwa upande wa mapato, JKU walikadiriwa kukusanya 12,167,000 kwa mwaka 2010/2011 lakini hadi kufikia Juni 2011, fedha walizokusanya ni Tsh.1,000,000 pekee sawa na 8.3%.

Maelezo ya JKU:

Kuhusiana na sababu zilizopelekea mapato kukusanywa kwa kiwango kidogo sana kinyume na makadirio, imesababishwa na mabadiliko ya hali ya hewa na upandaji haukuwa mzuri. Hata hivyo, JKU wanakusanya mapato kupitia mfuko wa Canteen, ikiwa pia ni pamoja na mapato yanayokusanywa kwenye huduma ya ulinzi wanayoitoa kwa watu binafsi na Taasisi mbali mbali za Serikali. Fedha hizo za Canteen kwa kawaida hukaguliwa na Wakaguzi wa Ndani wa Kikosi, ingawa bado haujaanza kukaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Maelezo ya Kamati:

Kamati imefahamu kwamba, JKU wanakusanya fedha nyingi zaidi kupitia Canteen na wanauwezo mkubwa wa makusanyo kinyume na vyanzo vyao vya mapato vilivyowazi na vinavyofahamika. Kitendo cha Fedha ama mapato ya Canteen kutokaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu, kinakiuka masharti ya Katiba, kifungu cha 112(3)(c), ni jambo lisiloweza kuvumilika.

Maoni ya Kamati:

Kamati inapendekeza kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, kufanya ukaguzi maalum katika mapato ya Vikosi vyote vya Serikali yanayohusiana na Canteeen ili usahihi wake uweze kufahamika kwa wananchi.

5.4.4 KIKOSI CHA ZIMAMOTO NA UOKOZI :

Hoja Namba 8.1 Kuhusiana na Malimbikizo ya Madeni, Tsh.226,809,556

Ukaguzi umebaini kwamba, Kikosi cha Zima Moto kinadaiwa na wafanyabiashara pamoja na Taasisi mbali mbali kwa ajili ya utoaji wa huduma. Deni hilo la Tshs. 226,809,556 limekuwa ni la muda mrefu.

Maelezo ya Kikosi

Kikosi kimekiri kuwepo kwa deni hilo kutokana na hali halisi ya upatikanaji wa fedha usio wa kuridhisha. Hii inatokana na ukomo wa bajeti wanaopewa lakini vile vile hata kile kidogo kinachokubaliwa, basi huwa ama hakipatikani kikamilifu au kwa wakati unahitajika. Kwa ujumla, Kikosi kinakabiliwa na upatikanaji wa uniiform, vifaa vya kulalia, vifaa vya mawasiliano, ushauri na samani ambazo Kikosi kinakabiliana nazo kwa upungufu mkubwa, na walilazimika kuingia katika madeni hayo kutoka kwa wafanyabiashara tofauti, kwa sababu kwa wakati huo wafanyabiashara hao waliwaamini na kuwapatia mkopo.

Hata hivyo, kuanzia mwaka 2005 ambapo kulikuwa na mabadiliko makubwa kutoka accrual basis, Serikali ilipoanzisha mfumo wa bash bases ulipelekea Kikosi kutakiwa kuorodhesha madeni yote waliyokuwa wanadaiwa na kupelekwa kwa Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali kwa ajili ya malipo. Hata hivyo, hadi Kamati imefika, Kikosi hakikuwa na taarifa zozote sahihi za kulipwa madeni hayo huku baadhi ya wafanyabiashara wametishia kuwapeleka Mahakamani.

Maelezo ya Kamati.

Serikali izingatie sana umuhimu wa Kikosi cha Zimamoto na Uokozi na hivyo ni vyema kuiangalia kwa kina bajeti yake kwani vifaa na nyenzo zake zinapatikana kwa bei ya juu. Zana ambazo ni muhimu vikosi hivyo kuwanavyo, ikiwa ni pamoja na magari ya Uokozi, Boti na vifaa vyenginevyo

Maoni ya Kamati.

Serikali ichukue juhudi ya kulipa deni la nyuma linalodaiwa kikosi, kwani kwa kutumia bajeti yake deni hilo si rahisi kukamilika. Hata hivyo, jambo ambalo Kamati inalisisitiza ni kulipwa kwa madeni hayo kwa haraka.

5.4.5 BARAZA LA MANISPAA:

Hoja Namba 14.1 Kuhusiana na Makadirio ya Mapato na Matumizi (Budget Revenue and Expenditure) kwa mwaka 2010/2011

Baraza la Manispaa limekadiriwa kukusanya mapato kutoka vyanzo vyake, kiasi ya jumla ya Ts.1,004,972,200 na makadirio ya ruzuku ya Tsh.1,328,315,533 kutoka Serikalini. Pia Baraza limetegemea kupata Tsh. 50,000,000 kutoka kwa mradi wa ZUSP na kufanya makadirio ya mapato yote kwa mwaka wa 2010/2011 kufikia Tsh.2,383,287,733.

Mapato halisi:

Kwa mwaka 2010/2011 Baraza la Manispaa lilifanikiwa kukusanya Tsh.1,098,193,950.20 ambayo ni sawa na 109%. Aidha Baraza lilipokea ruzuku ya Tsh.1,187,471,308 kutoka Serikalini ambayo ni sawa na 89% ya makadirio.

Matumizi:

Baraza la Manispaa lilikadiria kutumia Tshs2,383,287,732 kati ya hizo 2,294,887,732 kwa mishahara ya watumishi na kazi za kawaida na 88,400,000/- kwa miradi ya maendeleo.

Ukaguzi umebaini kwa mwaka 2010/2011, Baraza lilitumia Tsh. 2,219,521,225 ambayo ni sawa na 93% ya makadirio.

Ukaguzi wa Hesabu Nyengine za Baraza la Manispaa, Nje ya Hoja za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu:

Kwa busara za Kamati na kwa mamlaka iliyonayo chini ya kanuni ya 118 (2) (c) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi, Toleo la 2012, Kamati imeona vyema ufafanuzi wa mtumizi ya Baraza la Manispaa utizwamwe kwa kwama 2009/2010, kwa sababu katika mwaka 2010/2011, kumeonekana hakukuwa na hoja ya moja kwa moja kuhusiana na mapato na matumizi yao. Kwa hali hiyo, katika kuyapitia mahesabu ya mapato na matumizi ya Baraza la Manispaa, Zanzibar, Kamati ilichagua baadhi ya Kasma na kutaka ufafanuzi juu ya matumizi yaliyohusiana na Kasma hizo kwa mwaka wa 2009/2010 Kasma zenyewe ni:-

a) Kasma 23001 Viburudishaji na Chakula

Katika mwaka wa 2009/2010 ilitengewa jumla ya Tshs. 6,880,000/- na matumizi yalikuwa ni Tshs. 1,994,500/-

- Hoja ya Kamati ilihusu ufafanuzi wa matumizi hayo ya Tshs. 1,994,500/- ambayo yalizihusisha karatasi za malipo (Vocha) 25.

Aidha, kati ya vocha hizo 25 vocha nane (8) hazikuweza kuwasilishwa mbele ya Kamati katika uchambuzi ambazo zilikuwa na thamani ya malipo ya Tshs. 783,000/-

b) Kasma 23004 – Gharama za Hoteli.

Kasma hii ilitengewa jumla ya Tshs. 14,432,000/- na jumla ya Tshs. 12,540,000/- zilitumika.

- Ufafanuni wa malipo hayo kupitia karatasi za malipo uliridhiwa na Kamati.

c) Kasma 23005 - Matumizi ya Kazi zisizotarajiwa.

Hii ilitengewa jumla ya Tshs. 17,259,000/- na hadi kumalizika mwaka wa fedha jumla ya Tshs. 42,042,224/- zilitumika. Likiwa ni ongezeko la Tshs. 24,783,224/-

- Ufafanuzi wa malipo hayo kwa mujibu wa karatasi za malipo ulikuwepo ila Kamati haikuridhishwa na matumizi nje ya bajeti iliyotengwa ambayo ni Tshs. 24,783,224/-

d) Kasma 20010 - Safari za Nje

Kasma hii ilitengewa jumla ya Tshs. 44,555,640/- na matumizi halisi yalikuwa ni jumla ya Tshs. 52,855,040/- ikiwa ni ongezeko la Tshs. 8,299,400/-

- Ufafanuzi wa matumizi kupitia karatasi za malipo (vocha) haukuwepo ila Kamati haikuridhishwa na matumizi ya ziada ya kile kilichotengewa.

e) Kasma 20009 Safari za Ndani

Kasma hii ilitengewa jumla ya Tshs. 16,340,000/- na matumizi halisi yalikuwa ni Tshs. 26,162,000/- ikiwa ni ongezeko la Tshs. 9,822,000/-. Kamati haikuridhishwa na ongezeko la matumizi kinyume na yalivyoidhinishwa.

f) Kasma 17019 Ununuzi wa Feni, Air Condition

Kasma ilitengewa jumla ya Tshs. 2,900,000/- na matumizi halisi yakawa ni Tshs. 3,300,000/- ikiwa ni ongezeko la jumla ya Tshs. 400,000/-

- Pamojana ufafanuzi uliyotolewa Kamati haikuridhishwa na sababu za kutumia fedha za ziada.

Maelezo ya Kamati

Katika uchambuzi huo Kamati haikupata vielelezo vyenye kuthibitisha matumizi ya Tshs. 783,000/- kwenye Kasma 23001 – Viburudishaji. Aidha, Jumla ya Tshs. 43,304,624/- zilitumika kwa mwaka wa fedha 2009/2010 ambazo hazikutengwa kwenye bajeti.

Maoni ya Kamati

Fedha ambazo hazikupatikana vielelezo (Payment voucher) maana yake kwa mujibu wa kifungu cha 95(1) na (4) cha Kanuni za Fedha za mwaka 2005, ni kwamba fedha hizo zimeibiwa na

Kamati inaiagiza Serikali kuwachukuliwa hatua za kinidhamu za kuwakata mshahara watendaji waliohusika na kadhia hii, ikiwa ni pamoja na Afisa Mhasibu aliyeidhinisha matumizi hayo, Mhasibu, Cashier na aliyelipwa fedha hizo.

Katika suala zima la upangaji na matumizi ya bajeti, Baraza la Manispaa hupanga matumizi madogo madogo na kutumia sana jambo ambalo ni kinyume na taratibu hasa ikizingatiwa kwamba Kamati haikuoneshwa idhini na utaratibu uliotumika kwenye matumizi hayo ya ziada.

Dalili zinazoonesha kuwa ubadhirifu mkubwa wa fedha, na hivyo Kamati inasisitiza kwamba, maamuzi ya Baraza la Wawakilishi juu ya mapendekezo ya Kamati Teule ya Kuchunguza Mwenendo wa Baraza la Manispaa, yaendelezwe kufanyiwa kazi kwa umakini kabisa.

Aidha, Kamati inapanga kuonana na Waheshimiwa Madiwani, ili kuwaeleza udhaifu katika udhibiti wa matumizi ya fedha wanazoziidhinisha.

Hoja Namba 14.2 Kuhusu Ufungaji wa Hesabu za Mwsiho wa Mwaka, 2010/2011.

Baraza la Manispaa halikuweza kufunga na kuwasilisha hesabu zake za mwisho wa mwaka kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, hali ambayo inapingana na kifungu cha 24(2) cha Sheria ya Fedha ya mwaka 2005.

Maelezo ya Baraza la Manispaa :

Ni kweli walikuwa na tatizo hilo, ingawaje baada ya kupata muongozo wa Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu, wamerekebisha kasoro zao. Na katika kufanya hivyo, huwa wanapeleka mapato na matumizi yao ya kila mwaka kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu, ingawaje huwa hawapeleki ‘Fixed Asset Register’, kwani bado hawana utaalamu wa kuliandaa linavyotakiwa. Hata hivyo, wamo katika hatua za kuwasiliana na Chuo cha Uongozi wa Fedha, Chwaka, ili kuona namna gani watapata msaada huo.

Maelezo ya Kamati :

Pamoja na maelezo yote hayo, Kamati inasimamia hoja ya Mdhibiti kwamba Afisi ya Baraza la Manispaa haliwasilishi hesabu zake kwa Mdhibiti, na kufanya hivyo ni kukiuka sheria.

Maoni ya Kamati :

Kamati imeutaka Uongozi wa Baraza la Manispaa kuhakikisha kasoro hii haitajitokeza tena kuanzia mwaka 2013/2014. Aidha, kwa kitendo cha uzembe na kukiukwa sheria, kama ilivyofanyika awali, Kamati inaitaka Serikali kutoa onyo kwa Uongozi wa Baraza la manispaa na kutaka hili lisirejewe tena.

Hoja Namba 14.3 Kuhusiana na Mradi wa Michirizi (Maji Machafu).

Katika Ukaguzi uliofanyika, Baraza la Manispaa kwa upande wa Michirizi, uhifadhi kumbukumbu zao za mapato na matumizi kwa kutumia 'computerized accounting system' (STORM M.I.S). Katika kipindi cha ukaguzi, mapungufu yafuatayo yamebainika :

- Mtandao huo hupoteza muelekeo wa ufanisi na kupelekea kutoa taarifa zisizo sahihi.
- Kutokuwepo na daftari la mapato na matumizi jambo ambalo linapelekea kutopata usahihi baina ya makusanyo na fedha zilizowasilishwa benki.
- Hakuna taarifa ya urari kwa kila mwezi ; na
- Gharama za uendeshaji za mtandao huo ni kubwa kwani hulazimika kutafuta mtaalamu kutoka nje, endapo pakitokea tatizo.

Maelezo ya Baraza la Manispaa :

Uongozi wa Baraza umekiri kwamba huwa wanatumia mfuo wa kompyuta (computerized accounting system-STORM M.I.S) katika kitengo cha Michirizi, kwa ajili ya kuhifadhi kumbukumbu za mapato na matumizi, lakini kwa hivi sasa mfumo huo umekuwa na matatizo.

Hapo awali, mradi wa michirizi wa KFW ndio uliokuwa ukidhamini matengenezo yake kwa kupitia mtaalamu wake ambae yuko Kenya, na mara tu baada ya mradi kumalizika, kumekuwa na hitilafu kadhaa na Manispaa kushindwa kumudu gharama za matengenezo hayo, kila kunapotokea tatizo na kusababisha kuhifadhi baadhi ya kumbu kumbu zake kwa kutumia daftari.

Baada ya kuliona hili, Uongozi wa Baraza la Manispaa umeomba fedha kutoka Benki ya Dunia (World Bank) katika utekelezaji wa Mradi wa ZUSP, sehemu ya pili (Part II – ZUSP Institution Strengthening). Kwa hivyo, Manispaa imeandaa mpango wa kupatikana kwa taarifa hizo kwa kushirikiana na wataalamu kupitia Mradi huo na tayari utekelezaji wake umeshaanza.

Maelezo ya Kamati :

Suala la Uhifadhi wa Kumbukumbu za mapato na matumizi katika Baraza la Manispaa kwa upande wa michirizi kwa kutumia Computerized accounting (STORM M.I.S) haujaleta ufanisi hata kidogo. Kutokana na kutokuwepo kwa taarifa za ugavi wa kila mwezi, mtandao kupoteza muelekeo wa ufanisi na kupelekea kutoa taarifa zisozo sahihi na kuwa na gharama kubwa za uendeshaji.

Aidha, pamoja na maelezo ya Mradi (Divisheni ya Maji Machafu Michiriri na Takataka) wa kuchukua hatua zifuatazo kutokana na mapungufu yaliyojitokeza katika utekelezaji wa mradi huo, ambazo ni :

- Nyaraka za LPO kuhamishiwa katika 'Exe sheet' ya kawaida ambapo hutumika kopi ya delivery note yenye Leja folio za kuthibitisha mapokezi.
- Kuanzishwa kwa daftari la mahesabu ya matumizi na mapato (cash book)
- Stakabadhi zinazotumika za kawaida huchapwa kupitia Microsoft Word.

- Kuanzishwa kwa ‘Ledger’ na ‘Issue books’ na kutumika badala ya nyaraka ya ‘database’.
- Kuwasiliana na Mshauri Muelekezi kwa madhumuni ya kusaidia matengenezo na kutoa mafunzo mapya juu ya uendeshaji wa mfumo huo;

Bado Kamati inaamini kwamba mfumo huu hauna ufanisi. Kwa mfano, suala la kumtegemea Mtaalamu kutoka Kenya, limekwama kwani mtaalamu huyo kutoka Kenya alidai malipo ya Dola 7,000/- kwa mwaka, hali ambayo Manispaa ilishindwa kuimudu.

Maoni ya Kamati:

Pamoja na nia njema ya Serikali lakini mazingira ya mfumo huo wa ukusanyaji wa mapato umeongeza kuitia hasara Serikali badala ya kuleta tija iliyokusudiwa. Aidha, Serikali haikujiandaa vyema tangu mwanzo kabla ya kutekeleza kwa mradi huo katika suala zima la miundo mbinu, elimu kwa walipaji na taaluma kwa watumiaji wa chombo hicho, jambo ambalo hulazimisha kuajiri mtaalamu nje kwa kila tatizo dogo tu linalotokea.

Kamati haikuridhishwa na matumizi ya fedha yaliyotumika hapo kwani lengo halikufikiwa. Huku ikitoa indhari kwa Serikali kwenye hata huo mradi wenyewe wa V I System ambao unakusudia kuziunganisha sekta za mapato kama vile ZECCO, ZAWA na ZRB huenda usifikie azma iliyokusudiwa endapo tahadhari na mambo ya msingi ya uendeshaji isipochukuliwa.

Hoja Namba 14.4 Kuhusiana na Mikataba ya Ujenzi na Ukodishaji wa Maduka katika Soko la Matunda Darajani.

Jumla ya maduka 13 yamejengwa katika soko la Darajani ambapo yamekodishwa kwa wafanyabiashara mbali mbali. Makubaliano hayo yalifanyika tarehe 11/11/2010 baina ya Baraza la Manispaa na wafanyabiashara hao kwa ada ya Tsh.100,000 kwa kila duka kwa mwezi.

Ukaguzi umebaini kwamba,mapato yanayotokana na ukodishwaji wa maduka hayo hayapatikani ili kuongeza mapato ya Baraza la Manispaa.

Hoja Namba 14.4.2 Kuhusiana na Ujenzi na ukodishwaji wa maduka 16 Darajani.

Ukaguzi umebaini kwamba, Baraza la Manispaa limeingia mkataba na Abdalla Khalfan Siney kwa ajili ya ujenzi wa maduka 16 katika soko la matunda liliopo Darajani kwa gharama ya jumla ya Tsh.98,047,000. Kutokana na Mkataba huo, Mjenzi alitakiwa kukamilisha kazi kwa muda wa miezi saba (7) kuanzia tarehe ya kuingiwa mkataba huo (25/11/2009).

Ukaguzi umebaini kwamba ada ya ukodishwaji kwa kila duka ni Tsh.75,000 kwa mwezi ambapo Baraza la Manispaa lilitakiwa kuchukuwa 20% ambayo ni sawa na Tsh.15,000 kutokana na ada hiyo. Hadi ukaguzi unamalizika, ujenzi huo bado haujakamilika kulingana na makubaliano yaliyokuwepo kati ya Baraza na Mjenzi.

Maelezo ya Kamati kuhusiana na hoja zote mbili.

Baraza la Wawakilishi, liliunda Kamati Teule ya Kuchunguza Mwenendo wa Baraza la Manispaa, na katika Hadidu Rejea ilizopewa, ni pamoja na hoja zote mbili zinazohusiana na Mikataba ya maduka.

Maoni ya Kamati:

Kwa kuwa tayari Kamati Teule imekwishatoa ripoti yake, Kamati hii inakubaliana na maelezo yote yaliyotolewa na Kamati Teule ya Kuchunguza Baraza la Manispaa, ya mwaka 2012.

5.5 OFISI YA RAIS, UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA :

Hoja Namba 15.1 Kuhusiana na Gharaza za kukodi majengo kwa ajili ya madarasa ya Chuo cha Utawala wa Umma.

Chuo cha Utawala wa Umma, kimeingia mkataba na Glorious Academy na Willey Academy, taasisi za watu binafsi kwa kukodishwa majengo ili kufundishia wanafunzi wa chuo, kwa sababu wakati huo Chuo hakikuwa na majengo, kutokana na chuo cha Utawala wa Umma, kilichopo Tunguu, kimechelewa kukamilika. Jumla ya Tsh. 53,550,000/- zimetumika kwa kodi.

Maelezo ya Chuo cha Utawala wa Umma:

Ni kweli walikodi madarasa katika skuli ya Glorious Academy kutokana na ufinyu wa madarasa na kukosa majengo yao ya kudumu, hali iliyosababishwa na kuongezeka kwa wanafunzi kuanzia mwaka 2010, na baada ya kushindikana kwa jitihada za kupatikana kwa madarasa hayo katika Skuli na vyuo mbali mbali vya Serikali. Kwa mwaka 2010, walikodi kuanzia kipindi cha July hadi Disemba, na kila mwezi walilipa Tsh. 2,800,000 na hivyo kuwa na deni la Tsh. 16,800,000 na wala sio Tsh. 33,600,000 kama ilivyoelezwa na Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu.

Aidha, kwa mwaka 2011, walikodi Skuli Willey Academy iliyopo Mbweni Zanzibar, wakiingia mikataba miwili tofauti. Makataba wa kwanza unahusisha kipindi cha January hadi Disemba, kwa kukodishwa madarasa matano ambapo kwa kila darasa lilipiwa Tsh.500,000 na kwa kila mwezi Tsh. 2,500,000, malipo yaliyojumuisha gharama za umeme, maji na samani. Aidha, kutokana na ongezeko la wanafunzi katika muhula wa Julai-Disemba, 2011, walikodi tena madarasa matatu zaidi na kuingia Mkataba mwengine na kulifanya deni lote la mwaka 2011, kuwa Tsh. 36,750,000.

Maelezo ya Kamati:

Kamati imejiridhisha kuwepo kwa mikataba iliyoelezwa hapo juu inayohusiana na kodi ya madarasa, na kufahamu kwamba, kuchelewa kwa ujenzi wa Chuo huko Tunguu, kumekitia sana hasara chuo hichi. Aidha, pamoja na kuelezwa na Uongozi wa Chuo kwamba, fedha zilizopatikana kulipia deni hilo zinatokana na ada za wanafunzi, na wala hakuna hasara ama

tatizo lolote lililojitokeza kwa upande wa walimu waliokuwa wanasomesha Chuoni hapo, lakini ni wazi kwamba, deni hilo na malipo yake yamerudisha nyuma maendeleo ya Chuo. Iwapo fedha zote za deni zingelitumika kwa kuendeshea Chuo, chuo kingelikuwa kimepiga hatua kubwa kwa maendeleo yake.

Maoni ya Kamati:

Kamati inaishauri Serikali kuwa makini na madhubuti katika maamuzi ya Ujenzi wa vyuo kwamba, vimalizike kwa wakati, ili kuepusha gharama nyingi kutumika kwa malipo ya kodi zisizo zalazima.

5.6 WIZARA YA KATIBA NA SHERIA

5.6.1 AFISI YA MRAJIS MKUU WA SERIKALI:

Hoja Namba 16.1.1 Kuhusiana na Vifaa ambavyo havikuingizwa kwenye daftari la ghalani Tsh.8,393,132.

Ukaguzi umebaini kwamba kuna malipo yamefanyika kwa ununuzi wa vifaa mbali mbali, lakini vifaa hivyo havikuingizwa kwenye daftari la vifaa ili kuweza kuthibitisha uhalali wa mapokezi pamoja na matumizi yake. Kutokuwepo kwa kumbukumbu za vifa hivyo kwenye daftari, kunakiuka kanuni ya 198 ya kanuni za fedha za mwaka 2005.

Maelezo ya Afisi ya Mrajis Mkuu wa Serikali:

Wameeleza kwamba, Afisi tayari ilikwishaviingiza zamani vifaa vyote ambayo wakati wa ukaguzi vilishindwa kuthibitika katika daftari la ghalani. Baada ya hatua hiyo walimjuulisha Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu, na wanashangazwa sana kuona hoja hii imejitokeza katika ripoti yake.

Maelezo ya Kamati:

Baada ya maelezo yao, Kamati ilijiridhisha kwa kulipitia daftari hilo na kuangalia iwapo ni kweli vifaa hivyo vimeingizwa. Hata hivyo, Kamati imegundua kuwa vocha yenye namba 356500 haina vielelezo vya kuomba fedha za ununuzi wa ‘toner’ 2 pas, ingawa kwa maslahi ya hoja hii, Kamati imejiridhisha kwamba, vifaa vimenunuliwa na kurikodiwa katika daftari.

Maoni ya Kamati:

Kamati imeridhishwa kwamba, hoja hii imejibika na ifutwe kwa kutumia kanuni ya 52(5)(c) ya Kanuni za Fedha za mwaka 2005.

Hoja Namba 16.1.2 Kuhusiana na Madeni wanayodaiwa Afisi ya Mrajis Mkuu wa Serikali, Tsh.29,984,800.

Ukaguzi umebaini kwamba, Afisi ya Mrajis Mkuu wa Serikali inadaiwa na Taasisi na watu mbali mbali kutokana na huduma zilizotolewa kwa Afisi hii. Madeni yenyewe ni haya yafuatayo:

1. Idara ya Upigaji Chapa anadai Tsh.6,000,000 kwa ajili ya uchapishaji wa fomu za kuhaulisha.
2. Idara ya Upigaji Chapa anadai Tsh.18,000,000 kwa ajili ya uchapishaji wa vyeti vya uzazi.
3. Saleh Decoration anadai Tsh.5,984,800 kwa ajili ya ununuzi wa zulia.

Maelezo ya Afisi ya Mrajis kuhusiana na deni hilo:

Kwa upande wa Idara ya Upigaji Chapa, tayari Afisi ya Mrajis imeshawalipa Tsh.18,000,000 zilizotumika kwa uchapishaji wa vyeti vya uzazi. Lakini deni la Tsh.6,000,000 bado hawajalilipa, ingawaje wamo katika juhudi za kulipa deni hilo.

Kwa upande wa Tsh.5,984,800 zilizotumika kwa ununuzi wa zulia, Afisi ya Mrajis imeeleza kwamba deni hilo limetokana na mazingira ya kuhama na kuhamia jengo hilo la P.B.Z ya zamani walipo sasa. Waliwaandikia Wizara ya Katiba na Sheria kuwataka kulipa deni hilo nao waliwaandikia Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kulipa ama kuwapa fedha za kulipa.

Maelezo ya Kamati:

Kamati imetaka kupatiwa uthibitisho wa barua rasmi zilizotumika katika mawasiliano hayo, ingawa wakati wa kazi ilishindikana kutokana na kuelezwa kwamba, zipo Wizarani. Kuhusiana na uthibitisho wa malipo ya Tsh.18,000,000 kwa Idara ya Upigaji Chapa, Kamati imetaka pia ithibitishiwe, jambo ambalo lilifanyika.

Maoni ya Kamati:

Kamati inaitaka Afisi ya Mrajis Mkuu wa Serikali kuhakikisha inamaliza deni lake kwa Idara ya Upigaji Chapa Tsh.6,000,000. Aidha, inaitaka Serikali ihakikishe deni la Saleh Decoration la ununuzi wa zulia kutokana na Afisi ya Mrajis kuhama jengo la Mambo Msiige, linalipwa.

Mapato na Matumizi ya Afisi ya Mrajis Mkuu wa Serikali kwa mwaka 2010/2011.

Kamati imetaka kupatiwa ufafanuzi wa mapato na matumizi ya Afisi hii kwa mwaka 2010/2011, na baada ya kupatiwa uchambuzi wake, ilichagua kasma zifuatazo kama zinavyoelezwa:

a. Matumizi ya Tsh.13,437,400 zilizotumika kwa Mafunzo ya Ndani.

Fedha hizo zimetumika kwa mafunzo ya aina zote kwa wafanyakazi wa Afisi ya Mrajis, wanaobahatika kusoma katika vyuo vya ndani ya nchi. Hata hivyo, Kamati ilihoji juu ya matumizi ya Ndg. Abdulbaq Habib Ali ya Tsh.438,000 kwa ajili ya mahafali (graduation); fedha

za kujikimu Tsh.1,200,000 kwamba amelipiwa mara mbili na hata kufanyiwa malipo ya Utafiti (Field Research), Tsh.725,000. kinyume na wafanyakazi wengine, na kuelezwa kwamba suala hilo lilitokana na Afisi ya Mrajis kulazimika kumlipia gharama za master program zilizosalia kwa sababu waliandikiwa kufanya hivyo na Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kwa wafanyakazi wote ambao ufadhili wa masomo yao haukuangalia gharama zilizosalia.

Yaani mfanyakazi huyu na wenzake walipata ufadhili wa mashirika ya kimataifa na taasisi nyengine nje ya Serikali, lakini ufadhili huo kutokana na muda wa masomo ulivyokuwa ama kwa sababu nyengine, haukuhusu moja kwa moja kila gharama zilizohitajika. Na kwa hivyo, salio lililobakia la gharama, lilibebwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Maelezo ya Kamati:

Kamati imeridhishwa na hoja za matumizi haya kwa mafunzo, ingawa imeshangazwa kuona kwamba, fedha zinatolewa katika kasma hii na kutumika kwa shughuli nyengine kinyume na utaratibu. Kwa mfano Tsh.392,400 zimetumika kwa malipo ya posho kwa kikao cha Bajeti (Allowance for Budget Committee). Afisi ya Mrajis katika kulijibu suala hili, ilikiri kwamba imefanya hivyo bila ya kufuata taratibu zozote za uhaulishaji na sababu kubwa ya matumizi hayo ni kukosa fedha katika kasma zilizohusika.

b. Matumizi ya Tsh.42,600,000 zilizotumika kwa ajili ya Gharama za Uchapishaji.

Fedha hizo hutumika kwa ajili ya kulipia gharama zote za uchapishaji pamoja na ununuzi wa vifaa vya uchapaji. Afisi imewasilisha namna gani ilivyofanya matumizi ya Tsh.42,600,000 kwa mwaka 2010/2011, na kueleza kwamba imetumia kwa kufuata taratibu zilizowekwa.

Maelezo ya Kamati.

Kamati imegundua matumizi mengine yasiyohusiana na uchapaji yaliyofanywa katika Afisi ya Mrajis kwa kutumia kasma ya Gharaza za Uchapishaji kinyume na taratibu za Sheria. Kwa mfano, kuna matumizi ya Tsh.650,000 zimetumika kwa matumizi ya ‘installation’ ya umeme; huku pia Tsh.400,000 zikitumika kwa ufungaji wa shelves. Maelezo ya Afisi ya Mrajis kuhusu matumizi haya ni hoja zile zile za kuhama Ofisi kongwe kwa ghafla na bila ya matayarisho huku wakihamia afisi hii ya Jengo la P.B.Z ya zamani, Forodhani.

Aidha, kasma hii iliidhinishiwa kutumiwa kwa Tsh.42,600,000 kwa gharama za uchapishaji, lakini Afisi ya Mrajis imezidi makisio ya matumizi kwa kutumia Tsh.42,601,800, kinyume na ilivyoidhinishwa.

c. Matumizi ya Tsh.4,000,000 zilizotumika kwa matengenezo madogo ya Afisi.

Matumizi haya yalihusisha uhamishaji wa vifaa mbali mbali vya Afisi kutokana na kuhama jengo kongwe la Mji Mkongwe na kuhamia Forodhani, huku zikitumika kwa upakizi na utaremshaji; usafishaji wa vyoo na uzibuaji wa karo pamoja na matengenezo ya Aircondiditon.

Maelezo ya Kamati:

Katika upakizi na uteremshaji wa vifaa hivyo, Kamati ilielezwa kwamba Afisi ya Mrajis ilikodi magari kutoka kwa watu binafsi. Kwa mfano Tsh.1,740,000 zilitumika kwa kazi hiyo ya upakizi na uteremshaji; huku risiti za mapokezi ya fedha kutoka kwa wamiliki wa magari hayo hazina VAT namba. Aidha, risiti hazina jina la dereva, mwenyegari wala namba ya gari. Kwa ujumla risiti za mapokezi ya fedha hizo hazikubaliwi na Kamati.

d. Matumizi ya Tsh.3,500,000 zilizotumika kwa ununuzi wa fanicha.

Fedha hizo zimetumika kwa kununulia fanicha na mahitaji mengine yanayohusiana na fanicha.

Maoni ya Kamati:

Kitendo cha kutopokea risiti zilizo na sifa zinazokubalika, kunakiuka masharti ya kanuni ya 70 ya Kanuni za Fedha za mwaka 2005 na kitendo cha Afisi ya Mrajis kutofuata masharti ya kanuni hiyo, na kwa kuwa kanuni hiyo imevunjwa, Kamati initaka Serikali kutoa onyo kwa Mrajis Mkuu wa Serikali na kumtaka asimamie ipasavyo Sheria za fedha zinazohusika. Aidha, Kamati inaitaka Afisi ya Mrajis kuhakikisha inapata vielelezo sahihi juu ya matumizi ya fedha inazozisimamia.

5.6.2 KAMISHENI YA WAKFU NA MALI YA AMANA:

Hoja Namba 16.2.1 Kuhusiana na Madeni ya Kodi za nyumba za Wakfu, Tsh.47,228,000:

Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana inawadai wananchi binafsi na Taasisi za Serikali fedha za kodi ya nyumba za Wakfu kwa muda mrefu bila ya kulipa kodi za nyumba hizo kwa wakati, hali inayopelekea kukosekana kwa mapato hayo ambayo yanahitajika kwa ukarabati wa nyumba hizo. Jumla ya deni hilo ni Tsh. 47,228,000.

Maelezo ya Kamisheni ya Wakfu:

Ni kweli deni hilo lipo kwa muda mrefu, ingawaje kutokana na juhudi walizozichukua zimepelekea baadhi ya wadaiwa hao kulipa madeni, wengine wamepunguza na wengine bado hawajalipa kabisa madeni yao. Jumla ya Tsh.16,015,000 zimelipwa na deni lililobakia ni Tsh.31,213,000. Katika kulifuatlia deni hilo, Kamisheni kwanza ilifanya utafiti na kugundua kuwa wananchi wengi hawajui maana ya mali ya wakfu na namna inavyostahiki kulipwa kodi.

Na hivyo, walilazimika kuwaelimisha wananchi kupitai njia mbali mbali ikiwa ni pamoja na kuwatumia Wabunge na Wawakilishi.

Pia walikwenda kujifunza katika Shirika la Nyumba la Taifa la NHC, na kujifunza mambo mengi yaliyowasaidia katika kusimamia majukumu yao. Vile vile waliipitia mikataba yao upya ya ukodishaji wa nyumba hizo na kwa kiasi kikubwa wamefanikiwa.

Maelezo ya Kamati:

Kamati imepokea taarifa kuhusiana na madeni na namna gani Kamisheni inafanya juhudi ya kuyasimamia. Kamati imefurahishwa na namna gani Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana inaipitia mikataba yake ili kuendana na wakati, huku ikisisitiza kwamba suala hili liwe endelevu.

Maoni ya Kamati:

Kamati imeridhishwa na juhudi zinazochukuliwa na kusisitiza Kamisheni iendelee kutilia nguvu upatikanaji wa malipo ya kodi kwa wakati.

5.7 WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA AMALI:

Hoja Namba 25.1 Kuhusiana na Malipo yaliyolipwa kinyume na Taratibu. Tsh. 10,000,000.

Ukaguzi umebaini kwamba kuna malipo yamefanyika kwa ajili ya kulipia gharama za ununuzi wa vifaa vya ghala la Wizara. Mikataba midogo midogo ya ujenzi huo haikupatikana na malipo yamefanyika kwa njia ya taslim, ambapo ni kinyume na taratibu. Malipo yenyewe yanahusiana na vifaa vya ujenzi wa ghala la Wizara, Mazizini.

Maelezo ya Wizara:

Ni kweli Wizara imefanya malipo ya Tsh.10,000,000 kwa ajili ya kulipia vifaa mbali mbali vya ununuzi. Mikataba iliyohusika na ujenzi huo ipo na Kamati inaweza kuipitia kwa kujiridhisha zaidi. Kufanyika kwa malipo hayo kwa njia ya taslim, kunahusisha na udogo wa fedha hizo na namna zilivyolipwa, kwamba hazikulipwa kwa pamoja.

Maelezo ya Kamati :

Kamati imekabidhiwa Mikataba inayohusiana na Ujenzi. Mikataba hiyo imeingiwa na Wizara pamoja na mafundi waliopewa kazi ya ujenzi husika. Mikataba hii ni midogo midogo na hivyo, fedha zinazohusiana na hoja hii hazikulipwa kwa pamoja. Kwa mfano katika Mkataba baina ya Wizara na Ndg. Moh'd Ussi, gharama za ujenzi zilizohusika ni Tsh.5,150,000 na Mkataba mwengine baina ya Wizara na Ndg. Ramadhan Sheria aliyejenga paa la ghala hilo, alilipwa

Tsh.500,000. Hata hivyo, mikataba iliyoingiwa na namna fedha zilivyolipwa zinahusiana na ununuzi wa vifaa vya ujenzi wa ghala, na sio Mkataba wa kujengewa ghala hilo na fundi yoyote.

Maoni ya Kamati:

Kamati inaitaka Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, kuingia katika Mikataba pale inapofanya manunuzi yanayostahiki kufanyiwa Mkataba.

Hoja Namba 25.2 Kuhusiana na Mshahara wa Ndg. Masoud Kh. Said.

Ukaguzi umebaini kwamba kuna malipo ya mshahara wa Nd. Masoud Kh. Said, ambapo mfanyakazi huyo yupo likizo bila malipo na bado anaendelea kuchukua mshahara kutoka Serikalini. Mfanyakazi huyo ameajiriwa na mradi wa BADEA kwa mkataba namba CS/2/SMZ/B/10 ulio chini ya Wizara ya Elimu. Kitendo cha kuendelea kuchukua mshahara kwa kipindi cha likizo bila malipo ni kwenda kinyume na sheria na kanuni za utumishi, Serikalini.

Maelezo ya Wizara :

Ndg. Masoud Khamis Said ana nyadhifa tofauti ndani ya Wizara huku cheo chake rasmi ni Mkuu wa Kitengo cha Manunuzi, na kutokana na nafasi yake hiyo, pia Ndg. Masoud ni Afisa Manunuzi wa Mradi wa Uimarishaji wa Elimu ya Lazima unaotekelezwa kwa pamoja kati ya Serikali na Benki ya Dunia. Kwa dhamana hizi mbili, Ndg. Masoud analipwa mshahara na Serikali.

Mbali na dhamana hizo, Ndg. Masoud ni 'Project Engineer' wa Mradi wa Ujenzi wa Skuli mbili za Sekondari, unaotekelezwa kwa pamoja na Benki ya Maendeleo ya Kiarabu kwa Maendeleo ya Afrika (BADEA). Kupitia mradi huu, Ndg. Masoud analipwa mshahara kupitia fedha anazolipwa zinazotoka BADEA.

Ndg. Masoud amepewa majukumu yote hayo kutokana na uhaba wa watumishi wenye ujuzi katika nyanja hizo na utaalamu wake kwa wakati huo ulikuwa haujaenea. Hivyo, kulipwa sehemu mbili na kuzikamilisha zote kwa ufanisi mkubwa kumesaidia sana katika kuleta ufanisi wa miradi hiyo. Hata hivyo, hivi sasa Ndg. Masoud amepunguziwa majukumu mengine na amepewa likizo bila ya malipo, ili kushughulikia mradi mmoja tu wa Ujenzi wa Skuli Mbili kupitia BADEA.

Maelezo ya Kamati :

Kamati haikubaliani na kitendo cha Mfanyakazi mmoja kulipwa mishahara miwili, huku akiingia Mikataba tofauti ya ajira, kitendo kinachoonesha wazi kwamba ameajiriwa mara mbili.

Maoni ya Kamati :

Kwa kuwa Mfanyakazi huyo alikwishapokea Tsh.27,698,625 kutoka BADEA na kwa upande wa Serikali zilikuwa ni Tsh. 3,409,000, na Kamati imejiridhisha kwamba, hiyo ni mishahara miwili

kwa mfanyakazi mmoja ndani ya wakati mmoja wa kazi. Kamati inaagiza mshahara wa Tsh. 3,409,000 wa SMZ urejeshwe kwa kukatwa mshahara na stahiki nyengine za Mfanyakazi huyu, na hatua hii ianze mara moja mara tu baada ya kuwasilishwa ripoti hii.

Kibaya zaidi, kitendo cha Mfanyakazi huyu kupokea mishahara miwili wakati mmoja, ni kosa la jinai kwa mujibu wa kifungu cha 274(4) cha Sheria Namba 6 ya mwaka 2004. Kosa hili hili, pia linastahiki kuchukuliwa hatua za kinidhamu kwa mujibu wa taratibu za kiutumishi. Kamati inaitaka Serikali kumchukulia hatua zote hizo, Mfanyakazi huyo, pamoja na hatua za kinidhamu zilichukuliwa kwa Afisa Mhasibu wa Wizara hii, pamoja na watendaji wote wa fedha waliohusika katika kumlipa Mfanyakazi huyo.

Hoja Namba 25.3 Kuhusu Uhaulishaji wa Tsh.1,000,000,000 kwa ajili ya Mfuko wa Elimu ya Juu.

Ukaguzi umebaini kuwepo kwa uhaulishaji wa Tsh.1,000,000,000 kupitia barua yenye kumbu kumbu namba MI/62/VOL.XII kwenda Mfuko wa Elimu ya Juu. Uhaulishaji huo ulihusisha hesabu (account) ya Maendeleo (capital accout). Ukaguzi umebaini uhaulishaji huo umeathiri kwa kiasi kikubwa matumizi yaliyopangwa katika baadhi ya miradi ya Maendeleo.

Maelezo ya Wizara :

Ni kweli Wizara ilifanya uhaulishaji wa fedha hizo zilizoelezwa, na hii inatokana na ukweli kwamba, katika mwaka 2010/2011, Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu, ilitengewa Tsh.2,500,000,000. Kiwango ambacho kingelitosha kugharamia wanafuzi waliokuwa wapo masomoni, ila Bodi isingelikuwa na uwezo wa kuwagharamia wanafunzi wengine wowote wapya. Lakini hali hii isingeliwezekana kwa sababu wanafunzi wapya walioomba mkopo walikuwa wengi na wangeliathirika sana kama wasingelipewa mkopo.

Kwa mfano, fedha zote zilizotengwa zilipatikana, lakini bado Wizara ikawa ina madeni makubwa kwa wanafunzi walioko nje ya Tanzania. Aidha, wanafuzi 54 walioko China, walizuiwa kuendelea na masomo na walitakiwa kulipiwa au kurudi nyumbani. Kutokana na hali hiyo, Wizara iliomba fedha za ziada Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, lakini kwa kuwa hakukuwa na fedha zilizobakia, ilibidi waingiziwe fedha za miradi ya maendeleo na zitumike kwa ajili ya kulipia ada za vyuo vilivyoko nje na pia kulipia huduma za wanafunzi. Hatua hiyo imechukuliwa kwa sababu hakukuwa na njia nyengine mbadala.

Maelezo ya Kamati :

Kamati inakubaliana na hoja za Wizara na umuhimu wa kipekee kwa wanafunzi wetu kupata elimu. Hata hivyo, suala hili linatakiwa pia liangaliwe kwa makini na mapema tokea maandalizi ya bajeti. Aidha, kuna haja ya kuwepo utaratibu mzuri wa kusomesha vijana wetu, ili Wizara isiingizwe katika wakati mgumu wa kutoa huduma hiyo kwa vijana waliokopa.

Maoni ya Kamati :

Kamati inaitaka Serikali kutafuta njia mbadala itakayopelekea kupata fedha za kutosha kwa Bodi ya Mkopo wa Elimu ya Juu, ili kukabiliana na tatizo linalowakabili. Aidha, Kamati inaitaka Bodi kusimamia ipasavyo marejesho ya Mikopo, ili fedha hizo ziweze kuwasaidia wanafunzi wengine wanaohitaji.

5.7.1 TAASISI YA SAYANSI NA TEKNOLOJIA :

Hoja Namba 25.4.1 Kuhusu Utekelezaji wa Vifungu vya Matumizi ya Bajeti.

Ukaguzi umebaini kwamba katika vifungu vya matumizi kati ya makisio (Bdget) na matumizi halisi (Actual), hali hiyo imesababisha kupindukia kwa matumizi ya baadhi ya vifungu. Hivyo, kuna tofauti ya Tsh.28,159,623 sawa na 128% kati ya makadirio ya Tsh.107,873,572 na matumizi halisi ya Tsh.136,033,195.

Maelezo ya Taasisi ya Sayansi na Teknolojia :

Ni kweli Taasisi ilitumia zaidi ya makisio kutokana na Taasisi hii kuanzishwa Oktoba 2009, na bajeti yake ya kwanza imeandaliwa mwaka 2010/2011. Kwa kuwa Taasisi ilikuwa bado mpya na ilikuwa na vipaumbele vyake ambayo vinavyoijenga Taasisi kutoka Chuo cha Ufundi Karume, vilipaswa kushughulikiwa zaidi, ikiwa ni pamoja na kuboresha mazingira ya mafunzo ambayo yalikuwa ni changamoto kwa Taasisi. Hivyo, Taasisi imejikuta mipango yake ya Kibajeti na hali halisi ya mahitaji ni tofauti na hata baadhi ya vifungu kukosekana katika mpango na kulazimika kutumia zaidi kulingana na mahitaji na vipaumbele walivyoviweka, ili kukamilisha azma hiyo.

Maelezo ya Kamati :

Ni kweli kwamba, Taasisi hii imeanzishwa karibuni, huku ikikabiliwa na changamoto nyingi za kutekeleza majukumu yake. Hata hivyo, Uongozi wa Taasisi hii, kama ilivyo kwa Taasisi yoyote ya Serikali, unapaswa kufuata ipasavyo Sheria na Taratibu za matumizi ya fedha za Serikali. Ikiachiwa tu kujitumilia itakavyo, kwa hoja tu ya kuwa ni mpya, itapelekea matumizi mabaya ya fedha, kitu ambacho Kamati inapaswa kukikemea kwa nguvu zote.

Maoni ya Kamati :

Kamati inautaka Uongozi wa Taasisi ya Sayansi na Teknolojia, kuhakikisha inafuata ipasavyo Sheria za Fedha. Aidha, kitendo cha kutumia fedha kinyume na matumizi yaliyokubalika, hakupaswi kufanywa, kwani kunakiuka masharti ya kifungu cha 51 cha Kanuni za Fedha, na hivyo, Kamati inaitaka Serikali kutoa onyo kwa Afisa Mhasibu wa Taasisi hii na watendaji wake wa fedha waliohusika na kosa hilo.

Hoja Namba 25.4.2 Kuhusiana na Usimamizi na ukusanyaji wa Mapato:

Ukaguzi umebaini kwamba kuna miradi ndani ya Taasisi ya Sayansi na Teknolojia, inayoendeshwa na watumishi wa Taasisi pamoja na watumishi binafsi. Miradi ambayo inakusanya zaidi ya Tsh.76,000,000 kwa mwaka ulioishia Juni, 2011, lakini mchango wake kwa Taasisi ni Tsh.8,213,897. Hali inayoonesha kutokuwepo kwa mikakati, mikataba pamoja na sera nzuri za kusimamia vyanzo vya mapato ya ndani. Baadhi ya miradi yenyewe ni hii ifuatayo:

- Kompyuta inayo makusanyo na mapato kwa kila kozi ni Tsh.8,188,000; Makadirio ya Mchango kwa Taasisi ni Tsh.5,000,000, huku Makusanyo Halisi ni Tsh. 4,464,450 sawa na 89%.
- ABMA, makusanyo na mapato kwa kila kozi ni Tsh.30,207,168; Makadirio ya Mchango kwa Taasisi ni Tsh. 4,000,000, huku Makusanyo Halisi hakuna sawa na 0.0%.
- VETA makusanyo na mapato kwa kila kozi ni Tsh.38,102,400; Makadirio ya Mchango kwa Taasisi ni Tsh.5,000,000, huku Makusanyo Halisi ni Tsh. 1,249,447 sawa na 25%.

Maelezo ya Taasisi ya Sayansi na Teknolojia:

Ni kweli Taasisi kwa muda mrefu sasa imekuwa ikitoa mafunzo mbali mbali kwa lengo la kuwasaidia wananchi na mchango unaopatikana katika mafunzo hayo, husaidia kuongeza mapato ya Taasisi. Aidha, Taasisi imekuwa ikikodisha baadhi ya rasilimali zake bila ya kuathiri shughuli za kawaida za Taasisi.

Aidha, Ukusanyaji wa mapato ya shughuli zote unasimamiwa na Mhasibu Mkuu wa Taasisi na kuingiza moja kwa moja katika Mfuko wa Taasisi., malipo ya watendaji wa miradi hulipwa baada ya taratibu za utoaji wa fedha kufuatwa pamoja na taratibu za uzalishaji mali za Taasisi. Aidha, kwa upande wa ukusanyaji wa mapato ambao una mikataba, makusanyo yake huingia moja kwa moja katika Taasisi bila ya kufanyika malipo kwa msimamizi yeyote wa Taasisi.

Maelezo ya Kamati:

Ni jambo la kupongezwa kwa Taasisi hii kubuni miradi mbali mbali ambayo mara nyingi huwasaidia wananchi wetu kujinasua kimaisha, kwani hutoa elimu ya ufundi, elimu ya vitendo na kada mbali mbali. Aidha, pia ni sahihi kwamba, takriban malipo wanayofanya wanafunzi hao yapo katika hali ya chini, ukilinganisha na mafunzo kama hayo yanayotolewa na Taasisi nyengine za watu binafsi.

Maoni ya Kamati:

Taasisi isimamie ipasavyo makusanyo inayoyakusanya na iwe na mikakati imara katika kutoa mikataba pamoja na sera nzuri za kusimamia vyanzo vyake vya mapato, ili viweze kuisaidia Taasisi hii katika kujiendesha.

Hoja Namba 25.4.3 Kuhusu Ufungaji na Uwasilishaji wa Hesabu za Mwaka (Preparation of Final Account).

Taasisi ya Sayansi na Teknolojia hawafungi hesabu za mwisho wa mwaka na wala hawaziwasilishi kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu, kitendo ambacho kinapingana na maelekezo ya Sheria Namba 12 ya mwaka 2005, kifungu cha 24(2).

Maelezo ya Taasisi:

Ni sahihi kwamba kwa mwaka 2010/2010, Taasisi haikuweza kufunga na kuwasilisha hesabu zake za mwisho wa mwaka kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu. Uongozi wa Taasisi umeiona hali hii na umeanza kuchukua hatua kwa kuorodhesha mali zote za Taasisi na thamani ya mali hizo, ili ziweze kujulikana na kuwekewa kumbukumbu katika daftari la mali za Taasisi (Fixed Asset Register). Hata hivyo, wana changamoto ya kukosa utaalamu wa kuzitia thamani (valuation). Taasisi imeahidi kasoro hiyo ya kutowasilisha hesabu zake kwa Mdhibiti, itachukuliwa hatua kuanzia mwaka 2012/2013.

Maelezo ya Kamati:

Ufungaji na uwasilishaji wa hesabu za mwisho wa mwaka, ni amri ya kisheria, na ni wajibu wa kila Taasisi ya Serikali, ikijitegemea ama ikiwa chini ya Wizara, kufunga na kuziwasilisha hesabu hizo kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu, Zanzibar.

Maoni ya Kamati:

Kitendo cha kutowasilisha hesabu za mwisho wa mwaka kwa Mdhibiti ni kosa kwa mujibu wa kifungu cha 24(2) cha Sheria ya Fedha ya mwaka 2005, na Afisa Mhasibu wa Taasisi hii amekiuka masharti ya sheria hiyo. Hivyo, Kamati inaitaka Serikali kutoa onyo kwa kosa hilo na kuiagiza Taasisi hii, kuhakikisha mwaka 2012/2013, ikafunga mapema na kuwasilisha hesabu zake za mwisho wa mwaka, kwa Afisi ya Mdhibiti.

5.7.2 MAMLAKA YA MAFUNZO YA AMALI:

Hoja Namba 25.5.1 Kuhusiana na Ufungaji wa Hesabu za Mwisho wa Mwaka:

Kwa mwaka 2010/2011, Mamlaka ya Amali hawakuwasilisha hesabu zao za mwisho wa mwaka, kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu, Zanzibar. Hali ambayo sio tu inakiuka sheria ya Fedha ya mwaka 2005, lakini pia inaifanya Afisi ya Mdhibiti ishindwe kufahamu hali halisi ya mapato, matumizi na uwezo wa Mamlaka katika kutekeleza shughuli zake.

Maelezo ya Mamlaka ya Amali kuhusiana na hoja hii:

Ni kweli kwa mwaka 2010/2011 hawajafunga hesabu zao za mwisho wa mwaka na kuziwasilisha kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu w Hesabu hali iliyosababishwa na kukosa sera ya uchakavu (Depraciation Policy) na kukosekana kwa thamani halisi ya mali zao.

Maelezo ya Kamati:

Pamoja na utetezi huo, Kamati haikubaliani na hoja ya kutofunga hesabu kwa kisingizio cha kushindwa kujua mali zake. Suala la kutojua thamani halisi ya mali ni tatizo takriban la Serikali nzima na ndio maana Serikali kupitia Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, iko katika hatua ya kulitafutia ufumbuzi wa kudumu.

Maoni ya Kamati:

Kitendo cha kutowasilisha hesabu za mwisho wa mwaka kwa Mdhibiti ni kosa kwa mujibu wa kifungu cha 24(2) cha Sheria ya Fedha ya mwaka 2005, na Afisa Mhasibu wa Taasisi hii amekiuka masharti ya sheria hiyo. Hivyo, Kamati inaitaka Serikali kutoa onyo kwa kosa hilo na kuiagiza Taasisi hii, kuhakikisha mwaka 2012/2013, ikafunga mapema na kuwasilisha hesabu zake za mwisho wa mwaka, kwa Afisi ya Mdhibiti.

5.8 WIZARA YA AFYA:

Hoja Namba 26.1 Kukiukwa kwa taratibu za manunuzi, Tsh. 163,478,000.

Ukaguzi umebaini kwamba Wizara imefanya manunuzi mbali mbali yakiwemo madawa na vifaa bila ya kufuata taratibu za manunuzi. Taratibu zenyewe zilizokiukwa ni kama zifuatazo:

a. Kutotangazwa kwa zabuni husika.
b. Kutozingatia muda wa malipo kwa muuzaji wa bidhaa (suppliers).
c. Kutoheshimu maamuzi ya kikao cha zabuni ambapo kikao kilifanyika tarehe 24/06/2011, lakini malipo yote yalifanyika tarehe 27/06/2011.
d. Kutoheshimu barua ya muuzaji wa bidhaa yenye kumbu kumbu namba REF:REQUEST FOR ADVANCE PAYMENT OF 30% OF CONTRACT PRICE (MOH/PMU/TDR/09/2010/2011 ya terehe 25/06/2011.
e. Malipo yote yamefanyika bila (kabla) kupokea bidhaa.
f. Kumekuwepo na mgongano wa maslahi (conflict of interest) kwa sababu muuzaji wa madawa hayo ni Mkurugenzi wa IZMIR PHARMACY LTD, ambaye ni Mfanyakazi wa Wizara ya Afya, Kitengo cha Madawa.

Kukiukwa kwa taratibu za ununuzi ni kwenda kinyume na Sheria Namba 9 na Kanuni zake, za mwaka 2005.

Maelezo ya Wizara:

Katika kutoa ufafanuzi wa hoja hii, Wizara nayo kama alivyoeleza Mdhibiti, ilifafanua hoja baada ya hoja, na ufafanuzi huo ni kama ifuatavyo:

a. Kutotangazwa kwa zabuni husika.

Wizara inaamini imefuata utaratibu katika kuitangaza zabuni hiyo, kwa kutumia Tangazo la Ndani (Restricted Tendering Process), kama matakwa ya sheria ya Manunuzi inavyoelekeza. Utaratibu huo wameutumia kwa mujibu wa kifungu cha 35(1) cha Sheria Namba 9 ya mwaka 2005. Na haja ya kutumia njia hii imekuja baada ya fedha za manunuzi ya dawa kuidhinishwa mwezi wa Sita, ambapo fedha hizo za mwaka 2011/2012 zilitakiwa ziwe zimeshatumika kabla ya tarehe 30/06/2012.

b. Kutozingatia muda wa malipo kwa muuzaji wa bidhaa (suppliers).

Kwa sababu fedha hizo zilipatikana katika muda ambao matumizi yake yanaisha, hivyo fedha zote zilizobakia lazima zirejeshwe Hazina, wakati Mkataba ukotayari kwa utekelezaji wake, ndio ililazimika Mzabuni kulipwa fedha zake zote, ili kuondoa uwezekano wa kutopata fedha hizo baada ya kumalizika kazi yake.

c. Kutoheshimu maamuzi ya kikao cha zabuni ambapo kikao kilifanyika tarehe 24/06/2011, lakini malipo yote yalifanyika tarehe 27/06/2011.

Kutokana na upungufu na ucheleweshwaji wa upatikanaji wa fedha kutoka Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kwa kitengo husika, kimepelekea kutofanya malipo kwa mujibu wa tarehe iliyopangwa.

d. Kutoheshimu barua ya muuzaji wa bidhaa yenye kumbu kumbu namba REF:REQUEST FOR ADVANCE PAYMENT OF 30% OF CONTRACT PRICE (MOH/PMU/TDR/09/2010/2011 ya terehe 25/06/2011.

Kwa kuhofia kumalizika muda wa fedha hizo, ndio ilionekana kwamba, ni bora alipwe fedha zake zote kwa kuchelea kutopatikana fedha hizo. Kwa sababu fedha ilikuwa tayari inakaribia kumaliza muda wake wa matumizi, kwa mwaka wa fedha 2011/2012.

e. Malipo yote yamefanyika bila (kabla) kupokea bidhaa.

Hawakuwa na njia nyengine ya kufanya, ilibidi alipwe fedha yake kabla ya kupokea bidhaa kwa sababu, fedha ilikua inakaribia kumalizika muda wake wa matumizi.

f. Kumekuwepo na mgongano wa maslahi (conflict of interest) kwa sababu muuzaji wa madawa hayo ni Mkurugenzi wa IZMIR PHARMACY LTD, ambaye ni Mfanyakazi wa Wizara ya Afya, Kitengo cha Madawa.

Kwa wakati huo Ndg. Nizar ambaye ni Mfanyakazi anaedaiwa kuwa na mgongano wa kimaslahi, pamoja na kuwa ni mfanyakazi wa Kitengo cha Dawa na Mkurugenzi wa IZMIR PHARMACY LTD, alikuwa ni mfanyakazi wa kitengo cha Tiba Asilia, ambapo vitengo vinavyohusika katika ununuzi wa dawa na vifaa tiba kwa njia moja au nyengine, ni Afisi ya Mfamasia Mkuu, Bohari Kuu ya Dawa Zanzibar na Kitengo cha Ununuzi cha Wizara.

Hivyo yeye kuwa mfanyakazi wa Wizara hakuathiri utendaji kaika mchakato wa ununuzi. Aidha, wauzaji wote wa dawa na vifaa tiba wa ndani ya Zanzibar, wadhamini wao ni wafamasia wanaofanya kazi katika Wizara hii na wote wapo katika Kitengo cha Dawa, kiasi ambacho ukiwaondoa italazimika wauzaji (Pharmacy zilizopo Zanzibar) zote zisishiriki katika michakato ya ununuzi inayofanywa na Wizara ya Afya.

Maelezo ya Kamati:

Kamati haina pingamizi na maelekezo ya sheria, kwamba miongoni mwa njia za kufanya manunuzi, ni pamoja na kutumia 'Restricted Tendering' kama ilivyoelezwa na kifungu cha 35 cha Sheria ya Manunuzi, Namba 9 ya mwaka 2005. Hata hivyo, kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki cha 35, kinaelekeza masharti ya kutumiwa kwa njia hii, ikiwa ni pamoja na hali ambayo haiwezekani kuitisha tenda ya wazi.

Hoja ya Kamati ni kwamba, suala la ununuzi wa madawa linaambatana na mipango ya mwaka mzima ya Wizara, na ni wazi kwamba, iwapo Wizara ingelikuwa na mpango wa mwaka mzima wa manunuzi, haja ya uharaka wa suala hili isingelikuwepo. Aidha, Kamati ilipokuwa katika Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali na kumuuliza suala hili, aliihakikishia Kamati kwamba, Idara haikucheleweshe fedha kiasi ya Wizara kushindwa kufuata taratibu za manunuzi. Vile vile, kiwango cha fedha zilizotumika ni kikubwa kwa Wizara kutumia utaratibu huu, ambapo ililazimika kwa namna yoyote kuitisha zabuni.

Katika masharti yaliyoelezwa na Kanuni za Manunuzi, kanuni ya 31(e), inashurutisha kutumika kwa njia hii ya manunuzi pale ambapo kuna uharaka wa kufanyika kwa manunuzi husika, lakini kilichopelekea uharaka hakikuweza kufahamika na Wizara ama Serikali na kiwe hakijasababishwa na ucheleweshaji wa (makusudi) na Wizara ama Serikali. Hii inaleta uwazi kwamba, mazingira halisi ya kutumika kwa njia hii hayakuzingatiwa, na Wizara ilikuwa ina kila sababu ya kuziomba fedha hizo mapema, ili ziweze kutumika mapema pia.

Kwa kuzingatia hoja hizo, Kamati inaamini Wizara haikuwa na haja ya kutozingatia muda wa malipo kwa Muuzaji wa dawa hizo wala kutoheshimu maamuzi ya Kikao cha Bodi ya Zabuni wala barua ya Muuza dawa husika, na ni sawa na kusema, kitendo cha kumlipa pesa Muuzaji kabla ya kupokea dawa, hakikubaliki kisheria, na kinaonesha dhahiri kwamba, Wizara ilikusudia kumpa mtaji Mfanyabiashara huyo, ili aweze kuwapa dawa hizo.

Maoni ya Kamati:

Kwa ujumla, Afisa Mhasibu wa Wizara ya Afya, amekengeuka masharti ya Sheria Namba 9 ya mwaka 2005, kifungu cha 33; 34 ; 19; na vifungu vyengine vinavyohusika na Kanuni zake, na Kamati inaitaka Serikali kumchukulia hatua za kinidhamu, Afisa Mhasibu huyo pamoja na watendaji wote wa fedha waliohusika na makosa hayo.

Hoja Namba 26.2 Upokeaji wa madawa pungufu:

Ukaguzi umebaini kwamba, Wizara imefanya malipo ya madawa mbali mbali yenye thamani ya Ts. 23,902,000 yakiwa pungufu.

Maelezo ya Wizara:

Ni kweli wakati wa ukaguzi Mzabuni (Muuzaji) alikuwa bado hajakamilisha kuwasilisha mali (dawa) zote kama Mkataba wake ulivyoelekeza. Hii inatokana na baadhi ya dawa zilikosekana huko kwa watengenezaji (Manufacturers) wa dawa hizo. Hata hivyo, Wizara ilimfatilia Muuzaji huyo na kupata suluhisho juu ya tatizo hilo. Wizara inaendelea kusisitiza kwa kuzingatia ufafanuzi ufuatao:

Baadhi ya dawa ziliwasilishwa Bohari Kuu kama zilivyoainishwa katika orodha ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu.

Baadhi ya dawa zilifanyiwa mbadala (compensation) na vifaa tiba ambavyo vinahitajika Wizarani kwa makubaliano baina ya muuzaji.

Baadhi ya dawa zilipokelewa na kurikodiwa kwenye vitabu vya kumbukumbu kwa kukosewa ‘unit’ ya kupokelea. Ziliingizwa katika kumbukumbu ‘piece’ 100 za ishirini na tano kila moja kama ‘piece’ nne(4) kama zilvyoainishwa katika ripoti ya Mdhibiti, lakini badala ya kubaini mapungufu hayo, ziliingizwa piece 96 za ishirini na tano, sawa na piece elfu mbili na mia nne (2400) za moja moja kama idadi iliyouliziwa na Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu kw kutumia ‘invoice’ ile ile iliyoingiziwa mwanzoni.

Maelezo ya Kamati:

Pamoja na maelezo hayo, Kamati inahoji sasabu za msingi zilizopelekea kukiukwa kwa mkataba wa ununuzi wa dawa hizo, ikiwa pia na kufanywa mbadala (compensation), kitu ambacho hakitakiwi. Na hii ni wazi kwamba, suala la Mfanyakazi huyo huyo ambae ni Mkurugenzi wa Kampuni iliyouza dawa hizo (IZMIR PHARMACY) ana uhusiano wa karibu na maslahi ya pande zote, na ni wazi kwamba, Wizara inageuka dalali wa kumpatia kazi Izmir, wakati alitakiwa alete dawa kwa maslahi ya Mkataba.

Maoni ya Kamati:

Kamati imezingatia sababu zilizopelekea kupokelewa kwa dawa pungufu, na inaamini hakukuwa na sababu za msingi za kufanya hivyo. Aidha, kitendo cha kupokea dawa pungufu na kwa ufafanuzi ulioelezwa kwa muuzaji huyu kwamba ana mgongano wa kimaslahi, kinakiuka masharti ya mkataba, lakini pia ni wazi kwamba, imefanywa hivyo kutokana na uhusiano wa karibu wa mfanyakazi huyu wa Wizara ya Afya ambae pia ni Mkurugenzi wa IZMIR PHARMACY. Hivyo, Kamati inaitaka Serikali kumtaka Mfanyakazi huyu asihusishwe katika ununuzi wa dawa za hospitali hii.

5.9 WIZARA YA ARDHI, MAKAAZI, MAJI NA NISHATI:

5.9.1 IDARA YA NYUMBA, MAENDELEO NA MAKAAZI:

Hoja Namba 27.1 Kuhusu Madeni ya Idara ya Nyumba.

Ukaguzi umebaini kwamba, kwa baadhi ya nyumba za maendeleo zilizokodishwa kwa wananchi mbali mbali katika maeneo ya Michenzani, Makunduchi, Mtende, Mombasa A, Mombasa B, Gamba, Kikwajuni, Kizimkazi, Kijini na Kibigija, kumejitokeza kwa baadhi ya wananchi kushindwa kulipa malimbikizo ya kodi za nyumba hizo kwa muda mrefu. Jumla ya madeni hayo ni Tsh.304,368,529.

Maelezo ya Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati na Idara ya Nyumba:

Ni kweli kwa kipindi kirefu, wakodishwaji wa nyumba za maendeleo wanalimbikiza madeni, ingawa Wizara ya Ardhi na Idara ya Nyumba kwa pamoja wanaendelea kuyasimamia madeni hayo, na kwa kiasi kikubwa wanafanikiwa. Aidha, kati ya wananchi wenye kuishi katika nyumba hizo, wapo ambao wanaendelea kulipa madeni na kodi zao vizuri, wapo wanaodai nyumba hizo wamepewa na Mzee Abeid Aman Karume, wengine husema wanamiliki nyumba hizo kwa kile kinachodaiwa kuuziwa kwa njia ya vilemba na hata wengine wamewapeleka Mahakamani kwa ajili ya kuwataka walipe madeni wanayodaiwa.

Maelezo ya Kamati:

Kamati inaamini iwapo Wizara na Idara zitaendelea kuwa na mikakati madhubuti, wananchi wote wenye madeni watalipa. Aidha, kuna haja ya kufanywa uhakiki wa nyumba hizo, kwani kitendo cha wananchi waliokodishwa kuuza nyumba hizo kwa njia ya vilemba, haikubaliki kisheria na wala haina maslahi kwa maendeleo ya wananchi waliowengi.

Kamati pia inafahamu kama ilivyoeleza katika ripoti zake za awali, kwamba baadhi ya nyumba za maendeleo zinakaliwa na Viongozi mbali mbali wa Serikali na wakubwa wengine, ambao wananyumba zaidi ya hizo wala hawana shida ya kuzitumia. Na kiendelea kuwaonea haya, ni kuwanyima wananchi waliowengi, maslahi na kufurahia maendeleo ya nchi yao. Jambo baya zaidi ambalo halivumiliki, baadhi ya Viongozi hao hawalipi kodi.

Maoni ya Kamati:

Kamati inaitaka Wizara na Idara kwa ujumla kuhakikisha madeni hayo yanalipwa yote. Aidha, Kamati inaitaka Serikali kufanya uhakiki wa nyumba za maendeleo na kuzirejesha katika miliki yake, na sio kuwaachia baadhi ya wananchi kujimilikisha kwa kisingizio cha kuuziwa kwa njia ya kilemba. Vile vile Kamati inaitaka Serikali kuhakikisha Viongozi wachache wenye nyumba zao au waliopewa nyumba nyengine na Serikali, wazirejeshe nyumba hizi za maendeleo ili ziweze kuwasaidia wananchi walio wengi.

5.10 WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI:

Hoja Namba 29.1 Kuhusiana na Hesabu ya Mwisho wa Mwaka:

Kwa upande wa Mapato, Wizara haikuwa na makadirio yoyote, huku matumizi halisi yakiwa ni Tsh. 746.187,000/- na makadirio yake yalikuwa Tsh. 758.306,000/- kwa mwaka wa fedha 2010/2011. Kwa upande wa kazi za Maendeleo, jumla ya Tsh. 589,000,000/- zilikadiriwa kutumika na hali halisi ya matumizi ni Tsh. 347,000,000/-, sawa na 58.91% .

Maelezo ya Wizara kuhusiana na Hoja hii:

Wizara haikuwa na pingamizi na maelezo yote kuhusiana na makadirio na hali halisi ya fedha za Matmuzi, ingawaje haikuweza kutoa uchanganuzi wa kina juu ya namna fedha hizo ilivyozitumia, kutokana na kutofahamu utaratibu gani Kamati iliuhitaji katika kuwasilishiwa taarifa hizo. Hata hivyo, iliahidi kuwasilisha taarifa hiyo tarehe 18/03/2013.

Aidha, kuhusiana na Mradi wa AI (Artificial Insermination) wa kupandisha ng'ombe kwa sindano, Wizara imetoa ufafanuzi uliohitajika pamoja na kuwasilisha baadhi ya vielelezo vilivyohusika.

Maelezo ya Kamati:

Mradi wa AI, unaoelezewa kutumiwa fedha kwa ununuzi wa madume, Kamati imehitaji kupatiwa uthibitisho wa vielelezo na gharama za ununuzi wa madume hayo. Aidha, Kamati imeelezwa kwamba, wananchi waliofaidika na Mradi huu ni kote, Unguja na Pemba, na hivyo, inahitaji kupata muda wa kuwatembelea baadhi yao, ili kuona kwa kiasi gani wamenufaika.

Maoni ya Kamati:

Kamati inahitaji muda wa ziada kuukagua Mradi huu, ili iweze kufikia maamuzi yanayofaa. Aidha, inahitaji muda wa ziada kufuatilia matumizi halisi ya Wizara hii kwa mwaka 2010/2011.

5.11 WIZARA YA MIUNDOMBINU NA MAWASILIANO:

5.11.1 MAMLAKA YA UWANJA WA NDEGE:

Hoja Namba 30.1.1 Kuhusiana na Mikataba ya Ukodishwaji wa Sehemu za Ofisi ziliopo Uwanja wa Ndege, Zanzibar.

Ukaguzi umebaini kwamba, Mamlaka ya Uwanja wa Ndege ilikadiriwa kukusanya Tsh.120,000,000 kwa mwaka 2010/2011 kwa ajili ya ukodishwaji wa sehemu zilizomo katika jengo la abiria, lakini Mamlaka ilikusanya Tsh.92,228,782.61 ambapo ni sawa na 77%.

Ukaguzi umebaini kuwepo kwa mapungufu katika ukusanyaji wa mapato katika sehemu hiyo kwani kiwango kinachotozwa hakilingani na hali halisi ya soko la kodi katika maeneo hayo.

Aidha Ukaguzi umebaini kwamba kutokana na maapungufu yaliyojitokeza katika ufungaji wa mikataba, baadhi ya wakodishwaji hawakuweza kulipa kabisa.

Maelezo ya Mamlaka ya Uwanja wa Ndege:

Ni kweli wakati wa ukaguzi matatizo hayo yalikuwepo. Aidha, wakati huo kulikuwa na Idara ya Anga, lakini kufuatia kuanzishwa kwa Mamlaka ya Uwanja wa Ndege, kasoro zote hizo zimepatiwa ufumbuzi. Miongoni mwa hatua zilizochukuliwa ni hizi zifuatazo:

- Kufuatilia ulipwaji wa madeni kwa wakodishwaji.
- Kuwepo kwa mikataba mipya inayobainisha hatua za kutoza adhabu kwa wateja wanaochelewesha malipo ya kodi.
- Kufuatilia mara kwa mara kodi ya maeneo kwa wakodishwaji hao kwa lengo la kuondosha malimbikizo ya madeni.

Maelezo ya Kamati:

Hoja hii tayari imefanyiwa kazi na Kamati Teule iliyoundwa kufuatilia mambo mbali mbali yaliyoibuka katika Bajeti ya Serikali, 2011/2012, na Mwenyekiti na Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando) walikuwa ni wajumbe wa Kamati hiyo, na hivyo, Kamati haioni haja ya kubadili yaliyochunguzwa na Kamati hiyo.

Maoni ya Kamati:

Kamati inasimamia utekelezaji wa maagizo ya Baraza la Wawakilishi kufuatia mapendekezo ya Kamati Teule, kuhusiana na hoja hii.

Hoja Namba 30.11.2 Kuhusiana na Madeni ya Ada za Utuaji wa Ndege ya Muda mrefu (land charges), Tsh.273,276,878.

Ukaguzi umebaini kwamba, Mamlaka ya Uwanja wa Ndege inadai fedha nyingi zinzohusiana na utuaji wa ndege kutoka mashirika mbali mbali ya ndege. Madeni hayo ni ya muda mrefu ambapo jitihada za ufuatiliaji wake zinafaa kuchukuliwa ili kuongeza mapato ya Mamlaka.

Maelezo ya Mamlaka ya Uwanja wa Ndege:

Ni kweli walikuwa wanadai wa makampuni hayo fedha ambazo zimeainishwa na Mdhibiti. Aidha, kutokana na juhudi za Mamlaka katika kusimamia suala hili, Kampuni hizo zimeweza kulipa madeni yao.

Maelezo ya Kamati:

Kamati imepokea majibu yaliyowasilishwa kwa Kamati na imepongeza Mamlaka ya Uwanja wa Ndege kwa kusimamia ulipaji wa Madeni hayo. Hata hivyo, imegundua kuwa, ‘Invoice’ nyingi zilizowasilishwa kwake na Mamalaka ya Uwanja wa Ndege kuhusiana na malipo hayo, sio zile

zilizohojiwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu. Aidha, kutokana na wakati, Kamati haijapata muda wa kina wa kuvipitia kwa undani vielelezo vya malipo hayo, na hivyo, inakuwa vigumu kuthibitisha moja kwa moja kuthibitisha usahihi wa malipo hayo.

Maoni ya Kamati:

Kwa kutumia kifungu cha 52(5)(b) cha Kanuni za Fedha za mwaka 2005, Kamati inahitaji taarifa za ziada ili kufikia uamuzi wa hoja hii.

5.12 WIZARA YA BIASHARA, VIWANDA NA MASOKO:

Hoja Namba 31.0 Kuhusiana na Makadirio ya Mapato na Matumizi (Budget Revenue and Expenditure) kwa mwaka 2010/2011

Wizara ya Biashara Viwanda na Masoko iliidhinishiwa kukusanya Tsh. 23,525,000 kwa mwaka wa fedha unaoishia Juni 2011. Hadi kufikia Juni, 2011 jumla ya Tsh.28,108,000 zilikusanywa ambapo ni sawa na 119% ya kamadirio.

Matumizi:

Wizara iliidhinishiwa jumla ya Tsh.1,939,000,000 kwa kazi za kawaida ambazo ni sawa na 82.66 ya makadirio.

Kazi za Maendeleo

Wizara iliidhinishiwa kutumia Tsh. 1,200,00,000 kwa kazi za maendeleo katika kipindi kinachoishia Juni 2011. Hadi kufikia Juni, 2011 Tsh. 1,132,000,000 zimeingizwa na kutumika kwa kazi za maendeleo ambazo ni sawa na 94.37 ya makadirio.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko (Ndg Julian B. Rafaeli), hakuwa tayari kutoa mashirikiano na kukubali Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali kufanya kazi katika Wizara yake. Hali hii imejitokeza baada ya Kamati kuandaa ratiba ya kazi na kuwapelekea Wizarani pamoja na Taasisi nyengine, na siku ya kuthbitisha ratiba, Katibu Mkuu alihuduhuria mbele ya Kamati na kukubali Kamati ifanye kazi katika Wizara yake, tarehe 20/9/2012.

Hata hivyo, Katibu Mkuu hakuweza kutoa mashirikiano kwa Kamati siku ya kazi ilipowadia, kwa hoja ya kwamba Wizara yake inafanya kazi na Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo kwa siku hiyo, huku ikizingatiwa kwamba, ratiba ya pamoja na Taasisi zote za Serikali zilizohusika na kazi ya Kamati ya P.A.C ilithibitishwa saa 5 Asubuhi, na Katibu Mkuu pamoja na watendaji wake walihudhuria katika kikao hicho, huku ratiba ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo ilithibitisha ratiba yake saa 3:00 Asubuhi. Kwa maana hii hakuwa na sababu ya kuzikutanisha Kamati mbili za Baraza wakati mmoja, wakati haiwezekani kwa Kamati mbili kufanya kazi kwa Taasisi moja, wakati watendaji muhimu ni hao hao (hawataweza kujigawa).

Maoni ya Kamati:

Kamati haikuridhishwa na kitendo alichokifanya Katibu Mkuu wa Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko na kinaonesha dharau ya hali ya juu kwa Kamati za Baraza la Wawakilishi inayofanywa na Watendaji wa Serikali. Kamati inaitaka Mamlaka husika, kumchukulia hatua za kinidhamu Mtendaji huyu kwa kuidharau Kamati, ambacho ni sawa na kulidharau Baraza la Wawakilishi.

5.13 WIZARA YA KAZI, UWEZESHAJI WA WANANCHI, KIUCHUMI NA USHIRIKA:

5.13.1 IDARA YA MIKOPO:

Hoja. Nam. 35.1, inahusu Madeni:

Kwa mwaka 2010/2011, Idara ya Mikopo ilikuwa inawadai wananchi mbali mbali waliokopeshwa na Idara hii, kutoka Mkoa wa Kusini Unguja, Kaskazini, Unguja na Mkoa wa Mjini Magharibi jumla ya Tsh. 39,533,910.

Maelezo ya Idara ya Mkopo kuhusiana na Hoja:

Katibu Mkuu wa Wizara ya Kazi, Uwezeshaji wa Wananchi Kiuchumi na Ushirika akijibu mbele ya Kamati alikiri kwamba, wanachangamoto nyingi zinazowakalibili kuhusiana na Utoaji na urejeshwaji wa Mikopo. Na tatizo kubwa zaidi ni kutokuwa na uwezo wa kuwapeleka Mahakamani wananchi wanaodaiwa, kwa sababu kufanya hivyo kutaathiri kisiasa kwani mikopo hiyo imekusudiwa kuwasaidia wananchi wanyonge.

Maelezo ya Kamati:

Kamati imebaini kwamba, kuna baadhi ya wananchi waliokopa huitumia vibaya mikopo hiyo kinyume na malengo yaliyokusudiwa. Aidha, Idara ya Mikopo inatakiwa ifahamu kwamba, marejesho ya mikopo hiyo ni muhimu kwa lengo la kuendelea kuwasaidia wananchi wengine, kwa hivyo, hoja ya kushindwa kuwachukulia hatua za kisheria wale wasiorejesha mikopo hiyo, ikiwa ni pamoja na kuwapeleka Mahakamani kwa kuzingatia maslahi ya kisiasa, hazina msingi wowote. Aidha, imefahamika kwamba, kati ya Ths. 39,533,910/- zinazodaiwa, ni Tsh. 8,689,800/- pekee ndizo zilizolipwa, huku kukiwa na bakaa ya deni la Tsh. 30,844,110/-.

Maoni ya Kamati:

Kamati inaitaka Idara ya Mikopo kuhakikisha deni lililobakia linalipwa si zaidi ya mwaka 2013. Aidha, Idara ya Mikopo iendelee kusimamia Utolewaji wa mikopo hiyo na matumizi yake kwa mnasaba wa masharti yaliyowekwa.

Uchambuzi wa Bajeti ya Wizara, 2010/2011:

Kwa mnasaba wa mamlaka ya Kamati, ilihitaji kupatiwa Uchanganuzi wa Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2010/2011, ambapo baada ya kupatiwa, ilihitaji pia kupata uchanganuzi wa matumizi ya mambo yafuatayo:

1. Posho Maalum
2. Safari za ndani
3. Safari za nje.
4. Ununuzi wa Honda, Vespa na Ciao.
5. Msaada wa Wanafunzi
6. Gharama za Ushauri Nasaha.

Maelezo ya Wizara:

Wizara iliwasilisha taarifa hizo kama ilivyotakiwa na Kamati, na katika uchambuzi wa Posho Maalum, linakusudiwa ni posho lolote wanalipwa wafanyakazi, kuanzia watendaji wa ngazi ya juu hadi ya chini, kwa kufanya kazi maalum ama wadhifa maalum walionao. Posho hili linajumuisha kwa wanasheria, posho la wanasheria; posho la baskeli kwa Matarishi na mengineyo.

Safari za ndani zinakusudiwa kuwa safari zote wanazosafiri wafanyakazi pamoja na Viongozi wa Wizara hii, ndani ya Tanzania. Wakati posho la nje linahusiana na malipo ya safari za nje ya Tanzania, kwa wafanyakazi ama Viongozi wa Wizara hii. Ununuzi wa Vespa, Honda na Ciao, ni matumizi yanayofanyika kila siku, kutokana na mpangilio wa bajeti ya Wizara na kuwepo kwa haja ya ununuzi huo. Huku msaada wa wanafunzi, inajumuisha gharama za kuwasomesha wafanyakazi wa Wizara hii sambamba na Gharama za Ushauri Nasaha zinatokana na kazi inayofanywa ya Wizara kwa watendaji na wananchi tofauti wanaohitaji ushauri.

Maelezo ya Kamati:

Kamati imepokea taarifa ya Wizara na kuangalia baadhi ya Hati za matumizi na vielelezo mbali mbali kuhusiana na matumizi hayo. Katika maeneo ambayo yameonekana yanahitaji marekebisho ni pamoja na safari za ndani, ambapo baadhi ya vielelezo vimekosekana, vyengine vina kasoro kadhaa, na vengine ni vya udanganyifu. Kwa mfano Vocha Namba 10 ya tarehe 20/01/2011 inayohusu malipo ya safari za kikazi, Dar es Salaam, haina vielelezo.

Katika safari za nje, waliidhinishiwa kutumia Tsh. 10,993,000/- wakati wao walitumia Tsh.11,358,000/- kwa zaidi ya Tsh. 365,000/-bila ya kufanya ama kufuata taratibu za Uhaulishaji. Aidha, vielelezo vya baadhi ya hati za malipo ya safari za nje, vimekosekana na vyengine kuwa na kasoro. Kwa upande wa ununuzi wa Honda, jumla ya Tsh.4,510,000/- zimetumika kwa kutengenezea magari, kinyume na idhini ya matumizi ya fedha hizo. Hapa pamefanyika Uhaulishaji usiofuata taratibu za kisheria zilizowekwa.

Maoni ya Kamati:

Kitendo cha kutumia fedha bila ya kufuata taratibu za uhaulishaji ni kukiuka masharti na maelekezo ya kifungu cha 51 cha Kanuni za Fedha za mwaka 2005. Aidha, kitendo cha kutumia fedha za Serikali bila ya vielelezo ama kukosekana kwa kielelezo kimoja tu (kwa tafsiri ya kifungu cha 95(1) na (4) cha Kanuni ya Fedha, ya mwaka 2005) ni sawa na kwamba, fedha hizo zimetumika bila ya vielelezo na maaana yake, hapo fedha zimetumika sivyo, ama zimeibwa.

Hivyo, Kamati inaitaka Serikali kuwachukulia hatua za kinidhamu, Afisa Mhasibu, Mhasibu pamoja na watendaji wote wa Wizara hii, waliohusika na matumizi hayo kinyume na utaratibu.

5.14 TAARIFA YA UCHUNGUZI WA KAMATI KWA MASHIRIKA YA SERIKALI NA TAASISI ZINAZOJITEGEMEA, KWA MWAKA 2010/2011.

5.14.1 SHIRIKA LA BIMA LA ZANZIBAR.

Hoja Namba 36.1 Kuhusiana na Ufungaji wa Hesabu za Mwisho wa Mwaka, 2010/2011.

Shirika la Bima la Zanzibar halikuwasilisha hesabu zake za mwisho wa mwaka 2010/2011 kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu kwa ajili ya kufanyiwa ukaguzi. Kwa vile ukaguzi wa hesabu hizo haukufanyika itakuwa vigumu kuweza kutoa maoni kuhusu hesabu hizo pamoja na hali halisi ya fedha ya Shirika hilo.

Maelezo ya Shirika:

Tatizo la ufungaji wa hesabu za mwisho wa mwaka huanzia kwanza katika tarehe za ufungaji wenyewe. Kwa kawaida Shirika la Bima mwaka wake wa fedha ni Januari hadi Disemba ambapo mwaka wa fedha wa Serikali ni Julai hadi Juni.

Katika hali hiyo, Shirika hulazimika kuwasilisha hesabu zake kwa Kamishna wa Bima Tanzania kwa kutegemea mwaka wake huo, wakati Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu yeye angependa azione mwezi Machi nae hutegemea mwaka wa fedha (Julai – Juni). Utata huo umekuwepo kwa muda mrefu pamoja na kuwepo mazungumzo ya kulitatua tatizo hilo.

Maelezo ya Kamati:

Pamoja na ugumu ulioelezwa na Shirika, ifahamike tu kwamba, suala hili lina misingi wake wa Kikatiba na kisheria , kwamba Mdhibiti na Makaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ndie mwenye dhima ya kikatiba kufanya ukaguzi wa kila hesabu ya Serikali. Na ukaguzi huo pia unahusiana na ufungaji wa hesabu na kuziwasilisha kwake, ili apate wepesi zaidi ya kufanya ukaguzi. Aidha,

muda wa kuwasilisha hesabu hizo nao ni mrefu kisheria, kwamba pamoja na tofauti ya tarehe baina ya Serikali na Mashirika ya Bima, iwapo litatiliwa nguvu, ni jepesi sana kutekelezeka.

Maoni ya Kamati :

Kamati inaliagiza Shirika la Bima kuwasilisha hesabu zake za mwisho wa mwaka kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mujibu wa Katiba na Sheria zinavyoelekeza.

5.14.2 SHIRIKA LA BIMA LA ZANZIBAR (TAWI LA DAR ES SALAAM)

Kwa mwaka wa fedha 2009/2010 na 2010/2011, Shirika la Bima la Zanzibar kwa upande wa Tawi la Dar es Salaam, halikuwa na hoja yoyote ya Mdhibiti, ingawaje kwa upande wa Kamati, ilikuwepo haja ya kupata ufafanuzi wa Hesabu zao za mwaka 2010/2011. Aidha, ifahamike kuwa, Miongoni mwa Mashirika yanayofungwa hesabu zao na kukaguliwa na Wakaguzi wa Nje, ni pamoja na Shirika hili, kwa upande wa Zanzibar na Tanzaniabara.

Maelezo ya Shirika :

Kuhusu kukaguliwa na Wakaguzi wa Nje, Uongozi wa Shirika uliitwa na kukutana na Waziri, pamoja na Taasisi nyengine ikiwa ni pamoja na Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ), Shirika la Biashara la Taifa (ZSTC) na nyenginezo, na kukubaliana haja ya kukaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu, Zanzibar.

Aidha, katika kuongeza mapato ya Shirika, Shirika limeamua kuongeza gharama za Bima kwa vyombo vya moto, ikiwa ni pamoja na malipo ya Vespa na vyombo vya magari mawili kutoka Tsh.30,000/- kwa Bima ya Kawaida hadi Tsh.50,000/- na kutoka Tsh. 40,000/- kwa gari hadi 100,000/- huku Bima ya ‘Coprehensive’ itapanda kutoka 4% ya gharama ya chombo hadi 3% kuanzia July, 1 2013. Wanafanya hivi kwa hoja kwamba, Makampuni yote ya Bima yameshakubaliana juu ya mabadiliko hayo, (yasiyojali kiwango na uwezo wa wananchi wa Zanzibar), nao wanalazimika kuenda sambamba na mabadiliko hayo.

Katika changamoto zinazowakabili ni pamoja na kunyang’anywa majengo yao ya awali yaliyopo Vuga, baada ya Shirika hili kujenga Afisi mpya katika eneo la Maisara. Kinachowashangaza ni majengo hayo baada ya kunyang’anywa wao, wanapewa Wizara ya Elimu ambayo imeshajenga Afisi yake huko Mazizini, na pia majengo yake, ikiwa ni pamoja na Jengo liliopo Mambo Msiige, limeshauzwa kwa Mfanyabiashara, Ndg. Said Salum Bakhressa.

Maelezo ya Kamati :

Kamati imepokea taarifa na maelezo ya Shirika.

Maoni ya Kamati :

Kamati inaendelea kusisitiza haja ya Mashirika kukaguliwa na Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu, Zanzibar huku yakitakiwa kwa hatua ya awali kukabidhi ripoti zao za

ukaguzi zilizofanywa kwa miaka iliyopita, kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu, ili nae azipitie na kuziwasilisha Barazani.

Kuhusiana na mabadiliko mapya ya bei ya Bima, pamoja na kuongezeka kwa gharama hizo, Shirika linashauriwa kutumia muda mkubwa kuwaelimisha wananchi ili waweze kuelewa na sio kuwashtukiza. Vile vile, Kamati inaishauri Serikali kuzingatia haja na umuhimu wa Shirika kuwa na mtaji ikiwa ni pamoja na 'Assets' za Shirika. Kitendo cha kuyachukua majengo ya Shirika, kinalidhoofisha Shirika, huku ikishangazwa na kitendo cha Serikali kuuza majengo kwa wafanyabiashara, wakati Taasisi zake hazina Afisi ya kukaa.

5.14.3 MFUKO WA HIFADHI YA JAMII :

Hoja Namba 37.1 Ufungaji wa Hesabu za Mwisho wa Mwaka:

Mfuko wa Hifadhi ya Jamii hauwasilisha hesabu zake za mwisho wa mwaka 2010/2011 kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu kwa ajili ya kufanyiwa ukaguzi. Kwa vile ukaguzi wa hesabu hizo haukufanyika itakuwa vigumu kuweza kutoa maoni kuhusu hesabu hizo pamoja na hali halisi ya fedha ya Mfuko huo.

Maelezo ya Mfuko:

Kwa mujibu wa Sheria inayoanzisha Mfuko wa Hifadhi ya Jamii, Namba 2 ya mwaka 2005, Hesabu za Mfuko hukaguliwa na Mkaguzi wa Nje na kwa mwaka 2010/2011, zilikaguliwa na Kampuni ya TAC Associates ya Dar es Salaam na ukaguzi huo ulipokamilika, ripoti yake ilikabidhiwa kwa Mfuko kwa barua ya tarehe 27/02/2012, yenye kumbukumbu namba D/5/4/136/2 na nakla ya barua hiyo pamoja na ripoti yenyewe ilinakiliwa kwa Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo; Mhasibu Mkuu wa Serikali pamoja na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa hesabu za Serikali Zanzibar.

Aidha, Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu imekuwa na kawaida ya kukagua hesabu za Mfuko katika kipindi cha kila mwaka na Mfuko wa ZSSF umekuwa unatoa ushirikiano mkubwa mpaka kufikia kupatikana kwa ripoti ya ukaguzi. Hata hivyo, kwa mwaka huo kasoro iliyojitokeza ni kutopatikana kwa ripoti ya mahesabu ya Mfuko, lakini sio kama haikuwasilishwa kabisa kwa Mdhibiti.

Ili kuondosha kasoro hiyo, kuanzia sasa mara tu baada ya kufunga hesabu na kabla ya kuziwasilisha kwa Mkaguzi wa Nje atakaeteuliwa na Bodi ya Wadhamini ya Mfuko, taarifa zote za mahesabu zitafikishwa katika Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu Zanzibar kwa mazingatio yake na maelekezo zaidi.

Maelezo ya Kamati:

Kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar, kifungu cha 112(3)(c) Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu ndie mwenye dhima ya kufanya ukaguzi kwa takriban Taasisi zote za Serikali, ikiwa ni

pamoja na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii. Pamoja na ukweli kwamba, Sheria Namba 2 ya mwaka 2005 imeipa mfuko uhuru wa kuchagua Mkaguzi wa Nje, kupitia Bodi yake ya Wadhamini, maelekezo ya Katiba yana haja kubwa ya kusimamiwa na kutekelezwa ipasavyo, na pale sheria inapopingana na Katiba, basi Sheria hiyo ama kifungu chake, kwa kiasi cha kupingana kwake, itakuwa batili.

Maoni ya Kamati:

Kwa kuwa sasa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ana uwezo wa kufanya ukaguzi katika Hesabu za Mfuko, Kamati inauagiza mfuko kufunga hesabu zake na kuziwasilisha kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kama Katiba na Sheria zinavyoelekeza.

5.14.4 CHUO CHA UONGOZI WA FEDHA, ZANZIBAR:

Hoja Namba 38.1 Kuhusiana na Matokeo ya Hesabu za Mwaka, 2010/2011.

Kwa mwaka 2010/2011, mali za Mpito za Chuo zilikuwa kubwa ukilinganisha na dhima za mpito. Mali hizo zenye thamani ya Tsh. 379,400,000/- na dhima za Mpito Tsh.1,430,000/- zinafanya mali halisi ya mali za Mpito kuwa Tsh.377,970,000/-, hali inayoonesha faraja kwa Chuo, huku kikishauriwa kwamba mali za mpito ikiwa ni pamoja na fedha taslim, waweke katika mfumo wa 'Fixed Deposit'.

Kuhusu uwezo wa kujiendesha kwa faida, imeonekana wazi kwamba, Chuo kina uwezo huo kutokana na kuongeza faida ya 1,340,000,000/- kwa mwaka 2010/2011 ukilinganisha na faida ya Tsh.92,000,000/- kwa mwaka 2009/2010. Chuo kimeshauriwa kuongeza juhudi za kukusanya mapato.

Maelezo ya Chuo kuhusiana na Hoja hii:

Pamoja na kuonekana kuwa na fedha nyingi kwa mwaka 2011/2012, Chuo kilikopa fedha kutoka Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (ZSSF), kwa lengo la kukamilisha ujenzi wa dakhalia ya wanafunzi, huku kikihakikisha pia kina pesa za kutosha za kumlipa Mkandarasi wa Ujenzi. Aidha, ujenzi huo umekiingiza Chuo katika deni kubwa linalotakiwa kulipwa kipindi cha miaka 10, huku kiasi ya Tsh.30,000,000/- zinatakiwa kulipwa kwa kila mwezi, wakati huo huo Chuo kina dhima ya kuhakikisha kinaendelea na kuimarika.

Vile vile, pamoja na Mdhibiti kuripoti chuo kuongeza mapato ya makusanyo, ieleweke kwamba, Chuo kinafunga hesabu kwa kutumia mtindo wa 'Accrual basis' badala ya 'cash basis' kama inavyofanywa na Serikali. Kwa kutumia 'Accrual basis' Chuo huripoti matumizi ya kawaida tu kama ni gharama za mwaka husika wakati matumizi ya fedha za maendeleo huripotiwa kama rasilimali (Assets), hali iliyopelekea mapato yaliyoainishwa ya 2,640,000,000/- kuwa nia pamoja

na fedha za matumizi ya Maendeleo, Tsh.500,000,000/- na matumizi ya Tsh.1,300,000,000/- yanaonekana katika taarifa ya hali ya kifedha ya Chuo (Statement of Financial Position), na kuonekana katika taarifa ya mwenendo wa fedha (Cash flow Statement), ili kupata taswira halisi ya fedha zilizotumika.

Kwa lugha hii, maelezo ya Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu, yanatakiwa yaangaliwe upya, ili kuonesha sura halisi ya uwezo wa Chuo kulipa dhima zake za muda mfupi na kujiendesha kwa faida.

Maelezo ya Kamati:

Kamati imehoji vyanzo vya mapato vya Chuo, na kuelezwa kuwa ni Ada ya Wanafunzi; Ruzuku kutoka Serikalini na kazi za Ushauri (Consultancy). Wanapopata kazi hizi za Ushauri, 70% hulipwa kwa Mwalimu ama aliyeshughulikia kazi husika huku 30% pekee zikiingia katika Akaunti ya Chuo. Miongoni mwa kazi mashuhuri za kiushauri wanazozitoa ni pamoja na Ufungaji wa Hesabu za Mwisho wa Mwaka kwa Taasisi mbali mbali za Serikali na Ukaguzi wa Hesabu.

Maoni ya Kamati:

Kamati imeishauri Uongozi wa Chuo kuongeza mapato kwa kuongeza ada ya Ushauri wanaoutoa hususan, kazi za Ufungaji wa Hesabu kwa Taasisi mbali mbali. Aidha, Chuo kijitangaze kuwa na uwezo wa kutoa ushauri Tanzania bara na sio kuendelea kutambulikana ndani ya Zanzibar, pekee.

Chuo kimeshauriwa kutoa mafunzo ya muda mfupi (Short Coures) kwa Wahasibu mbali mbali wa Taasisi za Serikali juu ya Ufungaji wa Hesabu, ili kuondosha kasoro iliyopo kwa baadhi ya Wahasibu kushindwa kutekeleza dhima hii.

5.14.5 MFUKO WA BARABARA, ZANZIBAR (ZANZIBAR ROAD FUNDS):

Mfuko wa Barabara, haujawahi kuelezwa katika ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu, kwa kipindi kirefu sasa, huku pia kwa miaka yote hiyo ambayo Kamati ilikuwa inafuatilia Ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Mfuko wa Barabara haukuwa na hoja yoyote iliyoripotiwa.

Kabla ya mwaka 2009/2010, Mfuko ulikuwa unakaguliwa moja kwa moja na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu, ambapo kuanzia mwaka huo huo baada ya Mfuko kuomba idhini ya Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu kutafuta Mkaguzi wa Nje (External Auditor), kama inavyokubalika na kifungu cha 14(2) cha Sheria Namba 2 ya mwaka 2001, na kama walivyofanya kupitia barua yao ya tarehe 25/02/2010, yenye kumbu kumbu namba MKR/MT/MFB/AD/VOL.1/34, walikubaliwa na hatimae kukaguliwa na Wakaguzi mbali mbali kutoka nje.

Aidha, mnamo tarehe 2/03/2010, kupitia barua yenye kumbu kumbu namba AUD/D.30A/VOL.1/6, Mfuko huu uliruhusiwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu, kukaguliwa na wakaguzi wan je kama tunavyonukuu:

> "Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu haina pingamizi yoyote na taasisi yako katika suala zima la kuajiri au kuwatafuta wakaguzi wa Hesabu kwa kazi za kiufundi (Technical Audit) na kazi za fedha (Financial Audit), ikiwa taratibu zilizowekwa zitafuatwa"

Suala la msingi ambalo Kamati inalihimiza ni kwamba, pamoja na ruhusa hiyo, inastahiki kwa Mfuko wa Barababara kuwashirikisha ipasavyo Aifisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu, na sio kutegemea utaratibu tu, kwa kukidhi utashi wa Sheria iliyowaruhusu. Pia, Kamati itaendelea na juhudi zake za kuhimiza Taasisi hii na Mashirika yote kwa Ujumla, sasa yakaguliwe na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu.

Hivyo basi, kwa mamlaka ya Kamati kama yanavyoelezwa katika kanuni ya 118(2)©, ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi, Toleo la 2012, Kamati imefika katika Mfuko wa Barabara kwa lengo la kupata Ufafanuzi wa kazi zao na hesabu za matumizi yao kwa kazi za kawaida na kazi za maendeleo kwa mwaka 2010/2011.

Maelezo ya Mfuko wa Barababara kuhusiana na Mapato na Matumizi ya mwaka 2009/2010; 2010/2011.

Kwa mwaka 2009/2010, Mfuko wa Barabara ulipanga kukusanya Tsh.4,703,000,000 na kufanikiwa kukusanya Tsh.5,468,409,400/- sawa na 116% ya makusanyo. Hata hivyo, waliingiziwa na kutumia Tsh. 4,802,347,966.80/- huku Tsh. 538,148,588.20 zikitumika kwa kazi za uendeshaji wa Mfuko na Ths.4,264,199,378.60 zikilipwa kwa Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano, kwa kazi za matengenezo ya barabara.

Aidha, katika mwaka huo wa fedha (2009/2010), pamoja na kuongezeka kwa makusanyo, Mfuko haukuingiziwa Tsh.812,978,595.58 za makusanyo hayo, ambayo kisheria yalipaswa kuingizwa na kutumiwa na Mfuko. Aidha, walitakiwa deni hilo la fedha walizokuwa hawajaingiziwa, kulifuta rasmi kwenye vitabu vyao vya hesabu, mnamo mwaka 2012.

Kwa mwaka 2010/2011, Mfuko ulilenga kukusanya Tsh.5,451,000,000 ya makusanyo na kufanikiwa kukusanya Tsh.5,018,224,043/- sawa na 92% . Aidha, Tsh.5,005,866,609.10 zilitumiwa, huku Tsh.822,952,500.2 zikitumika kwa kazi za uendeshaji wa Mfuko na Tsh. 4,182,914,108.96 zikilipwa na kutumika kwa matengenezo ya barabara.

Maelezo ya Kamati:

Wakati Kamati inapitia gharama za Uendeshaji wa Mfuko kwa mwaka 2009/2010, imehoji gharama za Bodi ya Mfuko Tsh.93,586,170 kwa mwaka huku ikielezwa kwamba, huku Mwenyekiti pekee akilipwa posho la vikao kama Wajumbe wengine wa Bodi, lakini pia ana

posho la kila mwezi ambalo kwa mwaka huo lilikuwa 300,000/- wakati wajumbe waliobakia hawana posho hilo. Je idhini ya posho hilo la Mwenyekiti wa Bodi kwa kila mwezi limetoka wapi, na kwa maslahi gani ya posho hilo.

Jambo jengine lililohojiwa na Kamati ni matumizi ya fedha za Matengenezo ya Barabara zinazolipwa kwa Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano, huku udhibiti na usimamizi wake ukikosekana kwa Mfuko, na namna ya usahihi wa matumizi ya fedha hizo. Aidha, Kamati imehitaji kupata ufafanuzi wa kina kuhusiana na Tsh.18,547,500/ zikiwa ni gharama za Usafiri wa Ndani (Domestic Traveling); Tsh.19,010,763.60 gharama za Usafiri wa Nje (Foreign Traveling); Tsh.2,495,000/- za Matengenezo ya Kompyuta (Computer repair), kwa mwaka 2010/2011; Tsh. 9,960,800/- kwa matumizi ya spea (spear and maintenance); na Tsh. 16,585,515/- kwa matumizi ya Mafuta na Vilainishaji (Fuel and Lubricants).

Maoni ya Kamati:

Kamati inahitaji muda na taarifa za ziada kama ilivyopewa mamlaka haya na Kanuni ya 52(5)(b) ya Kanuni ya Fedha ya mwaka 2005, na hivyo itazifuatilia na kuchunguza matumizi yote hayo tuliyoyaainisha hapo juu katika kipindi kinachofuata.

5.14.6 BENKI YA WATU WA ZANZIBAR:

Hoja Namba 39.1 Kuhusu Ufungaji wa Hesabu za Mwisho wa Mwaka, 2010/2011:

Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ) haikuwasilisha hesabu zake za mwisho wa mwaka 2010/2011 kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu kwa ajili ya kufanyiwa ukaguzi. Kwa vile ukaguzi wa hesabu hizo haukufanyika itakuwa vigumu kuweza kutoa maoni kuhusu hesabu hizo pamoja na hali halisi ya fedha ya Benki hiyo.

Maelezo ya Benki (PBZ):

Hoja ya mdhibiti ina ukweli, na hali hii inatokana na mwaka wa fedha unaohesabiwa kwa Benki ukiwa tofauti na mwaka wa fedha wa Serikali. Aidha, Benki kuratibiwa na Benki Kuuu ya Tanzania, kunapelekea Benki hii kufuata zaidi vigezo vya ukaguzi vilivyowekwa na Mamlaka hii. Hata hivyo, mara zote baada ya kukamilika kwa ukaguzi, basi Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu, hujuulishwa na kushirikishwa ipasavyo.

Maelezo ya Kamati:

Tatizo la Benki ya PBZ ni sawa na Mashirika mengine, na sasa tayari umefika muda wa Mashirika yote kukaguliwa moja kwa moja na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Zanzibar.

Maoni ya Kamati:

Kamati inaitaka Benki ya PBZ kuhakikisha wanakaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, na kwa hatua hii wanatakiwa wafunge na wawasilishe hesabu zao za mwisho wa mwaka, Afisi ya Mdhibiti kama muda na utaratibu wa kuwasilisha huko ulivyoelezwa na Sheria.

5.14.7 CHUO CHA TAIFA ZANZIBAR (SUZA)

Hoja Namba 40.1 Kuhusu Ufungaji wa Hesabu za Mwisho wa Mwaka, 2010/2011.

Chuo cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) hakikuwasilisha hesabu zake za mwisho wa mwaka 2010/2011 kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu kwa ajili ya kufanyiwa ukaguzi. Kwa vile ukaguzi wa hesabu hizo haukufanyika itakuwa vigumu kuweza kutoa maoni kuhusu hesabu hizo pamoja na hali halisi ya fedha ya Chuo hicho.

Maelezo ya Chuo:

Chuo kilifanya juhudi kubwa ya kutekeleza wajibu wa sheria na kuweza kuzimaliza hesabu zake na kuziwasilisha kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu. Hata hivyo, kutokana na sababu zilizo nje ya Chuo, kwa mwaka 2010/2011 haikuwezekana kuwasilisha hesabu hizo kwa wakati, lakini kuanzia mwaka 2011/2012 Chuo kimewasilisha mapema hesabu hizo.

Maelezo ya Kamati:

Kamati imefurahishwa na uwazi na ukweli wa Uongozi wa Chuo kukiri makosa na kuonesha namna gani imefanya marekebisho kivitendo.

Maoni ya Kamati:

Kamati inakitaka Chuo kuhakikisha kinawasilisha hesabu zake za mwisho wa mwaka kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu ndani ya wakati uliowekwa kisheria.

5.14.8 SHIRIKA LA HUDUMA ZA MAKTABA :

Hoja Namba 41.1 Kuhusiana na Ufungaji wa Hesabu za Mwisho wa Mwaka, 2010/2011.

Shirika la Huduma za Maktaba halikuwasilisha hesabu zake za mwisho wa mwaka 2010/2011 kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu kwa ajili ya kufanyiwa ukaguzi. Kwa vile ukaguzi wa hesabu hizo haukufanyika itakuwa vigumu kuweza kutoa maoni kuhusu hesabu hizo pamoja na hali halisi ya fedha ya Shirika hilo.

Maelezo ya Shirika:

Shirika limekiri kwamba hesabu hizo hazikuwasilishwa kwa Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali kwa wao awali kutokujua kwamba ni wao moja kwa moja kama Shirika ndio wanao wajibu wa kupeleka kwa Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu ama ni Wizara yao ya Elimu, kwani huko ndiko wanakowasilisha hesabu zao.

Maelezo ya Kamati:

Kamati inafahamu kwamba, Shirika la Huduma za Maktaba linajitegemea na hivyo, linawajibika moja kwa moja kuwasilisha hesabu zake za mwisho wa mwaka kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu. Hata hivyo baada ya kupata ufafanuzi hesabu zao za mwaka 2011/2012 tayari wamezifunga na kuziwasilisha kwa Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali. Kuhusu mapato na matumizi kwa mwaka 2010/2011 Maktaba ilikadiriwa kutumia Tshs. 200,000,000/- na fedha iliyopatikana ni Tshs. 185,985,335/- wakati makusanyo makisio yalikuwa ni Tshs. 1.9 milioni na mapato ni Tshs. 3,739,550/- wakati fedha za mradi wa Maendeleo na International Book Aid ni Tshs. 12,256,133.50.

Maoni ya Kamati

Kamati inalitasha Shirika la Huduma za Maktaba kutekeleza maelekezo ya sheria kwa kufunga na kuwasilisha hesabu zao za mwisho wa mwaka kwa Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali kwa wakati. Kuhusiana na Makisio/ Makadirio ya Mapato ya Shirika, Kamati inapendekeza yaendane na uhalisia yasiwe madogo mno kama ambavyo yamekisiwa kwa mwaka wa 2010/2011 ambayo yalikuwa ni Tshs. 1.9 milioni. Wakati mapato halisi yalikuwa ni Tshs. 3,739,550/-, aidha, Shirika lijitahidi kuwa na uwezo wa mapato ya kujiendesha wenyewe.

5.14.9 MAMLAKA YA MAJI (ZAWA):

Hoja Namba 42.1 Kuhusu Matokeo baada ya kufunga Hesabu za mwisho wa mwaka, 2010/2011.

Matokeo ya uchambuzi wa hesabu za Mamlaka ya maji kwa mwaka 2010/2011 zinaonesha kuwa, Mamlaka ina uwiyano mkubwa wa mali zake za mpito, ukilinganisha na dhima za mpito, na hali hii imechangiwa zaidi kwa kuwepo kwa wadaiwa wengi wa Mamlaka.

Kwa upande wa uwezo wa Mamlaka kujiendesha kwa faida, Kwa mwaka huo Mapato ya Mamlaka yalikuwa ni Tsh.9,742,454,172 na matumizi halisi yalikuwa Tsh.6,505,072,577, hali iliyopelekea faida kuwa ni Tsh.3,237,381,595. Hali hii inaonesha kwamba, faida ya Mamlaka imepanda bilioni 2.69 kwa mwaka 2009/2010 hadi kufikia bilioni 3.237, sawa na wastani wa 20.3 kwa mwaka. Mwenendo wa hesabu hizo unaonesha kuwepo kwa uwezekano wa kuonegzeka kwa faida, iwapo Mamlaka itachukuwa juhudi za makusudi kwa kupunguza gharama za uendeshaji.

Maelezo ya Mamlaka:

Mamlaka inachukua juhudi za kila siku katika kuinua uwezo wa Mamlaka kujiendesha kwa faida. Katika jitihada kuu inazozichukua ni pamoja na kuongeza wigo wa wananchi kulipa madeni yao ya maji. Katika kufanikisha suala hili, Mamlaka inaendelea kuwafungia mita wananchi husika juu ya matumizi ya maji, huku pia ikiwataka wale wote wanaopata maji kulipia maji hayo au vyenginevyo ni kuwakatia maji hayo.

Maelezo ya Kamati :

Mamlaka iangalie uwezekano wa kuweka viwango vya ulipiaji wa maji kwa mujibu wa matumizi ya mteja husika. Si busara kwa wateja wote wa kawaida, kutakiwa kulipita Tsh. 2800 tu, wakati wengine wana viwanda vya matofali, wanamwagilia mashamba yao, na kadhalika.

Maoni ya Kamati :

Kamati inaitaka Mamlaka ya Maji, kuongeza juhudi zaidi katika makusanyo ya mapato, huku ikitakiwa kuongeza wigo wa vyanzo vya mapato yake na kuwa na mikakati imara ya kusimamia mapato hayo kwa maslahi ya Mamlaka.

5.14.10 SHIRIKA LA UMEME,ZANZIBAR :

Hoja Namba 43.1 Kuhusu Ufungaji wa Hesabu za Mwisho wa Mwaka, 2010/2011.

Shirika la Umeme la Zanzibar, halikuwasilisha hesabu za mwisho wa mwaka wa 2010/2011 kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, kwa ajili ya kufanyiwa ukaguzi. Hiyo, imekuwa vigumu kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu, kutoa maoni juu ya hesabu za Shirika hilo.

Maelezo ya Shirika :

Ni kweli hesabu hizo hazikuweza kuwasilishwa, ingawa Shirika linachukua hatua madhubuti kuona kasoro hiyo haitokezei tena.

Maelezo ya Kamati :

Tatizo hili la kutowasilisha hesabu za mwisho wa mwaka, takriban liko kwa Mashirika yote ya Zanzibar. Na hii inatokana na uwezo walionao wa kisheria, kutafuta Mkaguzi wao wa nje, na hivyo, hujisahau kuwasilisha hesabu zao kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu.

Maoni ya Kamati :

Kamati inalitaka Shirika la Umeme, kuhakikisha kwamba taarifa zao za mwisho wa mwaka zinawasilishwa kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu, ili kuendana na maelekezo ya Sheria.

5.14.11 BODI YA MAPATO, ZANZIBAR.

Hoja Namba 44.1 Kuhusu Matokeo baada ya kufunga Hesabu za Mwisho wa Mwaka, 2010/2011.

Hesabu za mwaka 2010/2011 zimefungwa kwa wakati na kuwasilishwa kwa Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu zikiwa na Takwimu zinazoonyesha ya kwamba faida ya Bodi ya

Mapato imepanda kutoka Tshs. 0.66 bilioni na kufikia Tshs. 1.20 bilioni ambapo ni sawa na wastani wa asilimia 81.8 kwa mwaka.

Maelezo ya Bodi ya Mapato na Kamati ya P.A.C :

Taarifa ya Mahesabu inaonesha kwamba katika kipindi cha mwaka 2010/2011 makadirio ya mapato yaliowekwa ni Tshs. 101.849 bilioni wakati mapato halisi yalikuwa ni Tshs. 105.075 bilioni, hii imeonesha wastani wa asilimia 103.17. Kamati ilihisi kwamba bado kuna eneo pana la ukusanyaji wa mapato na hivyo kutaka kujiridhisha kwamba anaekusanya anajipangia malengo, vigezo hivyo anavipata wapi?

Je ZRB wanashirikishwa kikamilifu katika kupanga viwango vya kuyafikia malengo hayo?. Au ni Wizara ya Fedha pekee ndio hupanga malengo.

Kutokana na kukosekana majibu yaliyowazi imeonekana kwamba hakuna umakini katika kwanza kupanga makadirio ya mapato kwani mchakato huo hauwashirikishi wadau wote, lakini la pili viwango vingi hupangwa na Taasisi zenyewe nazo hujipangia malengo ambayo ni rahisi kuyafikia na kwa maana hiyo hakuna kuchacharika katika kutafuta maeneo mengine mapyha ya kuongeza mapato yetu au kuyawekea mikakati madhubuti hata yale maeneo ya vyanzo vya mapato tulivyonavyo.

Kamati haijaridhika kabisa na ukusanyaji wa mapato ya Sekta ya Utalii hasa hasa ule utalii wa watalii kulipa kabisa huko wanakotoka (***Package Tours)***.

Viwango vya malipo vya ada za Hoteli, suala la misamaha ya Kodi, Ada za Viwanja vya Ndege na malipo yanayohusiana na viza.

Maoni ya Kamati.

Suala la ulipaji wa watalii kulipia moja kwa moja liangaliwe upya na Benki ya Wananchi wa Zanzibar (PBZ) ifungue Tawi lake Uwanja wa Ndege kwa madhumuni ya malipo ya Visa.

Aidha, Kuwe na utaratibu mzuri na unaoeleweka wa kupanga viwango vya mapato kwa kila Taasisi vyenye kuendana na uhalisia wenyewe. Huku suala la misamaha ya kodi liwe na vigezo ambavyo vinapunguza kundi la wanaohitaji msamaha badala ya kuongezeka.
Bila ya kusahau kwamba, Mamlaka zinazohusika zipage mikakati madhubuti ya kuhakikisha kwamba suala la magendo ya mafuta linamalizika.

5.14.12 SHIRIKA LA UTALII :

Hoja Namba 45.1 Kuhusu Ufungaji wa Hesabu za Mwisho wa Mwaka, 2010/2011.

Shirika la Utalii, halikuwasilisha hesabu za mwisho wa mwaka wa 2010/2011 kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, kwa ajili ya kufanyiwa ukaguzi. Hiyo, imekuwa vigumu kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu, kutoa maoni juu ya hesabu za Shirika hilo.

Maelezo ya Shirika :

Tatizo la Shirika la Utalii kuwa chini ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo huku bado hatma ya Shirika hili haijafahamika kwa uwazi, inachangia kwa kiasi kikubwa kwa Shirika hili kutotekeleza majukumu yake ipasavyo, ikiwa ni pamoja na kufunga na kuwasilisha hesabu za Mwisho wa Mwaka kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Maelezo ya Kamati :

Tatizo hili la kutowasilisha hesabu za mwisho wa mwaka, takriban liko kwa Mashirika yote ya Zanzibar. Na hii inatokana na uwezo walionao wa kisheria, kutafuta Mkaguzi wao wa nje, na hivyo, hujisahau kuwasilisha hesabu zao kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu. Hata hivyo, kwa Shirika hili, Kamati inasikitishwa kwa hatua iliyofikia.

Maoni ya Kamati :

Kamati inaitaka Serikali kuharakisha kukamilika kwa hatua za hatma ya Shirika hili. Aidha, inalitaka Shirika liwasilishe hesabu zake za mwisho wa Mwaka, kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, mapema iwezekanavyo.

5.14.13 SHIRIKA LA BANDARI :

Hoja Namba 46.1 Kuhusu Matokeo baada ya kufungwa kwa hesabu za Mwisho wa Mwaka, 2010/2011 :

Kuhusiana na Uwiyano wa mali za mpito kuwa kubwa kwa mwaka 2010 kulinganisha na mwaka 2011, hali hiyo inaonesha kwamba, mali za mpito kwa mwaka 2010 ilikuwa ni Tsh.10.24 bilioni wakati 2009 ilikuwa ni Tsh. 10.62 bilioni. Na kuhusu kujiendesha kwa faida, inaonesha wazi kwamba, kwa mwaka 2010, Shirika lilipata faida ya Tsh. 0.185 bilioni wakati mwaka 2009 faida ilikuwa ni Tsh. 0.344 bilioni.

Hali hiyo inaonesha kwamba faida imeshuka kwa wastani wa 46.2% kati ya miaka hiyo miwili, na hivyo ni wajibu wa Shirika kuchukua juhudi za makusudi za kupunguza gharama za uwendeshaji ili kuongeza mapato mbali mbali yatokanayo na shughuli za bandari.

Maelezo ya Shirika :

Shirika limekiri kuwepo kwa hali hiyo ya kushuka kwa faida kutoka wastani wa Tshs. 0.344 bilioni na kufikia Shilingi 0.185 bilioni ambapo ni sawa na asilimia 46.2 kwa mwaka. Hadi

kufikia mwishoni mwa mwaka 2010, Shirika lilikuwa na wastani wa Tshs. 3,079,297,428.72 zilizowekwa amana (Deposit) kwa hesabu tafauti zilizopo kwenye Benki ya Watu wa Zanzibar. (PBZ).

Kushuka kwa faida hiyo kumetokana na Shirika lenyewe kujikita zaidi kwenye uekezaji jambo ambalo limesababisha kuwepo kwa matumizi yasiyo ya rasilimali fedha (fedha taslim) yanayotokana na gharama za uchakavu ***(Depreciation)*** wa ongezeko hilo. Rasilimali katika mwaka huo wa fedha.

Maoni ya Kamati

Miradi inayoibuliwa na Shirika iwe ni ile inayotekelezeka na yenye kuleta tija. Madeni yote Shirika inayodai kwenye Sekta mbali mbali zikia za Serikali au za binafsi, lihakikishe yanalipwa mara moja.

Misaada inayotolewa na Shirika iwe katika mpango wa maendeleo ya jamii, au huduma za jamii nyengine, basi iratibiwe na utolewaji wake uwe kweli ni kwa sababu iliyokusudiwa na wala isiwe inatolewa kwa maeneo Fulani tu.

5.14.14 SHIRIKA LA MELI NA UWAKALA :

Hoja Namba 47.1 Kuhusu Ufungaji wa Hesabu za Mwisho wa Mwaka, 2010/2011.

Shirika la Meli na Uwakala, halikuwasilisha hesabu za mwisho wa mwaka kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa ajili ya kifunyiwa ukaguzi. Kwa vile ukaguzi wa mahesabu hayo haukufanyika, itakuwa vigumu kuweza kupata tathmini kuhusu hesabu hizo pamoja na hali ya kifedha ya Shirika.

Maelezo ya Shirika:

Pamoja na maelezo ya Mdhibiti, Shirika liliwasilisha hesabu hizo kinyume na maelezo ya Mdhibiti, na kama halikuwasilisha hesabu hizo, hata hizi hoja zilizowasilishwa kuhusiana na uwezo wa Shirika, zisingeliweza kuonekana katika ripoti hiyo. Aidha, hoja hii tayari Shirika lilifanya mawasiliano mapema kwa Mdhibiti nae alikubali kuiondoa katika ripoti, ingawaje wanashangaa bado kuona hoja hiyo hiyo imejitokeza tena.

Maelezo ya Kamati:

Pamoja na majibu hayo, Kamati inaamini kwamba Shirika halikuwasilisha hesabu hizo. Hii ina maana, kama hesabu hizo zingeliwasilishwa mapema ipasavyo, ni wazi kwamba hata katika

ripoti hii lisingeliweza kuonekana. Hata hivyo, Shirika baadae limekiri kwamba ni kweli halikuweza kufunga zao za mwaka kwa wakati matokeo yake ziliwasilishwa kwa Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu zikiwa zimechelewa. Hata hivyo Shirika liliahidi mbele ya Kamati kwamba kwa sasa limejipanga na halitachelewesha tena kufunga na kuwasilisha mahesabu Afisi ya Mdhibiti.

Maoni ya Kamati:

Kamati inalitaka Shirika kuwasilisha hesabu zake za mwisho wa mwaka mapema kwa Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu.

Mambo mengine yaliyojitokeza:

Katika uchunguzi wake Kamati imebaini kwamba kuna mgongano wa kimapato kati ya Shirika la Meli na Shirika la Bandari, hususan kwa zile meli za nje zinazoingia Bandarini, Zanzibar. Hasa linapokuja suala la malipo ya Uwakala.

Aidha katika utekelezaji wa Bajeti ya mwaka 2010/2011 kuna baadhi ya maeneo ya matumizi Kamati haikuridhishwa na utaratibu unaotumika kwa mfano Kasma 236 ya Vifaa vya Kuandikia, Makisio/Makadirio yalikuwa ni Tshs. 14,500,000 wakati matumizi halisi yalitumwa ni Tshs. 32,424,962.95 ***(Mara mbili zaidi)***

Eneo jengine ni suala la kulipwa mtu asiyetoa huduma iliyohusika, kwa mfano Ndg. Fatma Jaku – Katibu Makhsusi wa Meneja Mkuu wa Shirika amelipwa jumla ya Tshs. 115,000/- ikiwa ni malipo ya ununuzi wa Stabilizer kwa Vocha Nam. MZ/OC/NO.3/11/2010 ya Tarehe 12/11/2010 wakati yeye alichoomba kwa Shirika ni 'Stabilizer' na wala siyo fedha za kununulia (Barua yake ya Tarehe 9/11/2010 inahusika). Cha kushangaza zaidi ni kwamba vocha hiyo ilikuwa Invoice ***(Supporting Documents)*** tatu ambazo ni:-

i) Invoice No. 0034 ya Ndg. Moh'd Juma Moh'd yenye thamani ya Tshs. 135,000/- (ya tarehe 2010)

ii) Invoice No. 0185 y Baha Store yenye thamani ya Tshs. 115,000/- (ya tarehe 9/11/2010)

ii) Invoice No. 0506 ya Ndg. Moh'd Juma Moh'd (Haina Tarehe). Invoice mbili kati ya hizi tatu ni mtu mmoja na moja kati yake ndio iliyolipwa nayo ni ile yenye thamani sawa nay a mwenzake (Tshs. 115,000). Kamati ilipata maswali mawili yaliyokosa majibu sahihi. La kwanza kwanini Ndg. Fatma Jaku alipwe yeye wakati yeye siye aliyeuza na la pili ni kwani wachukue Invoice mbili kwenye duka moja tena zenye kuonesha bei tofauti kwa kitu kimoja! Hilo nalo limefanyika pia kwa Ndg. Omar Simai Pandu – Afisa Uagiziaji kwa ajili ya ununuzi wa Air Condition na vifaa vyake ambapo jumla ya Tshs. 1,575,300/- zimetumika wakati kumbe malipo hayo yanaenda kwa Eletrothermal Suppliers & Services.

Maoni ya Kamati

Shirika la Bandari na Shirika la Meli wakae pamoja kujadili na kufikia muafaka juu ya namna ya malipo ya meli katika suala zima la uwakala.

Utaratibu wa makadirio ni vyema ukaenda na matumizi halisi na pale dharura inapotokezea basi kuwe na utaratibu wa kutumia ziada hiyo uwe kwa mujibu wa Sheria na Kanuni za fedha.

Taratibu za manunuzi zifuate Sheria ya manunuzi Nam. 9 ya mwaka 2005 anayetoa huduma ateuliwe kwa mujibu wa sheria na ndie ahusike na kupewa malipo hayo na si mtu mwengine.

Shirika lifunge hesabu zake kwa wakati iziwasilishe Afisini kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali mapema.

Mambo mengine yaliyojitokeza:

Katika uchunguzi wake Kamati imebaini kwamba kuna mgongano wa kimapato kati ya Shirika la Meli na Shirika la Bandari, hususan kwa zile meli za nje zinazoingia Bandarini, Zanzibar. Hasa linapokuja suala la malipo ya Uwakala.

Aidha katika utekelezaji wa Bajeti ya mwaka 2010/2011 kuna baadhi ya maeneo ya matumizi Kamati haikuridhishwa na utaratibu unaotumika kwa mfano Kasma 236 ya Vifaa vya Kuandikia, Makisio/Makadirio yalikuwa ni Tshs. 14,500,000 wakati matumizi halisi yalitumwa ni Tshs. 32,424,962.95 ***(Mara mbili zaidi)***

Eneo jengine ni suala la kulipwa mtu asiyetoa huduma iliyohusika, kwa mfano Ndg. Fatma Jaku – Katibu Makhsusi wa Meneja Mkuu wa Shirika amelipwa jumla ya Tshs. 115,000/- ikiwa ni malipo ya ununuzi wa Stabilizer kwa Vocha Nam. MZ/OC/NO.3/11/2010 ya Tarehe 12/11/2010 wakati yeye alichoomba kwa Shirika ni 'Stabilizer' na wala siyo fedha za kununulia (Barua yake ya Tarehe 9/11/2010 inahusika). Cha kushangaza zaidi ni kwamba vocha hiyo ilikuwa Invoice ***(Supporting Documents)*** tatu ambazo ni:-

i) Invoice No. 0034 ya Ndg. Moh'd Juma Moh'd yenye thamani ya

   Tshs. 135,000/- (ya tarehe 2010)

ii) Invoice No. 0185 y Baha Store yenye thamani ya Tshs. 115,000/-

   (ya tarehe 9/11/2010)

ii) Invoice No. 0506 ya Ndg. Moh'd Juma Moh'd (Haina Tarehe)

Invoice mbili kati ya hizi tatu ni mtu mmoja na moja kati yake ndio iliyolipwa nayo ni ile yenye thamani sawa nay a mwenzake (Tshs. 115,000). Kamati ilipata maswali mawili yaliyokosa majibu sahihi. La kwanza kwanini Ndg. Fatma Jaku alipwe yeye wakati yeye siye aliyeuza na la pili ni kwani wachukue Invoice mbili kwenye duka moja tena zenye kuonesha bei tofauti kwa kitu kimoja! Hilo nalo limefanyika pia kwa Ndg. Omar Simai Pandu – Afisa Uagiziaji kwa ajili

ya ununuzi wa Air Condition na vifaa vyake ambapo jumla ya Tshs. 1,575,300/- zimetumika wakati kumbe malipo hayo yanaenda kwa Eletrothermal Suppliers & Services.

Maoni ya Kamati

Shirika la Bandari na Shirika la Meli wakae pamoja kujadili na kufikia muafaka juu ya namna ya malipo ya meli katika suala zima la uwakala. Aidha, Utaratibu wa makadirio ni vyema ukaenda na matumizi halisi na pale dharura inapotokezea basi kuwe na utaratibu wa kutumia ziada hiyo uwe kwa mujibu wa Sheria na Kanuni za fedha.

Taratibu za manunuzi zifuate Sheria ya manunuzi Nam. 9 ya mwaka 2005ili anayetoa huduma ateuliwe kwa mujibu wa sheria na ndie ahusike na kupewa malipo hayo na si mtu mwengine.

Aidha, Shirika lifunge hesabu zake kwa wakati iziwasilishe Afisini kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali mapema.

5.14.15 SHIRIKA LA BIASHARA LA TAIFA (PEMBA) :

Kwa upande wa Pemba, Shirika halikuwa na Hoja yoyote katika Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu, ingawaje, Kamati imeona ipo haja ya kufanya ukaguzi kwa kuangalia suala zima la ununuzi wa karafuu, kwa mwaka 2010/2011 na 2011/2012. Katika kuangalia huko, Kamati ilikuwa inataka kupata ufafanuzi wa namna ya karafuu zinavyonunuliwa, lakini vipi zinasafirishwa na kuuzwa nchi za nje. Kamati inafahamu kwamba, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inatumia fedha nyingi katika kuzitangaza, kuzilinda na hata kununua karafuu, huku Kamati ikishindwa kujua, kwa kiwango gani cha mapato, Serikali inapata kupitia Shirika hili, lakini pia mchango wa moja kwa moja wa Karafuu kwa pato la Taifa.

Maelezo ya Shirika :

Kwa kawaida, Shirika hununua karafuu Pemba na kusafirishwa hadi Unguja kwa ajili ya mauzo kwenda nchi za nje. Kwa mwaka 2011/2012, Shirika lilikopa Tsh. 14,500,000,000/- kutoka Mfuko wa Hifadhi ya Jamii, (ZSSF) ; Tsh. 4,500,000,000/- kutoka Serikalini na 5,000,000,000/- zilikuwa ni ‘overdraft’ katika hesabu za Shirika. Fedha zote hizo kwa pamoja zilinunuliwa karafuu na faida iligawiwa katika sehemu mbili ; 50% walilipa madeni na 50% walitumia kwa kuendesha shughuli za Shirika (Administrative Costs).

Kuhusu namna Serikali inavyofaidika na Uuzaji wa karafuu, ni kupata fedha za kigeni na kuwa na ‘Balance of Payment’ inayoridhisha, ambayo huonesha ukuaji wa uchumi wa nchi. Katika kuhakikisha mafanikio yanapatikana, Serikali hutumia gharama nyingi, ikiwa ni pamoja na gharama za ‘Task Force’ kwa ajili ya kulinda usafirishaji wa karafuu kwa njia ya magendo.

Maelezo ya Kamati :

Kuhusu kukaguliwa kifedha, Shirika linakaguliwa na wakaguzi wa Nje, Kampuni ya IFAD na wala halikaguliwi na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu Zanzibar. Tatizo lililopo ni kwamba, Shirika halijafunga hesabu zake, na hivyo limeshindwa kulipa kodi Serikalini. Kamati imehoji vipi wananchi wa Zanzibar wanafaidika na uuzaji wa Karafuu. Pamoja na ukweli kwamba, wao ndio wakulima na wanaoliuzia Shirika karafuu kwa bei inayoridhisha baada ya kufanyiwa marekebisho hivi karibuni, kuna tatizo la kutoonekana maendeleo ya wazi ya wananchi hawa, tena tofauti kabisa na wakati ule yaliposhamiri magendo ya karafuu.

Suala hili la namna ya wananchi wanavyobadilika kimaisha na kimaendeleo, linahitaji kufanyiwa utafiti ili kujuulikana tatizo liko wapi, lakini inaelezwa kwamba, kuna uwezekano mkubwa wa wafanyabiashara kutoka Tanzania bara, wamehodhi soko hilo kwa kukodi mikarafuu na hivyo na hatimae fedha zote wamezihamishia Tanznia bara kwa kuendelea na biashara zao.

Kamati imehoji juu ya gharama za usafirishaji zinazotumika katika harakati za ununuzi wa karafuu na kuelezwa kwamba, fedha hizo zinatokana na mtaji wa pamoja wa ununuzi wa karafuu, ambapo hulipwa na ZSTC, kwa ajili shughuli hizo. Kamati pia ilizipitia gharama hizo na kujiridhisha kwamba, ziko sahihi, ingawaje iliwachukua siku zaidi ya mbili Shirika, katika kuziandaa kwake.

UKAGUZI WA FEDHA ZA 'TASK FORCE'

Kamati imehoji juu ya fedha nyingi zinazotumika kwa ajili ya kuendesha ulinzi maalum wa karafuu, ulinzi ambao unahusika zaidi na magendo ya karafuu. Kwanza Kamati haikupata majibu ya moja kwa moja juu ya 'task force' kutoka Shirikani na kuelezwa kwamba, suala hili taarifa zake zipo Wizarani (Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko-Unguja), ingawaje taarifa ilizopata Kamati ni kwamba, 'Task Force' huundwa baada ya agizo la Mhe. Rais, huku Mwenyekiti wake huwa ni Waziri wa Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko. Kamati ilipomhoji Afisa Mdhamini wa Wizara hii, alieleza kwamba, yeye hajui utaratibu unaotumika katika kuteuliwa kwa wajumbe wa Kamati hiyo, ingawaje barua inayowateua Wajumbe hao hutoka kwa Katibu Mkuu Kiongozi, labda Katibu Mkuu wa Wizara hii ya Biashara, anafahamu kwa sababu yeye ni miongoni mwa wajumbe hao.

'Task Force' takriban huundwa na zaidi ya watu 18 wenye nyadhifa mbali mbali Serikalini, ikiwa ni pamoja na Mwanasheria Mkuu; Mkurugenzi wa Mashtaka; Dr. Malik wa Wizara ya Afya; Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Kilimo na Maliasili; Naibu Meneja Mkuu wa ZSTC; Wakuu wa Vikosi vya Ulinzi na Usalama; Wakuu wa Mikoa na wengineo.

Kamati imeshtuka kuona fedha nyingi zinatumika kwa ajili ya 'Task Force'. Kwa mfano, kwa mwaka 2011/2012, kwa muda wa siku 90 pekee, zimetumika takriban 455,000,000 (Milioni mia nne na hamsini na tano). Kamati imehoji juu ya Tsh. 50,603,000 zilizotumika Pemba kwa awamu ya tatu ya 'Task Force' hiyo.

Katika kupitia hesabu hizo za awamu ya tatu, Pemba, Kamati imekosa vielelezo vilivyohitajika kuthibitisha matumizi ya Tsh. 7,799,000 kupitia vocha iliyohusika. Aidha, matumizi ya hesabu hizo za 'Task Force' hazijakaguliwa na Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu, lakini jambo la kushangaza tayari zimeshakaguliwa na Mdhibiti wa Ndani, huku makosa kadhaa ya matumizi ya fedha hizo yakithibitishwa na Kamati.

Kamati ilipata pia kujiridhisha baada ya kupata maelezo ya kutumiwa kwa takriban Tsh. 20,000,000 na Madiwani, huku hakuna marejesho ya kuthibitisha matumizi ya fedha hizo. Aidha, malipo ya Tsh. 1,000,000 kwa ajili ya simu (Air Time), hayana risiti. Kamati pia imejiridhisha kwa kuangalia matumizi ya nauli mbali mbali za kwenda na kurudi Unguja, zikiwa hazina vielelezo. Aidha, matumizi ya 'Miscellanious' hayapo wazi na sahihi. Kwa mfano, katika sub-voucher ya tarehe 16/12/2011, No.64 imelipiwa chakula, wakati malipo ya chakula husika pia yamo kwenye vocha zake.

Kwa ujumla, Kamati hairidhishwi na matumizi ya fedha hizi za 'Task Force' na inaamini zinatumika kwa fujo na kujinufaisha watu Fulani. Na ndio maana wakati wa mavuno ya karafuu, huwa ni wakati wa mavuno pia kwa watu wengine.

Maoni ya Kamati:

Kamati, bila ya kuathiri masharti ya Katiba, inamshauri Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, kufanya ukaguzi maalum kwa fedha zinazotumika kwa ajili ya kusimamia 'Task Force'.

Kamati kwa kutumia kifungu cha 53(5)(b) cha Kanuni za Fedha za mwaka 2005, inahitaji taarifa zaidi ili kufikia maamuzi yanayofaa juu ya hoja hii.

5.15 TAARIFA ZA UCHUNGUZI WA MAHESABU, PEMBA:

5.15.1 OFISI YA RAIS, NA MWENYEKITI WA BARAZA LA MAPINDUZI :

5.15.2 BARAZA LA MJI MKOANI:

Hoja Namba 48.1 Kuhusu Ufungaji na Uwasilishaji wa Hesabu za Mwisho wa mwaka, 2010/2011.

Ukaguzi umebaini kwamba, Baraza la Mji Mkoani, halikuwasilisha hesabu zake za mwiso wa mwaka katika Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Jambo hilo linakiuka sheria ya fedha ya mwaka 2005 kifungu cha 24(2).

Maelezo ya Baraza la Mji:

Ni kweli Baraza halijafunga hesabu wala kuzikabidhi kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu, ingawaje hawajafanya kwa dharau, bali ni kukuosekana kwa mfumo wa utengenezaji wa 'Final Accout Report' kutoka kwa wahusika, ambao ni Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo. Baraza la Mji bado hata mwaka mmoja hawajawahi kufunga hesabu hizo, na ili waweze kufanya wanahitaji angalau kupatiwa mafunzo kutoka Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo.

Maelezo ya Kamati :

Kitendo cha Mhasibu wa Baraza la Mji kudai kutojua mpaka apate mafunzo, hakiiridhishi Kamati inayofahamu kwamba, sifa moja ya Uhasibu ni kuwa muelewa wa kufunga hesabu. Kwa udhaifu huu, Kamati ikahitaji kuangalia uwezo wa watendaji wa fedha wa Baraza kupitia 'Cash Book' na 'Bank Statement ' kama vinaendana na kuangalia kwa ujumla hesabu za Baraza. Katika hili, Kamati imejiridhisha kwamba Baraza halifanyi 'reconciliation ' na hivyo ni sawa na kusema, Baraza lina mapungufu kadhaa katika usimamizi wa fedha za Umma.

Kamati ilipouliza iwapo Baraza lina Daftari la kuhifadhia mali, ilielezwa kwamba hawana kwa sababu hawajapata mafunzo kamili kutoka Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, isipokuwa wamepata wiki moja tu ya mafunzo hayo. Majibu haya yameikasirisha Kamati kwa sababu inafahamu na tayari imethibitishiwa zamani kwamba, Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, imetoa zamani mafunzo hayo.

Jambo la kusikitisha zaidi ni kwamba, Hata Afisa Mdhamini wa Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi anaesimamia Mabaraza haya ya Miji, aliwasuta mbele ya Kamati kwamba, mafunzo hayo kutoka Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, waliyapa zamani tena kwa ufanisi kabisa. Hali hii ilimlazimu Katibu wa Baraza la Mji kukiri mbele ya Kamati kwamba kweli walipata mafunzo hayo, ila sasa hoja ikawa katika ugumu wa kuyatekeleza kivitendo.

Kamati baada ya hayo, iliangalia hilo daftari lenyewe na kugundua kwamba, halina hata kipengele kimoja kilichokamilika, na kujiridhisha kwamba, Baraza la Mji Mkoani, lina mapungufu kadhaa ya kiutendaji na usimamizi wa majukumu yake.

Maoni ya Kamati :

Kamati imelitaka Baraza la Mji kuhakikisha linawasilisha hesabu zake za mwisho wa mwaka kwa wakati katika Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu. Aidha, Kamati inawaagiza kukamilisha daftari la kuhifadhia mali zake na lijazwe kwa mujibu wa taarifa muhimu na sahihi zinazotakiwa ziwemo katika daftari hilo. Kamati imetoa onyo kwa Katibu wa Halmashauri, Mhasibu na watendaji wengine wanaothubutu kuidanganya Kamati.

Mapato na Matumizi ya Baraza la Mji, Mkoani :

Kamati ilihitaji kupatiwa uchanganuzi wa mapato na matumizi ya Barza la Mji kwa mwaka wa fedha 2010/2011 na kuelezwa kwamba, Baraza kwa mwaka huo wa fedha lilifanya makisio ya kukusanya Tsh.17,000,000 na kufanikiwa kukusanya Tsh. 25,031,400 huku matumizi halisi yakawa fedha hizo hizo Tsh. 25,031,400. Kamati imehoji sababu zilizopelekea kufanya makisio madogo ya makusanyo wakati walikuwa na uwezo wa kukusanya zaidi, na kuelezwa kwamba, waliimarisha vianzio vyao vya mapato na kubuni vianzio kadhaa ikiwa ni pamoja na maegesho ya magari.

Kwa upande wa matumizi, walipanga kutumia fedha Tsh.17,500,000 lakini walipoona wamekusanya zaidi (Tsh.25,031,400) wametumia hizo hizo bila ya Kikao cha Madiwani kukaa na kuidhinisha. Yaani Uongozi wa Halmashauri umejiidhinishia fedha kinyume na taratibu za kisheria.

Kamati imekemea tatizo la kukiuka masharti ya sheria.

5.15.3 BARAZA LA MJI CHAKE CHAKE:

Hoja Namba 48.2 Kuhusiana na Hesabu ya Baraza la Mji, Chake Chake.

Mapato:

Kwa mwaka wa fedha 2010/2011, Baraza la Mji Chake lilikadiriwa kukusanya Tsh.50,000,000 na ilipofikia June 2011, walifanikiwa kukusanya Tsh.64,617,900, sawa na 129% ya makadirio.

Matumizi

Baraza liliidhinishiwa kutumia Tsh.50,000,000, na hadi ilipofika June 2011, matumizi halisi yalikuwa Tsh.64,617,900 sawa na 129% ya makadirio.

Ufafanuzi uliohitajika kwa Kamati na Maelezo ya Baraza:

Baraza lilithibitisha kufanywa makisio ya makusanyo ya Tsh.50,000,000 na Kamati ilihoji iwapo kuna kikao chochote cha Madiwani kilichokaa na kupitisha makisio hayo ya makusanyo? Aidha, suala hili hili liliulizwa kwa matumizi ya Barazza iwapo yaliidhinishwa lakini zaidi matumizi ya ziada ya Tsh. 64,617,900 kinyume na Tsh.50,000,000 yaliyoidhinishwa.

Kamati ilijibiwa kwamba, ziada hiyo iliidhinishwa na Kamati ya Fedha ya Baraza la Mji Chake kupitia kikao cha tarehe 25/4/2011. Kamati hii ilipohoji uwezo wa Kamati ya Fedha ya Baraza kuidhinisha mapato na matumizi ya ziada kinyume na Baraza la Madiwani, ilikubaliwa kwamba, hilo ni kosa kisheria. Kinyume na kifungu cha 45(2) na kifungu cha 41(2)(3) cha Sheria Namba 4 ya mwaka 1995. Hata hivyo, watendaji wa Baraza la Mji, Chake waliendelea kusisitiza kwamba huo ndio utaratibu waliouzeoa.

Aidha, katika matumizi ya Tsh. 64,617,900, badala Tsh.50,000,000 kama ilivyoidhinishwa na Baraza la Madiwani, Watendaji wa Baraza la Mji Chake, wameshindwa kuonesha kwa Kamati matumizi ya Tsh. 14,617,900 ya nyongeza ya fedha zilizoidhinishwa.

Maoni ya Kamati:

Baraza la Mji, Chake linafanya matumizi ya ziada kinyume na matumizi yaliyoidhinishwa na Baraza la Madiwani, bila ya kupata idhini ya Baraza hilo la Madiwani na matokeo yake, Sheria huvunjwa bila ya kujali athari zake.

Kamati pia imelitaka Baraza la Mji Chake, kukusanya kodi kwa wamiliki wa nyumba na majengo mbali mbali katika maeneo yao, kwani hiyo nayo ni sawa na biashara nyengine. Kwa Mfano Kamisheni ya Utalii imekodi ofisi na kulipa kila mwezi, lakini hakuna kodi yoyote inayolipwa na mmiliki wa nyumba hiyo kwa Serikali.

Ufungaji na Uwasilishaji wa Hesabu za Mwisho wa Mwaka, 2010/2011.

Baraza la Mji Chake limeshindwa kufunga na kuwasilisha hesabu zake za mwisho wa mwaka kwa Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, kinyume na maelekezo ya kifungu cha 24(2) cha Sheria ya Fedha ya mwaka 2005.

Maelezo ya Baraza:

Ni kweli hawakufunga na hii pamoja na sababu nyengine imesababishwa na kwamba, mfumo wa kuwasilisha hesabu hizi bado haujatolewa na Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo.

Maelezo ya Kamati:

Hoja ya Baraza la Mji haina mashiko yoyote kwani hata sheria inayoanzishwa Baraza hili, Sheria Namba 4 ya mwaka 1995, katika kifungu cha 43 cha Sheria hiyo. aidha, ni majukumu ya Mhasibu wa Halmashauri kufunga na kuwasilisha hesabu za Baraza kwa wakati.

Maoni ya Kamati:

Kamati imewataka Baraza la Mji kuhakikisha hesabu zao za mwisho wa mwaka (2012/2013) na kila mwaka unaofuata, zinawasilishwa kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu kwa wakati.

5.15.4 BARAZA LA MJI, WETE.

Hoja Namba 48.3 Ufungaji na Uwasilishaji wa Hesabu za Mwisho wa Mwaka, 2010/2011.

Baraza la Mji Wete limeshindwa kufunga na kuwasilisha hesabu zake za mwisho wa mwaka kwa Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, kinyume na maelekezo ya kifungu cha 24(2) cha Sheria ya Fedha ya mwaka 2005.

Maelezo ya Baraza la Mji, Wete.

Ni kweli hawajafunga hesabu kutokana na kutokuwa na utaratibu mmoja na muongozo uliotolewa na Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo. Aidha, Mabaraza ya miji yamo katika marekrbisho (reforms), hivyo, kuna mapungufu mengi ikiwa ni pamoja na kutofunga hesabu kulikopelekea kuwepo kwa haja ya reforms hizo.

Maelezo ya Kamati.

Maelezo ya Baraza la Mji hayawezi kukubalika, na hoja ya marekebisho (reforms) isichukuliwe kuwa ni kisingizio cha wao kutofunga hesabu hizo.

Maoni ya Kamati :

Kamati inawataka Baraza la Mji, kufunga hesabu na kuziwasilisha kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu, na kosa hilo lisirejee tena kwa mwaka 2012/2013 na kuendelea.

Ufafanuzi wa Mapato na Matumizi ya Baraza la Mji Wete, 2010/2011.

Kasoro mbali mbali zilizojitokeza wakati wa Uchunguzi :

Kamati ililazimika kufanya kazi siku mbili katika Baraza la Mji Wete, kutokana na kutojiandaa kwa kazi katika siku ya awali. Kuhusiana na Mapato na Matumizi, Kamati kwa mara ya awali ilihitaji ya mwaka 2011/2012, lakini kwa kuwa Baraza walijiandaa kwa mwaka 2010/2011, Kamati ilihitaji kupatiwa hesabu hiyo.

Hata hivyo, ufafanuzi huo uliohitajika walishindwa kuutoa kwa kile kinachodaiwa Baraza hili la Mji, hujitenga sana baina ya watendaji na Madiwani. AAkitihibitisha hilo Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, alithibitisha kwamba alitoa muongoz wa kutosha kwa watendaji wa Baraza hili kuandaa taarifa inayohitajika kwa Kamati, jambo ambalo wamedharau na kutofanya.

Wakitoa maelezo Madiwani mbali mbali, ikiwa ni pamoja na Mwenyekiti wa Baraza ; Diwani wa Wadi ya Kizimbani na wengineo, wamethibitisha kwamba, kuna haja kubwa ya mabadiliko kwa watendaji wa Baraza hili, kwa kile kinachodaiwa kujifanyia maamuzi peke yao, wakati wao ni watendaji wa Baraza hilo.

Madiwani hao wamethibitisha kwamba, hakuna kumbu kumbu zozote zinazowekwa kuthibitisha namna gani Madiwani wanaidhinisha Makusanyo/Mapato na Matumizi ya Baraza hili. Aidha, Kamati imethibitishiwa pia kwamba hata Mkaguzi wa Ndani hakuna katika Baraza hili, jambo linalozidisha matumizi mabaya ya fedha za Serikali. Aidha, Baraza linamtumia Mkaguzi wa Ndani wa Wizara, ambapo Kamati imethibitishiwa kwamba hakuwahi kufanya kazi yake tokea 2011, huku ikizidishwa kuelezwa kwamba, yuko peke yake na Wizara ni kubwa.

Kuhusiana na matumizi yenye vielelezo na manunuzi yanayofuata taratibu za sheria, imethibitishwa kwa Kamati kwamba, Afisa Manunuzi wa Baraza hili hatekelezi ipasavyo majukumu yake, na Kamati ilipopitia baadhi ya vielelezo vya manunuzi na matumizi, imejiridhisha kwamba, hakuna vielelezo vilivyokamilika. Kwa mfano, katika hatua za ujenzi, ni fundi huyo huyo mmoja tu, Ndg. Juma Said Juma, ndie anaepewa pekee kazi za ujenzi, bila ya ushindani na taratibu zinazokubalika. Kwa Ufupi Afisa Manunuzi huyu hajasomea na hana uwezo wala elimu ya kazi hizo.

Maoni ya Kamati :

Serikali ichukue hatua za haraka kuondosha kasoro zilizojitokeza katika Baraza la Mji, Wete.

5.15.5 HALMASHAURI YA CHAKE CHAKE :

Hoja Namba 48.4 Kuhusiana na Ufungaji na Uwasilishaji wa Hesabu za Mwisho wa Mwaka, 2010/2011.

Halmashauri ya Chake Chake imeshindwa kufunga na kuwasilisha hesabu zake za mwisho wa mwaka kwa Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, kinyume na maelekezo ya kifungu cha 24(2) cha Sheria ya Fedha ya mwaka 2005.

Maelezo ya Halmashauri :

Wamekiri kwamba hawafungi wala kuwasilisha hesabu zao za mwisho wa mwaka kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu na hii imetokana na Serikali ilikusudia kuwepo kwa mfumo mmoja tu wa ufungaji wa hesabu za Serikali za Mitaa, lakini tatizo ni kwamba mfumo huo haujatoka.

Maelezo ya Kamati :

Kufunga Hesabu na kuwasilisha kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu ni suala linalohitajika kisheria, na sio sahihi kwa Halmashauri kuendelea kusubiri muongozo maalum ili iweze kutekeleza sheria.

Maoni ya Kamati :

Kamati inaitaka Halmashauri kufunga na kuwasilisha hesabu zake za mwisho wa mwaka kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu, kama inavyoelekezwa na sheria.

Ufafanuzi wa Mapato na Matumizi ya Baraza la Mji Wete, 2010/2011.

Kasoro mbali mbali zilizojitokeza wakati wa Uchunguzi :

Halmashauri ilikisiwa kukusanya Tsh.35,200,000, ila ilikusanya Tsh.36,800,000 na matumizi halisi yalikuwa ni Tsh.37,136,338. Matumizi haya ni makubwa kuliko makisio yao, na

imeelezwa sababu ya kuzidi kwake ni kutokana na uhaba wa fedha wanazopata kwa mnasaba wa mahitaji, hivyo hulazimu makusanyo yote yanatumika kama yalivyokusanywa.

Kuhusu iwapo kuna ridhaa ya Baraza la Madiwani, Mwenyekiti wa Baraza la Madiwani amethibitisha kwamba, matumizi hayo sio waliyoyaidhinisha, ila Katibu wa Halmashauri aliieleza Kamati kwamba, fedha hizo huzitumia kwa mahitaji mbali mbali ya Halmashauri. Hata hivyo, Kamati imejiridhisha kwamba, fedha hizo zimetumika kinyume na utaratibu wa sheria namba 4 ya mwaka 1995 na kinyume na Sheria ya fedha ya 2005.

Kufuatia hali mbaya ya Utekelezaji wa majukumu kwa Katibu wa Halmashauri hii, Madiwani waligoma tarehe 22/10/2012 kwa kufunga mlango wa Halmashauri na waliieleza Kamati kwamba hawawezi kurudi katika Halmashauri hii, mpaka Uongozi wake kwa ngazi ya watendaji utakapobadilishwa.

Aidha, Madiwani hao wamethibitisha kwamba, hawako tayari wananchi wao watozwe kodi mpaka watendaji wakuu utakapobadilishwa kwa sababu hawana imani na Uongozi huo, unaokusanya mapato kila siku, lakini huishia katika matumbo yao, kwa maslahi binafsi.

Maoni ya Kamati :

Kamati inaitaka Serikali kufanya mabadiliko makubwa kwa Katibu wa halmashauri na watendaji wake wa karibu, ili Halmashauri ibakie na amani na maendeleo. Aidha, Serikali inatahadharishwa na kufanya mabadiliko ya kumhamisha Katibu huyo kutoka hapo alipo kwenda Halmashauri ya Micheweni, kwamba kitendo hicho kitaidhoofisha Halmashauri hiyo, kwa sababu Katibu huwezi kutekeleza majukumu yake kwa maslahi ya Taifa.

5.15.6 HALMASHAURI YA WILAYA YA MICHEWENI:

Hoja Namba 48.5 Kuhusu Mapato na Matumizi ya Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni:

Kwa mwaka 2010/2011, Halmashauri ililenga kukusanya Tsh. 20,000,000, lakini mapato halisi yalikuwa Tsh. 40,580,114 sawa na 203% , kiwango ambacho kinaweza kuongezeka iwapo vyanzo vyote vya mapato vitasimamiwa ipasavyo.

Kwa upande wa matumizi, wametumia Tsh. 40,580,114 sawa na makusanyo yao, wakati hapo kabla, makadirio ya matumizi yao kwa kazi za kawaida ilikuwa Tsh. 20,000,000.

Maelezo ya Halmashauri:

Ni kweli Halmashauri iliongeza makusanyo ya mapato kutoka na kujipanga vizuri katika mwaka huo. Walitumia mbinu ya kufanya ‘study’ katika Halmashauri za Unguja na kuzungumza na wananchi wao juu ya umuhimu wa kulipia kodi na gharama nyengine kwa Halmashauri, jambo lililowasadia sana kuongeza wigo wa makusanyo. Kwa ujumla, uelewa wa wanachi umewasaidia sana kufanikiwa.

Maelezo ya Kamati:

Kamati imepokea taarifa ya matumizi ya Halmashauri na kuchunguza iwapo yamefuata taratibu za Sheria, na kwa kiasi kikubwa imeridhika. Kwa ujumla, katika Halmashauri za Kisiwani Pemba, Halmashauri hii ni ya kupigiwa mfano kwa maendeleo ya makusanyo na matumizi ya fedha za Serikali.

Maoni ya Kamati:

Kamati imeridhika na matumizi ya Halmashauri hii, na inazitaka Halmashauri nyengine kusoma na kuiga mwendo mzuri wa Halmashauri hii.

Hoja Namba 48.5.1 Kuhusu Wadaiwa wa Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni:

Ukaguzi umebaini kwamba, Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni inadai Tsh. 17,700,000 kwa watu bonafsi na Taasisi zisizokuwa za Serikali katika Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni. Wadaiwa hao ni Zantel kwa kuweka Minara anadaiwa Tsh. 2,400,000; Airtel kwa kuweka mabango, anadaiwa Tsh. 3,150,000; Swahili Divers kwa kujenga Swimming Pool na kuweka Bango, anadaiwa Tsh. 2,000,000; Kigomasha Hotel anadaiwa Tsh. 10,150,000 kwa kujenga Nyumba 63, Swimming Pool na mabango mawili; na Muyuni Hotel kwa kujenga fensi za nyumba 30, bango moja, swimming pool, uchukuaji wa mawe gari 150 na uchukuaji wa fusi gari 100, anadaiwa Tsh. 2,000,000.

Maelezo ya Halmashauri:

Ni kweli wanawadai taaasizi hizo fedha zilizoainishwa na wanakabiliwa na changamoto hizo. Hata hivyo juhudi ya kuwadai wadaiwa hao wanaendelea kuzichukuwa, kwa mfano kuhusu deni la Air Tel, walifika hata kuonana na Waziri wa Wizara zinazohusiana na Mawasiliano Tanzania bara na Zanzibar, kwa ajili ya kufuatilia deni hilo. Tatizo liliopo ni kwa Kampuni ya Zantel ambayo haiwalipi kabisa. Tena wamejenga minara bila hata ya kibali cha Halmashauri hiyo.

Kwa ufupi mdaiwa pekee aliyemaliza deni lake ni Muyuni Hotel pekee, na Air Tel kulipunguza kwa kulipa Tsh. 1,050,000, lakini taasisi zilizobakia zinaendelea kudaiwa kama mwanzo.

Maelezo ya Kamati:

Kamati haikuridhishwa na taarifa ya Kampuni ya Zantel kutolipa deni huku ikiwa pia imejenga minara yake bila ya kibali. Tatizo zaidi, haitoi mashirikiano ya karibu na watendaji pamoja na wananchi wanaokaa katika maeneo hayo. Aidha, Kamati hairidhishwi na hatua za kudai madeni hayo, na juhudi za kudai zaidi zinahitajika kuchukuliwa.

Maoni ya Kamati:

Kamati ianiagiza Halmashauri ya Micheweni kuendelea kuzidai taasisi hizo, ili madeni hayo yaweze kulipwa kama inavyotakiwa. Aidha, kuhusiana na Zantel, Kamati imeitaka Serikali

kuisimamia Kampuni hii bila ya muhali, ili iweze kutekeleza sheria na taratibu za tawala za Mitaa.

5.15.7 HALMASHAURI YA WILAYA YA MKOANI:

Hoja Namba 48.6 Kuhusiana na Taarifa za Mapato na Matumizi:

Kwa mwaka 2010/2011, Halmashauri ililenga kukusanya Tsh. 19,400,000, lakini mapato halisi yalikuwa Tsh. 19,900,000 sawa na 105% , kiwango ambacho kinaweza kuongezeka iwapo vyanzo vyote vya mapato vitasimamiwa ipasavyo.

Kwa upande wa matumizi, Halmashauri ililenga kutumia Tsh. 10,000,000, ingawaje hadi kufikia June 2011, iliweza kutumia Tsh.7,600,000 kwa kazi za kawaida, ambazo ni sawa na76% ya makadirio. Kwa upande wa matumizi ya maendeleo, Halmashauri ilitumia Tsh. 12,000,000 sawa na 61.8 ya makadirio yaliyokuwa yamekisiwa ambayo ni Tsh. 19,400,000.

Maelezo ya Halmashauri na Maelezo ya Kamati:

Kamati ilihoji juu ya vigezo vilivyotumika kufanya makisio, na kuelezwa kwamba, hakuna vigezo maalum isipokuwa Halmashauri inachofanya ni kuangalia vyanzo vyake vya mapato na kuvisimamia ipasavyo. Aidha, Kamati imejiridhisha kama zilivyo kwa Halmashauri nyengine, kwamba masuala ya kuidhinisha matumizi na makusanyo ya ziada hufanywa kwa Kamati ya Fedha, badala ya kufanywa na Baraza la Madiwani lenye mamlaka hayo kwa mujibu wa sheria Namba 4 ya mwaka 1995.

Maoni ya Kamati:

Kamati inazitaka Halmashauri za Wilaya kutumia fedha za Serikali kwa mujibu wa taratibu zilizowekwa.

Hoja Namba 48.6.1 Kuhusiana na Malipo yasiyokuwa na Vielelelezo ya Tsh. 6,123,000.

Ukaguzi umebaini kwamba, malipo yamefanyika lakini vielelezo husika havikuambatanishwa na hati za malipo, ili kuweza kuthibitisha uhalali wa malipo hayo. Kuoambatanishwa kwa vielelezo vya malipo ni kwenda kinyume na kanuni ya fedha ya 95(4) ya mwaka 2005.

Maelezo ya Halmashauri:

Ni kweli nah ii imetokana na kuchelewa kupewa risiti zinazohusiana na masuala ya ujenzi waliyokuwa wanayasimamia. Hata hivyo, walieleza kwa kujiamini kwamba, vielelzo hivyo tayari vipo.

Maelezo ya Kamati:

Kamati imezipitia hati hizo za malipo, ili kuona kwamba tayari vielelezo vyake vimeshapatikana kama ilivyoahidiwa, na ilipokuwa inapitia Hati Namba 2/1 yenye thamani ya Tsh. 160,000 kwa ajili ya ununuzi wa vitabu vya risiti, vilelelezo vyake vilikuwa bado havijakamilika.

Aidha, hati namba 14/3 ya Tsh.340,000 kamati pia imekosa vielelezo. Kwa ujumla, Kamati haijapata hata hati moja iliyokamilika vielelezo vyake. Na kwa ufupi Kamati imejiridhisha kwamba, hapa fedha zimetumika kinyume na utaratibu.

Jambo la kushangaza zaidi, Kamati pia imekosa vielelezo vya malipo yaliyofanywa kwa Idara ya Ardhi na Upimaji, kwamba, hata hii taasisi ya Serikali, nayo pia haitoi risiti halali kwa malipo yanayofanywa.

Kamati ilipohoji sababu zilizopelekea tatizo hilo, iligundua pamoja na sababu nyengine, Mhasibu wa Halmashauri hii, amefika 'Form IV' wala hajasomea masuala ya uhasibu.

Maoni ya Kamati:

Kitendo cha kufanya matumizi ya fedha za Serikali, bila ya kuwa na vielelezo, kunapingana na masharti ya Sheria ya Fedha kifungu cha 95(1) na (4). Aidha, ni wazi kwamba, katika maeneo yaliyojaa udhaifu wa matumizi mabaya ya fedha za Serikali, ni pamoja na Halmashauri za Wilaya. Kamati inaiagiza Serikali, kuwachukulia hatua za kisheria na kinidhamu Afisa Mhasibu wa Halmashauri hii, Mhasibu pamoja na watendaji wote wa Halmashauri hii waliohusika na kadhia hii.

Hoja Namba 48.6.2 Kuhusu Ufungaji na Uwasilishaji wa Hesabu za Mwisho wa Mwaka, 2010/2011:

Kwa mujibu wa sheria ya fedha, Namba 12 ya mwaka 2005, kifungu cha 24(2) kinaeleza wajibu wa taasisi za Serikali kufunga hesabu za mwisho wa mwaka na kuziwasilisha kwa kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu kwa ajili ya kufanyiwa ukaguzi. Halmashauri hii kwa mwaka 2010/2011, haikuwasilisha hesabu hizo na hivyo, Afisi ya Mdhibiti haikuweza kutoa maoni kuhusu hesabu hizo pamoja na hali halisi ya fedha za Halmashauri hiyo.

Maelezo ya Halmashauri:

Ni kweli kasoro hiyo imejitokeza kwa mwaka huo, nah ii inatokana na utaalamu unaohitajika wa kufunga hesabu hizo. Hata hivyo, Halmashauri itajitahidi kujirekebisha na kuweza kuwasilisha hesabu hizo kwa Mdhibiti.

Maoni ya Kamati:

Kamati inaitaka Serikali kufanya marekebisho makubwa ya kitengo cha Fedha katika Halmashauri hii, huku ikieelewa kwamba, Mhasibu wa Halmashauri hii hana elimu ya fani hiyo, na amefika Kidato cha Nne (Form IV).

5.16 WIZARA YA ARDHI, MAKAAZI, MAJI NA NISHATI, PEMBA.

5.16.1 MAMLAKA YA MAJI, PEMBA:

Hoja Namba 48.9.1 Kuhusu Malipo yasiyokuwa na Vielelezo, Tsh.28,365,000.

Ukaguzi umebaini kwamba, kuna matumizi yamefanyika kwa ajili ya sensa ya kuwatambua watumiaji wa maji, Pemba lakini vielelezo husika, havikuambatanishwa na hati za malipo ili kuweza kuthibitisha uhalali wa malipo hayo. Aidha, kutoambatanisha vilelezo vya malipo ni kwenda kinyume na kanuni ya 95(4) ya Kanuni za Fedha za mwaka 2005.

Maelezo ya Mamlaka ya Maji:

Ni kweli Mdhibiti amehoji juu ya fedha ambazo zinadaiwa kutumika bila ya kuwa na vielelezo vya matumizi yake. Matumizi ambayo yametumika kwa ajili ya Sensa ya kuwatambua watumiaji wa maji Pemba. Hata hivyo, Mamlaka ilieleza kwamba, suala la sensa limefanywa kwa watendaji mabali mbali wa Mamlaka na utekelezwaji wake upo katika utaratibu wa ripoti ambayo inaandaliwa Makao Makuu ya Mamlaka Unguja.

Maelezo ya Kamati:

Kamati ilibaini kwamba Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu hakuweza kupewa Ripoti ambayo ndio kielelezo cha utekelezaji wa kazi hiyo. Matokeo ya Ripoti hiyo ingeweza kuonesha thamani halisi ya matumizi hayo.

Hata hivyo Mamlaka ya Maji Pemba iliarifu Kamati kwamba suala la utayarishaji wa Ripoti hiyo linatekelezwa kwa ujumla wake (Zanzibar nzima) na haitakuwa Ripoti ya Pemba peke yake, na matayarisho hayo yanafanyika Afisi ya Takwim Unguja kwa pamoja na Mamlaka ya Maji (Makao Makuu).

Maoni ya Kamati:

Kamati kwa kutumia kifungu cha 52(5)(b) cha Kanuni za Fedha za mwaka 2005, inahitaji taarifa zaidi ili kufikia maamuzi, na hivyo, hoja hii itafuatiliwa katika kazi zijazo za Kamati.

5.16.2 IDARA YA NYUMBA, MAENDELEO NA MAKAAZI – PEMBA

Hoja Namba 48.10.1 Kuhusu Madeni ya Nyumba Tsh. 122,439,440.

Ukaguzi umebaini kwamba, nyumba nyingi zimekodishwa kwa taasisi za Serikali na watu binafsi, lakini malipo ya kodi kwa nyumba mhizo hayapatikani kutokana na waliokodishwa kutolipa kodi za nyumba hizo. Aidha, kukosekana kwa kodi hizo kunapelekea kukosesha mapato ambayo yangelisaidia kuzifanyia matengenezo nyumba hizo kwani baadhi yake zipo katika hali mbaya. Kati ya jumla ya madeni, Tsh.67,943,400 ni madeni ya Taasisi za Serikali na Tsh. 54,496.040.

Maelezo ya Idara

Katika suala zima la malipo ya wakaazi wa nyumba zilizokodishwa na Wizara , Idara imewaandikia baadhi ya Taasisi tu barua za ukumbusho. Kati ya Wadaiwa ishirini na moja (21) (Taasisi) Idara imeziandikia Taasisi kumi tu. Baadhi ya Taasisi kama vile:-

i) Pemba Airport

ii Polisi – Kaskazini (P)

iii) Shirika la Meli

iv) Afisi ya Utawala Bora

v) Afisi ya Rais

vi) Mshauri wa Rais

vii) Idara ya Ardhi

viii) Mkuu wa Wilaya

x) Afisa Mdhamini – (WAMMN)

xi) Tume ya Uchaguzi

xii) Afisi ya Uhamiaji

Maelezo ya Kamati.

Kamati ilipata mashaka juu ya nia ya dhati ya Idara ya kutaka kulipwa. Ni kwanini ichague wa kuwakumbusha madeni. Aidha maelezo yamekuwa na utata mwingi juu ya nani hasa anastahiki kulipa deni – kwa mfano unapomuandikia Kamanda wa Polisi Mkoa wakati kodi hili amepangiwa askari ni usumbufu usio wa lazima kwani anaedaiwa ni askari na wala sio jeshi la Polisi. Pamoja na Taasisi nyengine ambapo muhusika ni mfanyakazi tu wa Taasisi lakini suala la kodi au pango la nyuma ni jambo binafsi.

Aidha Kamati ilishangazwa juu ya deni Afis Mdhamini wa Wizara ya Ardhi, Makaazi na Nyumba kuwa na deni la Tshs. 1,141,000 wakati maelezo ni kwamba alitakiwa alipe mtu binafsi pamoja na kwamba kwa wakati huo alikuwa na wadhifa huo. Deni likabakia na utata.

Maelezo yaliyotolewa pia yameipa wasiwasi Kamati juu ya utambuzi wa kweli wa nyumba za watu binafsi na zile zilizobakia Serikalini hasahasa zile za vijiji kwani kuna baadhi yake zimeuzwa lakini kuna nyengine bado ambazo nazo baadhi ya wakaazi wanadai kuwa ni zao.

Kwa mfano nyumba za Maendeleo – Micheweni karibu nyumba zote zimeuzwa zimebakia nyumba tano tu. Hata hivyo Idara inadai zaidi ya Tshs. 13 milioni.

Kwa ujumla Kamati kwa eneo hili haikuweza kupata majibu muwafaka na bado hoja hii haikujibika. Kamati haikuridhika.

Maoni ya Kamati :

Kamati inaiagiza Serikali kuwa na udhati wa kusimamia madeni ya nyumba. Aidha, Idara ihakikishe madeni yote ya nyumba yanalipwa mara moja, vyenginevyo ni dhahiri kwamba, Katibu Mkuu, Mkurugenzi wa Idara hii na watendaji wote wanaohusika, wanastahiki kuwajibishwa kwa kutosimamia ipasavyo madeni hayo. Aidha, Kamati inaidata Idara ya Nyumba kuendelea kudai malipo hayo, huku taarifa za madai hayo, ikiwa ni pamoja na barua, zinakiliwe kwa Mwenyekiti wa Kamati ya P.A.C.

Kamati inaishauri Serikali kuangalia uwezekano wa Idara hii kuwa Mamlaka, ili iachiwe moja kwa moja usimamizi wa nyumba, huku wakiwezeshwa ipasavyo.

HOJA KUHUSIANA NA MALIPO YA TSH. 300,000 YA UPIMAJI WA KIWANJA YALIYOFANYWA NA HALMASHAURI YA WILAYA YA MKOANI.

Wakati Kamati inafuatilia Ripoti hii kwa upande wa Halmashauri ya ya Wilaya ya Mkoani, ilikutana na hoja namba 48.6.1 inayohusiana na malipo yaliyofanywa na Halmashauri hii ya Mkoani, bila ya kuwa na vielelezo. Kati ya malipo hayo, hati namba 6/2 ya hundi namba 536745, na thamani ya Tsh.300,000 imelipwa kwa Idara ya Ardhi na Mipango Miji, kwa ajili ya upimaji wa kiwanja, bila ya kuwa na vielelezo.

Kwa kuwa Idara hii ni Taasisi ya Serikali, Kamati ilihofia kwamba, fedha hizo zimeshaingia mikononi mwa wajanja wachache na kwa nini risiti za serikali zisitolewe kuthibitisha malipo halisi.

Suala hili lilipatiwa maelezo na Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati pamoja na Idara husika na kwa mashirikiano na Halmashauri ya Mkoani kwamba, Katibu wa Halmashauri aliomba kwa barua kutaka kupimiwa viwanja vinne vya masoko ya Mkanyageni, Kengeja, Kangani na Mtambile, na alikuja mwenyewe Wizarani na kukutana na wahusika. Hata hivyo, Kamati imejiridhisha kwamba, taratibu za maombi ya kupimiwa hapa zilikiukwa na hoja iliyoelezwa kwa hali hiyo, inatokana na haraka ya kuhitajika upimaji huo.

Kamati ilipotaka kuelezwa taratibu zipi zinatumika katika kuomba na kupatiwa huduma ya upimaji, Wizara kwa mashirikiano na Idara ya Upimaji na kuelezwa ni kwanza Muombaji aombe kwa njia ya barua ; Baaada ya hapo, Wahusika wa Upimaji wanakwenda kulikagua eneo linalotaka kupimwa na kujiridhisha kwamba liko halali kisheria ; Baadae wanatoa gharama za upimaji kwa muombaji na iwapo malipo hayo yatakuwa taslim, basi fedha hizo huzipokea Idarani kupitia Mpokeaji wao wa fedha (Casheir), na hatimae huduma ya kupimiwa inafanyika.

Ilipohojiwa kwa nini wapimaji wa kiwanja hicho wamelipwa fedha taslim wakati ilitakiwa fedha hizo zilipwe Idarani kupitia Cashier na mlipaji kupewa risiti, Kamati ilielezwa kwamba, hupokea fedha hizo kwa kazi wanazozifanya. Jambo baya zaidi katika hili ni kwamba, Ndg. Hamad Khamis Ali, mfanyakazi wa Idara ya Ardhi na Mipango Miji ameomba fedha hizo kwa Katibu wa Halmashauri, kinyume nataratibu za malipo zinavyotakiwa, na fedha hizo kaziomba kama yeye kwa barua ya tarehe 20/02/2011 (Siku hiyo, ingawaje kulikuwa hakuna kazi kwa kuwa ni Jumapili)

Aidha, Kamati imegundua kuwa, fedha zote zilizotolewa kwa kazi hiyo haikuwa Tsh.300,000 pekee bali ni Tsh. 1,100,000 ambazo zimepotea katika mikono ya wafanyakazi wachache wala hazijaingia katika hesabu ya Idara. Fedha hizo walilipwa wafanyakazi wafuatao :

1. Ndg. Mkubwa Issa Juma.
2. Ndg. Hamad Khamis
3. Ndg. Moh'd Kombo.
4. Ndg. Kombo Mussa.
5. Ndg. Mwalim Zaidani.
6. Ndg. Said Khatib ; na Ndg.
7. Haji Hamad Haji;

Kwamba wamehusika kwa namna moja ama nyengine na kazi zilizofanywa kwa Halmashauri hiyo. wakati Kamati inafanya mahojiano na Ndg. Hamad Khamis, alisema kwamba yeye ni Mpimaji tu, taratibu za fedha na malipo hazijui. Hivyo, anachofahamu yeye ni kupokea fedha hizo kutoka kwa Katibu wa Halmashauri na alizitumia na wenzake walioshiriki katika kazi ya upimaji wa viwanja vyao vya soko. Na yeye kazitumia fedha hizo kwa kuwasiliana na Boss wake, Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Ardhi na Mipango Miji, na ndipo alipopata uhalali wa kuzitumia.

Maoni ya Kamati:

Kamati imejiridhisha kwamba, baadhi ya Watendaji wa Idara ya Ardhi na Mipango Miji, hutumia fedha za Serikali kwa kujinufaisha wao wenyewe, na Kamati inaiagiza Serikali kuwachukulia hatua za kinidhamu watendaji wote wa Idara hii tuliowataja hapo juu kwa kushiriki kwao kutumia fedha za Halmashauri ya Wilaya ya Mkoani, bila ya kutoa risiti halali ya malipo ambayo yangeliingia Serikalini, na matokeo fedha hizo kugawana wao wenyewe.

(RIPOTI YA TANO)

6.0 RIPOTI YA UKAGUZI YAKINIFU KWA MIRADI YA TAASISI ZA SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR KWA MWAKA WA FEDHA 2010/2011.

6.1 OFISI YA RAIS, FEDHA, UCHUMI NA MIPANGO YA MAENDELEO:

Ripoti hii inahusiana na ukaguzi yakinifu kwa miradi iliyokaguliwa kwa Taasisi mbali mbali za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kwa kipindi cha mwaka 2010/2011. Kamati imeifanyia kazi ripoti hii kwa kuzingatia sheria na kanuni zilizopo zinazohusiana na namna matumizi ya fedha za umma katika Miradi ya Serikali, yanavyotakiwa yawe.

Lengo la uchunguzi wa Kamati na kutoa ripoti hii, ni kutoa picha halisi ya namna ya miradi mbali mbali ya Serikali inavyotekelezwa. Katika kipimo hicho, Kamati ilizingatia namna gani utekelezaji wa miradi hiyo unaendana na Sheria zilizopo. Aidha, lengo pia la ripoti hii, ni kutoa picha halisi namna gani fedha na rasilimali za umma zinatumika kama zilivyokusudiwa au laa. Hivyo basi, Ripoti hii najumuisha ufafanuzi wa miradi iliyofadhiliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar pamoja na Wahisani wa Maendeleo. Ufafanuzi huo unahusika na hoja zifuatazo :

OFISI YA RAIS, FEDHA, UCHUMI NA MIPANGO YA MAENDELEO :

Hoja Namba 1.2 Kuhusiana na Ujenzi wa Jengo la Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo-Pemba.

Mradi huu wa Ujenzi wa Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kwa mwaka 2010/2011, umebainika kukiukwa kwa taratibu tokea kumpata mjenzi; Usimamizi na Ufuatiliaji katika hatua za awali; Usimamizi na Ufuatiliaji katika hatua ya ujenzi na taratibu nyengine. Hali hii imepelekea hasara kubwa kwa Serikali, na kuifanya Ofisi hii kwa upande wa Pemba kuendelea kukosa Ofisi na kubakia kukodi.

Maelezo ya Kamati:

Hoja hii tayari ilikwishafanyiwa kazi na Kamati Teule ya Kufuatilia mambo mbali mbali yaliyoibuka katika Bajeti ya Serikali ya mwaka 2011/2012, wakati huo huo, Mwenyekiti wa Kamati hiyo Teule pia ni Mwenyekiti wa Kamati ya P.A.C, Mhe. Omar Ali Shehe na Mjumbe Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando), alikuwa pia ni Mjumbe wa Kamati hiyo Teule, huku Katibu wa Kamati hiyo, Ndg. Othman Ali Haji, pia ni Katibu wa Kamati hii ya P.A.C.

Maoni ya Kamati:

Hoja hii haikufanyiwa kazi na Kamati, kwa sababu tayari ilikwishafanyiwa kazi na Kamati Teule na Kamati hii inaendelea kuitaka Serikali iyafanyie kazi mapendekezo yaliyoamuliwa na Baraza la Wawakilishi, kama yalivyopendekezwa na Kamati hiyo Teule.

6.2 WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA AMALI:

Hoja Namba 2.1 Kuhusiana na Uimarishaji wa Elimu ya Lazima (Zanzibar Basic Education Impreovement Project)

Mradi huu unaoshughulikia huduma za elimu kwa ajili ya maendeleo ya elimu Zanzibar, umehusika na ujenzi wa Maskuli, kutoa huduma za maabara, huduma za maktaba na huduma nyenginezo. Mradi ulipata fedha kutoka Serikalini na Benki ya Dunia kwa miaka mitano kuanzia 2008 jhadi 2013. Thamani ya Mradi wote ni USD 48,000,000 (Dola Arubaini na Nane Elfu) sawa na 72,000,000,000 (Bilioni Sabiini na Mbili), huku 63,000,000,000 (Bilioni Sitini na Tatu) zikitolewa kuwa ni mkopo kutoka Benki ya Dunia na Tsh.6,000,000,000 (Bilioni Sita) kutoka Serikalini.

Lengo la Mradi ni kuongeza idadi ya wanafunzi wanaoingia skuli za sekondari na kuimarisha miundombinu na ubora wa skuli za sekondari; pamoja na kuimarisha ubora wa elimu kwa kuwapatia mafunzo walimu na kufanya mapitio ya mitaala na upatikanaji wa vifaa vyua kufundishia. Skuli zilizohusika na mradi huu ni hizi zifuatazo:

1. Skuli ya Matemwe; iliyopo Mkoa wa Kaskazini Unguja, ilikitengewa Tsh. 1,475,761,520 na ipo katika hatua za mwisho za ujenzi.
2. Skuli ya Muwanda iliyopo Kaskazini Unguja, imetengewa Tsh.1,534,986,827, ipo katika hatua za mwisho za ujenzi.
3. Skuli ya Chaani, iliyopo Mkoa wa Kaskazini Unguja, ipo katika hatua ya mwisho ya ujenzi, imetengewa Tsh.1,297,683,591.
4. Skuli ya Uzini, iliyopo Mkoa wa Kusini Unguja, ipo katika hatua za mwisho na imeingiziwa Tsh. 1,287,099,957, ipo katika hatua za mwisho za ujenzi.
5. Skuli ya Dole iliyopo Mkoa wa Mjini Magharibi, imeingiziwa Tsh.1,025,727,359 na ipo katika hatua za mwisho za ujenzi.
6. Skuli ya Paje Mtule, iliyopo Mkoa wa Kusini Unguja, ipo katika hatua za mwisho za ujenzi na ilitengewa Tsh.1,329,956,779.
7. Skuli ya Tunguu iliyopo Mkoa wa Kusini Unguja, ipo katika hatua za mwisho za ujenzi na ilitengewa Tsh.1,069,713,280.
8. Skuli ya Dimani iliyopo Mjini Magharibi imetengewa Tsh.1,178,194,424, na ipo katika hatua za mwisho za ujenzi.
9. Skuli ya Pandani iliyopo Mkoa wa Kaskazini Pemba imetengewa Tsh.1,444,057,290 na ipo katika hatua za mwisho za ujenzi.

10. Skuli ya Chwaka/Tumbe iliyopo Mkoa wa Kaskazini Pemba ipo katika hatua za mwisho za ujenzi na imetengewa Tsh.1,512,898,346.
11. Skuli ya Konde iliyopo Mkoa wa Kaskazini Pemba imetengewa Tsh.1,179,616,867 na ipo katika hatua za mwisho za ujenzi.
12. Skuli ya Wawi iliyopo Mkoa wa Kusini Pemba ipo katika hatua za mwisho za Ujenzi na imetengewa Tsh. 1,489,460,402.
13. Skuli ya Kiwani Mauwani, ipo Mkoa wa Kusini Pemba na imetengewa Tsh.1,489,723,627 na ipo katika hatua za mwisho za ujenzi.
14. Skuli ya Ngwachani iliyopo Mkoa wa Kusini Pemba imetengewa Tsh.1,044,394,909 na ipo katika hatua za mwisho za ujenzi.
15. Skuli ya Utaani iliyopo katika hatua za mwisho za ujenzi, ipo Mkoa wa Kaskazini Pemba na imetengewa Tsh.1,232,866,581.
16. Skuli ya Mchanga Mdogo iliyopo Mkoa wa Kaskazini Pemba, ipo katika hatua za mwisho za ujenzi na imetengewa Tsh. 1,947,433,900.
17. Skuli ya Shamiani ipo Mkoa wa Kusini Pemba imetengewa Tsh.1,663,434,950 na ipo katika hatua za mwisho za ujenzi.
18. Skuli ya Fidel Castro iliyopo Mkoa wa Kusini Pemba, inaendelea na ujenzi na imetengewa Tsh 1,822,811,000.

Aidha, kwa upande wa Huduma za Ushauri (Consultancy Services); Mradi huu pia umelenga kufanya mambo yafuatayo:

- Kitengo cha CS/12, kazi ya Kuimarisha walimu wa skuli za msingi kwa sayansi na hisabati, tarehe iliyopangwa kukamilika ni 22/07/2009, fedha zilizotengwa ni USD 4,000 wakati hatua ya utekelezaji inaeleza kwamba ripoti ya mwanzo imeshatayarishwa.
- Kitengo cha CS/29, kwa ajili ya mapitio ya mitaala kwa elimu ya Diploma ya msingi, ilitarajiwa kukamilika tarehe 20/12/2010, huku fedha zilizotengewa ni USD 45,000 na hatua ya utekelezaji inaonesha kwamba, ripoti ya mwanzo imetayarishwa.
- Kitengo cha CS/31 kwa ajili ya kufanya tathmini ya ushiriki wa wanafunzi wa kike katika masomo ya sayansi, ilitarajiwa kukamilika tarehe 6/6/2011, kwa thamani ya USD 20,000 na hatua iliyofikia ni kuendelea kwa tathmini.

Kuhusiana na kazi za Ujenzi, Mradi umegawiwa kwa vitengo kadhaa kama ifuatavyo:

- Kitengo cha CW/4 kazi zilizopangwa zinahusiana na Ujenzi wa Skuli ya Kwamtipura Unguja; Skuli ya Kiembesamaki, Unguja na Skuli ya Mpendae, Unguja. Skuli zote hizo zilitajariwa kukamilika 22/02/2011, huku zikitengewa USD 2,350,524, ingawaje hadi wakati wa ukaguzi, skuli hizo zilikuwa zinasubiri ruhusa kutoka Benki ya Dunia.
- Kitengo cha CW/8 kilihusika na Ukarabati wa Skuli ya Forodhani, Unguja; Ukarabati wa Skuli ya Tumekuja, Unguja na Ukarabati wa Skuli ya Hamamni, Unguja. Kazi zote zilitarajiwa kukamilika tarehe 2/12/2010, huku zikitengewa USD 964,775, na ujenzi wa

Skuli ya Forodhani na Tumekuja umechelewa kuanza ingawaje baadae kazi za ujenzi zilikuwa zinaendelea, huku Skuli ya Hamamni haijaanza kabisa shughuli za ujenzi.

- Kwa Kitengo cha CW/9 kazi iliyopangwa ni Ukarabti wa Skuli ya Fidel Castro, Pemba; Ukarabati wa Skuli ya Uweleni, Pemba na Ukarabati wa Skuli ya Utaani, Pemba. Kazi ilitarajiwa kukamilika tarehe 2/12/2010, na fedha zilizotengwa ni USD 3,124,021 wakati Ukarabati wa Skuli ya Fidel Castros na Skuli ya Utaani ulichelewa kuanza, huku Skuli ya Uweleni wakati wa ukaguzi ilikuwa bado haijaanza kukarabatiwa.

Maelezo ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, kuhusiana na Mradi huu (Unguja):

Mradi huo umekuwa na mafanikio makubwa na ni kwa kihistoria kwa Wizara ya Elimu na Zanzibar kwa ujumla. Wizara imesimamia ipasavyo mradi huo, ingawaje kuna baadhi ya Skuli hadi Kamati inafika katika ukaguzi, Ujenzi wa Skuli hizo haukukamilika. Kwa ujumla Ujenzi wa Skuli hizo umekuwa na mafanikio kwa kiasi kikubwa, ambapo muhtasari wake ni kama ufuatao:

1. Skuli ya Matemwe; iliyopo Mkoa wa Kaskazini Unguja, ilikitengewa Tsh. 1,475,761,520. Hatua ya Ujenzi-Imekamilika, inasubiri kukabidhiwa kwa Wizara.
2. Skuli ya Muwanda iliyopo Kaskazini Unguja, imetengewa Tsh.1,534,986,827. Hatua ya Ujenzi-Imekamilika, inasubiri kukabidhiwa kwa Wizara.
3. Skuli ya Chaani, iliyopo Mkoa wa Kaskazini Unguja, imetengewa Tsh.1,297,683,591. Hatua ya Ujenzi-Imekamilika, inasubiri kukabidhiwa kwa Wizara.
4. Skuli ya Uzini, iliyopo Mkoa wa Kusini Unguja, ipo katika hatua za mwisho na imeingiziwa Tsh. 1,287,099,957. Hatua ya Ujenzi-Imekamilika, inasubiri kukabidhiwa kwa Wizara.
5. Skuli ya Dole iliyopo Mkoa wa Mjini Magharibi, imeingiziwa Tsh.1,025,727,359. Hatua ya Ujenzi-Imekamilika, inasubiri kukabidhiwa kwa Wizara.
6. Skuli ya Paje Mtule, iliyopo Mkoa wa Kusini Unguja, ilitengewa Tsh.1,329,956,779. Ipo katika Hatua za Mwisho za Ujenzi.
7. Skuli ya Tunguu iliyopo Mkoa wa Kusini Unguja, ipo katika hatua za mwisho za ujenzi na ilitengewa Tsh.1,069,713,280.
8. Skuli ya Dimani iliyopo Mjini Magharibi imetengewa Tsh.1,178,194,424, na ipo katika hatua za mwisho za ujenzi.
9. Skuli ya Pandani iliyopo Mkoa wa Kaskazini Pemba imetengewa Tsh.1,444,057,290. Hatua ya Ujenzi-Imekamilika, inasubiri kukabidhiwa kwa Wizara.
10. Skuli ya Chwaka/Tumbe iliyopo Mkoa wa Kaskazini Pemba na imetengewa Tsh.1,512,898,346. Hatua ya Ujenzi-Imekamilika, inasubiri kukabidhiwa kwa Wizara.

11. Skuli ya Konde iliyopo Mkoa wa Kaskazini Pemba imetengewa Tsh.1,179,616,867. Hatua ya Ujenzi-Imekamilika, inasubiri kukabidhiwa kwa Wizara.
12. Skuli ya Wawi iliyopo Mkoa wa Kusini Pemba na imetengewa Tsh. 1,489,460,402. Hatua ya Ujenzi-Imekamilika, inasubiri kukabidhiwa kwa Wizara.
13. Skuli ya Kiwani Mauwani, ipo Mkoa wa Kusini Pemba na imetengewa Tsh.1,489,723,627. Hatua ya Ujenzi-Imekamilika, inasubiri kukabidhiwa kwa Wizara.
14. Skuli ya Ngwachani iliyopo Mkoa wa Kusini Pemba imetengewa Tsh.1,044,394,909. Hatua ya Ujenzi-Imekamilika, inasubiri kukabidhiwa kwa Wizara.
15. Skuli ya Utaani iliyopo katika hatua za mwisho za ujenzi, na imetengewa Tsh.1,232,866,581. Hivi sasa Ujenzi-umekamilika, inasubiri kukabidhiwa kwa Wizara.
16. Skuli ya Mchanga Mdogo iliyopo Mkoa wa Kaskazini Pemba, ipo katika hatua ya kuendelea kwa ujenzi kwa awamu ya pili na imetengewa Tsh. 1,947,433,900.
17. Skuli ya Shamiani ipo Mkoa wa Kusini Pemba imetengewa Tsh.1,663,434,950. Ujenzi-umekamilika, inasubiri kukabidhiwa kwa Wizara.
18. Skuli ya Fidel Castro iliyopo Mkoa wa Kusini Pemba, hatua ya ujenzi imekamilika na imetengewa Tsh 1,822,811,000.

Maelezo ya Kamati:

Katika kulifanyia kazi suala hili, Kamati ilihitaji kuzitembelea skuli zote zilizoainishwa katika ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu w Hesabu, ingawaje kutokana na muda kuwa mdogo ilitembelea baadhi ambazo ufafanuzi wake ni kama ufuatao:

i. Skuli ya Uzini, iliyopo Mkoa wa Kusini, Unguja:

Ujenzi wa Skuli hii tayari umeshakamilika na imeshaanza kutumika. Kamati imeshuhudia walimu 14 waliopo, huku wawili ni wageni kutoka Nigeria. Walimu wote wanaosomesha hapo wana elimu isiyopungua Degree, huku walimu 10 wanaoishi Mjini na nyumba tatu zilizopo zinakaliwa na Mwalimu Mkuu na Msaidizi wake, huku nyumba mbili zilizobakia, kila moja inakaliwa na mwalimu wa Kigeni kutoka Nigeria.

Kinyume na matarajio na taswira ya Kamati, wanafunzi wanaosoma katika skuli hiyo wanatoka Uzini, Bambi na Dunga, hali ambayo kwa namna moja ama nyengine imechangia utoro kwa wanafunzi wanaotoka maeneo ya mbali. Jambo jengine la kushangaza ni upatikanaji wa wanafunzi hao, kwamba takriban ni wale walioshinda katika skuli walizotoka, hii inatokana na kutokuwepo kwa mikakati madhubuti ya kuwatafuta wanafunzi wa kusoma skuli hizo. Imekuwa ni khiyari ya Mwalimu Mkuu wa Skuli husika, kutoa idadi kadhaa ya

wanafunzi wake, hali ambayo kwa kawaida inamfanya Mwalimu huyo kuteuwa wale walioshinda na manunda.

Aidha, pamoja na uzuri wa Skuli hiyo na malengo yaliyokusudiwa, bado dakhalia ya kukaa na kutumiwa na wananfuzi haijajengwa kwa kuelezwa kwamba, bajeti yake haikuruhusu na Wizara inatarajia kujenga katika awamu nyengine ye mradi.

Maoni ya Kamati:

Kamati inapongeza kumalizika kwa ujenzi wa Skuli hii na kuanza kutumiwa, lakini haijaridhishwa na matumizi yake. Inaitaka Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, kuitumia Skuli hiyo kwa matumizi sahihi yaliyoombwa katika Mradi.

ii. Skuli ya Pale Mtule, iliyopo Mkoa wa Kusini Unguja:

Skuli hii bado haijakamilika na tayari imeshatelekezwa. Kwa ujumla inajengwa chini ya Mkandarasi na Makao Makuu ya Kampuni yapo Dar es Salaam. Ujenzi huu ulipaswa kumalizika August 2011, lakini kutokana na uhaba wa fedha kwa Mjenzi huyo, hadi Kamati inafanya ukaguzi, ujenzi umelala na hakuna tamaa ya kumalizika. Tatizo jengine lipo katika malipo, ambapo mjenzi anataka alipwe fedha zote ili akamilishe ujenzi, huku Wizara ya elimu bila ya 'Guarantee' ya Benki' hawako tayari kumlipa.

Maoni ya Kamati:

Kamati inahitaji kuchunguza sababu ya kufeli majengo hayo kwa kuangalia utaratibu mzima uliotumika kuwapata wakandarasi. Hata hivyo, kutokana na kukosa muda wa kufuatilia hoja hii, kwa kutumia kifungu cha 52(5)(b) cha Kanuni za Fedha za mwaka 2005, Kamati inahitaji taarifa hizo, ili izifanyie kazi na hatimae kutoa taarifa na maamuzi yanayofaa.

Aidha, Kamati inaitaka Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, kuhakikisha inakamilisha taratibu zilizopo ili ujenzi ukamilike. Katika kulitafutia ufumbuzi suala hili, Wizara inashauriwa kuangalia fursa ya kisheria, ili hatua zinazofaa ziweze kuchukuliwa kwa maslahi ya mradi ulivyokusudiwa. Kwa ujumla, Ujenzi wa Skuli ya Pale Mtule haujatimia na lengo lililokusudiwa halijafikiwa.

iii. Skuli ya Dimani:

Kwa upande wa Unguja, Kamati pia ilibahatika kutembelea Skuli ya Dimani, ambayo Mkandarasi wake ni yule yule wa Skuli ya Pale Mtule, na imefikia hatua ile ile bila ya kumalizika.

Maoni ya Kamati:

Kamati inaendelea kushauri kuwa ni vyema kuchukuliwa hatua zinazofaa ili ujenzi wa Skuli hii uweze kukamilika.

KWA UPANDE WA PEMBA:

Kamati iliona ni vyema kupata ufafanuzi wa Skuli ambazo zimo katika ukarabati na kwa utaratibu huo, ilitembelea Skuli hizo zinazotolewa ufafanuzi wake kama ifuatavyo:

i. Skuli ya Uweleni:

Kwa mujibu wa ripoti ya Mkaguzi, Mradi huu unahusiana an Ukarabati wa Skuli ya Uweleni, Pemba, umetarajiwa kutekelezwa na kukamilika tarehe 2/12/2010, ukikadiriwa kutumia USD 3,124,021 ambapo ulianza tarehe 1/7/2012. Wakati Kamati inafanya ukaguzi, Skuli ya Uweleni ilikuwa inaendelea kujengwa ikiwa katika hatua ya uwezekwaji, ukarabati wa jengo la walimu, kuongeza urefu, ujenzi wa stoo na mambo mengine.

Maelezo ya Wizara ya Elimu kuhusiana na Ukarabati wa Skuli ya Uweleni:

Pamoja na juhudi za utekelezaji wa mradi huu, Mshauri Mwelekezi wa Wizara ameeleza kwamba tathmini ya gharama za ujenzi iliyotolewa na Mjenzi, haikuwa sahihi kwa mnasaba wa ujenzi wenyewe. Hii inatokana kuwepo kwa majengo, mfano jengo la ghorofa na nyumba ya Mwalimu, hayatoweza kukarabatiwa kinyume na mkataba wa awali. Kinachoelezwa kusababisha hali hii ni kutokana na ghrama kubwa zilizoibuka wakati wa kufanya ukarabati, kinyume na tathmini iliyofanywa awali na Mjenzi.

Aidha, kutokana na kutokea kwa gharama zisizotarajiwa, kwa mfano wakati Mjenzi alipokuwa anaezua paa la jengo moja kati ya majengo yaliyopo, ukuta ulianguka ambapo kuinuliwa kwake kumetumia gharama zisisotarajiwa, kwani katika hesabu za awali, gharama za namna hiyo hazikuwemo. Aidha, hasara hiyo pia haikuonekana wakati wa ‘survey’ ya kazi yenyewe.

Maelezo ya Kamati:

Pamoja na maelezo ya Wizara, Kamati imepata shaka ya namna gani Wizara kwamba haikuwa makini na utendaji wa Mjenzi. Kwa mfano, inahoji kwa nini ukarabati huo usifanywe kwa majengo yote, wakati tokea mwanzo ndio dhamira ya mradi huu. Na kwa nini kama kuna gharama zisiwe kwa Mjenzi, kutokana na uzembe wake wa kutoona athari ya kuporomoka kwa baadhi ya kuta za majengo hayo, wakati kabla ya kupewa kazi ya ujenzi, alifanya tathmini na kuridhika kwamba, kazi hiyo angeliiweza kwa gharama zilizoainishwa katika Mkataba.

Maoni ya Kamati:

Kamati inaitaka Wizara kusimamia ipasavyo miradi ya maendeleo, kwa kuzingatia uzalendo na haja ya kutetea maslahi ya wananchi, kuliko maslahi ya Wakandarasi.

ii. Ukarabati wa Skuli ya Fidel Castro, Pemba.

Ukarabati wa Skuli ya Fidel Castro, ni sambamba na ukarabati wa Skuli ya Uweleni na Utaani, ambapo kwa pamoja fedha zilizotengwa kwa ajili ya shughuli hiyo zinafikia USD 3,124,021.

Ukarabati huo ulihusisha majengo yote ya Skuli hiyo, Jengo la Utawala, Maabara, Maktaba, ukumbi na jiko, majengo ya madarasa, nyumba 7 za walimu, mabweni ya wanafunzi wanaume na wanawake na maeneo mengineyo.

Maelezo ya Wizara kuhusiana na Ukarabati huo:

Ukarabati wa Skuli hii ulitarajiwa kumaliza May 2012, lakini uliongezwa muda hadi Novemba 15, 2012, lakini kutokana na kutokamilika, uliongezwa tena muda na kutarajiwa kumalizika Disemba 2012. Wakati Kamati inafanya Ukaguzi Novemba 2012, ujenzi tayari ulikwishakamilika kwa 90% huku likibakia suala zima la uungaji maji, umeme na maji hayo kufika katika maabara. Ukarabati pia umeongeza madarasa 6, Nyumba za walimu, bweni na mengineyo.

Sababu zilizopelekea kuongezwa muda ni kuongezeka kwa kazi kwa sababu, Mshauri Mwelekezi alipofanya 'feasibility study' hakuweza kugundua mambo mengi, ambayo wakati wa ukarabati wenyewe yaliweza kuonekana.

Maelezo ya Kamati:

Pamoja na sababu zilizoelezwa, Kamati haioni haja ya Mshauri Mwelekezi kushindwa kugundua kasoro ambazo kwa kiasi kikubwa kilipelekea mradi huo kuchelewa, lakini pia kuongezeka kwa gharama zisizotarajiwa. Hii yote inatokana na baadhi ya masuala ya msingi (items) kutoingizwa katika BOQ tokea awali, suala ambalo kwa miradi mikubwa kama hii, ilitarajiwa Mkandarasi na Mshauri Mwelekezi, waweze kuzingatia katika kufanya makisio ya ujenzi.

Hata hivyo, Kamati iliridhika kuelezwa kwamba, Wizara ilisimamia kwa kuandaa 'feasibility study' ya mara ya pili, baada ya ile ya mwanzo kutoainisha maeneo mengi tena kwa gharama za Mshauri Mwelekezi, kawni ni yeye aliyezembea katika 'feasibility study' ya awali, ingawaje hili nalo lilichukua tarkiban mwezi mzima.

Maoni ya Kamati:

Kamati inaipongeza Wizara kwa kusimamia Mradi huu, na kuitaka kuendelea kusimamia kwa makini, ili Skuli hiyo iweze kufikia lengo lililokusudiwa.

iii. Ujenzi wa Skuli ya Mchanga Mdogo:

Skuli hii iliyopo Kaskazini Pemba, ilitengewa Tsh.1,947,433,900 na wakati ukaguzi unafanyika, ilikuwa katika hatua za mwisho za ujenzi wake. Mradi huu ulikuwa una awamu mbili, ulihusisha madara 12, 'laboratory' 3, Chumba cha Kompyuta, library na madarsa 6, chini na juu.

Maelezo ya Wizara:

Mradi huu ulikuwa na awamu mbili, awamu ya kwanza ilimalizika na kukabidhiwa tarehe 5/3/2012 ambayo ilihusisha ghorofa ya chini, ila awamu ya pili iliyohusisha ghorofa ya pili,

ndiyo inayoendelea kujengwa. Pia inahusisha na kujengwa kwa hosteli za wanafunzi wakike na wakiume, na kila hosteli inatarajiwa kuwa na vyumba 26, na inatarajiwa kuchukua wanafunzi 114 kwa kila hosteli moja. Mjenzi wa Skuli hiyo ni Quality Building Constractor.

Maelezo ya Kamati:

Kamati imepata masikitiko ya namna utokaji wa fedha za ujenzi wa skuli hii, kwamba kwa awamu ya kwanza, fedha zilitolewa vizuri na kumuwezesha mjenzi kujenga kwa haraka na kwa ufanisi, ingawa katika awamu ya pili, fedha hazikutolewa kama kawaida, hali inayopelekea ujenzi kusita na kuchelewa, huku lengo la mradi likishindwa kutimia kwa wakati muafaka.

Maoni ya Kamati:

Kamati inaishauri Serikali kuharakisha upatikanaji wa fedha, huku pia iendelee kuwahimiza Wahisani kutoa fedha kwa wakati, ili ujenzi wa miradi ya Skuli, iweze kukamilika kwa wakati.

iv. Ujenzi wa Skuli ya Utaani

Mradi wa Ujenzi wa Skuli ya Utaani iliyopo Mkoa wa Kaskazini Pemba, ulitengewa Tsh.1,232,866,581, ambapo wakati wa ukaguzi, ulikuwa katika hatua ya mwisho ya kukamilika kwake. Mradi huu hatimae ulikamilika na kukabidhiwa June, 2012, na wanafunzi walihamia mwezi wa Novemba 2012.

Maelezo ya Wizara ya Elimu na Mfunzo ya Amali, kuhusiana na Mradi huu:

Mradi huu tayari umeshakamilika na tayari skuli imeshaanza kutumiwa, huku Wizara ikikabiliwa na changamoto kadhaa kuhusiana na mradi huu. Tatizo kubwa linalowakabili ni kutokuwepo kwa uzio huku uwanja wa mpira ukiwa ndani ya eneo la Skuli. Aidha, kunafanyika uharibifu wa makusudi wa kutia mawe katika ‘chambers’ za vyoo, huku vioo vya madirisha na mali nyengine za Skuli hiyo, vikihujumiwa na wananchi mbali mbali kwa sababu ya uwepo wa uwanja uanochezewa na timu za nje ya Skuli na kutokuwepo kwa uzio.

Maelezo ya Kamati:

Kamati pia imeshuhudia namna gani hujuma zinazofanyika katika skuli hiyo, wakati ilipofika mpira unaendelea kuchezwa, huku magoli ya uwanja huo, yameelekea kunako madirisha ya vioo vya skuli husika. vile vile Kamati imegundua matatizo madogo madogo, yakiwa ni pamoja na sehemu ya vyoo kuzidiwa na maji wakati wanafunzi wa kike wanapovitumia kwa kukoga, tatizo la umeme, karo kutofunikwa na choo kinakuwa nje.

Maoni ya Kamati:

Kamati imeitaka Wizara kukaa pamoja na Mkandarasi, kurekebisha kasoro ndogo ndogo zilizojitokeza ukizingatia bado wakati Kamati inafanya ziara, ujenzi huo ulikuwa haujakabidhiwa rasmi kwa Wizara kutoka mikononi mwa Mkandarasi.

Kamati inaitaka Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, kuharakisha ujenzi wa uzio kwa skuli hii, pamoja na uwanja uliomo ndani kupatiwa ufumbuzi unaofaa, ili kusiwepo kwa hujuma zinazoendelea kufanyika, kila siku.

6.3 WIZARA YA KILIMO NA MALIASILI:

Hoja Namba 3.1 Kuhusiana na Mradi wa Mpango wa Kuendeleza Huduma za Kilimo (Agricultural Service Support Program-ASSP).

Mradi huu wa kuendeleza Huduma za Kilimo ni mradi unaotoa huduma kwa wananchi, uliofadhiliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Mkopo kutoka Shirika la Kimataifa (IFAD) pamoja na nguvu za wananchi.

Malengo yake ni kuimarisha upatikanaji na utumiaji wa elimu na maendeleo ya kilimo kwa wananchi wa vijijini pamoja na kushajiisha upatikanaji wa akiba ya chakula na kuongeza pato la wananchi.

Mradi huu unatekelezwa kwa kiwango kinachoridhisha kwa kufikia wastani wa 69% wa utekelezaji wake kwa mwaka 2010/2011, ingawa mwenendo mzima wa usimamizi wake ulihitaji kuangaliwa kwa makini kwa sababu kumejitokeza kmapungufu ambayo yanaweza kusababisha hasara kwa kuchelewa kutekelezwa kwa majukumu yaliyopangwa na hatimae kupelekea kutokamilika kwa mradi kwa wakati. Na kwa hali hii, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu, alishauri kuharakishwa kwa utekelezwaji wa mradi huo ili uweze kukamilika kwa wakati na hatimae kutoa tija iliyokusudiwa kwa wananchi.

Maelezo ya Wizara:

Wanakiri kuchelewa utekelezaji wa mradi huo, hali inayosababishwa na kuchelewa kwa kuingizwa fedha.

Maelezo ya Kamati:

Pamoja na majibu ya Wizara, kwa kua suala la mradi linahitaji muda mrefu na mpana, ni vyema kwa Kamati ikapata muda kwanza kuelimishwa kwa undani kuhusiana na mradi huu, namna unavyotekelezwa, kupitia masharti ya Mkataba na mambo mengine yanayohusiana.

Maoni ya Kamati:

Kwa kutumia kifungu cha 52(5)(b) cha Kanuni za Fedha za mwaka 2005, Kamati inahitaji muda wa ziada kuufanyia kazi Mradi huu.

Hoja Namba 3.2 Kuhusiana na Mpango wa Kuendeleza Huduma Sekta ya Ufugaji (Agricultural Support Development Program-Livestock/ASDP-L)

Mradi huu wa kuendeleza Huduma sekta ya ufugaji ni mradi unaotoa huduma kwa wananchi, uliofadhiliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Mkopo kutoka Shirika la Kimataifa (IFAD) pamoja na nguvu za wananchi.

Malengo yake ni kuimarisha uwezo na kipato cha wafugaji wadogo wadogo; Kushajiisha upatikanaji wa huduma za maendeleo kwa wafugaji wadogo wadogo na Kuimarisha miundombinu ya masoko kwa wafugaji wadogo wadogo.

Hali ya utekelezaji wa Mradi huu ni ya kuridhisha kwa mujibu wa malengo yaliyopangwa kwa kufikia wastani wa 77% ya utekelezaji wa mradi. Hata hivyo, inaonekana bado mwenendo mzima wa usimamizi wa utekelezaji wa mradi huu unahitaji kuangaliwa kwani kumejitokeza mapungufu ambayo yanaweza kusababisha hasara kwa kutotekelezwa kwa baadhi ya shughuli muhimu zinazoimarisha ukuaji wa sekta ya mifugo. Shughuli muhimu ambazo zimeonekana kutopewa kipaumbele katika utekelezaji ni ujenzi wa miundombinu na upatikanaji wa zana. Ukaguzi pia ulibaini kuwepo kwa matumizi makubwa katika shughuli za uendeshaji na huduma za mikataba. Hali inayoweza kupelekea kutokamilika kwa mradi kwa wakati uliopangwa.

Maelezo ya Wizara:

Ni kweli maelezo ya Mdhibiti an Mkaguzi Mkuu wa Hesabu, ingawaje uchelewaji wa utekelezwaji wa mradi huu unasababishwa na utaratibu mzima wa uingizwaji wa fedha, suala ambalo liko nje ya uwezo wa Wizara.

Maelezo ya Kamati:

Kama ilivyo kwa Mradi wa ASSP, ni vyema kwa Kamati kupata muda mzuri zaidi wa kuupitia Mradi huu kwa kina, tokea malengo yake, maombi ya fedha na utekelezaji wake, kito kwa kituo. Na kwa kuzingatia muda mdogo uliopewa Kamati, Kamati haikuweza kuufatilia Mradi huu kwa undani.

Maoni ya Kamati:

Kamati inahitaji muda na taarifa zaidi za Mradi huu, ili iweze kutoa maoni yake ipasavyo.

6.4 WIZARA YA ARDHI, MAKAAZI, MAJI NA NISHATI.

Hoja Namba 4.1 Kuhusiana na Mradi wa Maji Safi n Salama.

Mradi wa Maji Safi na Salama unashughulikia utoaji wa huduma ya maji safi na salama kwa wananchi wa Zanzibar, huku sehemu kubwa ya mradi huu ni mkopo kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika na kusimamiwa na Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA). Pia mradi huu unapata fedha kutoka vianzio mbali mbali ikiwemo Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, UN Habitat na RWSSI.

Mradi huu ni wa miaka minne kuanzia mwaka 2009 hadi 2013 ambapo thamani yake ni UA 33.3 Milioni, kati ya hizo ADB ni UA 25 milioni, RWSSI ni UA 3.0 milioni na RGOZ ni UA 4.07 milioni na UN Habitat ni UA 1.23 milioni.

Lengo kuu la mradi huu ni kusambaza maji safi na salama mijini na vijijini, Unguja na Pemba, huku Mdhibiti akieleza kuwa, kwa upande wa utekelezaji wake, hauridhishi kutokana na malengo yaliyopangwa kutotekelezwa kama ilivyokusudiwa. Ukaguzi pia umebaini kwamba,shughuli zilizotekelezwa katika mradi huu hazikufikia kiwango cha kuleta matumaini kwani utektelezaji wa kazi ulifikia 15% tu ya utekelezaji. Pia imebainika kwamba, mwenendo mzima wa usimamizi wa utekelezaji wake unahitaji kuangaliwa kwani kumejitokeza mapungufu ambayo yanaweza kusababisha kutofikiwa lengo kwa kutotekelezwa baadhi ya shughuli zinazoimarisha upatikanaji wa maji safi na salama.

Shughuli muhimu zilizopewa kipaumbele ni kutowa mafunzo kwa wadau na watumiaji wa huduma za maji, huku matumizi makubwa yamefanyika katika shughuli za uendeshaji na ununuzi wa vifaa vya Ofisi, hali ambayo inaweza kupelekea kutokukamilika kwa mradi kwa wakati uliopangwa na kutofikiwa kwa malengo yaliyokusudiwa.

Maelezo ya Mamlaka ya Maji, kuhusiana na Mradai huu:

Mamlaka ilikiri kwamba wakati wa kuanza mradi hatua za mwanzo zilikuwa ni matayarisho na kuweka miundombinu itakayowezesha utekelzaji wa mradi huo. Na hivyo kuonekana kwamba fedha nyingi zimeanza kutumika katika shughuli za uendeshaji na ununuzi wa vifaa.

Maoni ya Kamati

Kamati baada ya kutembelea mradi huo na kupata maelezo iliridhika kabisa na hatua ya mradi iliyofikiwa na kutokana na mwenendo wa utekelezaji wake basi hapana shaka lengo hilo litafikiwa kwa wakati uliopangwa.

Aidha, msisitizo wa Kamati ni kufanywa kwa utafiti wa kina, ili kuweza kubaini maeneo yaliyo na maji ya kutosha na uhakika wa umeme katika vituo.

6.5 WIZARA YA MIUNDOMBINU NA MAWASILIANO:

Hoja Namba 5.1 Kuhusu Mradi wa Uimarishaji wa Barabara za Zanzibar :

Mradi huu unahusika na utengenezaji wa barabara mbali mbali za Unguja, uanopata fedha kutoka kwa ADB kupitia mkopo na msaada. Thamani ya mradi wote ni UA 16.93 milioni , kati ya hizo UA 16.22 milioni ni mkopo na UA 0.71 milioni ni msaada kutoka ADB. Kwa upande wa Serikali ya mapinduzi ya Zanzibar nayo inawajibika katiak kuchangia fedha za ufanikishaji wa mradi huo.

Malengo ya Mradi ni kupunguza matengenezo ya magari na barabara pamoja na kuimarisha huduma za usafiri wa barabara katika kisiwa cha Unguja pamoja na kuweka mtandao mzuri wa barabara.

Kwa mwaka unaoishia Juni 2011, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilikwishachangia Tsh. 3.100 bilioni, huku matumizi halisi kwa mnasaba wa fedha zote zilizopatikana pamoja na kutoka kwa wahisani, zilitumiwa kwa matumizi yafuatayo:

Tsh. 3,129,950,511 alilipwa Mwananchi Engineering and Constracting Company Ltd.

Tsh. 1,998,430,109 alilipwa S.S Mehta & Sons Ltd.

Tsh. 304,563,968 alilipwa Mshauri wa Ujenzi wa barabara,

Tsh. 3,000,000 zililipwa kwa ajili ya ada za ukaguzi, na

Tsh. 1,073,316,003 ni malipo kwa ajili ya fidia kwa wananchi.

Hivyo, jumla ya Tsh. 6,509,260,591 zimetumika kwa shughuli za hapo juu.

Aidha, kwa mwaka 2010/2011, Mradi umetekeleza ujenzi wa barabara na ulipaji wa madeni ya nyuma uliotokana na ujenzi wa barabara na hivyo, barabara zilizojengwa ni Amani – Dunga na Mfenesini – Bubwini. Vile vile mradi umelipa bakaa ya deni kwa kampuni ya S.S Mehta & Sons Ltd iliyojenga barabara ya Paje-Makunduchi na Kinyasini –Tunguu.

Tatizo ni kwamba, utekelezaji wa mradi huu uko nyuma kiwakati kutokana na uchelewaji wa kutekeleza shughuli mbali mbali zinazohusiana na ujenzi wa bara bara.

Kwa upande wa malipo ya fidia, ukaguzi wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu, umebaini kwamba, mradi umefanya malipo ya fidia kwa wananchi walioathirika na ujenzi wa barabara mbali mbali, lakini tathmini ya malipo hayo iliyofanywa na wataalamu (Valuer) haikuzingatiwa katika kufanya malipo. Hali hii imepelekea kujitokeza kwa dosari mbali mbali wakati wa kulipa fidia hizo, ikiwa ni pamoja na kulipwa waathirika kima tofauti na kile kilichoainishwa katika ripoti kwa mujibu wa tathmini ; kulipwa watu wengine ambao hawakuwemo katika ripoti ya kitaalamu. Kwa ujumla hali hii imepelekea malalamiko makubwa kwa wananchi walioathirika na kuchelewesha zoezi zima la ulipaji wa fidia pamoja na ujenzi wa barabara hizo.

Maelezo ya Wizara :

Ujenzi wa barabara za mradi wa Uimarishaji wa barabara za Zanzibar, umechelewa kutokana na sababu mbali mbali ikiwa ni pamoja na kutopewa eneo la ujenzi kwa wakati, kubadilishwa usanifu (change design) wa madaraja yaliyokuwa katika mradi huo na kuongezeka kwa kazi za mradi (increase of quantities). Matatizo haya yalipelekea Mkandarasi kuongezewa muda kama Mkataba ulivyoainisha. Aidha, kwa ucheleweshaji ambao ulisababishwa na Mkandarasi mwenyewe, Wizara ilimtoza faini (liquidated damage) ambayo ilikatwa katika madai aliyokuwa

anaidai Serikali. Hivi sasa tayari Mkandarasi huyo ameshakamilisha kazi yake na ameshaikabidhi Serikalini.

Kuhusu malipo ya fidia, ni kweli kuwa waathirika wa ujenzi wakati mwengine hulipwa tofauti na ripoti ya wataalamu wa tathmini. Hali hii husababishwa na Serikali kuzifanyia uhakiki tathmini hizo na kugundua mapungufu ambayo hufanyiwa marekebisho. Utaratibu huu wa kuzifanyia uhakiki ripoti za fidia, kwa kiasi kikubwa umepunguza malalamiko kwa vile mapungufu yanayoonekana katika ripoti hizo hurekebishwa kabla ya ulipaji. Aidha, utaratibu huu kwa kiasi kikubwa umekuwa ukiisaidia Serikali kuokoa fedha nyingi ambazo zingelilipwa kwa watu ambao malipo yaliyoainishwa kwenye ripoti ya mtathmini, hayaendani na hali halisi ya mali zao. Vile vile katika kutatua tatizo la fidia, Wizara imepeleka warak Serikalini na kutoa mapendekezo ambayo yanaweza kumaliza tatizo hilo.

Maelezo ya Kamati :

Ili Kamati kujiridhisha juu ya usahihi wa maelezo ya Wizara kuhusiana na dosari zilizoainishwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu, Kamati ilihitaji kupatiwa Mkataba ulioingiwa baina ya Wizara na Mkandarasi. Hata hivyo, ilielezwa kwamba, Mkataba huo uko nje ya Afisi, na hivyo, ulichukua muda wa kufuatwa na kuwasilishwa, jambo ambalo lilipelekea mpaka Kamati inaondoka Wizarani, Mkataba huo haukuweza kuwasilishwa.

Pamoja na Wizara kueleza namna ya ulipaji wa fidia kwa wananchi, Kamati inafahamu kwamba, jukumu zima la ulipaji wa fidia hiyo husimamiwa na Serikali, kwa maana fedha hutolewa na Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, huku kitendo cha Wizara hii kuonesha kwamba, fedha hizo huchelewa kutolewa pamoja na kwamba, tayari zilikwishakisiawa tokea awali, hakioneshi kwamba, ni sababu ya msingi inayopelekea wananchi kukosa haki zao za fidia kwa mnasaba wa tathmini ya kitaalamu iliyofanywa. Ni jukumu la Serikali na Wizara kwa ujumla kuhakikisha kwamba, wananchi wanalipwa fidia zao, kabla mradi wowote haujaanza kutekelezwa, ili ridhaa ya wananchi itangulie katika utekelezaji wa mradi husika.

Kamati imehoji kuhusu kumtoza faini Mkandarasi, kama ilivyoelezwa na Wizara, kwamba kwa mujibu wa taarifa zilizowasilishwa kwa Kamati na Wizara hii, Mkandarasi ndie aliyewadai Wizara Tsh. 11.887,762,159 kupitia madai mawili, ingawaje baadae kwa mashauriano ya Mshauri Mwelekezi wa Wizara pamoja na kukaa pamoja baina ya Wizara na Mkandarasi, ndipo Mkandarasi alipokubali dai lake hilo kupungua hadi Tsh. 3,400,000,000 na kwa kuwa Wizara hapo kabla ilikuwa inamdai Tsh.1,537,667,541.18, ndipo Mkandarasi alipokuwali kupewa Tsh. 1,862,332,458.82 ya fedha zote (Tsh. 11 bilioni).

Pamoja na maelezo hayo, Kamati imeshindwa kuthibitisha iwapo kweli kikao hicho kilimhusisha Mshauri Mwelekezi, kinyume na maelezo ya Wizara, kwa sababu kumbukumbu za mkutano zilizokabidhiwa kwa Kamati, zinathbitisha kwamba, kikao hicho kilikuwa ni baina ya Wizara na Mkandarasi (Kampuni ya MECCO).Aidha, Kamati inamashaka mwakubwa sana juu ya utaratibu mzima wa kukubaliana juu ya malipo ya fidia iliyotoka, kwani tokea madai ya 11 bilioni hadi

kukubali milioni 1, ni lazima kuna mambo mengi yanayotia mashaka iwapo kweli makubalino ya malipo hayo ni halisi.

Kuhusiana na malipo ya fidia, Kamati haikuridhishwa na hatua za Wizara na Serikali kwa ujumla, za kukataa ripoti ya mtaalamu, iliyowashirikisha ipasavyo wananchi, na hivyo ni sawa na kusema kwamba, Serikali haioni haja ya kulipa fidia kwa mujibu wa thamani halisi ya soko kwa mali za wananchi wanaoathirika na ujenzi, jambo ambalo hata katika Sheria za Ardhi, halikubaliki.

Maoni ya Kamati :

Kamati inahitaji muda zaidi wa kuipita hoja hii na kwa kutumia kifungu cha 52(5)(b), cha Kanuni za Fedha za mwaka 2005, Kamati itaifanyia kazi tena hoja hii.

Hoja Namba 5.2 Kuhusiana na Mradi wa Ujenzi wa barabara ya Amani–Mtoni, Awamu ya Pili.

Mradi huu umeanza Mei hadi Disemba 2011 na kudhaminiwa na Serikali ya Jnamhuri ya Muungano wa Tanzania chini ya ahadi ya Rais Mstaafu, Mhe. Benjamin W. Mkapa, aliyoitoa mwaka 2005 katika ufunguzi wa barabara ya Amani-Mtoni, awamu ya mwanzo yenye urefu wa 3.8km.

Lengo la Mradi huu ni kukamilisha ujenzi wa barabara ya Amani-Mtoni na kuimarisha huduma za miundombinu, Unguja. Mradi huu ulikabidhiwa Idara ya Ujenzi na Utunzaji wa Barabara, ambapo msimamizi Mkuu ni Mhandisi Mkuu wa Ujenzi wa Idara hiyo.

Jumla ya Tsh. 1,600,000,000 zimepokelewa kutoka Serikali ya Jamhuri ya Muungano kupitia Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na baadae kuingizwa kupitia hesabu za mradi wa Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano, Februari 2011. Fedha zilizotumika hadi ukaguzi unafanywa ni Tsh. 1,599,194,090 kama ifuatavyo:

Kazi ye Ujenzi	Tsh. 1,185,596,162
Utengenezaji wa magari	Tsh. 406,821,778,
Mtayarisho	Tsh. 6,776,150

Huku bakaa likiwa ni Tsh. 805,910.

Ukaguzi umebaini kwamba, matumizi mengi yaliyofanyika hayakufuata utaratibu na sheria za manunuzi. Aidha, shughuli zilizofanywa hazikulenga kufanikisha lengo lililokusudiwa na kupelekea kukosekana kwa ufanisi katika utekelezaji wa mradi huo na tija kwa wananchi. Mambo yaliyobainika kukiukwa taratibu zake ni haya yafyatayo :

1. ***Ununuzi wa Kifusi Tsh. 144,720,000.***

Ukaguzi umebaini Wizara imefanya malipo ya ununuzi wa kifisu kwa muuzaji binafsi, Salum Civil Engineering & Construction Works. Hali iliyopelekea kutumika kiasi kikubwa cha fedha kwa kulinganisha iwapo kifusi hicho kingelinunuliwa katika machimbo ya Serikali. Pia utaratibu wa manunuzi haukufuatwa kulingana na sheria za manunuzi za Zanzibar.

2. Lami iliyonunuliwa kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya Amani-Mtoni.

Lami iliyonunuliwa kwa 'supplier' Southshore International Limited ya Mombasa Kenya kwa ajili ya ujenzi wa barabara hiyo ambayo ilipelekwa Kibele, tarehe 29/08/2011 kama ilivyoelezwa katika kumbukumbu za ghalani, baada ya miezi miwili tu, lami hiyo ilikopeshwa Kampuni ya MECCO kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa barabara za Amani-Dunga na Mfenesini-Bumbwini, ili kuwahi muda uliopangwa kwa barabara hizo.

Aidha, lami hiyo ilitakiwa kurejeshwa katika kipindi cha miezi miwili lakini hadi ukaguzi unakamilika, lami hiyo bado haijarejeshwa na hakuna hatua yoyote iliyochukuliwa.

3. Malipo ya posho.

Ths.91,564,937 zimelipwa kwa ajili ya posho kwa wafanyakazi 151ambao waliotegemewa kufanya kazi katika mradi wa ujenzi wa barabara ya Amani-Mtoni awamu ya pili, lakini kiwango cha fedha hizo zilizolipwa ni kikubwa ukilinganisha na kazi iliyofanywa pia na madhumuni ya mradi wenyewe.

4. Matumizi ya manunuzi ya vipuri

Fedha nyingi zimetumika kwa ajili ya ununuzi wa vipuri pamoja na mipira ya gari. Matumizi hayo hayakulenga kutekeleza ujenzi wa barabara iliyokusudiewa. Kutokana na hali hii, matumizi hayo hayakuleta tija kwa mradi huo kwani hatua iliyofikiwa hailingani na fedha zilizotumika. Aidha, Sheria, Kanuni na taratibu za manunuzi hazikufuatwa.

Kwa ujumla, wakati ukaguzi unafanyika, iligundulika kwamba, hali ya utekelezaji wa mradi huu hairidhishi kwani muda uliopangwa kukamilisha umeshapita na fedha zilizotolewa kwa ajili ya mradi huo zimeshatumika kwa asilimia 99.9, huku kiwango cha barabara kilichofikiwa hakilingani na fedha zilizotumika na hakuna tija iliyopatikana.

Maelezo ya Wizara.

Kuhusu ununuzi wa kifusi, Tsh.144,720,000, Wizara ililazimika kununua kwa kampuni hiyo binafsi baada ya kutumia 'Single Source of Procurement' kutokana na fedha za ununuzi wake kuingia mwishoni mwa mwaka 2009, huku wakitakiwa wazitumie fedha hizo kwa haraka kubwa. Aidha, wamelazimika kutumia machimbo ya Serikali, kwa sababu wakati wanafanya ujenzi huo, kulikuwa na 'conjuctions' kubwa za barabara iliyotokana na ujenzi wa barabara ya Mwanakwerekwe, hali ingeliwapelekea kupata usumbufu wa upitishaji wa magari yao.

Maelezo ya Kamati:

Kamati haijaridhishwa na majibu ya Wizara kuhusiana na Ununuzi wa Kifusi, kwa kuzingatia fedha zilizotumika ni nyingi, huku Wizara ikitumia machimbo binafsi badala ya Serikali. Aidha, kwa kutumia kifungu cha 32(2) cha Sheria ya Manunuzi ya mwaka 2005, Wizara ilitakiwa iombe idhini ya kutumia njia hiyo walioyoitaja, na kwa kutumia dokezo la tarehe 8/02/2011 lililowasilishwa kwa Kamati kuhusiana na kikao cha dharura cha Bodi ya Zabuni ya Wizara, Kamati imeridhika kwamba, hatua hii imefuatwa. Hata hivyo, suala hili limeelezwa kugharimu Tsh.108,000,000 na wala sio Tsh.144,720,000 kama ilivyoripotiwa katika ripoti ya Mdhibiti. Suala hili kutokana na muda na undani wa taratibu zilizotumika, Kamati haikupata muda wa kujitosheleza kupata ufafanuzi wake, na hivyo ni vyema suala hili likarejewa kwa kina katika vikao vijavyo vya Kamati.

Maoni ya Kamati:

Kwa kutumia kifungu cha 52(5)(b) cha Kanuni za Fedha za mwaka 2005, Kamati inahitaji taarifa zaidi na muda wa kutosha, kabla ya kufikia maamuzi ya suala hili.

Maelezo ya Wizara kuhusiana na Lami iliyonunuliwa kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya Amani-Mtoni.

Ni kweli lami hiyo haikurrejeshwa baada ya miezi miwili na badale yake imerejeshwa baada ya miezi mine, lakini la kupaswa kuzingatiwa ni kurejeshwa kwa lami hiyo. Hatua za kurejeshwa kwa lami hiyo ni Idara ya Ujenzi na Utunzaji wa Barabara iliikabidhi lami hiyo kwa Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano, kupitia Kitengo cha Manunuzi cha Wizara ambacho kiliikabidhi kwa MECCO na hata kurejeshwa kwake, imerejeshwa kwa taratibu zinazofaa.

Maelezo ya Kamati:

Kwa mujibu wa Mkataba ulioingiwa baina ya Wizara na Kampuni ya MECCO, lami hiyo ilitakiwa irejeshwe ndani ya miezi miwili, na iwapo isingelirejeshwa, ni wajibu wa Kampuni ya MECCO kulipa fidia kwa Wizara chini ya 10% ya gharama za lami hiyo katika bei ya soko kwa wakati husika. jambo la kushangazwa ni kwamba, Kampuni ya MECCO imevunja Mkataba, na Wizara haijachukua hatua zozote za kudai fidia kama ilivyoelezwa kwatika Mkataba.

Maoni ya Kamati:

Kamati inaelekeza Serikali kuwa makini na Kampuni binafsi, kwa kutumia mali za wananchi kinyume na makubaliano yaliyoingiwa baina yao. Aidha, kwa uzembe huu uliofanyika, Kamati inaitaka Serikali kutoa onyo kwa Watendaji wa Wizara kutosimamia ipasavyo Mikataba inayoingiwa baina ya Wizara na Makampuni binafsi.

Maenelezo ya Wizara kuhusiana na Malipo ya Posho Tsh.91,564,937

Wizara inasema malipo hayo yaliyoripotiwa kufanyika ni kidogo ukilinganisha na usahihi halisi wa fedha hizo. Fedha zilizotengwa kwa ajili ya malipo haya ni Tsh.171,976,750 na zilizotumika

mpaka wakati wa ukaguzi ndio hizo Tsh.91,564,937 kama ilivyoripotiwa. Na kwa mnasaba wa mradi, matumizi yake ni sahihi kwa mujibu wa taratibu zinazohusika. Fedha hizo zimeombwa kwa ajili ya chakula cha mchana kwa miezi yote mitano iliyohusika na kazi za ujenzi. Huku kazi iliyobakia ni ndogo sana, kulinganisha na ile iliyomaliza, na hivyo kwa matumizi ya fedha hizo, hakuna tatizo lolote la kusema kwamba, fedha zimetumika nyingi zaidi kuliko zilizokusudiwa.

Maelezo ya Kamati:

Kamati pia haina pingamizi na ulipwaji wa posho kwa mnasaba wa maombi yake yaliyohusika, ingawaje tatizo lipo katika wingi wa fedha zilizoombwa za posho tu, hali inayopelekea kama kwamba mradi huu kuwa kutumika zaidi kwa matumizi hayo tu. Kwa mfano, malipo hayo ya posho yanafikia wastani wa 10% kulipiwa chakula pekee, mbali na posho jengine zinazostahiki kwa watendakazi hawa. Tatizo jengine, posho hiyo pamoja na kukubaliwa na Wizara, lakini inashindwa kuonesha vigezo sahihi vilivyotumika kuwalipa baadhi ya watendakazi, ambao kwa kawaida ilipaswa ielezwe tokea kwenye mradi malipo yao. Kwa mfano, watu kama Support Cashier wanne, kwa kila mmoja kulipwa Tsh. 7,500 kunashindwa kuonesha ulazima wa wote kuwepo katika kazi. Aidha, Internal Auditor, Accountants, sio lazima washiriki katika kazi hiyo kwa takriban siku zote, jambo linaloonesha malipo haya yapo kwa msingi wa kujuana zaidi.

Maoni ya Kamati:

Kamati inakubaliana kwamba, malipo ya posho hayakuwa ya msingi kiasi ya kutumika fedha nyingi katika Mradi ambao haukukamilika na ni sawa na kwamba, fedha za mradi huo zimetumika zaidi kwa maslahi ya watendaji wa Wizara hii na sio kwa mradi.

Maelezo ya Wizara kuhusiana na Matumizi ya Manunuzi ya Vipuri, Tsh. 342,641,778

Ukaguzi umebaini kwamba, fedha nyingi zimetumika kwa ajili ya ununuzi wa vipuri pamoja na mipira ya gari, lakini matumizi hayo hayakulenga kutekeleza ujenzi wa barabara iliyokusudiwa. Hivyo, matumizi hayo hayakuleta tija kwa mradi huo kwani hatua iliyofikiwa hailingani na fedha zilizotumika huku sheria za ununuzi wake hazikufuatwa.

Maelezo ya Wizara kuhusiana na Ununuzi wa Vipuri:

Matumizi ya mashine, zana nzito na magari yaliyotumika kwenye ujenzi, ni sehemu ya gharama za ujenzi kwa barabara husika. katika kufanikisha hili, jumla ya Tsh. 123,456,000 zilitengwa katika mradi huo, ingawaje kutokana na uchakavu wa zana nzito pamoja na baadhi ya magari ya Idara ya UUB, matangenezo ya dharura ya mara kwa mara yalifanywa na hivyo kuwalazimi kutumia Tsh. 342,641,778.

Utaratibu walioutumia katika kununua vipuri hivyo ni njia ya ‘three qoutation’ kwa sababu matumizi ya mradi huu yalihusiana na dharura (Emergency Breakdowns) huku vipuri hivyo vilinunuliwa kwa mujibu wa mahitajio na taratibu husika za uhifadhi (store procedures). Vile

vile thamani halisi ya vipuri hivyo kwa kila muda wa kununuliwa ulipowadia, haikuzidi kima kinachohitajika kuitishwa kwa zabuni.

Maelezo ya Kamati:

Wizara wakati inatoa ufafanuzi mbele ya Kamati ilieleza kwamba, hakuna bajeti iliyotengwa kwao kwa ajili ya ununuzi wa vipuri, hali ambayo kwa namna moja ama nyengine imeifanya kutumia fedha nyingi kutoka katika mradi huu, kinyume na bajeti husika, kwa lengo la kuhakikisha mradi unafanikiwa. Katika hili, waliiomba Kamati iwasaidie kuifahamisha Serikali kwamba, ununuzi wa zana nzito ni bei kubwa, na Serikali iizingatie katika upitishaji wa bajeti ya Idara ya UUB, ili tatizo hili liweze kuondoka.

Kwa upande wa hoja halisi, Kamati haikupata muda muafaka wa kuangalia kwa kina namna gani suala la vipuri limetekelezwa ipasavyo. Suala hili kwanza linahitaji ufafanuzi wa bajeti halisi ya fedha za mradi zilizotolewa, taratibu zilizotumika kununua, uthibitisho wa vielelezo vilivyohusika na manunuzi, na hata kujiridhisha iwapo kweli Idara haikuwa na Bajeti ya Ununuzi wa Vipuri kwa mwaka husika.

Maoni ya Kamati:

Kamati inahitaji kupata muda zaidi wa kuifanyia kazi hoja hii.

Hoja Namba 5.3 Kuhusu Ujenzi wa Barabara tatu, Pemba.

Mradi wa ujenzi wa barabara tatu za Pemba, umeanzishwa kwa ajili ya kuzijenga upya barabara za Wete-Konde na Wete-Gando kwa awamu ya kwanza na barabara ya Wete-Chake katika awamu ya pili. Mradi huu ujefadhiliwa na Benki ya Kiarabu ya Maendeleo ya Afrika (Arab Bank of Economic Development in Africa) (BADEA) pamoja na Mfuko wa Saudia (Saudi Fund).

Mradi huu ni wa miaka mitatu, ambapo awamu ya kwanza itachukua miaka 2 na miezi 5 na awamu ya pili ni miezi 7. Mradi huu ulianza 2009 na kumalizika Septemba 2012, huku wajenzi wa barabara hizo ni M/S MEECCO na Construction General Rainone S.P.A kwa pamoja. Mradi umekadiriwa kutumia Tsh.53,255,251,093.66

Mradi umekusudia kukamilisha ujenzi wa barabara za Wete-Gando kwa awamu ya mwanzo na Wete-Chake kwa awamu ya pili, ili kuimarisha huduma za miundombinu, Pemba. Fedha zilizoidhinishwa kutumika mwanzo ni Tsh.23,389,551,848.75, ambapo Tsh. 7,787,931,949.12 zilitumika sawa na 33% ya fedha zilizoidhinishwa.

Hata hivyo, ukaguzi ulibaini kwamba, awamu ya mwanzo ya ujenzi wa barabara ya Wete-Konde na Wete-Gando, haijakamilika kwa wakati ambapo ilitakiwa kukamilika Januari 30, 2012, lakini hadi ukaguzi unakamilika, ujenzi huo bado ulikuwa haujakamilika.

Maelezo ya Wizara kuhusiana na Mradi huu:

Ni kweli kwamba utekelezaji wa mradi huu ulichelewa kwa mujibu wa wakati uliopangwa, hali iliyotokana na upatikanaji mdogo wa fedha kutoka kwa Wafadhili (BADEA). Kwa upande wa Wizara inapotokezea hali kama hii, hufanya juhudi za namna yoyote iwezekanayo kuwasiliana mara kwa mara na Wafadhili hao, lakini hupata tatizo la kujibiwa kwa wakati.

Maelezo ya Kamati:

Kamati ilizipitia barabara zote tatu za Wete –Konde, Wete-Gando na Wete-Chake ambazo zinafadhiliwa na Benki ya Kiarabu ya Maendeleo ya Kiuchumi ya Afrika,(Arab Bank of Economic Development in Africa) pamoja na Mfuko wa Saudia (Saud Fund), huku ikielewa kwamba Mradi huu ambao ni wa miaka mitatu, awamu ya mwanzo ingelichukua miaka miwili na miezi mitano na awamu ya pili ya mradi ni miezi saba. Kutokana na makubaliano, mradi huu ulitakiwa uanzie tarehe 1 Septemba, 2009 na kumalizikia tarehe 30 Septemba, 2012. Wajenzi wa njia hizo ni M/s MECCO na Construction General Rainone S.P.A kwa pamoja. Mradi huo ulikadiriwa kutumia jumla ya Tsh. 53,255,251,093.66.

Hata hivyo, Kamati haikuridhika hata kidogo juu ya mwenendo mzima wa ujenzi wa barabara hizo. Hasa kwa kuzingatia kwamba matatizo yake yapo kwa pande zote mbili , upande wa Serikali kama mjengewa na vilevile kwa upande wa mjenzi na mfadhili wa ujenzi huo.

Kamati imearifiwa kwamba Mradi huo ni wa awamu mbili (Two Phase) Ambapo kwa Awamu ya mwanzo jumla ya Sh.233,989,551,848.75 zilipangiwa kufanya kazi hiyo na ilikuwa ikabidhiwe Tarehe 31/1/2012 hata hivyo ilishindikana na kuongezwa hadi Tarehe 30/9/2012 na hadi Kamati inapita hakuna dalili ya kukamilisha ujenzi huo.

Ieleweke tu kati ya fedha hizo zilizopangwa asilimia 28.6 yake ni mchango wa SMZ ambazo ni sawa na Sh. 6.6 Bil. Ikiwa ni mbali na malipo ya fidia kwa waathirika wa majumba na vipando vyao wakati wa ujenzi, fidia ambayo Sh. 3.7 bilioni. Kwa ujumla SMZ ina mchango wa Sh. 10.3 Bilioni.

Kamati inakubali kwamba matatizo makubwa yaliyokwamisha ujenzi huo ni kutokupatikana kwa wakati fedha kwa ajili ya fidia za wananchi walioathiriwa na ujenzi lakini jengine hata ni namna ya utoaji wa fedha hizo kutoka kwa wafadhili , nao unachukua muda mrefu na una urasimu mkubwa .

Ijapokuwa wakati Kamati inafanya kazi kwenye Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano Kisiwani Pemba ilipata taarifa kwamba tayari Serikali imeshaingiza fedha Sh. 520 Milioni kwa ajili ya fidia.

Maoni ya Kamati:

Serikali wakati wa kufunga mkataba unaohusu mikopo kwa miradi kama hii ya ujenzi, iangalie sana kipengele kinachohusu mtiririko wa upatikanaji wa fedha, ili usiwe ni wenye urasimu mkubwa.

Serikali vilevile ijitahidi kutimiza ahadi kwa kutoa mchango wake kwa wakati.

Kamati inaitaka Serikali kukaa karibu sana na wafadhili na kuwafahamisha athari zinazopatikana kutokana na ucheleweshwaji wa fedha zao walizoazimia kuisaidia nchi, huku Kamati ikiitaka Serikali ianze kuwa na mipango ya kujitegemea na sio kila siku kutegemea wafadhili.

Kamati pia inaitaka Wizara (Makao Makuu, Unguja) kukaa pamoja na kuwashirikisha ipasavyo Wizara, Pemba, ili wafahamu kwa kina na washiriki kikamilifu katika kuisimamia Miradi ya wananchi iliyochini ya Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano, Pemba.

6.6 WIZARA YA AFYA:

Hoja Namba 6.1 Kuhusiana na Mradi wa Kupunguza vifo vya mama na watoto:

Mradi huu ni mkopo uliotolewa na Benki ya Maendeleo ya Afrika na kusimamiwa na Wizara ya Afya. Mradi unatoa huduma ya afya ya mama na watoto kwa lengo la kupata uzazi salama na kupunguza vifo vya mama na mtoto Zanzibar. Mradi ni wa miaka mitano kuanzia 2007 hadi 2012, ambapo thamani halisi ya mradi wote ni UA 44.44 milioni. Kati ya hizo, 40.00 milioni ni mkopo kutoka ADB na UA 4.44 milioni ni mchango wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Hata hivyo, tatizo linajitokeza katika utekelezaji wa mradi huu, kwamba ulitegemea kumalizika 2012, laikini hadi ukaguzi unafanyika 2010/2011, ulibaini kwamba, hatua za utekelezaji wa mradi huo kwa baadhi ya maeneo hairidhishi ikiwemo ujenzi wa majengo pamoja na utunzaji wake. Hali hiyo imejitokeza katika majengo yafuatayo:

Jengo la Wagonjwa wa Akili, Hospitali ya Wete.

Wizara imeingia mkataba na Kampuni ya Stance Technic & Civil Engineering Ltd, Mkataba namba MOH/SMMRP/MW-PBA tarehe 12/04/2011, wenye thamani ya Tsh. 360,788,585.60 kwa ajili ya ujenzi wa jengo la wagonjwa wa akili hospitali ya Wete, Pemba. Hadi ukaguzi unamalizika, fedha zilizotumika kwa ujenzi huo ni Tsh.225,609,163.04 ni sawa na 62.5 ya fedha za ujenzi wote, huku ukaguzi ukishindwa kuridhishwa kwa hatua iliyofikiwa ya ujenzi kulingana na fedha zilizotumika.

Maelezo ya Wizara:

Ni kweli kwamba, Wizara ya Afya imeingia kwenye mkataba na Kampuni ya Stance Technic & Civil Engineer Ltd Tarehe 12/04/2011 wenye thamani ya Sh. 360,788,585.60 kwa ajili ya ujenzi wa Jengo la Wagonjwa wa Akili Hospitali ya Wete Pemba. Jengo ambalo lilitarajiwa kukamilika ujenzi wake mwezi wa Februari, 2012. Hata hivyo, hadi kufikia mwezi wa Januari, 2012 gharama ambazo amelipwa mjenzi ni kiasi cha Sh. 225,609,163.04, kati ya hizo Sh. 72,157,717.00 zilikuwa kitangulizi ambacho kinakuwa kinarejeshwa kidogo kidogo kiasi

ambapo ujenzi unapokamilika atakuwa amekamilisha marejesho. Kwa maana hiyo fedha ambazo zimetolewa kwa ujenzi ni Sh.153,451,446.04.

Kilichoonekana ni kwamba mjenzi hakuweza kukamilisha kwa wakati kutokana na mkataba ulivyo, lakini vile vile idadi ya fedha ilikuwa ni kubwa na hailingani kabisa na hali halisi inayoonekana. Hata hivyo uongozi wa Hospitali ulikiri mbele ya Kamati juu ya kile kinachoonekana na Mkaguzi kuwa ni kasoro kwamba kimetokana na sababu nyingi miongoni mwa hizo ni mazingira ya eneo la ujenzi na uharaka wa upatikanaji wa vifaa. Ardhi ya eneo hilo sio nzuri kwa ajili ya kuhimilimaina ya ujenzi uliokusudiwa kujengwa, hivyo panahitajika uangalifu mkubwa katika aina na ubora wa vifaa jambo ambalo si tu linaongeza gharama bali pia hata muda nao hasa kwa vile vifaa vingi vinavyojengewa huwa havipatikani kisiwani Pemba hivyo suala la usafirishaji nalo lilichangia kwa kiasi kikubwa.

Maelezo ya Kamati:

Wakati Kamati inatembelea eneo hilo la ujenzi iliridhirika na hatua iliyopo kwani jengo lilikuwa karibu asilimia 80 na linatia moyo kwamba halikuwa na muda mrefu lingemalizika.

Maoni ya Kamati:

Kamati inaitaka Wizara ya Afya, kuharakisha kukamilika kwa ujenzi huo, ili lengo lililokusudiwa liweze kufikiwa.

Ukarabati na Ujengaji wa Vituo vya Afya vitatu na Nyumba za Wafanyakazi, Pemba:

Wizara imeingia Mkataba na Kampuni ya Mazrui Building Constractors Ltd, namba MOHSW/SMMRP/SLD-SH/P/LOT-4/2008 wenye thamani ya Tsh. 3,926,328,987 kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa vituo vya Afya na nyumba za wafanyakazi. Ujenzi huo ulitakiwa kukamilika kwa kipindi cha muda wa miezi 18, kutoka Januari, 2009 hadi Juni 2010. Aidha, ukarabati na ujenzi wa nyumba za wafanyakazi wa Afya kwa kiasi kikubwa umekamilika, lakini kuna baadhi ya nyumba zilizojengwa, tayari zimeshaanza kuathirika kutokana na ujenzi kuwa chini ya kiwango. Ujenzi huo ni huu Ufuatao:

Sehemu ya Sakafu ya Kituo cha Afya, Kengeja.

Kwa ujumla Wizara inakiri juu ya kasoro zilizojitokeza. Hata hivyo, katika sehemu hiyo ya sakafu, kituo cha Afya Kengeja, uharibifu huo ulitokea katika kipindi cha dhamana (warranty period) na hivyo, Mkandarasi alitakiwa na Wizara kufanya marekebisho yaliyotakiwa nae bila ya pingamizi yoyote amerekebisha semehu hiyo ya sakafu kwa kuitoa tarazo yote iliyokuwemo kabla na kutia taizi.

Maelezo ya Kamati:

Ni kweli Kamati ilipatiwa taarifa hiyo katika sehemu ya tukio na imejiridhisha kwamba taizi tayari zimeshatiwa katika sakafu husika, na hivyo mipasuko hiyo iliyokuwepo awali, haipo tena.

Maoni ya Kamati:

Kamati inaipongeza Wizara ya Afya kwa kulifuatilia suala hilo na kulipatia ufumbuzi wake, kabla halijawa kubwa lakini zaidi katika wakati muafaka.

Sehemu ya Sakafu ya Nyumba ya Wafanyakazi, Tundauwa.

Kama ilivyokuwa Kengeja, Ujenzi baada ya kumalizika mwaka 2011, kweli sehemu ya sakafu ya nyumba ya wafanyakazi, Tundauwa, ilifanya ufa. Kwa kuwa kasoro hiyo imejitokeza katika wakati wa 'guarantee', Wizara iliwasiliana na Mjenzi ambae alikuja fanya marekebisho hayo.

Maelezo ya Kamati:

Kamati imejiridhisha kwa kuona hatua za kuondosha kasoro za awali zimechukuliwa ipasavyo. Hata hivyo, imegundua kuwepo kwa mipasuko midogo midogo ambapo ilipata maelezo kwamba imesababishwa na ardhi yenyewe ya eneo hilo. Hata hivyo, mipasuko pia imeonekana wazi katika eneo la baraza za nje (apron), hali ambayo kama itaachiwa, baadae inaweza kuleta madhara kwa uhai wa nyumba hizo.

Maoni ya Kamati:

Kamati inaitaka Wizara ya Afya, kuhakikisha mipasuko hiyo katika baraza za nje, inazimbwa na kuondoshwa.

Sehemu ya Nyumba ya Wafanyakazi, Pujini.

Na sehemu ya nyumba ya wafanyakazi, Pujini nayo imeonekana kasoro zake, na Wizara imechukua hatua ya kuziba nyufa zilizokuwemo, kazi iliyofanywa katika kipindi cha 'guarantee' mara tu baada ya kukabidhiwa kwa nyumba hizo.

Maelezo ya Kamati:

Kamati imetembelea eneo husika na kupata ufafanuzi ambao iliupokea. Hata hivyo, imegundua pia kuvuja kwa sink katika sehemu iliyohusika na matengenezo. Aidha, nyuba hii imefanya ufa mkubwa sehemu za baraza ya nje na kunako mashimo ya karo, pamoja na kufanya ufa katika baadhi ya kuta, hali ambayo Kamati imeelezwa kwamba, inatokana na ubaya wa ardhi katika sehemu husika.

Maoni ya Kamati:

Kamati inaitaka Wizara ya Afya, kuhakikisha kasoro zote zilizojitokeza na zinazoendelea kujitokeza hivi sasa zinashughulikiwa kwa haraka katika wakati unaofaa.

6.7 WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, UTALII NA MICHEZO :

Hoja Namba 7.1 Kuhusiana na Jengo la Kamisheni ya Utalii, Pemba.

Kamisheni ya Utalii, Pemba, inamiliki jengo lililonunuliwa kutoka kwa Ndg. Ali Abeid Nassir, kwa thamani ya Tsh. 30,000,000 tangu mwaka 1992 kwa ajili ya ujenzi wa Ofisi ya Kamisheni ya Utalii, Pemba. Hata hivyo, bado jengo hilo halijafanyiwa matengenezo yoyote kwa kipindi cha miaka 20 sasa tokea liliponunuliwa.

Kutokana na hali hiyo, Kamisheni ya Utalii, bado inaendelea kukodi jengo kwa amtumizi ya Ofisi kutoka kwa Ndg. Said Rashi Mbarouk, tokea mwaka 1992 hadi leo. Aidha, kutofanyiwa kwa matengenezo ya jengo hilo kwa kipindi kirefu sasa, kumesababisha kutumiwa kwa fedha nyingi ya kukodi nyumba na kupelekea kuendelea kutelekezwa kwa rasilimali ya nyumba iliyonunuliwa kwa fedha nyingi za Serikali.

Maelezo ya Kamisheni ya Utalii :

Tngu kuanziwshwa kwa Ofisi hapa Pemba, Kamisheni imekuwa inakodi nyumba hadi leo. Kodi hiyo ilinaza kwa thamani ya Tsh.2,400,000 kwa mwaka, hali ianyoikwaza sana Kamisheni. Tatizo kubwa linalopelekea Ofisi hiyo iliyonunuliwa tangu mwaka 1997, ishindwe kukamilishwa kunatokana na ukosefu wa fedha, ambapo Kamisheni inaamini laiti kama Asilimia 5 (5%) ya Kodi ya Hoteli (Hotel Levy), ambayo iliidhinishwa na Baraza la Wawakilishi kwamba ipewe kwa Kamisheni ya Utalii, basi Kamisheni ingeliweza kujenga Ofisi yake Pemba. Aidha, wana matumiani sana kwamba, Kamati ya P.A.C itawasaidia katika kuifahamisha Serkali, umuhimu wa kupatiwa 5% kama ilivyokubaliwa awali.

Katiak kufanya juhudi za kulipatia ufumbuzi tatizo hili, Kamisheni ya Utalii waliwahi kufanya mazungumzo na Mshauri Mwelekezi (Consultant Runs) ambae alitaka alipwe Tsh. 25,745,000 kwa ajili ya kulifanyia matengenezo jengo hilo, fedha ambazo walishindwa kuzipata. Kwa hivi sasa wamepata ushauri kutoka kwa Waziri anaeshughulikia masuala ya ardhi, kwamba, kwanza jengo hilo lifanyiwe tathmini , ingawaje hadi Kamati inafika, bado tahmini hiyo haijafanyika.

Kamisheni imekubali kwamba inaendelea kukodi nyumba kaw ajili ya Afisi, nyumba ambayo mmiliki wake ni Ndg. Shaaban Mbarouk Ali na sio Ndg. Said Rashid Mbarouk kama ilivyoripotiwa na Mdhibiti.

Maelezo ya Kamati :

Kamati ilitaka kufahamu iwapo hapo kabla, Kamisheni ya Utalii waliwahi kutenge fedha kwa ajili ya ujenzi wa Afisi yao, na kuelezwa kwamba, hawajawahi kutenga fedha zozote kwa wajili ya ujenzi na badala yake wamewahi kuliingiza katika bajeti yao na kuomba fedha za ujenzi, lakini hawajafanikiwa, hata hivyo, wameshindwa kuthibitisha mbele ya Kamati, madai yao hayo.

Kamati imepitia malipo ya kodi ya mwaka 2012, yenye thamani ya Tsh. 3,600,000s na imegundua kwamba, hayana uthibitisho wa risiti za kuthibitisha mapokezi ya fedha hizo kwa Mkodishaji. Tatizo hilo pia lilipatikana kwa takriban malipo yote yaliyokaguliwa na Kamati,

huku Kamisheni ikisisitiza kwamba, Mmiliki wa jengo hilo anatoa risiti za malipo, mara tu wanapomlipa fedha za kodi. Majibu ya Kamisheni yalitakiwa yathibitishwe na Mshika Fedha na Mkaguzi wa Ndani wa Kamisheni ambao alishindwa bila ya dharura, kuhudhuria mbele ya Kamati.

Maoni ya Kamati:

Kamati inaitaka Serikali kuhakikisha wamiliki wa nyumba binafsi zinazokodishwa, wawe wanalipa kodi Serikalini, hali itakayopelekea kutoa risiti halali za malipo. Aidha, Kamati haikufurahishwa na kitendo cha Mkaguzi wa Ndani pamoja na Mshika Fedha wa Kamisheni ya Utalii, kukimbia kikao cha Kamati, wakati taarifa kamili wanazo na wamefanya hivyo, bila hata ya kutoa taarifa kwa Uongozi wa Kamisheni. Kamati inaeshauri watendaji hawa wachukuliwe hatua za kinidhamu.

Kuhusiana na jengo la Kamisheni, Kamati inaiagiza Serikali kuliendeleza jengo hilo ili liweze kuisaidia Kamisheni ya Utalii kwa shughuli za Ofisi na kuacha kukodi jengo kwa matumizi hayo. Katika kufanikisha hili, Serikali kupitia miradi mbali mbali na kwa njia yoyote iliyo halali, watenge pesa na kujenga.

6.8 OFISI YA RAIS, UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA :

Hoja Namba 8.1 Kuhusiana na Ujenzi wa Jengo la Chuo cha Utawala wa Umma, Tunguu.

Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa mwaka 2007/2008 iliandaa mpango wa Mradi wa Ujenzi wa Chuo cha Utawala wa Umma, kupitia fedha za Serikali na kuingiziwa Tsh.150,000,000/- kwa ajili ya kusafisha kiwanja, ujenzi wa uzio na kutafuta hati miliki ya eneo hilo. Kwa mwaka huo huo, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi iliitisha zabuni ya ujenzi kwa taasisi za ndani ya Vikosi vya SMZ ambapo Kikosi cha Kuzuia Magenzo (KMKM) kilishinda zabuni hiyo, iliyoshindaniwa na vikosi vyengine vya Mafunzo na JKU.

Mkataba wa Ujenzi baina ya Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na KMKM ulitaka Ujenzi huo umalizike kwa kipindi cha wiki 104, sawa na miaka miwili, huku gharama zote za ujenzi wa Chuo hicho kwa hatua ya ghorofa Moja ni Tsh. 1,061,233,400/-. Jumla ya Tsh. 750,000,000/- sawa na 74% ya Mkataba wa Ujenzi, tayari zilikwishalipwa, huku huku Ujenzi huo kwa mwaka 2010/2011 wakati Ukaguzi unafanyika, ulikuwa hauridhishi na haikulingana na hali halisi ya fedha zilizotumika pamoja na makubaliano ya Mkataba. Aidha, taarifa mbali mbali za kitaalamu kuhusiana na ujenzi huo, hazikuweza kupatikana kwa ukaguzi, hali iliyopelekea Wakaguzi kushindwa kuelewa mipango ya kuliendeleza jengo hilo kwa kuzingatia muda mrefu ujenzi huo ulikuwa umesita na kuwepo uwezekano mkubwa wa kutokea uharibifu, kupanda kwa

gharama za ununuzi wa vifaa na hatimae kutofikiwa kwa malengo yaliyokusudiwa kwa wakati uliopangwa.

Maelezo ya Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora:

Ujenzi huo umechelewa kutokana na ukosefu wa fedha, kwani unafadhiliwa moja kwa moja na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, ambapo kwa mwaka wote wa fedha 2007/2008, ni Tsh. 150,000,000/- pekee ziliingizwa kwa lengo la usafishaji wa kiwanja, ujenzi wa uzio kuzunguka eneo lote la kiwanja na kutafuta hati miliki ya eneo. Aidha, kwa miaka iliyofuatia, kutokana na hatua ya ujenzi, mwaka 2008/2009; 2009/2010 mradi ulipangiwa kutumia Tsh.600,000,000/- ambapo kila mwaka uliingiziwa Tsh.300,000,000/-, na kwa miaka mitatu fedha zote za Ujenzi kwa hatua ya kwanza (Tsh.750,000,000/-) ndizo zilizopatikana.

Aidha, sababu nyengine ya kuchelewa ni maamuzi ya kufanywa marekebisho ya nondo zilizotumika katika ujenzi wa nguzo za kusimamisha jengo, ambapo nondo za 24mm zilitumika badala ya nondo za 16mm zilizokubaliwa mwanzo. Marekebisho hayo yamefanywa na mtaalamu (Msimizi Elekezi), Ndg. Ramadhan Mussa Bakar (Rama China), kwa lengo la kuimarisha umadhubuti wa jengo.

Sababu ya tatu ni kutokana na Uongozi wa Juu wa Baraza la Mapinduzi kuamua kufanywa kwa marekebisho mengine ya kuongeza kumbi mbili kubwa, yaliyoamuliwa wakati Uongozi huo ulipolitembelea jengo hilo, marekebisho ambayo hapo kabla hayakuwahi kuingizwa katika thamani ya mwanzo ya ujenzi (Contract Price).

Kuhusia na na taratibu zipi zilizotumika kupatika kwa Mjenzi (KMKM); Mshauri Mwelekezi, Ndg. Ramadhan Mussa Bakari, na hata Kampuni ya ZECCON Limited ya Zanzibar, iliyotoa michoro ya Ujenzi wa Jengo hilo, hazikuweza kuelezwa kwa Kamati, kwa sababu ni Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ndiyo iliyohusika na upatikanaji wao. Aidha, Ujenzi huo tayari umeshakamilika kwa ghorofa ya chini, na tayari Chuo cha Utawala wa Umma kimeshahamia huko, ingawaje ulikamilishwa na Chuo cha Mafunzo, badala ya KMKM, kama Mjenzi aliyekubalika awali, chini ya Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Kuhusiana na matumizi ya Tsh. 150,000,000 zilizotumika kwa kusafisha kiwanja, ujenzi wa Uzio na kutafuta hati miliki, Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora, hawana uwezo wa kutoa ufafanuzi kwa Kamati, na badala yake ni Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ndiyo iliyohusika. Aidha, kuhusiana na ushauri wa kutumika nondo za 24mm badala ya 16mm, ni suala linaloweza kutolewa ufafanuzi na Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Maelezo ya Kamati:

Hoja hii inahusika zaidi na taratibu za kupatikana kwa Mkandarasi, Mshauri Mwelekezo na Mtoaji wa Michoro. Aidha, kuna haja ya kujiridhisha matumizi ya Tsh. 150,000,000

zinazoelezwa kwamba zimetumika kwa kusafisha kiwanja, kutia uzio, ambao Kamati ilipotembelea haijakuta uzio wowote zaidi ya nguzo za zege, ambapo kadhaa zimeshaanguka. Aidha, Kamati inahitaji pia kujiridhisha juu ya fedha zilizotumika, huku ikishangaa na kutaka kufuatilia kwa kina, sababu zilizopelekea jengo hilo kumalizwa na Chuo cha Mafunzo badala ya KMKM ambao tokea mwanzo ndie mjenzi aliyepewa kazi baada ya kushinda zabuni ya ujenzi wa jengo hilo.

Maoni ya Kamati.

Kamati haiwezi kujiridhisha na ufafanuzi wa hoja hii, mpaka itakapokutana na Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, ambapo hatimae ilipanga kukutana na Uongozi huo, na Kikosi cha KMKM, Chuo cha Mafunzo na Mtaalamu Elekezi, Ndg. Ramadhan Mussa Bakar tarehe 17/03/2013, lakini kutokana na sababu za kutokuwa na nafasi kwa baadhi ya Watendaji wa Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kikao hicho hicho hadi hii leo hakijafanyika, licha ya Kamati kutaka kufanyika, lakini watendaji walio na kazi nyingi na muhimu zaidi kuliko Kamati, hatimae kikao hicho hakikufanyika. Aidha, kwa kutumia kanuni ya 52(5)(b) ya Kanuni za Fedha ya mwaka 2005, Kamati itafuatilia tena suala hili kwa mwaka ujao.

SEHEMU YA TATU :

HITIMISHO :

Sehemu hii ya Ripoti inahusiana na Maoni ya Kamati na Mapendekezo yake kwa Baraza la Wawakilishi, ili iiagize Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kutekeleza yale yote ambayo Kamati imeyapendekeza. Kwa ujumla, Ripoti yetu inatofautiana sana na ripoti za Kawaida za Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi. Kwa Kamati hizo inakuwa rahisi sana kupendekeza Mapendekezo yote ya Kamati katika sehemu moja, lakini kwa kuwa Kamati ya P.A.C inachunguza hoja moja baada ya moja inayotokana na Ripoti ya Mdhibiti na Mkauguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, inakuwa kwa namna yoyote ile, lazima mapendekezo ya Kamati yawe katika baada ya ufafanuzi wa Hoja husika.

Hii ina maana kwamba, katika ripoti hii tumeeleza vitu vinne kwa takriban kila hoja. Jambo la kwanza tumeitaja Hoja yenyewe na kutoa maelezo yake kama Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu alivyofanya katika Ripoti zake ; jambo la pili tulieleza maelezo ya Wizara. Sehemu hii inamaanisha majibu yote ya Wizara iliyojibu mbele ya Kamati kuhusiana na Hoja ya Mdhibiti. Maelezo ya tatu ni Maelezo ya Kamati. Sehemu hii inahusiana na uchambuzi na ufafanuzi wa Kamati kuifafanua hoja ya Mdhibiti kwa namna ilivyokuwa inaifanyia kazi na kwa kuzingatia uchunguzi wake mbele ya Taasisi husika ; na maelezo ya mwisho ni Maoni ya Kamati. Hapa

panahusiana na maagizo na mapendekezo ya Kamati kuhusiana na hoja ya Mdhibiti na Majibu yaliyotolewa na Taasisi husika.

Hivyo basi, katika kuifanyia kazi ripoti hii, mapendekezo ya Kamati yote yanapatikana katika ripoti yenyewe na katika sehemu hii ya tatu ya Hitimisho, Kamati inaliomba Baraza la Wawakilishi, iiagize Serikali kutekeleza maoni yote ya Kamati kama yalivyo katika ripoti hii.

Baada ya maelezo hayo, Kamati inapenda kutoa shukurani za dhati kwa Wizara, Mashirika na Taasisi zote za Serikali kwa mashikiano makubwa waliyoyaonesha wakati wote wa kazi za Kamati. Shukurani pia ziwafikie Watendaji wote wa Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu kwa mashirkiano mazuri waliyoipa Kamati wakati wote, aidha Kamati inatoa shukurani za pekee kwa Afisi hii ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu, Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, Afisi ya Baraza la Wawakilishi, na Taasisi zote zilizohusika kwa kuiandalia mafunzo kuhusu mada mbali mbali yanayohusiana na majukumu yake, kwa lengo la kuiwezesha kutekeleza vyema majukumu hayo.